# Itifaki ya Kimataifa kuhusu Utayarishaji wa Nyaraka na Upelelezi wa Unyanyasaji wa Kijinsia katika Mfarakano



Viwango vya Msingi vya Njia Bora za Kutayarisha Nyaraka za Unyanyasaji wa Kijinsia kama Uhalifu chini ya Sheria ya Kimataifa

**TOLEO LA KWANZA: JUNI 2014**

# Itifaki ya Kimataifa kuhusu Utayarishaji wa Nyaraka na Upelelezi wa Unyanyasaji wa Kijinsia katika Mfarakano

## Viwango vya Msingi vya Njia Bora za Kutayarisha Nyaraka za Unyanyasaji wa Kijinsia kama Uhalifu chini ya Sheria ya Kimataifa

Toleo la Kwanza: Juni 2014

# Yaliyomo


## MWANZO 04

## i. UTANGULIZI 06

## ii. MATUMIZI YA ITIFAKI 10

a) Kusudi 10
b) Watazamaji 10
c) Itifaki ni ipi 11
d) Matumizi ya siku zijazo 12

## SEHEMU I: UNYANYASAJI WA KIJINSIA 14

### 1. KUELEWA UNYANYASAJI WA KIJINSIA 15

1.1 Muktadha wa Unyanyasaji wa Kijinsia 15
1.2 Kukabili Unyanyasaji wa Kijinsia 16

### 2. UNYANYASAJI WA KIJINSIA KAMA UHALIFU CHINI YA SHERIA YA KIMATAIFA 16

2.1 Maelezo ya Mwanzo 16
2.2 Ufafanuzi wa hatia za unyanyasaji wa kijinsia kwa ujumla 17
2.3 Sehemu A: Hatia maalum za unyanyasaji wa kijinsia au uhalifu ambao unaweza kufanywa kwa kupitia unyayasaji wa kijinsia: "Nini kilitokea?" 18
2.4 Sehemu B: Vipengele vya muktadha wa uhalifu wa kimataifa: "Nini kilitokea mazingira ambayo (tendo la unyanyasaji wa kijinsia) lilitokea"? 23
(i) Unyanyasaji wa kijinsia kama uhalifu wa kivita au kama uvunjwaji wa sheria na desturi za vita 23
(ii) Unyanyasaji wa kijinsia kama uhalifu dhidi ya utu 24
(iii) Unyanyasaji wa kijinsia kama mauaji ya kimbari 24
2.5 Sehemu C: Mfumo wa dhima kwa matendo ya uhalifu wa kimataifa: "Ni vipi anayeshukiwa kufanya lile kosa anabeba jukumu la kufanya tendo la unyanyasaji wa kijinsia kama uhalifu dhidi ya sheria za kimataifa?" 25

## SEHEMU 2: NYARAKA KATIKA MATUMIZI 28

### 3. MASUALA YA AWALI 29

3.1 Usifanye madhara 29
3.2 Mafunzo 29
3.3 Tathmini 30
(i) Utafiti 31
(ii) Tathmini za athari 33
3.4 Mipangilio kwa ujumla 35

### 4. MPANGILIO WA MADA ZA MSINGI 36

4.1 Uratibu 36
4.2 Tafsiri 38
4.3 Kuandaa taarifa 41

## 5. KUWATAMBUA WALIONUSURIKA NA MASHAHIDI WENGINEO 41

5.1 Utambulisho wa moja kwa moja 42
5.2 Wasuluhishi 42

## 6. USHAHIDI 44

6.1 Ridhaa kamili 45
6.2 Siri 47
6.3 Rufaa 48

## 7. MAHOJIANO 50

7.1 Mazingira ya mahojiano 52
7.2 Orodha ya mahojiano 53
7.3 Aina za maswali 54
7.4 Njia za mahojiano 56
7.5 Kurekodi taarifa za mahojiano 61

## 8. VYANZO ZAIDI VYA TAARIFA 61

8.1 Ushahidi dhahiri 61
(i) Sehemu za mashambulizi 63
8.2 Ushahidi wa nyaraka 66
(i) Aina za nyaraka 66

## 9. KUHIFADHI TAARIFA 68

9.1 Kuhifadhi nyaraka na taarifa nyingine zilizo dhahiri 69
9.2 Kuhifadhi taarifa za dijitali 69
9.3 Kuhifadhi taarifa za matibabu kisheria/ushahidi wa kisayansi kuhusu uhalifu (forensiki) 70

## BIBLIOGRAFIA 72

## ORODHA YA NYONGEZA 76

1. Kitabu cha kazi cha Ushahidi kwa ajili ya Nyaraka za Uhalifu wa Unyanyasaji wa Kijinsia: chombo cha kuwasaidia wapelelezi kuziba mapengo ya ushahidi 76
2. Vipengele vya kimsingi kwa Sekta mbalimbali kuhusu Kukabili Unyanyasaji wa Kijinsia 113
3. Kufanya mahojiano: Kanuni za msingi na vielelezo muhimu kwa matendo ya kazi 114
4. Kigezo kwa data binafsi za kukusanywa kutoka kwa walionusurika/mashahidi 118
5. Mifumo ya rufaa na aina za usaidizi kwa walionusurika/mashahidi 120
6. Ushahidi dhahiri: kanuni juu ya mlolongo wa utunzaji 121
7. Ushahidi wa nyaraka: kanuni juu ya mlolongo wa utunzaji 124
8. Mwongozo wa kupiga picha na kuchora maeneo ya uhalifu, ushahidi dhahiri na majeraha ya kimwili 127
9. Sheria za ushahidi na utaratibu kama vyombo vya kulinda walionusurika/mashahidi 135
10. Mfano wa Cheti cha Uvamiaji wa Kijinsia 138

# MWANZO

Itifaki hii ya Kimataifa, ya kwanza kwa aina yake, ni tokeo la hekima na uzoefu wa mamia ya watu duniani. Tunataka kuwashukuru zaidi ya wataalamu 200, watu walionusurika na mashirika yaliyoshirikiana kutoa maarifa yao na kuungana katika mchakato wa kuitayarisha rasimu.


Kwa miongo mingi – kama si karne nyingi – kumekuwa na ukosefu wa haki uliopindukia kwa walionusurika kutokana na kubakwa na unyanyasaji wa kijinsia katika mfarakano. Tunategemea kwamba Itifaki hii itakuwa ni sehemu ya juhudi mpya duniani za kuuvunja huu utamaduni wa kutowajibika, ili kuwasaidia walionusurika na kuwazuia watu tangu awali kufanya matendo haya ya jinai.

Tunawasifia watendaji wa kitaifa na kimataifa kwa ujasiri wao wa kuchunguza na kuandika katika nyaraka unyanyasaji wa kijinsia dunia nzima. Itifaki ina lengo la kuwasaidia katika kazi zao, na kusaidia kuhakikisha kwamba watuhumiwa wanaohusika na ubakaji na unyanyasaji wa jinsia katika mfarakano wanawajibishwa.

Tunategemea kwamba Itifaki haitokuwa tu chombo muhimu cha vitendo kinachoboreshwa na kujengwa zaidi miaka inavyoenda, bali pia njia ya kuhamasisha na kuendeleza kipaumbele duniani, hatua za matendo na utetezi wa suala hili ambalo ni muhimu.



**Mhe. William Hague MB**
Waziri wa Nchi wa Mambo ya Nje na Mahusiano ya Jumuiya ya Madola



**ANGELINA JOLIE**
Mwakilishi Maalum wa Umoja wa Mataifa anayesimamia Wakimbizi

Kwa miongo mingi – kama si karne nyingi – kumekuwa na ukosefu wa haki uliopindukia kwa walionusurika kutokana na kubakwa na unyanyasaji wa kijinsia katika mfarakano. Tunategemea kwamba Itifaki hii itakuwa ni sehemu ya juhudi mpya duniani za kuuvunja huu utamaduni wa kutowajibika, ili kuwasaidia walionusurika na kuwazuia watu tangu awali kufanya matendo haya ya jinai.

**Mhe. William Hague MB, Waziri wa Nchi wa Mambo ya Nje na Mahusiano ya Jumuiya ya Madola**

# i. UTANGULIZI

**Muktadha au mazingira:** Unyanyasaji wa kijinsia, ukitendwa kama uhalifu wa kivita, uhalifu dhidi ya utu na/au kama tendo la mauaji ya kimbari, mara nyingi huwa ni pamoja na mfano wa vitendo vya jinai vyenye kutisha na vya kikatili vinavyofanywa wakati wa vita na katika muktadha wa ukatili kwa umma. Unyanyasaji wa kijinsia hauathiri mamia hadi maelfu ya wanawake na wasichana tu, bali pia huathiri na kuonea wanaume na wavulana. Zaidi ya trauma/kiwewe dhahiri cha kimwili na cha kisaikolojia ambacho walionusurika/mashahidi huteseka nacho, unyayasaji wa kijinsia unaweza kuzidisha tofauti za kikabila, kidhehebu na mifarakano mingineo katika jamii. Hii inajenga mfarakano na kuyumbayumba na kudhohofisha ujenzi wa amani na juhudi za kuleta utulivu. Hata hivyo idadi kubwa mno ya walionusurika haipati haki kamwe na hukabiliwa na vipingamizi vyenye changamoto nyingi katika kupata msaada wa matibabu, kijamii inayohusika na saikolojia na uchumi, ambao ni muhimu ili kuwasaidia kujenga maisha yao upya. Kutokuwajibika kwa wahalifu wanaofanya matendo ya unyanyasaji wa kijinsia katika mfarakano hutia nguvu ukatili. Jumuiya ya kimataifa inaanza kutambua uhusiano mkubwa kati ya kutokuwepo kwa uwajibikaji na haki na kutokuwepo kwa maridhiano.

Itifaki hii haina lengo la kushughulikia uhalifu wote kabisa unaohusika na unyanyasaji wa kijinsia; dhumuni lake linalenga hasa katika mada maalum ya nyaraka na upelelezi wa uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia chini ya sheria za kimataifa za jinai. Hata hivyo, iwe wazi kwamba, walionusurika kutoka katika uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia ambao wapo nje ya mazingira haya, wanahitaji sana haki, msaada na tiba pia; inategemewa kwamba Itifaki hii itakuwa kichocheo cha kuongezeka kwa hatua zitakazochukuliwa ili kuzuwia na kuwajibisha kwa kila hali aina zote za unyanyasaji wa kijinsia katika mfarakano.

**Kutayarisha Itifaki:** Kushauriana na wadau kulifanywa kwa mfululizo mwaka 2012 ili kuhifadhi njia bora zitumiwazo kimataifa katika kutayarisha nyaraka na kuchunguza unyanyasaji wa kijinsia katika mfarakano na kutathmini mapengo na changamoto zitakazotakiwa kutekelezwa na jumuiya ya kimataifa. Kushauriana huku pamoja na kongamano za kimataifa zilizofuata kulionyesha kwamba, kiujumla, kuliungwa mkono kuwepo kwa itifaki mpya ya kimataifa isiyofungamana na upande wowote ambayo inaonyesha viwango vya kimsingi vya kufuatilia kwa njia bora za kutayarisha nyaraka na kuchunguza unyanyasaji wa kijinsia kama tendo la kihalifu chini ya sheria ya kimataifa.

Kuungwa mkono zaidi kwa maendeleo ya Itifaki kulipatikana kwa kupitia Tamko la G8 la Kuzuia Unyanyasaji wa Kijinsia kwenye Mfarakano mnamo Aprili 2013 na pia Tamko la Dhamira ya Kusitisha Unyanyasaji wa Kijinsia katika Mfarakano uliozinduliwa wakati wa Mkutano Mkuu wa Wiki ya Mawaziri wa Umoja wa Kimataifa (UN) mnamo Septemba 2013

Wizara ya Uingereza ya Mambo ya Nje & Jumuiya ya Madola (FCO) ingependa kuwashukuru wote waliochangia ujuzi wao, uzoefu wao na muda wao katika kuendeleza Itifaki hii. Hasa, Wizara ya mambo ya nje & Jumuiya ya Madola ingependa kutambua mchango wa wale watu na mashirika yaliyoshiriki latika mikutano ya kitaalam huko Hague na London miezi ya Mei, Juni na Julai ya mwaka 2013 na pia Februari 2014:

**Washiriki wa Kikundi hai cha Wataalamu:** Letitia Anderson, Utekelezaji wa Umoja wa Mafaita Dhidi ya Unyanyasaji wa Kijinsia katika Mfarakono; Gloria Atiba-Davies, Mahakama ya Kimataifa ya Jinai (ICC); Véronique Aubert, Save the Children (Kuokoa Watoto); Stephanie Barbour, Amnesty International; Shamila Batohi, ICC; Veronica Birga, Ofisi ya Balozi kwa Haki za Binadamu (OHCHR); Théo Boutruche, (zamani) REDRESS, (sasa) Mwalimu wa Haki za Binadamu, Chuo Kikuu cha London (UCL); Diane Brown, Women's Initiatives for Gender Justice (Haki za Wanawake); Gloria Carrera, Timu ya Umoja wa Mataifa ya wataalam wa Unyanyasaji wa Kijinsia katika Mfarakano na OHCHR; Evelyn Chijarira, Pan African Lawyers' Union (Wakili wa Umoja wa Kiafrika); Božidarka Dodik, Idara Maalum ya Uhalifu wa Kivita

katika ofisi ya Mwendesha Mashitaka wa Bosnia na Herzegovina pia Jaji Mahakama Kuu ya Shirikisho la Bosnia na Herzegovina; Erin Gallagher, Daktari wa Haki za Binadamu; Claudia García Moreno, Shirika la Afya la Umoja wa Mataifa (WHO); Liesl Gerntholtz, Human Rights Watch (Haki za Binadamu); Niamh Hayes, Taasisi ya Upelelezi wa Uhalifu wa Kimataifa; Brenda J. Hollis, Mahakama Maalum kwa Sierra Leone; Brigid Inder, Women's Initiatives for Gender Justice (Haki za Wanawake); Michelle Jarvis, Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu kwa Yugoslavia ya zamani (ICTY); Kristin Kalla, Trust Fund for Victims (Mfuko kwa Waathirika), ICC; Erin Kenny, Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa idadi ya Watu (UNFPA); Maxine Marcus, (zamani) ICTY, (sasa) Mshauri mkuu wa kimataifa wa sheria za jinai na mambo ya Kijinsia kwa PSVI; Cristina Michels, OHCHR; Kate Orlovsky, Women's Initiatives for Gender Justice (Haki za Wanawake); Martina Pomeroy, Ofisi ya Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa linalohusika na Wakimbizi (UNHCR); John Ralston, Taasisi ya Upelelezi wa Uhalifu wa Kimataifa; Madeleine Rees, Shirikisho la Wanawake kwa Amani na Uhuru; Cristina Ribeiro, ICC; Indira Rosenthal, Amnesty International; Nina Sahinpasic, Idara Maalum ya Uhalifu wa Kivita katika ofisi ya Mwendesha Mashitaka wa Bosnia na Herzegovina; Susannah Sirkin, Madaktari kwa Haki za Binadamu; Danaé van der Straten Ponthoz, TRIAL (Track Impunity Always – Fuatilia Ukatili Daima); Silke Studzinsky, Trust Fund for Victims (Mfuko wa Waathirika), ICC; Margriet Veenma, UNHCR; na Monika Volkhausen, Ofisi ya Mwendesha Mashitaka wa Umma, Cologne (Generalstaatsanwaltschaft Köln).

Pia Wizara ya Mambo ya Nje & Jumuiya ya Madola ingependa kutambua mchango wa wale watu na mashirika yaliyoshiriki kama wachambuzi wa ziada wa Itifaki:

**Wachambuzi wa ziada:** Kelly Askin, Shirikisho la Jamii Huria la Haki (OSJI); Elisabeth Baumgartner, Swisspeace; Leah Bellshaw, Idara ya Mambo ya Nje, Marekani; Linda Bianchi, Huduma ya Mwendesha Mashitaka wa Canada; Megan Bradley, Taasisi ya Brookings; Anne-Marie de Brouwer, Chuo Kikuu cha Tilburg; Jeannette Böhme, Medica Mondiale; Jorge Calderón Gamboa, Inter-American Court of Human Rights (Mahakama ya Haki za Binadamu); Danya Chaikel, Chama cha Waendesha Mashitaka wa Kimataifa; Juliet Cohen, Freedom From Torture (Uhuru kutoka katika mateso); Alison Cole, OSJI; Shukria Dini, Kituo cha Masomo cha Wanawake wa Kisomali; Ingrid Elliott, Timu ya Wataalam ya UK PSVI; Laura Francis, Survivors Speak OUT! (Walionusurika Wanaongea); Renata Giannini, IGARAPE; Gavin Ganendran, Freedom From Torture (Uhuru kutoka katika Mateso); Erica Hall, World Vision; Kolbassia Haoussou, Survivors Speak OUT! Network and Members (Wajumbe na mtandao wa Walionusurika Wanaongea); Claire Hawkins, Wanawake wa Umoja wa Mataifa; Elizabeth Howe, Chama cha Kimataifa cha Waendesha Mashitaka; Amrita Kapur, International Center for Transitional Justice (Kituo cha Kimataifa cha Haki ya Mpito); Andy Keefe, Freedom From Torture (Uhuru kutoka katika Mateso); Baudouin Kipaka, Arche d'Alliance; Gisela de León, Centre for Justice and International Law (Kituo cha Haki na Sheria ya Kimataifa); Anna Lise Domanski, Canadian Peace Operations and Fragile States Policy Division (kitengo cha Sera cha Shughuli za Amani na dola dhaifu cha Canada); Mendy Marsh, Mfuko wa Watoto wa Umoja wa Mataifa (UNICEF); Faiza Mohamed, Equality Now (Usawa Sasa); Jaimie Morse, Chuo Kikuu cha Northwestern; Lars Munk Plum, Naibu Mwendesha Mashitaka, Denmark; Tamah Murfet, International Rescue Committee (Tume ya Uokoaji wa Kimataifa); Antonia N'Gabala-Sodonon, Umoja wa Nchi za Kiafrika, idara ya Amani na Ulinzi; Valerie Oosterveld, Chuo Kikuu cha Western Ontario; Blake Peterson, Wizara ya mambo ya Nje ya Marekani; Feride Rushiti, Kituo cha Kuwawezesha Waathirika wa Mateso wa Kosova; Alejandro Sanchez, Kituo cha Unyanyasaji wa Kijinsia katika Mfarakano, MONUSCO; Duong Savorn, Mradi wa Kikambodia wa Walindaji; Sandesh Sivakumaran, Chuo Kikuu cha Nottingham; Isabelle Solon Helal, Mtaalamu wa Utawala na Haki za Binadamu, Canada; Kim Thuy Seelinger, Kituo cha Haki za Binadamu, Chuo Kikuu cha California - Berkeley; Sidney Thompson, Huduma za Umma za Mwendesha Mashitaka wa Canada; Charlotte Triggs, Huduma ya Ufalme ya Mwendesha Mashitaka; Diana Trimiño, International Rescue Committee (tume ya Uokoaji wa Kimataifa); Catherine Turner, World Vision; Aneeta Williams, Tearfund.

Zaidi ya hapo, Wizara ya Mambo ya Nje & Jumuiya ya Madola ingependa kutambua mchango muhimu sana wa wale watu na mashirika yaliyojumuika kama washiriki katika mashauriano ya utafiti unaofanywa katika maeneo ya kazi kuhusu Itifaki huko Bosnia, Colombia, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo DRC, London na Uganda.

Itifaki inatokana na mchakato wa kutayarisha na kuandika rasimu kwa kushirikiana inayojumlisha ushauriano kwa marefu na mapana yaliyofanywa pamoja na wataalam waliotajwa hapo juu. Mamlaka ya kuhariri Itifaki yamebakia na Wizara ya Mambo ya Nje & Jumuiya ya Madola na mwandishi mkuu wa itifaki, Sara Ferro Ribeiro, pamoja na Chido Dunn, mratibu wa mradi kwa itifaki (aliyeazimwa kutoka Freshfields Bruckhaus Deringer LLP) na Maxine Marcus, Mshauri mkuu wa kimataifa wa sheria za jinai na mambo ya Kijinsia kwa PSVI Jukumu la Uingereza limekuwa ni kuwezesha, kutoa msaada kifedha na kuhamasisha maendeleo ya Itifaki, kuhakikisha kujumuika kwa utaalamu wa kiwango cha juu zaidi na kuendeleza malengo yake na mataifa pamoja na washirika wa kimataifa. Wizara ya Mambo ya Nje & Jumuiya ya Madola ililenga kuiendeleza kazi iliyokwisha kuwepo na kutoa nafasi ya kuchunguza na pia kusambaza mbinu asilia zenye ufanisi na zinazofaa duniani kote ambazo mafanikio yake yamethibitishwa katika ngazi za chini kabisa.

Pia Wizara ya Mambo ya Nje & Jumuiya ya Madola ingependa kushukuru mashirika mengine ya ziada ambayo yameunga mkono mchakato huu: Freshfields Bruckhaus Deringer LLP, Save the Children na TRIAL (Track Impunity Always).

> Kwa watuhumiwa, hakutakuwa na sehemu yoyote ya kujificha; hakuna msamaha; sehemu ya usalama. Wao watafuatwa kwa njia yoyote na uwezo wote tuliokuwa nao kwa pamoja.

**Zainab Hawa Bangura, Mkutano wa Waziri wa mambo ya Nje wa G8, Aprili 2013**

# ii. KUTUMIA ITIFAKI

## a) Madhumuni

Dhumuni kuu la Itifaki ni kuendeleza uwajibikaji wa uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia chini ya Sheria ya kimataifa. Hufanya hivi kwa kuweka wazi misingi ya kanuni za kutayarisha nyaraka za Unyanyasaji wa Kijinsia kama uhalifu chini ya sheria ya kimataifa, zilizopatikana kutoka katika njia bora za kufanya kazi katika maeneo husika. Si lazima kwa mataifa kufuata Itifaki. Hata hivyo, inaweza kutumika kama chombo kinachounga mkono juhudi za watendaji wa haki za kitaifa na kimataifa na haki za binadamu, kuweka nyaraka na kuzilinda kiufanisi, kama uhalifu wa kijinai dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia chini ya sheria ya kimataifa – kama uhalifu wa kivita, uhalifu dhidi ya utu au mauaji ya kimbari.

Uwajibikaji wa unyanyasaji wa kijinsia unaweza kuwepo katika aina nyingi. Unaweza kufanikishwa kwa kupitia mashtaka ya jinai, lakini pia unaweza kuwezeshwa kwa madai ya haki za binadamu dhidi ya mataifa yanayohusika au wahusika ambao si mataifa, madai ya kiraia, madai ya kufidia walionusurika/mashahidi wa unyanyasaji wa kijinsia, na michakato ya haki za mpito.

Kama utaratibu wa uwajibikaji upo katika sehemu yenye mfarakano au iliyowahi kuwa na mfarakano au kama hakuna uwajibikaji, taarifa zitakazosombwa na watendaji ambao wanaweza kuwapata walionusurika na mashahidi hapo hapo au kwa kupitia njia rahisi, zinaweza kuwa ushahidi muhimu kwa juhudi za kuwajibika za wakati ujao. Hasa, jinsi taarifa hii itakavyopatikana na kukusanywa na mbinu za utafiti zitakazotumiwa katika mchakato wa kuweka nyaraka ni muhimu sana ili kuhakikisha uadilifu wa ushahidi, usalama wa jamii inayohusika, na kuwezeshwa kwa walionusurika kwa kushiriki katika mchakato wa haki. Itifaki hii ina lengo la kuweka wazi na moja kwa moja kanuni za msingi za kufuatilia ikiwa malengo haya yanapewa kipaumbele.

Lengo la Itifaki hii ni kuweka nyaraka kuhusu uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia chini ya sheria ya kimataifa. Hata hivyo, kanuni nyingi za msingi zilizowekwa katika Itifaki zitahusika na kutayarisha nyaraka ya uhalifu huu katika mazingira mengine, kuvunjwa na kutumia vibaya haki za binadamu, na sheria ya jinai ya kimataifa zisizohusiana na unyanyasaji wa kijinsia.

## b) Hadhara

Kimsingi, miongozo hii imeundwa ili kutumiwa na wahusika wa haki za binadamu kitaifa na kimataifa. Pia mtu mwingine yeyote au shirika linalokabiliwa na changamoto za kuweka katika nyaraka unyanyasaji wa kijinsia kama uhalifu chini ya sheria ya kimataifa.

Kutumika kwa Itifaki pia kunapendekezwa katika juhudi za ujengaji wa uwezo kwa madhumuni ya usalama wa kitaifa na jamii, kwa mahakama, utekelezaji wa sheria, matibabu ya ushahidi wa kisayansi kuhusu uhalifu (forensiki) na sayansi, pia kuchunguza taasisi zenye lengo la kuboresha maelewano ya jinsi ya kukusanya na kuweka nyaraka za habari kuhusu unyanyasaji wa kijinsia kama uhalifu wa kimataifa.

Miongozo hii haikulengwa kwa ajili ya mashirika ya misaada ya kibinadamu hasa hasa, wataalamu wa afya, wafanyakazi wa jamii au watoa huduma wengineo wanaoweza kuweka nyaraka kuhusu unyanyasaji wa kijinsia kutokana na mbinu za utafiti zao wenyewe zinazolingana na maagizo yao wenyewe. Hata hivyo, mtazamo wa mkusanyiko wa sekta mbalimbali ambao unajumlisha ushirikiano kati ya wataalamu wa afya, mawakili, polisi na mahakama ni muhimu ili kupata haki kwa walionusurika. Kwa hivyo, inategemewa kwamba wale watendaji wanaweza kukuta vipengele fulani fulani ndani ya mwongozo wa Itifaki kuwa muhimu kwa kazi zao, zinazotambua haja ya kuboresha uratibu na msimamo wa mbinu kati

ya watendaji wanaofanya kazi za kuponya, kusaidia na kuwakilisha haki za walionusurika na mashahidi wa unyanyasaji wa kijinsia. Hii ni katika mazingira ya haki za kitaifa au kimataifa, utaratibu wa kuwajibika au utetezi.

Muhimu zaidi, watu na mashirika yanayojitahidi kuweka katika nyaraka za unyanyasaji wa kijinsia kufuatana na miongozo ya Itifaki hii wahakikishe kwamba wamepata mafunzo ya kutosha na wana vifaa vya kutosha kufanya hivyo. Pia watendaji watambue sheria husika za kitaifa zinazozingatia utafiti wa mhusika wa tatu katika eneo wanalofanyia kazi, hasa zile sheria zinazodhibiti ukusanyaji wa ushahidi na wajibu wowote wa kuwapelekea ushahidi mamlaka ya kitaifa.

### c) Itifaki ni nini

Sehemu 1 ya Itifaki inatoa ufafanuzi wa unyanyasaji wa kijinsia kama uhalifu wa kimataifa: ni kitu gani, ni tendo linalojumlisha hatia za ukatili wa kijinsia, na mambo yanayohitajika ili kushtaki unyanyasaji wa kijinsia kama uhalifu chini ya sheria ya kimataifa. Pia inaelezea matokeo mazito yanayohusika na unyanyasaji wa kijinsia, vipingamizi ambavyo walionusurika na mashahidi hukumbana navyo wanapojaribu kupigania haki na itikadi zilizobuniwa pamoja na udanganyifu unaohusiana na unyanyasaji wa kijinsia; mambo ambayo yanaweza kukwaza juhudi za kifanisi zinazolenga katika Upelelezi na uandishi wa nyaraka kuhusu hatia na msaada kwa walionusurika/mashahidi.

Sehemu 2 inatoa muhtasari wa yaliyomo katika nyaraka yanapotumiwa kazini: nini cha kufanya ili kuuwezesha utafiti, kutayarisha na kuanzisha upelelezi na mchakato wa kutayarisha nyaraka, njia za kufanya mahojiano salama na fanisi, na mahitaji ya chini kabisa ya kufanyia kazi ushahidi kwa kiaudio-visual, yaani unaosikika na kuonekana, ushahidi dhahiri na ulio katika nyaraka ambao unahusiana na unyanyasaji wa kijinsia. Kanuni muhimu isemayo "usifanye madhara" ndiyo iliyobandikwa wazi katika kipengele hiki, na inapendekeza mbinu za kufanyia kazi ambazo watendaji wanaweza kutumia ili kusuluhisha na kushughulikia athari zinazoweza kuhusiana na utayarishaji wa nyaraka na utafiti wa unyanyasaji wa kijinsia katika mfarakano, pia kuondokana na vikwazo vingine ambavyo vingeweza kuingilia juhudi za uwajibikaji.

Habari za nyongeza zilizoambatanishwa zina baadhi ya vyombo na taarifa zaidi ambazo inategemewa zitathibitisha moja kwa moja kuwa muhimu kwa waandalizi wa nyaraka pale watakapokuwa wanafanya Upelelezi wao. Hii inajumlisha Kitabu cha Kazi za Ushahidi **(****angalia Nyongeza 1,** **"Kitabu cha kazi cha Ushahidi kwa ajili ya Nyaraka za Uhalifu wa Unyanyasaji wa Kijinsia: Chombo cha Kuwasaidia Wapelelezi Kuziba Mapengo ya Ushahidi")**, ambacho kimetoa mifano kuhusu aina za taarifa ambazo ni muhimu kukusanya ili kuthibitisha uhusiano maalum na wa kimuktadha wenye vipengele vinavyoweza kuunganishwa kuhusiana na suala zima la unyanyasaji wa kijinsia kama uhalifu wa kivita, hatia dhidi ya utu au tendo la mauaji ya kimbari. Habari za nyongeza pia zinajumlisha muhtasari na mwongozo wa kufanya mahojiano, kushughulikia ushahidi dhahiri na ule uliopo katika nyaraka, na kufanya kazi kwa kutumia modeli ya kusaidiana kati ya sekta mbalimbali, na pia taarifa kuhusu aina za marejeo muhimu na nyaraka za kimatibabu ambazo madhumuni yake ni ushahidi.

**d) Matumizi ya wakati ujao**

Wakati ujao, tunategemea kwamba Itifaki itakuwa chombo muhimu cha vitendo kitakachotumika kuondokana na changamoto zitakazowakumba wale watakaotayarisha nyaraka na kufanya upelelezi juu ya unyanyasaji wa kijinsia kama hatia chini ya sheria ya kimataifa. Itakuwa nyaraka hai itakayohitaji kurekebishwa upya mara kwa mara kufuatana na maendeleo na mabadiliko ya njia bora za kufanyia kazi.

Hasa, tunategemea kwamba: Nchi zitaunga mkono, zitasaidia na kuwezesha kutayarishwa kwa nyaraka kuhusu unyanyasaji wa kijinsia kufuatana na misingi ya kanuni na mbinu zilizowekwa katika Itifaki; nchi zinazotoa misaada, pale zitakapofadhili miradi nje ya nchi ambayo inahusiana na uwajibikaji katika hatia zinazohusika na unyanyasaji wa kijinsia kimataifa, zitahamasisha miradi hii kutumia kanuni na mbinu za msingi katika Itifaki hii. Nchi zenye mfarakano zitaunda mipango ya kitaifa kwa kutumia Itifaki hii ili kuleta uelewa na kujenga uwezo kati ya serikali, vyama vya kiraia, wataalam wa afya na sheria pamoja na washirika wengineo wanaohusika; wafadhili watatoa msaada wa kifedha kwa serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO) kwa kutumia Itifaki, na/au kuunda mafunzo ili kuleta uelewa na kujenga uwezo; NGO zenye uwezo mkubwa zinazofanya kazi katika nchi husika zitatumia Itifaki kama mbinu yao ya utafiti ya msingi ili kuwafunza wafanyakazi na kuandaa nyaraka kuhusu unyanyasaji wa kijamii kama uhalifu chini ya sheria ya kimataifa katika maeneo yenye mfarakano.



# SEHEMU I: UNYANYASAJI WA KIJINSIA

## 1. KUELEWA UNYANYASAJI WA KIJINSIA 15

1.1 Muktadha wa Unyanyasaji wa Kijinsia 15
1.2 Kukabili Unyanyasaji wa Kijinsia 16

## 2. UNYANYASAJI WA KIJINSIA KAMA UHALIFU CHINI YA SHERIA YA KIMATAIFA 16

2.1 Maelezo ya Mwanzo 16
2.2 Ufafanuzi wa hatia za unyanyasaji wa kijinsia kwa ujumla 17
2.3 Sehemu A: Hatia maalum za unyanyasaji wa kijinsia au uhalifu ambao unaweza kufanywa kwa kupitia unyayasaji wa kijinsia: "Nini kilitokea?" 18
2.4 Sehemu B: Vipengele vya muktadha wa uhalifu wa kimataifa: "Nini kilitokea mazingira ambayo (tendo la unyanyasaji wa kijinsia) lilitokea"? 23
(i) Unyanyasaji wa kijinsia kama uhalifu wa kivita au kama uvunjwaji wa sheria na desturi za vita 23
(ii) Unyanyasaji wa kijinsia kama uhalifu dhidi ya utu 24
(iii) Unyanyasaji wa kijinsia kama mauaji ya kimbari 24
2.5 Sehemu C: Mfumo wa dhima kwa matendo ya uhalifu wa kimataifa: "Ni vipi anayeshukiwa kufanya lile kosa anabeba jukumu la kufanya tendo la unyanyasaji wa kijinsia kama uhalifu dhidi ya sheria za kimataifa?" 25

# SEHEMU I: UNYANYASAJI WA KIJINSIA

## 1. Kuelewa Unyanyasaji wa kijinsia

### 1.1 Muktadha wa Unyanyasaji wa Kijinsia

Unyanyasaji wa kijinsia ni aina ya ukatili unaochukiza sana, na unajumlisha kubaka na aina yoyote ya mashambulizi yanayohusu ngono ambayo hufanywa dhidi ya wanawake, wasichana, wanaume na wavulana. Matokeo yake yanaweza kuwa ya kikatili na huweza kuwa na madhara ya kimwili na kisaikolojia kwa walionusurika na mashahidi na pia huyumbisha mno jumuiya na raia kwa ujumla.

Ni muhimu kutambua kwamba wanawake, wanaume, wasichana na wavulana wote wanaweza kuwa waathirika wa unyanyasaji wa kijinsia. Hata hivyo, kihistoria na kimuundo, kutokuwepo kwa usawa kati ya wanaume na wanawake na mifumo mbalimbali ya ubaguzi wa jinsia, ambapo wanawake dunia nzima wamekuwa wakionewa, kumechangia kufanya wanawake na wasichana kuathirika zaidi na unyanyasaji wa kijinsia katika mazingira yenye mfarakano. Zaidi ya hapo, unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya watoto hasa upo kwa kiasi kikubwa, na unaweza kuwa na uharibifu mkubwa sana.

Makundi mengine huweza kulengwa mara nyingi zaidi na unyanyasaji wa kijinsia. Makundi haya ni pamoja na wale waliosambaratishwa ndani ya nchi, wakimbizi, watoto, wanawake ambao ni wakuu wa kaya, wanawake wanaotetea haki za watu, wafungwa (ikiwa ni pamoja na wale ambao wamekamatwa na vikundi vinavyojihami na silaha), wale wanaohusishwa na jeshi au vikundi vinavyojihami na silaha, wale wanaotoka katika kabila maalum, na makundi mengine yanayoweza kudhuriwa.

Katika mazingira yenye mfarakano, na mazingira ambapo ukatili wa kudhuru umma unatendeka katika au kwenye mfarakano au bila ya kuwepo mfarakano, unyanyasaji wa kijinsia hufanywa na makundi yenye silaha dhidi ya watu, ikiwa ni pamoja na raia wa kawaida: kama mkakati wa kuendeleza malengo ya kijeshi na huweza kuwa sehemu ya mashambulizi yaliyotapakaa au yenye mfumo fulani, yanayofanywa dhidi ya raia wa kawaida. Unyanyasaji wa kijinsia huweza kutumiwa ili kudhoofisha au kushikilia na kudhibiti jamii. Unaweza kutumika kuadhibu au kuharibu kundi fulani maalum, kuwatia woga, kulipiza kisasi dhidi yao au kuwafanya wakimbie kutoka mahali fulani. Unyanyasaji wa kijinsia pia unajumlisha matendo – yanayofanywa kama sehemu ya mashambulizi au kama si sehemu ya mashambulizi – ambayo hutendwa kama matokeo ya kuvunjika kwa miundo ya kijamii au kifamilia, kutokuwepo kwa usalama na pia kutokuwepo kwa utawala wa sheria. Hizi ni sifa za hali zenye mfarakano, zenye dharura na kusambaratika, ambapo wahalifu wanaweza kutumia nafasi ya kutokuwepo kwa usalama na mazingira ya kutowajibika ili kufanya unyanyasaji wa kijinsia.

Katika mazingira mengine, unyanyasaji wa kijinsia unahesabika kuwa ni hatia katika sheria za kimataifa: hatia ya kivita, uhalifu dhidi ya utu na/au mauaji ya kimbari ambapo vipengele vya kihalifu vilivyoainishwa vinaonekana kuridhia na vinaweza kufanyiwa utafiti na kushtakiwa katika ngazi za kitaifa na kimataifa. Unyanyasaji wa kijinsia kama uhalifu chini ya sheria ya kimataifa mara nyingi hufanywa kama sehemu ya mifumo iliyoenea ya uhalifu dhidi ya watu na jumuiya – mfumo ambao unajumlisha hatia za kijinsia na zile zisizo za kijinsia. Katika muktadha wa uhalifu wa kivita, hatia dhidi ya utu na mauaji ya kimbari, ubakaji pamoja na aina zingine za unyanyasaji wa kijinsia zinaweza kutendwa kama tendo mojawapo la kikatili katika mengine mengi, ambalo huwa sehemu ya mashambulizi yanayofanywa kwa raia na yanaweza kuhusishwa na mapigano yenye kutumia silaha, na/au yanayoweza kuwa yametendwa ili kuangamiza kundi fulani ama lote au sehemu tu ya kundi.

Kuelewa athari zinazosababishwa na unyanyasaji wa kijinsia ni muhimu ili kuwaongoza walionusurika/mashahidi kwenye huduma itakayowafaa na kutengeneza nyaraka sahihi

zinazoonyesha madhara ya unyanyasaji wa kijinsia kwa watu, familia na jamii. Unyanyasaji wa kijinsia unaweza kuwa na matokeo yanayodumu muda mrefu na yanayotishia maisha kimwili na kisaikolojia na pia madhara ya kijamii, kiuchumi na kisheria ambayo matokeo yake huongeza athari na udhaifu kwa walionusurika.[1] Muhimu ni kwamba wanawake, wanaume, wasichana na wavulana wanaweza kupata athari tofauti kutokana na unyanyasaji wa kijinsia. Jamii na miundo ya kijamii huweza kuharibika au kuvunjika kwa undani kutokana na kufanyiwa uhalifu wa kunyanyaswa kijinsia dhidi ya wanajumuiya wao.

### 1.2 Kukabili Unyanyasaji wa Kijinsia

Kukabili Unyanyasaji wa Kijinsia kunahitaji mtazamo thabiti wenye mkusanyiko wa sekta mbalimbali ambao unajumlisha mpango mzuri wa utoaji uratibu wa huduma za afya, usalama, msaada wa kisaikolojia katika jamii, uwezekano wa kupata haki kwa walionusurika **(angalia Nyongeza 2, "Mambo ya Kimsingi kwa Sekta mbalimbali kuhusu Kukabili Unyanyasaji wa Kijinsia")**. Kuwekwa kwa huduma hizi za kimsingi ni muhimu sana ili kuongeza uwezekano wa walionusurika kushtaki uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia.

Hata hivyo, wanusurika wa unyanyasaji wa kijinsia hukumbana na vikwazo vikubwa ili kupata huduma, taratibu za haki na njia za tiba zingine baada ya vita. Walionusurika wengine hawapati haki kwa sababu ya kutengwa, aibu, udhalilishaji na trauma/kiwewe ambavyo huwaathiri walionusurika pamoja na familia zao. Wengine huogopa kuachwa na wanandoa wenzao (wake na waume), ndugu wengine katika familia na jamii zao, huogopa kuongezeka kwa unyanyasaji, na huwa na ukosefu wa uaminifu kwa polisi wa nchi.

Wale watendaji watakaokuwa wanashughulikia, na hasa kufanya upelelezi na kutayarisha nyaraka za unyanyasaji wa kijinsia wasidhani kwamba walionusurika hawajitokezi kwa sababu wanahisi aibu kupita kiasi – mara nyingi kushindwa kwao kupata haki huwa ni kwa sababu ya ukosefu wa mazingira yenye usalama na yenye msaada ili kufanya hivyo, na/au kwa sababu ya hatari zinazoweza kumkumba mnusurika/shahidi anapojitokeza. Kwa umoja, watendaji wote wajitahidi kuwezesha uwepo wa mazingira salama yenye msaada ambamo wanusurika na mashahidi wa unyanyasaji wa kijinsia watajihisi salama na vizuri vya kutosha ili kujitokeza kushtaki uhalifu.

Lazima ijulikane kwamba Mataifa yana wajibu wa msingi wa kuchunguza na kutayarisha nyaraka. Usalama wa kitaifa na taasisi za haki zipate mafunzo ya kutosha na zijiandae ili ziweze kuwajibu kwa ufanisi na kwa haki walionusurika kutokana na unyanyasaji wa kijinsia, kuchunguza uhalifu na kuwalinda walionusurika na mashahidi. Hata hivyo, pale ambapo taasisi za kitaifa zimeshindwa, au hazitaki, kufanya utafiti na kutayarisha nyaraka za unyanyasaji wa kijinsia, pale ambapo ufafanuzi wa kitaifa wa unyanyasaji wa kijinsia una vizuizi, au dawa za nyumbani zimeshatumiwa vya kutosha na kufika kikomo, watendaji ambao wana mafunzo yanayofaa, wenye vyombo na mamlaka wana uwezo wa kutayarisha nyaraka kuhusu unyanyasaji wa kijinsia kama uhalifu wa kitaifa kwa ufanisi na usalama.

## 2. Unyanyasaji wa Kijinsia kama Uhalifu chini ya Sheria ya Kimataifa

### 2.1 Maelezo ya Mwanzo

Katika miaka 20 iliyopita, sheria ya kimataifa imeendelea katika mwelekeo wa kusaka uwajibishaji zaidi kwa hatia mbaya sana, ikiwa ni pamoja na hatia za unyanyasaji wa kijinsia pale zinapofanywa kama uhalifu wa kivita, uhalifu dhidi ya utu au matendo ya mauaji

1 Kwa maelezo ya ziada juu ya athari na matokeo ya unyanyasaji wa kijinsia, angalia: UNHCR, Sexual and Gender-Based Violence against Refugees, Returnees and Internally Displaced Persons: Guidelines for Prevention and Response, 2003; Institute of Medicine, Social and Economic Costs of Violence Against Women: The Value of Prevention, 2011; na World Bank, The Costs and Impacts of Gender-Based Violence in Developing Countries: Methodological Considerations and New Evidence, 2004.

wa kimbari. Jinsi hatia ya jinai na falsafa ya sheria ya kimataifa ilivyoendelea – kwanza katika muktadha wa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai kwa nchi ya zamani ya Yugoslavia na Mahakama ya Kimataifa ya Jinai kwa Rwanda (mahakama za hapa na pale, au ICTY na ICTR) ndivyo zilivyopangwa kanuni katika mpango ulioitwa Rome Statute (Sheria ya Roma) wa Mahakama ya Jinai ya Kimataifa (ICC). Na hii iliendelezwa zaidi katika Mahakama Maalum kwa Sierra Leone (SCSL) – ubakaji na aina nyingine za unyanyasaji wa kijinsia unafanyiwa upelelezi na kushtakiwa: kama uhalifu wa kivita pale unapotendwa katika muktadha wa kuhusishwa na vita; [2] kama uhalifu dhidi ya utu pale unapotendwa katika muktadha wa mashambulizi yaliyotapakaa au yenye mfumo maalum yanayotendwa dhidi ya raia; na/au kama tendo la mauaji ya kimbari pale linapotendwa likiwa na lengo la kuangamiza kabila, dini, taifa au kundi la watu wenye kabila au rangi fulani kwa ujumla au kwa kiasi fulani. [3]

Mwanzo wa mazungumzo kuhusu uhalifu wa kimataifa unaoweza kuhusika na matendo ya unyanyasaji wa kijinsia katika muktadha wa Itifaki hii ni Sheria ya Roma ya ICC. Mipango iliyopo katika kanuni za Sheria ya Roma inaweza kuakisiwa katika mifumo mingi ya kitaifa inayoidhinisha Mkataba huo na kutumia mipango hii ya kimataifa katika utungaji wa sheria zao za ndani ya nchi. Hata hivyo, Sheria ya Roma (Rome Statute) haijajumuisha masuala yote ya sheria ambazo zinaonyesha mfano wa matumizi ya sheria ya kimataifa ya jinai kwa mapana na marefu; sheria ya kimataifa ya mila kwa namna nyingi imejumuisha zaidi. Mahakama za hapa na pale, Vyumba vya kusikilizia kesi Visivyo vya kawaida katika Mahakama za Cambodia (ECCC) na SCSL zimetumia kanuni za sheria za kimataifa za mila [4] na falsafa ya sheria zinazojitokeza katika hizo taasisi na pia zinafundisha na kuakisi kwa mapana kanuni hizi. Wakati Itifaki hii inalengea mipango kama ilivyowekwa katika Sheria ya Roma, watendaji wanatakiwa kukumbuka umuhimu wa falsafa ya sheria katika mahakama ya hapa na pale na mahakama mseto kama chanzo cha kanuni zinazotumika, hasa kwa sababu mengi yaliyomo katika Sheria ya Roma hayajaenda mahakamani au hayajasuluhishwa. Kutokana na hivi, falsafa ya sheria kwenye mahakama ya hapa na pale na mahakama mseto zitaweza kuwa mwongozo pekee uliopo.

Ufafanuzi wa sheria ya jinai, na vipengele vinavyohusika nayo, vinaweza kuwa tofauti kwa kiasi fulani kufuatana na mamlaka ya mahakama ambamo hatia zinachunguzwa na kuhukumiwa. Ingawa nchi nyingi zinazohusika na Sheria ya Roma zimeshirikisha ufafanuzi wake wa unyanyasaji wa kijinsia katika sheria zao za kitaifa, wengine wengi hawajafanya hivyo. Watendaji wanaoandaa nyaraka za uhalifu za unyanyasaji wa kijinsia wanatakiwa kufahamu misingi ya uhalifu kama ilivyofafanuliwa katika Sheria ya Roma na vile vile ile ya mfumo wa kisheria ambao wao wanautumia kufanyia kazi, pia kukumbuka falsafa ya sheria kwenye mahakama ya hapa na pale na mahakama mseto.[5]

## 2.2 Ufafanuzi wa uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia kwa ujumla

Kama ilivyowekwa kwa kina zaidi katika Kitabu cha Kazi za Ushahidi **(angalia Nyongeza 1, "Kitabu cha kazi cha Ushahidi kwa ajili ya Nyaraka za Uhalifu wa Unyanyasaji wa Kijinsia: Chombo cha Kuwasaidia Wapelelezi Kuziba Mapengo ya Ushahidi")**, ili kila kitendo cha ubakaji na unyanyasaji wa kijinsia kihitimu na kukubalika kama uhalifu wa kimataifa, inabidi watendaji kupata taarifa kuthibitisha aina tatu za vipengele:

2 Chini ya sheria ya ICTY na ICTR, lazima kuwe na uhusiano kati ya tendo na vita.

3 Hatia za unyanyasaji wa kijinsia pia zinaweza kushitakiwa kama mateso, ukatili na udhalimu (ambayo, kimataifa, yangeweza kuchunguzwa na kushitakiwa chini ya sheria za kimataifa za jinai kama uhalifu wa kivita au uhalifu dhidi ya utu, kama itakavyobainika.) Kwa mujibu wa falsafa ya sheria iliyopo muda mrefu. Mateso, katika baadhi ya mamlaka ya mahakama ya ndani ya nchi, huweza kuchunguzwa na kushitakiwa kama tendo la uhalifu.

4 Kumbuka kwamba ndani ya Itifaki hii taasisi hizo zitakuwa zinajulikana kama "mahakama ya hapa na pale na mahakama mseto".

5 Kama ilivyoelezwa katika Kitabu cha Kazi za Ushahidi **(angalia Nyongeza 1)**, misingi ya uhalifu kama ilivyoelezwa na Sheria za Roma inaweza kutumika kama orodha muhimu ya kuwasaidia watendaji katika kukusanya taarifa za kina kuhusu unyanyasaji wa kijinsia. Watendaji wanaweza kuboresha uadilifu na ufanisi wa uchunguzi wao kwa kukumbuka taarifa gani zinahitajika na kwa nini; na misingi ya uhalifu husika katika mamlaka za mahakama ambamo mtendaji anafanyia kazi, inaweza kutumika kama miongozo kwa kusaidia jambo hili. Watendaji lazima wajitahidi kuandaa "kitabu cha kazi za ushahidi" (kulingana na mfano wa Kitabu cha Kazi za Ushahidi) chao wenyewe kikiwa kama chombo cha marejeo ili kuhakikisha kwamba hakuna mapengo katika mchakato wa kukusanya taarifa.

- **vipengele maalum** (vimejitosheleza na taarifa inayoonyesha tendo gani hasa limetendwa);
- **vipengele vya muktadha** [6] (kuridhishwa na taarifa zinazoelezea mazingira ambayo tendo hilo lilitendwa na kulinyanyua tendo hilo kufikia daraja la uhalifu wa kivita, uhalifu dhidi ya utu au tendo la mauaji ya kimbari); na
- **vipengele vya kuunganisha** [7] (kuridhishwa na taarifa zinazoelezea jinsi m(wa)halifu mmoja au wengi wanadaiwa kulitenda tendo hili kama hatia ya kimataifa).

Aina hizi tatu za taarifa zinaweza kuchukuliwa kuwa ni Sehemu A, B na C za taarifa kamili inayotakiwa kuonyesha kwamba unyanyasaji wa kijinsia (au uhalifu mwingine wowote chini ya Sheria ya kimataifa) unaweza kuwa umetendwa na kumpendekeza mtu ambaye anahusika na uhalifu kwa kutenda hatia hizo.

Sehemu zifuatazo zitamwonyesha mtendaji matakwa ya kila hatua katika upelelezi wa uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia. Mifano ya maswali wanayoweza kuulizwa mashahidi pamoja na tamko, nyaraka na picha zinazoweza kuridhisha vile vipengele vya ushahidi vinavyoridhisha hivyo vipengele ambavyo vyote vimejumuishwa katika Kitabu cha Kazi za Ushahidi **(angalia Nyongeza 1)**.

## 2.3 Sehemu A: Uhalifu maalum wa unyanyasaji wa kijinsia au uhalifu ambao unaweza kufanywa kwa unyayasaji wa kijinsia: "Nini kilitokea?"

Wajibu wa mtu binafsi kuhusu hatia kwenye matendo ya unyanyasaji wa kijinsia kama uhalifu wa kivita, uhalifu dhidi ya utu na/au vitendo vya mauaji ya kimbari huweza kuambatanishwa kupitia hatia ambazo zina kipengele chenye uhalifu wa kijinsia cha wazi wazi. Kadhalika kwa kupitia uhalifu ambao hauhusiki na unyanyasaji wa kijinsia, kutegemea ukweli unaopatikana.

Mifano mengine ya aina za uhalifu ambao unaweza kuonekana kuwa na misingi ya vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia inatajwa hapa chini. Orodha ya mifano iliyoorodheshwa katika Itifaki hii inajumlisha hatia ambazo kimsingi zina vipengele wazi vyenye unyanyasaji wa kijinsia, vile vile mifano michache ya hatia inayoweza kuhusika na matendo yanayofanywa ambayo yanahusisha unyanyasaji wa kijinsia lakini ambayo hayaonyeshi wazi asili ya jinsia ya hatia hiyo. Kuna hatia zingine katika Sheria ya Roma zinazoweza kufanywa kwa namna ya kijinsia au ile isiyo ya kijinsia ambayo haijaorodheshwa hapa kwa sababu ya urefu. Pia kuna uhalifu mwingine ambao misingi yake ipo katika matendo ya unyanyasaji wa kijinsia lakini wenyewe haumo katika Sheria ya Roma, na kuna baadhi ambayo imeshahukumiwa kimataifa. Kwa mfano, hapo SCSL, kulikuwa na hatia ya uhalifu wa ndoa za kulazimishwa kama tendo ambalo si la utu (hatia dhidi ya utu). [8]

Kuna uhalifu katika sheria ya kimataifa ambayo inahusu matendo ya unyanyasaji wa kijinsia kama vile ubakaji au ukahaba wa kulazimisha, lakini kuna hatia nyingine ambazo hutendwa kwa matendo ya ngono au yale ambayo si ya ngono, kwa mfano utesaji. Mifano mingine ya aina zote mbili za uhalifu imetajwa hapa chini.

Inapendekezwa kwa watendaji kuanza mchakato wa kuandaa hatia ambazo watazitayarishia nyaraka na upelelezi, wasisite tu kushughulikia hatia ambazo zinaweza kutendwa pamoja na matendo ya unyanyasaji wa kijinsia pekee. Ila, pale ambapo ukweli upo, watafute kuandaa nyaraka na kupeleleza tabia za unyanyasaji wa kijinsia zilizoorodheshwa kama hatia za unyanyasaji wa kijinsia au uhalifu mwingine. Hii inaweza kuongeza uwajibikaji wa mienendo ya unyanyasaji wa kijinsia kwa kuonyesha kwamba, kama hatia chini ya sheria ya kimataifa,

6 Mara nyingi huitwa vipengele vya "chapeau" au vya "kawaida".

7 Pia inajulikana kama "mfumo wa dhima".

8 Pia Kumbuka kwamba uhalifu huu wa ndoa za kulazimishwa unaweza kushitakiwa kama kitendo cha kinyama au kama aina nyingine ya unyanyasaji wa kijinsia chini ya Sheria ya Roma.

mwenendo kama huo ni aina nyingine ya jinai ya kutumia mabavu na sio kitu tofauti na hatia nyingine zinazofanywa, hasa katika muktadha wa ukatili wa kudhuru umma. Hii pia inaweza kutusaidia kuhakikisha kuwa asili ya madhara hayo inaakisiwa na kuhukumiwa.

Sheria ya Roma inaorodhesha hatia za unyanyasaji wa kijinsia ambayo ni sehemu ya hatia za kivita, uhalifu dhidi ya utu na matendo ya mauaji ya kimbari. Pia inajumuisha hatia ambazo zinaweza kufanywa kuwa za kijinsia na ambazo ni kama hatia za kivita, uhalifu dhidi ya utu na matendo ya mauaji ya kimbari. Hizi pia zinaweza kufanyiwa upelelezi na kushtakiwa kutokana na ukweli ambao unajumlisha unyanyasaji wa kijinsia.

Hatia maalum za unyanyasaji wa kijinsia na uhalifu mwingine unaohusika katika matendo yenye unyanyasaji wa kijinsia na ule usiokuwa wa kijinsia umeelezewa pamoja na vipengele vyao katika Kitabu cha kazi cha Ushahidi **(angalia Nyongeza 1)**. Mkusanyiko mkubwa zaidi wa hatia chini ya sheria za kimataifa na vipengele vyake kama zilivyotajwa katika Sheria ya Roma zimo katika Misingi ya Uhalifu ya ICC zaidi ya hapo, sheria na misingi ya uhalifu ya mahakama ya hapa na pale na ile ya mahakama mseto na kuwepo kwa mfumo wa sheria za ndani ya nchi zinaweza kutumika kama vyanzo vya ufananuzi na masharti husika.

Hatia nyingine ambazo zimeorodheshwa katika Sheria ya Roma ambazo zinaweza kujumlishwa kama matendo ya unyanyasaji wa kijinsia zimetajwa hapa chini.

## Hatia za kivita (mfarakano wa kimataifa wenye kutumia silaha) (Ibara ya 8.2(b))

Hatia maalum za unyanyasaji wa kijinsia:

- Ubakaji, utumwa wa ngono, ukahaba wa kulazimishwa, mimba za kulazimishwa,[9] uuaji wa kizazi wa kulazimishwa, au aina nyingine ya unyanyasaji wa kijinsia.

Hatia zingine ambazo zinaweza kuhusisha mwenendo wenye asili ya ngono:

- Kuwanyenyekesha watu ambao wapo chini ya utawala ulio upande wenye uhasama nao kwa kuwaumiza kimwili au kuwakatakata maungo au kwa kuwafanyia majaribio ya kisayansi au ya kimatibabu ya aina yoyote ambayo hayajahalalishwa kidaktari, kimatibabu ya meno au kihospitali. Majaribio kufanyiwa mtu anayehusika bila ya kujali maslahi yake, na kuweza kuleta kifo au kuhatarisha afya ya huyo mtu au watu.[10]
- Kutangaza katika mahakama ya sheria, mwisho au kuahirishwa au kutoruhusiwa kwa haki na matendo ya raia walio katika upande wenye uhasama. [11]
- Kutenda vitendo viovu na vya ukatili dhidi ya hadhi ya mtu, hasa kufanya matendo ya kufedhehesha na kushusha hadhi.[12]

9 "Mimba za kulazimishwa" maana yake ni kifungo kinyume na sheria ambapo mwanamke analazimishwa kupata mimba, kwa nia ya kuathiri muundo wa makabila ya watu fulani au kutekelezwa kwa ukiukwaji mkubwa wa sheria za kimataifa. Kwa vyovyote, ufafanuzi huu hautatafsiriwa kama vile unaathiri sheria za nchi kuhusiana na ujauzito.

10 Kwa mfano, kuwaweka kizuizini raia na kufanya majaribio juu yao kwa kusababisha madhara kwenye sehemu zao za siri, au kufanya majaribio juu yao yanayowalazimisha kuwa uchi kama vile kuwavua nguo na kuwamwagia maji yanayozidi kuwa na moto ili 'kuangalia' ingewachukuwa muda gani kuonyesha dalili za kuungua.

11 Katika hali ambapo haki zilizopigwa marufuku huleta matokeo ya kuwepo kwa unyanyasaji wa kijinsia, kwa mfano mtuhumiwa (katika nafasi yake) anatoa amri kwa wanawake ambao ni raia wa upande wenye uadui walazimishwe kutoa mimba.

12 Sheria hii inaweza kutumika kwa ajili ya uhalifu wa kijinsia pamoja na uhalifu usiohusika na jinsia au ngono - kwa mfano kulazimisha mahabusu wa kiume kuramba sehemu za siri za mtuhumiwa au mtu mwingine, au kumlazimisha mahabusu kuramba viatu ya mtuhumiwa au mtu mwingine, kunaweza kuchukuliwa kama ufedheheshaji na udhalilishaji. Kijadi, sheria hii ilitumika kama sheria husika kwa uhalifu wote unaohusika na unyanyasaji wa kijinsia; Hata hivyo, sheria za jinsia zimependekeza kutafakari sahihi kwa madhara yanayosababishwa na unyanyasaji wa kijinsia, ambayo, ingawa huleta hasira kuhusu upotovu wa hadhi ya binadamu, lakini pia ni kitendo chenye vurugu kinacholeta madhara mwilini na akilini na kinahusika na mateso na ukatili.

- Kuwaandikisha watoto walio na umri chini ya miaka 15 katika jeshi la taifa au kuwatumia ili wahusike katika uhasama unaoendelea.[13]

### Uhalifu wa kivita (vita vya ndani) (Ibara ya 8.2(c)-(e))

Hatia maalum za Unyanyasaji wa kijinsia:

- Matendo ya kubaka, utumwa wa ngono, ukahaba wa kulazimishwa, mimba za kulazimishwa, uuaji wa kizazi wa kulazimishwa, au aina nyingine yoyote ya unyanyasaji wa kijinsia ambayo ni ukiukaji mkubwa wa Ibara ya 3 ya Mikataba minne ya Geneva.

Hatia zingine ambazo zinaweza kuhusisha mwenendo wenye asili ya ngono:

- Vurugu katika maisha na kwa mtu, hasa aina zote za kukatakata viungo vya mwili, ukatili na mateso.

- Kutenda vitendo viovu na vya ukatili dhidi ya hadhi ya mtu, hasa kufanya matendo ya kufedhehesha na kushusha hadhi.

- Kuwaandikisha watoto walio na umri chini ya miaka 15 katika jeshi la taifa au kuwatumia ili wahusike katika uhasama unaoendelea.

- Kuwanyenyekesha watu ambao wapo chini ya utawala ulio upande mwingine wa mfarakano kwa kuwaumiza kimwili au kuwakatakata maungo au kwa kuwafanyia majaribio ya kisayansi au ya kimatibabu ya aina yoyote ambayo hayajahalalishwa kidaktari, kimatibabu ya meno au kihospitali. Majaribio kufanyiwa mtu anayehusika bila ya kujali maslahi yake, na kuweza kuleta kifo au kuhatarisha afya ya huyo mtu au watu hao.

### Hatia dhidi ya utu (Ibara ya 7)

Matendo yoyote kati ya haya yafuatayo kama yakitendwa kama sehemu ya mashambulizi yaliyotapakaa au yenye mfumo maalum yanayofanywa dhidi ya raia, huku wakijua kuhusu mashambulizi hayo:

Hatia maalum za unyanyasaji wa kijinsia:

- Kubaka.
- Utumwa wa ngono.
- Ukahaba wa kulazimishwa.
- Mimba ya kulazimishwa.
- Uuaji wa kizazi wa kulazimishwa, au aina nyingine ya unyanyasaji wa kijinsia wenye uzito unaoweza kufananishwa.

Hatia zingine ambazo zinaweza kuhusisha mwenendo wenye asili ya ngono:

- Mauaji.[14]
- Uangamizaji. [15]

13 "Kuwatumia" watoto ili kushiriki kikamilifu katika uhasama kunajumlisha, kwa mfano, kulazimisha watoto kufanya vitendo vya ukatili wa kijinsia au kuwalazimisha kushiriki katika vitendo vya ngono kwa lengo la kuleta athari fulani kughilibu nia zao wapendelee kushiriki katika vitendo vingine vya unyanyasaji. Pia huweza kujumlisha mazingira ambapo watoto ambao ni maaskari wanateswa tena na tena, ili wao, kwa upande wao, waweze kutekeleza vitendo aina hivyo vya mateso kijinsia dhidi ya raia.

14 Kwa mfano, ubakaji wa genge (ubakaji wa mande) na hatima kuwa kifo.

15 Kwa mfano, kuwakusanya raia pamoja kwenye mkutano, kuwaweka kizuizini, kuwavua nguo, kuwapiga katika maeneo yao ya siri (na maeneo mengine) hadi wanapokufa, ikiwa ni kama sehemu ya mauaji wa raia wengi sana.

- Kufungwa au aina nyingine ya kunyima uhuru kwa kiasi kikubwa kama uvunjwaji wa sheria za msingi za kimataifa.[16]
- Mateso.
- Kuadhibu kundi fulani linalotambulika au kwa ujumla kufuatana na sababu za kisiasa, rangi, utaifa, kabila, utamaduni, dini, jinsia kama ilivyofafanuliwa katika aya ya 3 ya Ibara ya 7. Au sababu zingine ambazo zinatambulika duniani kote kwamba haziruhusiwi chini ya sheria ya kimataifa, inayoambatana na tendo lolote lililotajwa katika aya hii au hatia yoyote iliyo ndani ya mamlaka ya mahakama ya ICC.
- Watu kulazimishwa kupotea.[17]
- Hatia za ubaguzi wa rangi.[18]
- Matendo mengine yasiyo ya kiutu ambayo yanafanana na haya na yanayofanywa kwa makusudi ili kuleta mateso makubwa au madhara makubwa katika mwili au katika afya ya kiakili na hisia na ile ya viungo vya mwili.

### Mauaji ya kimbari (Ibara ya 6)

Matendo yoyote yafuatayo yakifanywa kwa lengo la kuangamiza taifa, kabila, rangi au dini fulani kwa ujumla au sehemu ya hilo kundi:[19]

- Kuwaua wanajumuiya wa kundi.
- Kusababisha madhara makubwa katika mwili au kisaikolojia kwa wanajumuiya wa kundi.
- Kushurutisha kwa kusudi masharti ya maisha ambayo yanalenga kuangamiza kundi fulani lote kabisa au sehemu ya kundi hilo.
- Kulazimisha hatua ambazo zinazuia uzazi katika jumuiya.
- Kulazimisha uhamisho wa watoto kutoka kundi lao kuenda katika kundi lingine.

### Mateso kama uhalifu pekee

Katika mazoea ya uhalifu wa kimataifa, unyanyasaji wa kijinsia kama mateso hushitakiwa kama uhalifu wa kivita au uhalifu dhidi ya utu. Hata hivyo, sheria nyingi za jinai huweka hatiani kosa la mateso kama hatia ya kipekee na sio chini ya mwamvuli wa uhalifu wa kivita, uhalifu dhidi ya utu au mauaji ya kimbari. Katika mamlaka yao husika, watendaji wanaweza kufanya uchunguzi na kuanzisha mashitaka kwa makosa ya unyanyasaji wa kijinsia kama uhalifu wa mateso. Ili kufanya hivyo, wanapaswa kuhakikisha kwamba wanafahamu misingi ya hatia za mateso katika sheria za jinai za ndani ya nchi.

16 Kwa mfano, sehemu za mahabusu ambapo raia wanafanywa kuwa watumwa kwa ajili ya ngono na pia bila kujamiiana, na kuteswa, kwa ngono au bila ya kujamiiana.

17 Kwa mfano, ambapo wanawake au wasichana wanapotekwa nyara na kutoweka, na wakati wa upotevu wao wanateswa kwa kutumia ngono.

18 Kwa mfano, ndoa za kulazimishwa zilizofanywa katika mazingira ya mfumo wa utaratibu wa kutawala kwa ukandamizaji na utawala wa watu wenye rangi au kabila moja juu ya kundi la watu wenye rangi au kabila nyingine.

19 Wakati falsafa ya sheria ya jinai kuhusu unyanyasaji wa kijinsia kama tendo la mauaji ya kimbari ni haba, hiyo hiyo ndogo iliyopo inaunganisha hatia za unyanyasaji wa kijinsia na mauaji ya kimbari kwa kutumia sheria ya "Kusababisha madhara makubwa katika mwili au kisaikolojia". Ni hakika jambo hili linawezekana, hata hivyo, ili kuchunguza na kushitaki maovu ya unyanyasaji wa kijinsia kama vitendo vya mauaji ya kimbari kupitia njia tofauti na ile ya sheria hii; Kwa mfano, kituo cha kizuizi ambapo wafungwa wa kiume wanahasiwa kwa utaratibu fulani kwa nia ya kuzuia uzazi na hivyo kuharibu kundi lao lote au sehemu ya kundi hilo, kunaweza pia kushitakiwa chini ya sheria ya kulazimisha hatua za kuzuia uzazi au kujenga mazingira ya maisha ambayo yanalenga katika kuleta uharibifu wao.

# SEHEMU I:
## Unyanyasaji wa kijinsia



### Hatia zingine

Sheria zote za SCSL na za Roma zinashughulikia hatia dhidi ya utu kwa "vitendo vyengine vya kinyama". Uhalifu huu unafanya kazi kama sheria ya mabaki au inayoshikilia kila kitu, kwa sheria zingine za jinai ambazo hazijaorodheshwa kipekee. Hapo SCSL, uhalifu huu ulitumiwa kama msingi wa upelelezi, uendeshaji wa mashtaka na mwisho kupatikana kwa hatia kutokana na mienendo ya ndoa za kulazimishwa. Mienendo mingine ya kihalifu inayoweza kushtakiwa kama hatia dhidi ya utu katika "vitendo vyengine vya kinyama" inaweza kujumlisha kulazimishwa kwa ndoa, kulazimisha kutoa mimba na kulazimisha utupu au kuwa uchi.

Jinsi watendaji wa sheria wa ndani ya nchi wanavyoanza kutayarisha nyaraka na kuchukua kesi zinazohusu uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia katika muktadha wa ndani ya nchi, kutaweza kuwa na mipango mingine katika sheria za kihalifu zitakazoweza kutiwa hatiani na sheria hizi za jinai. Watendaji wahakikishe kwamba wanafahamu sheria ili kurahisisha uwezo wa kupata haki.

## 2.4 Sehemu B: Vipengele vya muktadha wa uhalifu wa kimataifa: "Nini kilitokea katika mazingira ambayo (tendo la unyanyasaji wa kijinsia) lilitokea?"

Kushtaki vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia chini ya sheria ya kimataifa kunahitaji kuthibitishwa kwa vipengele vya muktadha wa hatia hizo, na pia kwa vipengele vinavyohusika na matendo ya unyanyasaji wa kijinsia wenyewe. Vipengele vya muktadha ni vipengele vinavyonyanyua hatia fulani ifikie daraja la kuwa hatia ya kimataifa – hatia ya kivita, hatia dhidi ya utu au tendo la mauaji ya kimbari. Ili kushutumu kwamba matendo ya uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia ni ukiukaji wa sheria za kimataifa za jinai, ni lazima taarifa zitakazopatikana na timu ya watendaji ziwe na ukweli ambao unaweza kuusaidia muktadha wa vipengele husika vya uhalifu wa kimataifa. Muktadha wa vipengele (kama vilivyo katika Sheria ya Roma) vimeelezewa kwa ufupi hapa chini. [20] Ndani ya Kitabu cha kazi cha Ushahidi **(angalia Nyongeza 1)**, Watendaji wanaweza kuangalia mifano ya aina ya maswali ambayo yanaweza kuulizwa wakati wa mahojiano ili kupata taarifa hii, na mifano mingine ya ushahidi, ya kutoka kwenye nyaraka na ushahidi wa picha unaoweza kuthibitisha muktadha wa vipengele vyenye hatia hizi za kimataifa. Ufupisho wa maelezo ya jumla umewekwa hapa chini.

### (i) Unyanyasaji wa kijinsia kama uhalifu wa kivita au kama uvunjwaji wa sheria na desturi za vita

Tendo la unyanyasaji wa kijinsia linaweza kuwa hatia ya kivita au ukiukaji wa sheria na desturi za vita kama likitendwa au kuhusika na muktadha wa vita vya kimataifa au visivyo vya kimataifa, na mtuhumiwa anayeifahamu hali halisi inayofanya mazingira yenye kutumia silaha katika mapigano. [21] Sheria ya Roma inaorodhesha uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia

20 Falsafa ya mahakama ya hapa na pale na mahakama ya mseto inaelewesha jinsi ambavyo sheria za kimataifa za uhalifu zilivyotafsiriwa. Maendeleo mengi katika falsafa ya sheria yalijitokeza katika Sheria ya Roma, wakati baadhi hazikujitokeza. Ingawa ufafanuzi na mambo ya uhalifu wa kimataifa yanaweza kutofautiana kwa kiasi fulani baina ya mahakama mbalimbali, kupata ushauri wa falsafa ya sheria kutoka mahakama kunaweza kuwa muhimu sana katika kuelewa jinsi baadhi ya masuala haya yalivyotafsiriwa na majaji, na katika uwezekano wa kupata ukweli na jinsi sheria inavyoweza kuchambuliwa katika mazingira ya baadaye.

21 Sheria za kimataifa katika mapambano ya silaha zimeweka utawala tata kuhusiana na hadhi ya waathirika wa uhalifu wa kivita. Kwa kawaida, ni lazima ithibitishwe kwamba muathiriwa alikuwa ni "mtu anayehifadhiwa/mkimbizi" chini ya Mikataba ya Geneva ili uhalifu uhisabiwe kama uhalifu wa kivita au ukiukaji wa sheria na desturi za vita. Kwa kurahisisha, hii ina maana kwa ujumla kwamba mwathirika lazima ama awe raia au "hors de combat" yaani mtu nje ya mapambano, yaani asiwe anashiriki kikamilifu katika uhasama wakati uhalifu ulipotendwa. Hata hivyo Kwa makosa ya unyanyasaji wa kijinsia uliofanywa wakati wa mapambano ya silaha, hakuna haja ya kuwa na sharti la kuthibitisha kuwa waathirika walikuwa ni watu wanaohifadhiwa/wakimbizi. Alimradi tu kuzingatia kuwa mambo mengine ya uhalifu wa kivita au ukiukwaji wa sheria na desturi za vita ni za kuridhisha; kitendo cha unyanyasaji wa kijinsia unakuwa uhalifu wa kivita au ukiukaji wa sheria na desturi za vita bila kujali hali ya mwathirika kama raia, mtu nje ya mapambano au vinginevyo. Angalia Jean-Marie Henckaerts na Louise Doswald-Beck, ICRC Study on Customary Rules of International Humanitarian Law, Vol. I Rules, Vol. II Practice, Cambridge University Press, March 2005: Rule 93: Rape and other forms of sexual violence are prohibited in international and non-international armed conflicts. Pia angalia ICRC, Sexual violence in armed conflict: questions and answers (7 March 2014), "Every single rape committed during and in connection with an armed conflict constitutes a war crime and must be prosecuted" iliyopo: http://www.icrc.org/eng/resources/documents/faq/sexual-violence-questions-and-answers.htm.

kama hatia za kivita za kimataifa na zile zisizo za kimataifa. Watendaji wanapokusanya taarifa kuhusu hatia za unyanyasaji wa kijinsia zilizofanywa katika muktadha wa kivita (kutokana na Sheria ya Roma) wanahitaji kuhakikisha kwamba wanakusanya taarifa za kutosha kuonyesha kwamba tendo lilitendwa katika muktadha wa kivita au unaohusika na vita, na kuunga mkono uamuzi wako wa mwisho kwamba watuhumiwa walikuwa wakifahamu kuwepo kwa vita. [22]

### (ii) Unyanyasaji wa kijinsia kama uhalifu dhidi ya utu

Pia unyanyasaji wa kijinsia unaweza kuwa hatia dhidi ya utu pale ambapo unyanyasaji wa kijinsia umefanywa kama sehemu ya mashambulizi yaliyotapakaa au yenye mfumo maalum yanayotendwa dhidi ya raia. *Sio tendo lenyewe la unyanyasaji wa kijinsia ambalo ni lazima litapakae au liwe na mfumo maalum ili kuwa hatia dhidi ya utu; ni mashambulizi [23] kwa raia ambapo mtuhumiwa mwenyewe alifahamu kwamba tabia hiyo ilikuwa au alitegemea tabia hiyo kuwa sehemu ya mashambulizi yaliyotapakaa au yenye mfumo maalum yanayotendwa dhidi ya raia. Kwa kweli, tendo moja au kubaka au aina nyingine ya unyanyasaji wa kijinsia unaweza kuwa hatia dhidi ya utu.*[24]

Mahakama ya ICC imejumlisha ombi la ziada ambalo ni maalum kwa mamlaka ya mahakama hiyo: [25] kwamba shambulizi ambalo linahusishwa na hatia dhidi ya utu liwe limefanywa "kwa mujibu wa au katika kuboresha sera ya taifa au shirika ili kutenda shambulizi kama hilo". Ombi hili linaweza kutakiwa na mamlaka ya mahakama ambamo mtendaji anakusanya taarifa, au linaweza lisitakiwe; ni wajibu wa mtendaji kujua nini kinahitajika kisheria katika muktadha ambao anakusanyia taarifa, ili awe na uhakika wa kukusanya taarifa ya kutosha ambayo inaweza kujumlisha kufanywa kwa hatia dhidi ya utu.

Hatia dhidi ya utu hazihitaji kuwa na kiunganishi katika mapigano yanayotumia silaha – hatia inaweza kufanywa wakati wa amani. Hata hivyo, ni kawaida kwa hatia za vita au uhalifu dhidi ya utu kufanywa katika muktadha huo au unaofanana na huo.

### (iii) Unyanyasaji wa kijinsia kama mauaji ya kimbari

Mauaji ya kimbari yanafafanuliwa kama tendo lolote kati ya haya yafuatayo ambayo yanatendwa kwa lengo la kuangamiza kwa ujumla au sehemu ya taifa, kabila, rangi au kikundi cha dini fulani kwa: kuwauwa wanajumuiya wa kundi hilo, kuwaumiza vibaya sana kimwili au kisaikolojia, kushurutisha kwa kusudi masharti ya maisha ambayo yanalenga kuangamiza kundi fulani lote kabisa au sehemu ya kundi hilo; Kulazimisha hatua ambazo zinazuia uzazi katika jumuiya, Kulazimisha uhamisho wa watoto kutoka kundi lao kuenda katika kundi lingine. Unyanyasaji wa kijinsia utakubalika kama tendo la mauaji ya kimbari pale ambapo muktadha wa vipengele vya mauaji ya kimbari unajitosheleza kutokana na taarifa zilizopatikana. Kama, kwa mfano, unyanyasaji wa kijinsia "unatendwa kwa lengo la kuangamiza kwa ujumla au sehemu ya taifa, kabila, rangi au dini ya kundi fulani" kwa kusababisha "madhara mabaya sana kimwili au kiakili na hisia kwa wanajumuiya wa kundi hilo" kitendo hicho cha unyanyasaji wa kijinsia kitakubalika kama tendo la mauaji ya kimbari.[26] Watendaji wanaopeleleza matendo yanayoshutumiwa kuwa mauaji ya kimbari waangalie taarifa ambazo zinaunga mkono: (a) tendo la ngono linajitosheleza kimsingi kwa

22 Watuhumiwa wa "moja kwa moja" au wa "kimwili" ni wale ambao kwa hakika, wamefanya uhalifu wao binafsi na moja kwa moja. Washtakiwa na walengwa wa uchunguzi wa kimataifa wa jinai wanaweza kuwa watuhumiwa wa moja kwa moja; lakini pia wanaweza kuwa watuhumiwa ambao waliondolewa kutoka kwenye uhalifu halisi, lakini ambao hata hivyo wao binafsi walihusika na kutendwa kwa uhalifu. Angalia kipengele **"Mfumo wa dhima"** kwa ufafanuzi.

23 Sheria ya Roma Ibara ya 7 imefafanua "mashambulizi" kwa mantiki hii, kwamba ni "mwenendo unaoshirikisha kutendwa kwa matendo mengi" ambayo ni hatia dhidi ya utu.

24 Kama yalifanywa kama sehemu kuu ya kueneza au utaratibu wa mashambulizi unaowalenga raia.

25 Kwa vile hili ni sharti la utawala, halichukuliwi kama kipengele cha uhalifu dhidi ya utu chini ya sheria za kimataifa za kimila. Sheria za mahakama ya hapa na pale na mahakama ya mseto hazina mahitaji haya ya ziada. Ushirikishwaji wa mahitaji haya katika misingi ya uhalifu ulio dhidi ya utu ya mahakama ya ICC unawekea mipaka zile hatia dhidi ya utu ambazo zingeweza kuwa chini ya mamlaka ya ICC.

26 Kumbuka kwamba vitendo vingine vya mauaji ya kimbari kama vilivyotajwa katika misingi ya muktadha (zaidi ya "kusababisha madhara makubwa katika mwili au akili") vinaweza pia kuhusu vitendo vya kushirikisha ukatili wa kijinsia.

kuwa ni tendo la mauaji ya kimbari (kuua, madhara mabaya sana kimwili/kiakili na hisia, mazingira ya maisha, kulazimisha hatua ambazo zinazuia uzazi, n.k); na taarifa za kuunga mkono uamuzi wako wa mwisho unaoonesha kwamba tendo lilikuwa (b) limetendwa kwa lengo la kuangamiza kwa ujumla au sehemu ya taifa, kabila, rangi au dini ya kundi fulani.

## 2.5 Sehemu C: Mfumo wa dhima kwa matendo ya uhalifu wa kimataifa: "Ni vipi anayeshutumiwa kufanya makosa ana jukumu la kufanya tendo la unyanyasaji wa kijinsia kama uhalifu dhidi ya sheria za kimataifa?"

"Mfumo wa dhima" unaelezea nadharia ya kisheria inayotumika kuhusu wajibu wa hatia kwa anayeshtakiwa kuhusiana na hatia mbalimbali zilizoelezwa hapo juu. Kwa mfano, je anayeshtakiwa alitenda, alisaidia kutenda jinai, aliamrisha, pangilia n.k? Ili mtu kuonekana kama yeye binafsi ana jukumu la uhalifu kwa hatia iliyo chini ya sheria ya kimataifa, vipengele vya hatia nzito/maalum (kama vile ubakaji), muktadha wa vipengele vya aina ya hatia (kama vile hatia dhidi ya utu), na mfumo wa dhima (kama vile kutenda tendo), ni lazima vithibitishwe kabisa kwa kuridhisha bila ya kuwa na shaka yoyote.

Kwa pamoja, hadhi ya mahakama za hapa na pale na za mseto na mahakama za ICC zinaorodhesha aina nyingi za wajibu binafsi wa hatia ambazo, kufuatana nazo, mtu anaweza kuwajibika na hatia kwa ajili ya matendo ya unyanyasaji wa kijinsia kama hatia ya kivita; Kama hatia dhidi ya au kama tendo la mauaji ya kimbari. Dhima zilizowekwa hapa ni mifano kutoka katika Sheria ya Roma, ambazo zimeorodheshwa kutokana na sababu zilizoelezewa hapo juu. Watendaji wakumbuke kwamba sheria za ndani ya nchi kuhusu muktadha fulani ambao wanaufanyia kazi zinaweza kuwa na mfumo wa dhima tofauti na zile zinazotumika kimataifa.

Kanuni ya msingi katika kifungu hiki ni kwamba, pamoja na kukusanya taarifa kuhusu tendo lenyewe la kihalifu, na pamoja na kukusanya taarifa kuhusu muktadha ambao tendo lenyewe la kihalifu limetendwa, ni lazima mchakato wa kutayarisha nyaraka ulenge katika kukusanya taarifa kuhusu jinsi wanaoshutumiwa kuwa watuhumiwa, wanavyoweza kuwa kweli wanahusika na kutenda hatia hiyo. Hii ina maana ya kwamba jinsi hiyo hatia inavyoshutumiwa kufanyika, na nini ilikuwa asili ya jukumu la anayeseshutumiwa kuwa mtuhumiwa wakati alipotenda hatia hiyo ya unyanyasaji wa kijinsia.

Sheria ya Roma inaelezea mfumo wa dhima inayohusika kwa mtuhumiwa anayeshtakiwa kwenye mahakama ya ICC. [27] Nyingine inaelezwa hapa chini.

### Kuhusika kwa pamoja (Ibara ya 25(3)(a)) na madhumuni ya dhima ya kawaida (Ibara ya 25(3)(d))

Hii mifumo ya dhima inahusika na makundi ya watu wanaojiunga na kupanga kufanya hatia chini ya sheria ya kimataifa. Kwa kutumia nadharia za jambo linaloitwa "ubiya wa kijangiri", mahakama za hapa na pale zimeunda sheria za kesi kwa watuhumiwa wanaoungana kufanya uhalifu.

### Ukosaji usio dhahiri (Ibara ya 25(3)(a))

Kama ukweli unaonyesha kwamba m(wa)husika anaweza kuwa alihusika chini ya mfumo wa dhima wa ukosaji usio dhahiri, watendaji watahitaji kukusanya taarifa ya kuonyesha kwamba anayeshutumiwa kuwa mtuhumiwa alikuwa na mamlaka ya kuongoza na kudhibiti hatia. Kudhibiti huku kunaweza kuonyeshwa kwa njia tofauti, kama vile kwa kuwa na mamlaka ya kutawala matakwa ya mtuhumiwa ambaye alitenda tendo moja kwa moja au kwa kuwa na mamlaka ya kuongoza chombo ambacho kina muundo wa mamlaka, kama vile muundo wa

27 Kumbuka kwamba Mifumo ya dhima chini ya sheria za mila kimataifa ni kubwa zaidi kuliko zile katika mpango ulio wazi ndani ya Sheria ya Roma.

polisi au jeshi. Zaidi ya hapo, mtuhumiwa inabidi awe alikuwa na nia ya kufanya uhalifu, na kufahamu mazingira ambayo yalimwezesha kuweza kuwa na mamlaka juu ya hatia.[28]

### Kuamuru (Ibara ya 25(3)(b))

Ili kupendekeza kwamba m(wa)kosaji angeweza kuamuru hatia za unyanyasaji wa kijinsia, watendaji watahitaji kukusanya taarifa zinazoonyesha kwamba mtuhumiwa alikuwa na mamlaka ya kuamuru na kutegemea kwamba amri hiyo itafanyika.

### Kushawishi/Kuvutia (Ibara ya 25(3)(b))

Taarifa ambazo zitaonyesha kwamba anayeshutumiwa kuwa mtuhumiwa alishawishi au alimvutia mtu mwingine ili afanye hatia za unyanyasaji wa kijinsia zikiwa kama hatia chini ya sheria za kimataifa zitaonyesha kwamba mtuhumiwa alimhamasisha, chochea, vutia au alimshurutisha mtuhumiwa wa moja kwa moja kufanya hatia hizo.

### Saidia kutenda jinai (Ibara ya 25(3)(c))

Kuonyesha kwamba mtuhumiwa amesaidia kutenda jinai wakati wa kutendwa kwa unyanyasaji wa kijinsia kama hatia ya kimataifa, ni lazima kudhihirishwa kwamba mtuhumiwa aliwasaidia watuhumiwa moja kwa moja (mfano alitoa njia iliyofanya kutendwa kwa jinai), au aliwahamasisha na kuwaunga mkono.

### Majukumu ya Makamanda na wakuu wengine (Ibara ya 28)

Watuhumiwa wa unyanyasaji wa kijinsia kama hatia chini ya sheria ya kimataifa wanaweza kuwa walifanya uhalifu huu katika madaraka yao kama wakuu au makamanda wanowasimamia  moja kwa moja watuhumiwa.

Kama mtuhumiwa ni kamanda wa jeshi, watendaji wanahitaji taarifa zitakazoonyesha kwamba alikuwa na mamlaka juu ya wale waliokuwa chini yake, kwamba alijua au angetakiwa kujua kwamba walio chini yake walikuwa wanatenda jinai, kwamba alishindwa kuchukua hatua zenye kuridhisha ili kuzuia au kuadhibu au kuwasilisha taarifa kwa wakuu wenye mamlaka na ustadi ili wapeleleze, na kwamba, matokeo yake ni kuwa hatia imefanywa.

Kama hatia zimefanywa na raia ambaye ni mkuu, ni lazima taarifa zilizokusanywa na mtendaji zidhihirishe kwamba kulikuwa na uhusiano wa mkuu – uhusiano wa usaidizi baina ya mkuu na mtuhumiwa anayehusika moja kwa moja. Na kwamba mkuu alijua au alipuuzia kwa makusudi taarifa ambazo zilionyesha kwamba watu wa chini yake walikuwa wakifanya uhalifu, kwamba hatia hizo zilikuwa ni shughuli katika madaraka na udhibiti wa wakuu, kwamba alishindwa kuchukua hatua zenye kuridhisha ili kuzuia au kuadhibu au kuwasilisha taarifa kwa wakuu wenye mamlaka na ustadi ili wapeleleze, na kwamba, matokeo yake ni kuwa hatia imefanywa.

28 Kumbuka kwamba baadhi ya nguzo sahihi za aina hii ya mfumo wa dhima huweza pia kutumika ili kuthibitisha mifumo mingine, kama vile jukumu la amri la makamanda wa kijeshi kwa mujibu wa Ibara ya 28(a).

> Uchache wa mashitaka ya uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia ndani ya nchi, kiasi kidogo cha mashitaka ya kimataifa kwa hatia hizi, na udogo wa uhalifu huu wa vurumai za ngono duniani kote - hasa katika hali ya vita - unaendelea kuwacha pengo wazi la kutowajibika...

**Jane Adong Anywar, Women's Initiatives for Gender Justice (Haki za Wanawake), UNSC Mjadala 2013**

# SEHEMU 2: NYARAKA KATIKA MATUMIZI


## 3. MASUALA YA AWALI 29

3.1 Usifanye madhara 29
3.2 Mafunzo 29
3.3 Tathmini 30
(i) Utafiti 31
(ii) Tathmini za athari 33
3.4 Mipangilio kwa ujumla 35

## 4. MPANGILIO WA MADA ZA MSINGI 36

4.1 Uratibu 36
4.2 Tafsiri 38
4.3 Kuandaa taarifa 41

## 5. KUWATAMBUA WALIONUSURIKA NA MASHAHIDI WENGINEO 41

5.1 Utambulisho wa moja kwa moja 42
5.2 Wasuluhishi 42

## 6. USHAHIDI 44

6.1 Ridhaa kamili 45
6.2 Siri 47
6.3 Rufaa 48

## 7. MAHOJIANO 50

7.1 Mazingira ya mahojiano 52
7.2 Orodha ya mahojiano 53
7.3 Aina za maswali 54
7.4 Njia za mahojiano 56
7.5 Kurekodi taarifa za mahojiano 61

## 8. VYANZO ZAIDI VYA TAARIFA 61

8.1 Ushahidi dhahiri 61
(i) Sehemu za mashambulizi 63
8.2 Ushahidi wa nyaraka 66
(i) Aina za nyaraka 66

## 9. KUHIFADHI TAARIFA 68

9.1 Kuhifadhi nyaraka na taarifa nyingine zilizo dhahiri 69
9.2 Kuhifadhi taarifa za dijitali 69
9.3 Kuhifadhi taarifa za matibabu kisheria/ushahidi wa kisayansi kuhusu uhalifu (forensiki) 70

# SEHEMU II: NYARAKA KATIKA MATUMIZI

## 3. Masuala ya Awali

### 3.1 "Usifanye Madhara"

Kushughulika na watu, familia zao na jumuiya ili kuchunguza na kutengeneza nyaraka kuhusu unyanyasaji wa kijinsia kunahitaji kufanywa kwa kutumia njia ambazo, kwa kiasi kikubwa, zinawawezesha walionusurika kupata haki. Na kujitahidi iwezekanavyo kupunguza athari mbaya zinazoweza kujitokeza wakati wa mchakato wa kutayarisha nyaraka.

Wakati wa kutayarisha nyaraka kuhusu unyanyasaji wa kijinsia, ni lazima watendaji wajitahidi "Usifanye Madhara" au wapunguze madhara ambayo kuwepo kwao au mamlaka yao yanaweza kuleta bila kukusudia.

Kwa hivyo, watendaji wajitahidi kufanya yafuatayo hata kwa kiasi kidogo:

1. **Fahamu hatari ya kushiriki katika kutayarisha nyaraka kuhusu unyanyasaji wa kijinsia.**
2. **Hakikisha wajumbe wa timu wanaotayarisha nyaraka za unyanyasaji wa kijinsia wana mafunzo ya kutosha.**
3. **Hakikisha walionusurika na mashahidi wanatoa ridhaa yao sahihi kwa kushiriki katika udadisi.**
4. **Linda taarifa katika nyaraka.**
5. **Chukua hadhari maalum wakati wa kufanya kazi na watoto walionusurika na mashahidi.**

Mikakati ya kuhakikisha kwamba kanuni ya "Usifanye Madhara" inatumika wakati wa kutayarisha nyaraka, inaingizwa katika mchakato wa Itifaki yote.

### 3.2 Mafunzo

Watendaji wawe na ujuzi unaofaa na mafunzo ili kutayarisha nyaraka za unyanyasaji wa kijinsia. Hasa, watendaji wanatakiwa:

- Wahakikishe kwamba wajumbe wote wa timu, ikiwa ni pamoja na wanaofanya mahojiano, wakalimani, wachambuzi na waajiriwa wanaosaidia wanachakachuliwa kihakika na wanafundishwa kutayarisha nyaraka za uhalifu kutokana na misingi iliyokubalika katika Itifaki hii.
- Hakikisha kwamba wajumbe wote wa timu wanafahamu na wana uzoefu wa kushughulikia kesi za unyanyasaji wa kijinsia, pia, hasa, wanafahamu njia bora za kufanya mahojiano, misamiati na mikakati inayotumika kujibu kwa makini na kwa busara pale taarifa ya unyanyasaji wa kijinsia inapotolewa na wanawake pamoja na wanaume walionusurika/walioshuhudia.
- Pale inapowezekana, kuwafundisha waajiriwa ili waweze kushughulikia maumivu yenye trauma/kiwewe na kufahamu njia za kuyatambua na kushughulikia matatizo yanayotokea baada ya msongo au stresi, yaani 'post-traumatic stress disorders' na hatari za kujiua na kujiumiza mwenyewe.

**Wanapokuwa wanafanya kazi na watoto ambao[29] walionusurika na walioshuhudia, watendaji wanatakiwa hasa kuwa na:**

- Mafunzo maalum yatakayowawezesha watendaji kuwa na mtazamo, kuhoji na kuwapeleka watoto sehemu husika ili kushughulikia mazingira magumu na uwezo wa mtoto.
- Uwezo wa kuelewa jinsi ya kutumia kanuni za "Usifanye Madhara", kwa ujasiri na ridhaa kamili kuhusiana na kufanya kazi na watoto, ikiwa ni pamoja na mbinu za kutumia kutokana na umri wa watoto pale mawasiliano yanapofanywa na walionusurika pamoja na mashahidi.[30]
- Mafunzo kuhusu ujuzi wa kuwahoji watoto ambayo yanafuatilia umri, na yanaelewa kwamba mahusiano na watoto wadogo yanahitaji ujuzi tofauti na ule unaotakiwa kwa vijana.
- Kuwa na mafunzo kuhusu mbinu za kuzuia kuwapa watoto kutopata trauma/kiwewe tena na tena, kama vile kuwaruhusu kuwa na hisia za kimwili na kiroho (kutetemeka, kutingishika na kulia).
- Kuelewa changamoto ambazo makundi tofauti ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu wanaweza kukabili, kwa mfano athari ya kukataliwa na jamii ambazo wasichana wadogo wanaohusiana na makundi yenye silaha au majeshi huweza kupata.

## 3.3 Tathmini

Kuna masuala mengi ambayo yanatakiwa kutathminiwa kabisa na kufanyiwa utafiti na watendaji kabla ya kuanza mchakato wa kutayarisha nyaraka. Taarifa hiyo huweza kuwa ndiyo msingi wa kutumia kwa mpango wa kutayarisha nyaraka – inahitaji ujuzi mkubwa wa muktadha wa jamii na kujali sana ili kuhakikisha kwamba walionusurika kutokana na hatia za unyanyasaji wa kijinsia hawajihisi kama hawana uwezo, wanaweza kupata haki na usalama wao hautishiwi.

Hatua ya kwanza ni kwamba watendaji watathmini, jinsi iwezekanavyo, kama taarifa inayohitajika imewekwa katika nyaraka na watendaji wengine pamoja na mashirika mengine, na kama taarifa hiyo inapatikana. Pia kama kutayarisha nyaraka kwa mara nyingine tena, ikiwa ni pamoja na kufanya mahojiano, kunahitajika. Kama lengo ni kupata utaratibu wa haki, basi inawezekana kwamba kufanya mahojiano tena hakutoweza kuepukika. Hata hivyo, kama maagizo ni utetezi, basi hili halitokuwa na ulazima.

Kabla ya kuwahoji walionusurika na mashahidi wengine au kukusanya taarifa yoyote ya ziada, ni lazima watendaji: **(i) wafanye utafiti kuhusu uhalifu, mazingira na jamii; (ii) watathmini hatari kwa walionusurika, watendaji na taarifa na (iii) waamue huduma gani walionusurika wanaweza kuwa tayari wameshapata**. Watendaji wanashauriwa kuwa majukumu haya hayana haja ya kufanyika kwa mlolongo maalum, bali kwa wakati mmoja. Kwa mfano, ni vigumu kutathmini hatari maalum za usalama kwa walionusurika bila ya kutafiti mfumo wa ukiukaji uliofanyika katika eneo maalum; vile vile, kutafiti vikwazo vya uwajibikaji kwa walionusurika kutahusisha kiwango fulani cha tathmini ya hatari.

29 Mkataba wa Haki za Mtoto umefafanua mtoto kama "kila binadamu ambaye ana umri ulio chini ya miaka 18 isipokuwa, chini ya sheria husika kwa mtoto, huhesabika kuwa mtu mzima mapema zaidi". Kuhakikisha umri halisi wa mtu binafsi aliyenusurika/shahidi ni muhimu sana katika kuelewa jinsi ya kupata ridhaa kamili, na pia kuwa na athari katika uendeshaji wa kesi za jinai. Ambapo watoto hawana nyaraka za usajili wa kuzaliwa, hatua nyingine zichukuliwe ili kubaini umri wa mtoto, ikiwa ni pamoja na kupitia rekodi ya ubatizo, kumbukumbu za jamii za uzazi, na mifumo ya muda mfupi au ya dharura iliyoanzishwa na mashirika ya misaada ya kibinadamu Kwa mwongozo wa ziada ona UNICEF, Innocenti Research Centre, Innocenti Insight: Birth Registration and Armed Conflict, (Usajili wa Uzazi na Vita), 2007.

30 Angalia IRC, UNICEF, Caring for Child Survivors of Sexual Abuse: Guidelines for Health and Psychosocial Service Providers in Humanitarian Settings (Utunzaji wa Watoto Walionusurika kwa Unyanyasaji wa Kijinsia: Mwongozo wa Afya na Watoa Huduma za Kisaikolojia katika Mazingira ya Kibinadamu), 2012.

### (i) Utafiti

Hapa chini kuna mada chache za msingi ambazo zinahusiana na unyanyasaji wa kijinsia ambao watendaji wanatakiwa kufahamu kama chanzo cha maswali yao.

Taarifa nyingine hapa chini zitapatikana kwa urahisi kutoka katika ripoti zitakazokuwa wazi, nyaraka na tovuti. Nyingine zitahitaji utafiti wa kina zaidi, na huweza kupatikana kutoka katika mashirika tofauti ya kimataifa kama vile Umoja wa Mataifa, Mashirika yasiyo ya kiserikali ya kitaifa na kimataifa, mashirika ya kienyeji na ya ngazi za chini na jumuiya ya washauri mabingwa. Watendaji watakaokuwa wanafanya kazi moja kwa moja katika muktadha wa kitaifa wataweza kupata taarifa nyingine moja kwa moja katika maeneo husika. Watendaji wanaweza kushindwa kujibu maswali yote haya kabla ya mchakato wa kukusanya taarifa. Hata hivyo, kujibiwa kwa maswali mengi iwezekanavyo kutawawezesha watendaji kuboresha mipango ya mbinu zao, kukusanya taarifa zinazofaa na zenye maana na kupunguza athari kwa walionusurika/mashahidi na wao wenyewe.

### Utafiti wa awali kwenye hatia maalum

- Katika eneo kuna mienendo gani ya kijinsia – yaani nchini na katika maeneo tofauti – ambayo uhalifu unafanywa? Kuna imani gani za jadi na kitamaduni katika jamii kuhusu majukumu ya kijinsia? Vipi hii inaathiri uwezo wa walionusurika kutoa taarifa ya hatia za unyanyasaji wa kijinsia na kupata haki?[31]

- Nini asili na eneo la matendo ya unyanyasaji wa kijinsia ambayo yanashutumiwa kufanyika? Nini mfumo wa matendo haya ya jinai na jinsi yanavyojitosheleza katika mfumo mzima wa mashambulizi?

- Mambo gani yameripotiwa rasmi? Ripoti zimeelekezwa kwa nani? Watu wamelengwa wapi?

- Jumuiya inaelewaje, na ina mtazamo gani kuhusu aina tofauti za unyanyasaji wa kijinsia, pia ulio dhidi ya watoto? Kuna madhara gani, kama yapo yoyote, kwa walionusurika/mashahidi? Je jamii au familia itachukuliaje habari ya kuwa mwanajumuiya mmojawao alifanyiwa hatia ya kunyanyaswa kijinsia? Jinsi habari hii itakavyowagusa itategemea umri au jinsia ya aliyenusurika/shahidi?

- Nini hali ya usalama na kuna vipingamizi gani dhidi ya walionusurika pale wanapojaribu kufuatilia utaratibu wa uwajibikaji?

- Aina tofauti za unyanyasaji wa kijinsia huadhibiwa vipi kama makosa ya jinai, na je, huwapo adhabu? Kuna matakwa gani ya kisheria yanayohitajika ili kuthibitisha unyanyasaji wa kijinsia? Je mfumo wa taifa wa sheria unakimu vipi haki mbele ya sheria? Kama ndiyo, hii hutumika katika matendo? Je sheria za utaratibu na ushahidi huwezesha au huzuia fursa ya kupata haki kwa walionusurika? Kwa mfano, ushahidi wa wanaume na wanawake hupewa uzito sawa? Je kuna masharti maalum ya kisheria ambayo yamewekwa kuhusu watoto?

- Kesi hupelelezwaje na hushtakiwaje kitaifa na katika ngazi za chini? Kuna vitengo maalum vya polisi vinavyopeleleza na kuendesha mashtaka ya hatia za unyanyasaji wa kijinsia, ikiwa ni pamoja na vitengo vyenye utaalam maalum wa kushughulikia watoto?

31 Chombo muhimu cha kufanya utafiti huu kinaitwa Initiatives for Gender Justice's Gender Equality Traditions (GET) Indicators Checklist orodha kutoka katika makala yake Gender in Practice: Guidelines and Methods to address Gender Based Crime in Armed Conflict, pp 9-14 (kinapatikana hapa - http://www.iccwomen.org/whatwedo/training/docs/Gender_Training_Handbook.pdf).

- Kuna aina gani tofauti za upatikanaji wa haki, zilizo rasmi na zisizo rasmi, kwa walionusurika/mashahidi? Nini umadhubuti na udhaifu wa aina hizi za haki? Je taratibu zisizo rasmi zinaonyesha au kufungisha kutokuwepo kwa usawa wa kijinsia nchini? Je wanaume na wanawake wanatendewa sawa katika taratibu za haki zisizo rasmi? Nini matokeo kwa mnusurika/shahidi anapoamua kwamba hataki kuendelea na utaratibu wa kidesturi ila anapendelea zaidi kufuatilia taratibu zilizo katika ngazi ya kitaifa (kama zipo)? Je anaweza kupata zote? Je watoto wanaweza kupata zote?

**Utafiti wa awali katika muktadha**

- Nini hali ya kisiasa na usalama? Nini historia ya mfarakano au uhasama? Je kuna historia ya mateso ya kikabila, kidini na kirangi? Je kuna historia ya mateso ya kijinsia hasa (kama vile kunyimwa kabisa kwa haki za kimsingi kwa sababu ya jinsia)?

- Nani amelengwa? Makundi maalum yamelengwa? Watoto wanalengwa kwa makusudi? Imejulikana vipi kwamba makundi hayo yamelengwa? Nani amewalenga? Wamelengwa na wanaume, wavulana, wanawake au watoto?

- Kumekuwa na ripoti au kumbukumbu zilizofanywa kuhusu matendo mengine ya kihalifu yaliyofanywa kama mashambulizi? Je kumekuwa na ripoti za matukio ya nyumba kuvamiwa, kukamatwa na kufungwa kwa raia au ripoti za utesaji wa kijinsia au ule usio wa kijinsia. Nini mfumo wa hatia?

**Utafiti wa awali kwa wanaoshutumiwa kuwa watuhumiwa**

- Vipi mpangilio wa jeshi na mfumo wa usalama? Makundi gani yaliyo na silaha yanaendeshwa katika eneo? Nini uhusiano wao na wananchi wenyeji?

- Makundi yaliyo na silaha yanatoka wapi? Wana ushirikiano gani? Je makundi haya yameundwa na wanaume na wanawake? Makundi haya yameundwa na wasichana na wavulana? Nini majukumu tofauti ya makundi?

- Nini ushirikiano (kama upo) kati ya makundi yanayoshutumiwa kuwa na makosa na vikosi vya usalama vilivyopo katika eneo ambalo utayarishaji wa nyaraka utafanywa? Je watuhumiwa au washiriki wao wowote wanaathiri jamii iliyoathirika wakati upelelezi unavyoendelea?

**Utafiti wa awali katika huduma zilizopo na zinazopatikana**

- Walionusurika wamepata huduma gani za kimatibabu za kijamii zinazohusiana na saikolojia?

- Chaguo gani la msaada wa afya, kijamii unazohusiana na saikolojia, sheria na kiuchumi unapatikana kwa walionusurika/mashahidi wa unyanyasaji wa kijinsia? Mifumo gani ya marejeo au njia gani zimewekwa?

- Wahusika gani wanatoa huduma hizi katika maeneo ya karibu, katika wilaya na kitaifa?

- Kuna vipingamizi vyovyote kwa walionusurika/mashahidi ili kupata huduma hizi (mfano, wasiwasi wa usalama, vikwazo vya kifedha, au tabia na sera za kibaguzi) ?

### (ii) Tathmini ya athari

Pale watendaji watakapokuwa wanapangilia mipango ya kutayarisha nyaraka na kufanya upelelezi kuhusu unyanyasaji wa kijinsia, itabidi wafanye tathmini ya vitisho (ya kweli, yanayofikiriwa au yanayohisiwa) ambayo yangeweza kuathiri walionusurika na mashahidi wengine, ikiwa ni pamoja na kuangalia athari kwamba vitisho haya yanaweza kufanywa. Kabla ya kuunda mpango wa kutayarisha nyaraka, watendaji wanatakiwa pia watathmini wasiwasi kuhusu athari na usalama wa wanajumuiya wote wa timu ya kutayarisha nyaraka na wote wale watakaohojiwa. Fikra kuhusu watumishi, ugavi na usafirishaji, tafsiri, Mifumo ya kupangilia taarifa na mikakati ya kuwapata walionusurika/mashahidi zitaeleweka vizuri zaidi kama thathmini ya athari itafanywa kuhusiana na walionusurika/mashahidi, timu ya watendaji na pia taarifa zenyewe.

### Kutathmini athari kwa walionusurika/mashahidi

**1. Athari kwa walionusurika/mashahidi zinazohusiana na utayarishaji wa nyaraka kwa unyanyasaji wa kijinsia unajumlisha:**

- kulipiza visasi/vitisho/vitisho vya wale wanaoshutumiwa kuwa ni watuhumiwa/familia zao/watu wanaowaunga mkono dhidi ya walionusurika/mashahidi na/au familia zao;
- adhabu, ikiwa ni pamoja na unyanyasaji wa kimwili, unaofanywa na wanajumuiya wa jamii/familia/walezi wanaohusika moja kwa moja;
- kulazimisha kwa kuwashurutisha walionusurika/mashahidi ili wapatane na watuhumiwa (walionusurika/mashahidi wanaweza kulazimishwa kuolewa na/kuoa watuhumiwa);
- jitihada za kupata faida ya kifedha kwa familia za walionusurika/mashahidi zinachukua kipau mbele dhidi ya haki kwa walionusurika/mashahidi;
- kupata trauma/kiwewe tena;
- kukataliwa na wanandoa, watu ndani ya familia au jamii, ambayo huwa na matokeo ya kutengwa, au kutelekeza watoto;
- kupoteza riziki;
- kupoteza uwezekano wa kupata shule na nafasi za kusomea ufundi kwa watoto; na
- inapozidi sana, kukamatwa na kuadhibiwa – kwa mfano pale matendo ya ngono kufanywa nje ya ndoa au ushoga, yanapochukuliwa kama makosa ya jinai.

**2. Hasa, watendaji wajiulize:**

- Je kuna kituo cha matibabu karibu, na kama ndiyo, ni rahisi kukitumia? Je itasaidia walionusurika/mashahidi wote ambao unawashughulikia au wachache, na kama si wote basi nani anaweza kutoa huduma kwa wengine?
- Utayarishaji wa nyaraka utafanyika katika eneo ambamo uhasama unaendelea, watuhumiwa bado wamo katika eneo, au kuna athari ya vitisho kwa walionusurika/mashahidi kutishwa, kushambuliwa zaidi (ikiwa ni pamoja na kulipiziwa kisasi kwa kuongea) au kuhamishwa makazi? Kama ni hivyo, mikakati gani itawekwa ili kuondokana na vipingamizi hivi?

- Je taarifa kuhusu kuwepo kwa eneo fulani imetoka kwa aliyenusurika/shahidi ambaye kuna hatari kwa yeye kujulikana iwapo taarifa hiyo inaweza kuunganishwa na kumrudia yeye? Kama ni hivyo, kuna taratibu gani zitakazotumika ili kumlinda aliyenusurika/shahidi kutokana na athari yoyote?

- Je, kuyatembelea maeneo fulani ya hatia kunaweza kuwaweka hatarini zaidi watu waliokuambia kuhusu maeneo? Kama ni hivyo, kuna njia zingine (kama vile kwa kupitia mpatanishi) za kukusanya taarifa kuhusu maeneo haya?

- Athari gani maalum huwakumba watoto wanapojitokeza? Je watoto huweza kudharauliwa au kutengwa kama wakishtaki uhalifu? Itifaki gani zimewekwa ili kushughulikia athari zilizobainiwa au madhara kwa watoto?

- Je umezingatia maarifa yako binafsi ya athari na yale ya walionusurika/mashahidi? Ni lazima watendaji washauriane na walionusurika/mashahidi, kwani ni wao tu wanaoweza kufahamu watu fulani, na athari zinazoweza kutokea katika maeneo au jamii tu.

### Kutathmini athari kwa watendaji

**1.** Je inawezekana kwamba fursa ya kufika katika eneo, na kusafiri ndani ya eneo ina athari?

- Je kuna athari za makundi yenye silaha, magaidi au mitandao ya wahalifu yanayofanya kazi katika eneo au katika sehemu yenyewe?

- Je timu yako ina hatari ya kulengwa kipekee? Je kuna hatari ya wewe au timu yako kutumiwa vitisho kutoka kwa waliokosa, familia zao na wasaidizi (hili hasa ni tatizo kwa watendaji ambao ni wananchi)?

**2.** Je umefikiria athari za ziada ambazo si za kimwili? (hasa mashirika yasiyo ya kiserikali ya kitaifa)? Kwa mfano mashirika yasiyo ya kiserikali yanaweza kutishiwa kufutwa kama yakiendelea kufanya kazi.

**3.** Kuna sehemu maalum ambazo ni salama kuzitembelea?

- Je fursa ya kufika katika eneo au sehemu ina usalama na haina hatari ya kuwepo na mafuriko, mporomoko wa ardhi au hali ya hewa mbaya sana ?

- Je maeneo mengine ni mbali sana kuyafikia bila ya kulala usiku kucha, na kama ni hivyo, je kulala huko kunawezekana?

- Je kuna hatari ya kuwepo mizinga ambayo haijalipuka katika eneo?

- Je eneo lipo ndani ya au karibu na jengo lisilo salama?

**4.** Nini athari ya kukutwa ukiwa umemiliki taarifa yoyote na ushahidi ambao umekusanya?

**5.** Taratibu gani zinaweza kuwekwa ili kupunguza athari?

- Je unao mpango wa usalama na uokoaji?

- Unao mpango wa mawasiliano?

- Je utakuwa na vifaa vinavyotosha ili kukabiliana na lolote litakaloweza kutokea? Kwa mfano, utakuwa na mafuta ya kutosha, vifaa, vifaa vya huduma ya kwanza na vifaa vya mawasiliano?

- Timu yako inaweza kupata fursa ya kufika katika kituo cha matibabu kilicho karibu?

- Kama itahitajika, utaweza kutoa alama zitakazoonekana vyema na zitakazokuwa katika magari yako au vifaa?

- Umeweka mpango, sera na chaguo la rufaa kuhusu kuwepo kwa dharura au usafiri kwa walionusurika/mashahidi wowote, watoto peke yao au watu watakaokutikana katika maeneo maalum?

**6.** Kuna athari kwako au katika timu yako ya kuteseka na trauma/kiwewe kwa niaba ya wengine? Wanaposhughulika na trauma/kiwewe kinachotokea kwa niaba ya wengine, watendaji ambao wanashughulikia kesi nyingi wapewe fursa kubwa ya kuchukua likizo ndefu/za mara kwa mara ili kupona. Watendaji pia wapewe moyo kuongelea msongo au stressi walizonazo.

### Kutathmini athari kwenye taarifa

- Unao mpango uliopangiliwa vizuri wa kukusanya taarifa na kuzihifadhi kwa usalama?

- Utaziwekaje kwenye usalama na siri, taarifa ambazo umekusanya? Lini, kwa nini na vipi utaharibu taarifa ambazo kuna hatari ya kunyang'anywa? **(angalia kipengele cha 9, "Kuhifadhi Taarifa").**

- Utasafirishaje taarifa zozote na ushahidi ambao utakusanya?

- Unaweza kuendeleza "mlolongo wa utunzaji" na unao uwezo wa kuweka salama taarifa kwa muda mrefu? **(angalia Nyongeza 6 na 7, "Ushahidi dhahiri: kanuni juu ya mlolongo wa utunzaji" na "Ushahidi wa nyaraka: kanuni juu ya mlolongo wa utunzaji").**

## 3.4 Mipangilio kwa ujumla

Kabla ya kuanza mchakato wa kutayarisha nyaraka za unyanyasaji wa kijinsia, watendaji waunde mkakati ulio wazi au mpango ambao unahusu mambo yaliyo hapo juu na majibu kwa maswali:

Ukichukulia utafiti wako na tathmini ya athari:

- **Kwa nini unatayarisha nyaraka kuhusu unyanyasaji wa kijinsia?** Nini matokeo, unayotafuta?

- **Unao uwezo wa kutayarisha nyaraka kuhusu unyanyasaji wa kijinsia kama inavyotakiwa?** Umepata mafunzo ya kutosha, unavyo vifaa vinavyofaa na upo tayari kufanya hivyo? Unaufahamu mfumo wa kisheria ambao utakuwa unaufanyia kazi?

- **Utazitumiaje taarifa?** Utazipangaje kwa usalama, kuzitathmini na kuzihifadhi. Utamwasilishia nani taarifa? Utatangaza nini kwa umma, na nini utajitahidi kuweka siri?

- **Utachaguaje taarifa za kupewa kipau mbele na kuchagua vidokezo vipi kuvifuatilia?** Unaweza kuwa na taarifa nyingi za kufuatilia lakini ukawa huna muda au huna rasilimali za kutosha – kama ni hivyo, utachaguaje?
- **Juhudi zako zitaelemea wapi?** Nini sababu za msingi za kuchagua sehemu maalum au tukio au jamii? Mkakati wako utafuatilia mkondo wa kijiografia au dhana au vyote?
- **Nini wasiwasi kuhusu usalama kwa walionusurika, taarifa na timu yako?** Mikakati gani inaweza kuwekwa kupunguza athari hizo? Chaguo gani la rufaa unaweza kutayarisha?
- **Utatayarishaje nyaraka?** Kuna mahitaji gani ya ugavi na usafirishaji, kifedha na kitaalam?
- **Unaweza kupata vyanzo gani vya taarifa?** Utatafuta kupata vyanzo gani vya taarifa? Utavipataje? Utajiwekea kikomo kwenye vyanzo gani vya taarifa?
- **Utawasilisha vipi lengo la utafiti wako kwa jamii na walionusurika?** Utatumia mchakato gani ili kupata ridhaa, ikiwa ni pamoja na kukubali kwa watoto?
- **Utachukua muda gani kufanya hivi?** Nini kikomo cha muda wako?

## 4. Mpangilio wa mada za Msingi

### 4.1 Uratibu

Katika wakati wowote kunaweza kuwa na jitihada nyingi zinazofanywa ili kukusanya, kurekodi na kuchambua taarifa kuhusu unyanyasaji wa kijinsia katika maeneo yaliyoathirika na migogoro. Jambo hili lina ukweli zaidi katika maeneo ambamo unyanyasaji wa kijinsia unaaminika kutapakaa, ambamo maitikio ya hisani za kibinadamu ni imara, au ambamo upelelezi rasmi wa kimataifa au kitaifa umeshazinduliwa. Kuwepo kwa aina nyingi za milolongo ya uchunguzi kunaweza kuwa na madhara kwa watu na jamii, kukaleta athari katika ubora wa taarifa zinazokusanywa na uwezo wake kutumiwa katika mahakama ya jinai na pia kudhuru kazi ya mashirika yanayofanya kazi katika eneo. Baadhi ya matokeo ya kuwepo kwa aina nyingi za uchunguzi ni kama yafuatauo:

- Walionusurika/mashahidi wanaweza kuhitaji kurudia kusimulia hadithi zao mara nyingi, kwa ajili ya sababu tofauti, kwa watu tofauti. Wakati mwingine hii huweza kufanya trauma/kiwewe kirudi tena na tena. Kuulizwa maswali, hata kama kwa makini na nyeti, kunaweza kumfaya aliyenusurika/shahidi ahisi kama anahojiwa.
- Tathmini ya uchovu – jamii huchoka kwa kuwepo kiwango kikuu cha aina nyingi za uchunguzi, kuingiliwa na kupewa ahadi bila ya msaada kuletwa.
- Watu na jamii huwekwa hatarini kutokana na kupewa kipaumbele mno na kuwa na mtazamo kwamba wanasaliti wanajumuiya wenzao au wanashtaki wenzao.

**Ili kuwaheshimu walionusurika/mashahidi na kuhakikisha kwamba taarifa bora inakusanywa, michakato hii iratibiwe kwa mpangilio pale inapowezekana. Kwa hivyo, watendaji wanatakiwa kufanya yafuatayo:**

- Kuwa na uhusiano na mashirika mengine kabla ya kusafiri katika eneo, na ikiwezekana kutathmini aina, ubora, marudio na madhumuni ya taarifa ambazo wamekusanya au hawakukusanya.

- Tafuta taratibu zilizopo za uratibu wa unyanyasaji wa kijinsia katika ngazi za kitaifa, kieneo na za kienyeji. Kufahamu mifumo iliyopo kunaweza kuwezesha utumiaji wa taarifa kwa pamoja na upatikanaji wa data, pia upatikanaji wa ufumbuzi wa ulinzi kwa walionusurika/mashahidi.

- Kufahamu hali ya usalama na mengine yoyote ambayo mashirika mengine yanayokusanya taarifa yanaweza kuwa nayo. Mashirika mengine ambayo hukusanya taarifa kisiri na hivyo yasiombwe kutoa taarifa zao hadharani.

- Fahamu mashirika na watu ambao wanatumia vibaya jamii husika iliyoathirika kwa kubadili taarifa kijanja, kuwatisha wanajumuiya kwa kuwaambia kwamba wakijitokeza wataona matokeo mabaya, na kutangaza taarifa za uongo ili kudhalilisha juhudi za kutayarisha nyaraka.

- Wafahamu mifumo iliyopo ya kukusanya data kuhusu unyanyasaji wa kijinsia: madhumuni yake, yanavyotekelezwa, na nini mapungufu ya kushirikiana taarifa wanazozikusanya. Hii ni pamoja na Mfumo wa Taarifa za Unyanyasaji wa Kijinsia yaani (Gender-Based Violence Information System (GBVIMS))[32] na Ufuatiliaji, Uchambuzi na Mipango ya kutoa Taarifa, yaani (Monitoring, Analysis and Reporting Arrangements (MARA))[33] ulioanzishwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa 1960.[34]

- Heshimu mamlaka ya mashirika mengine yanayofanyia kazi ajenda tofauti ndani ya jamii. Mara nyingi wanaotoa huduma hufanya kazi ili kutoa msaada usio na upendeleo kwa wote, na hupatanisha migogoro, huwa huru mbele ya juhudi za kushtaki, na kuunganisha jamii yote ndiyo muhimu sana katika jukumu hilo. Watendaji wawe waangalifu zaidi wanapotembelea mashirika na jamii katika kambi na sehemu za wakimbizi au watu waliosambaratika, ofisi za watoa msaada, kliniki na sehemu salama za kijamii. Ikiwezekana, wapangilie ziara hizo mapema na sio kutokezea tu bila ya kutegemewa huku wakitafuta taarifa.

- Fahamu kwamba mara nyingi kutolewa huduma kwa walionusurika/maashahidi hufanywa kufuatana na matarajio ya siri ambayo hayavunjwi, ikiwa ni pamoja na kushirikiana kwa habari au data bila kutambulisha muhusika. Hii huweza kutumika kwa manufaa ya kuweka taratibu za sampuli, sehemu, majibu na aina za unyanyasaji wa kijinsia ambao ulitendwa.

32 Mpango wa GBVIMS ulizinduliwa mwaka 2006 na UNOCHA, UNHCR na IRC, uliundwa kuoanisha ukusanyaji wa data kuhusu unyanyasaji wa kijinsia (GBV) katika mazingira ya kibinadamu, ili kutoa mfumo rahisi kwa mameneja wa mradi wa GBV wanaokusanya, hifadhi na chambua data zao, na ili kuwezeshamatumizi kwa wote yaliyo salama na yenye maadili. (Angalia http://www.gbvims.org).

33 Lengo la MARA ni kuhakikisha utaratibu mzuri wa ukusanyaji taarifa kwa wakati, usahihi, kwa kuaminika na kwa malengo, juu ya migogoro inayohusiana na unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya wanawake, wanaume na watoto katika hali zote zinazoleta wasiwasi. Taarifa zilizokusanywa kupitia MARA hutumika kukuza hatua kwa wakati ili kuzuia na kukabiliana na migogoro inayohusiana na unyanyasaji wa kijinsia. Angalia Mwongozo huu: Implementation of Security Council Resolution 1960 (2010) on Women, Peace and Security (Conflict-related Sexual Violence) - (Migogoro inayohusiana na Unyanyasaji wa Kijinsia).

34 OP8, UN Security Council, Security Council resolution 1960 (2010) [on women and peace and security] [wanawake na amani na usalama], 16 Desemba 2010, S/RES/1960 (2010).

- Kumbuka Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa 1888,[35] ambamo Umoja wa Mataifa na mashirika ya kiserikali na mashirika yasiyo ya kiserikali, katika ngazi za kitaifa na kimataifa, yanaombwa yatoe msaada wa kuboresha ufuatiliaji, utayarishwaji wa nyaraka na kuripoti hatia za unyanyasaji wa kijinsia. Watoa huduma na taasisi nyingine zinazosaidia walionusurika zinaweza kuchagua kuitikia wito huu kwa kushiriki katika kushirikiana taarifa kuhusu walionusurika kwa kufuatilia mbinu bora za kimaadili na kutolewa ridhaa kwa walionusurika.

## 4.2 Tafsiri

Wakalimani huwa ni sehemu muhimu sana ya timu ya watendaji. Wakalimani wawe wana mafunzo ya kutosha, sio tu kwa tendo lenyewe la kutafsiri lakini kwa kufanya kazi na walionusurika/mashahidi wa unyanyasaji wa kijinsia na, inapotakiwa, na watoto.

Wakalimani wanatakiwa waweze kutoa tafsiri wakati wowote ambapo watendaji wanaweza kuwa na mawasiliano na wanajumuiya wa jamii, ikiwa ni pamoja na wakati wa mahojiano. Wanatakiwa pia wawape watendaji tafsiri sahihi ya kilugha na kitamaduni ya maneno ya msingi, tabia na misemo inayohusiana na unyanyasaji wa kijinsia katika mazingira maalum, bila ya kubadili au kushawishi taarifa kama inavyotolewa na walionusurika au mashahidi wengine.

Hasa wakati wa mahojiano, wakalimani wanatakiwa waweze kufanya kazi kwa makini na kitaalam, na kwa kufuatilia kanuni na kwa maadili ya "usifanye madhara". Ni lazima pia waelewe vizuri kabisa dhana ya kutoa ridhaa, na kufuatilia kanuni za timu zinazohusu siri.

Hasa wakalimani wanatakiwa:

- Wakubaliane na msimamo wa usalama wa kufanya kazi katika eneo hilo na katika mazingira au muktadha ambao watendaji watawataka wao wafanyie kazi.
- Kuelewa mazingira ya kienyeji lakini kuwa wakweli katika maoni yao.
- Kuwa na uzoefu wa (na kuwa makini kwa) mwingiliano kati ya unyanyasaji wa kijinsia na utamaduni wa kienyeji, na kuelewa jinsi masuala haya yanavyoweza kuathiri mawasiliano na wale wanaohojiwa.
- Kuelewa vizuri na kwa undani mada ya unyanyasaji wa kijinsia na misamiati yake, ikiwa ni pamoja na maneno na tafsida, yaani maneno ya staha ambayo yanaweza kutumika ili kuelezea unyanyasaji wa kijinsia katika maeneo yanayohusika.
- Kutumia maneno ya aliyenusurika/shahidi na anayehoji tu; na sio maneno yake yeye mwenyewe wakati wa mahojiano.
- Kuwa makini kuhusu mahitaji ya watu na uwezo wa watoto – ikiwa ni pamoja na kufanya mafunzo kuhusu mbinu za kufanya kazi na watoto hasa kuhusiana na matatizo yao ya mawasiliano.
- Onyesha imani kwa wengine lakini sio kuhurumia, kushtuka au kuhukumu.

35 Lengo la MARA ni kuhakikisha utaratibu mzuri wa ukusanyaji taarifa kwa wakati, usahihi, kwa kuaminika na kwa malengo, juu ya migogoro inayohusiana na unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya wanawake, wanaume na watoto katika hali zote zinazoleta wasiwasi. Taarifa zilizokusanywa kupitia MARA hutumika kukuza hatua kwa wakati ili kuzuia na kukabiliana na migogoro inayohusiana na unyanyasaji wa kijinsia. Angalia Mwongozo huu: Implementation of Security Council Resolution 1960 (2010) on Women, Peace and Security (Conflict-related Sexual Violence) - (Migogoro inayohusiana na Unyanyasaji wa Kijinsia).

- Fahamu kwa makini kuwepo kwao kunavyoweza kuathiri walionusurika/mashahidi, na kuwa waangalifu wanapoingia, wanapozunguka ndani ya chumba na kukaa ili wasiwatishe au kuwaogopesha walionusurika/mashahidi.

Mkalimani anatakiwa *asifanye* hivi:

- Asibadilishane maneno yoyote kuhusiana na taarifa zilizotolewa na aliyenusurika/shahidi mwengine zaidi ya wale wanaoongelewa moja kwa moja na mtendaji. Mkalimani hahusiki na mazungumzo, lakini yeye ni njia muhimu ya mawasiliano kati ya mhojaji na mhojiwa. Maneno yanayosemwa kati ya mkalimani na aliyenusurika/shahidi yawe machache na yasiyo na kutilia maana, kama vile wapi kukaa na mazungumzo ya kirafiki na kijamii, na pia yazungumzwe tu wakati wa mapumziko katika mchakato wa mahojiano.
- Kueleza kitu chochote kwa aliyenusurika/shahidi au mhojaji, isipokuwa kama umeelekezwa waziwazi kufanya hivyo na mtendaji.
- Kubadili maneno ya mtu yeyote. Kama aliyenusurika/shahidi anatumia maneno ya staha au kupunguza makali, mkalimani unapaswa kutumia neno hilo hilo kwa mtendaji na kumwarifu kwamba hili linaweza kuwa na maana nyingine ili mtendaji aweze kuuliza maswali ya ufafanuzi.
- kuacha au kutoa sehemu ya mahojiano ambayo kwa maoni yake hayana umuhimu.
- Pendekeza jinsi ya kufanya mahojiano.

**Wakati wa kuchagua wakalimani**

- Weka fungu la kutosha la pesa na rasilimali ya watu ili kupata na kuajiri wakalimani waliosomea na wanaojitegemea. Mara nyingi watu kama hawa hawapatikani kirahisi.
- Usitumie ndugu ndani ya familia kama wakalimani kwa sababu ya kutunza siri. Kwa sababu hiyo hiyo, wakalimani watoke katika jamii ya walionusurika/mashahidi pindipo tu, hakuna njia nyingine yoyote ile – hii ni hasa kama jamii ni za wenyeji wenyewe.
- Kuchukua muda ili kutathmini uwezo wa wakalimani. Kuhakiki wakalimani ili kuona historia yao ya uhalifu, uadilifu, uaminifu, uwezo wao kwa nafasi hiyo ya kazi, uhusiano wao na uwezo wao wa kufanya kazi na watoto.
- Tambua kwamba jinsia ya mkalimani, umri, utambulisho na kabila, uhusiano wake wa kitamaduni na kisiasa pia unaweza kuwa sababu ya kuathiri jinsi aliyenusurika/shahidi atakavyoweza kumwaamini, lakini kuwa makini unapoangalia mambo kama haya ili usiendeleze ubaguzi wenye taswira potovu au itikadi za kubagua.
- Tathmini maoni binafsi ya mgombea kuhusu unyanyasaji wa kijinsia na usawa wa kijinsia kabla ya kumwaajiri. Hakikisha kwamba anafahamu misamiati ya unyanyasaji wa kijinsia ili atakahisi dhiki (mfano kwa kusikitika, kushtuka) asiathiri vibaya mchakato wa kukusanya ushahidi.
- Inapowezekana weka wakalimani wanawake na wanaume katika timu.
- Unapowahoji watoto, tumia wakalimani ambao wamepitia mafunzo na wana mazoea ya kufanya kazi na watoto.

SEHEMU II:
Nyaraka katika Matumizi



### 4.3 Kuandaa taarifa

Jinsi taarifa zinavyokusanywa, andaliwa na hifadhiwa ni sehemu muhimu ya kutayarisha nyaraka na inahitaji kufikiriwa vizuri kabisa tangu kabla ya mazoezi yoyote ya utayarishwaji wa nyaraka. Itakuwa bora kama msingi wa data wa kielektroniki utatumiwa, na utajazwa taarifa zote zitakazokusanywa. Hizo data zinaweza kuunganishwa kwa ndani, na katika kiwango cha chini, kuwa na taarifa zifuatazo **(pia angalia kipengele cha 9, "Kuhifadhi Taarifa")**:

- Data binafsi kuhusu kila aliyenusurika/shahidi atakayehojiwa.
- Wasiwasi wa usalama kwa kila aliyenusurika/shahidi atakayehojiwa.
- Ushahidi wa ridhaa kamili kushiriki katika mahojiano.
- Ushahidi binafsi wa taarifa zitakazotolewa na huyo aliyenusurika/shahidi.
- Taarifa za nyaraka zitakazotolewa na huyo aliyenusurika/shahidi.
- Taarifa kuhusu kuwepo kwa rekodi za matibabu au za polisi.
- Taarifa za picha au za kuona na kusikia kuhusiana na aliyenusurika/shahidi.
- Kama itawezekana, tafsiri ya yoyote kati ya yaliyotajwa hapo juu.

Kama itawezekana, msingi wa data uwe umeendelea kiasi kwamba data zinaweza kutafutwa kufuatana na vigezo tofauti.

## 5. Kutambua walionusurika na mashahidi wengineo

Wakati mwingine, kuwatambua walionusurika au mashahidi wengineo wa unyanyasaji wa kijinsia huweza kuwa vigumu zaidi kuliko kuwatambua walionusurika na mashahidi wengineo wa hatia nyingine chini ya sheria ya kimataifa. Hata sehemu ambapo hadithi fupi fupi za michapo mingi zimetengenezwa, walionusurika na mashahidi wengine wanaweza kutokutaka kujipeleka mbele rasmi kutokana na sababu tofauti. Walionusurika wanaweza wasitake kujiathirisha kwa kupata kumbukumbu za trauma/kiwewe walichopata kuhusiana na unyanyasaji wa kijinsia, kufikiri kwamba unyanyasaji wa kijinsia ulikuwa ni kosa lao, au kufikiri kwamba hakuna mtu atakayewaamini kwa sababu hawana ushahidi thabit. Kutegemea na mazingira ya jamii na kitamaduni au desturi, walionusurika na unyanyasaji wa kijinsia wanaweza kuwa hatarini, au kufanyiwa hila, ndani ya jamii zao. Hii huweza kuwa kutoka kwa wanajumuiya wa kundi la watuhumiwa ambao wapo karibu, au hata kutoka ndani ya jamii yao wenyewe au familia, ambao wanaweza kuwa na tabia ya kuwashtaki, kuwafanya wahisi aibu, kuwaadhibu, au kutumia unyanyasaji wa kijinsia kama sababu ya kuwatenganisha walionusurika kutoka katika nyumba zao, familia zao, maisha yao na nafasi za kupata elimu. Walionusurika wanaweza kutaka, lakini kushindwa, kuongea. Wengine wanaweza kuwa na matatizo fulani kama wana ulemavu wa akili au mwili.

Ni muhimu kuunda mazingira yanayosaidia na yaliyo salama ambamo walionusurika na mashahidi wanajihisi kuwa salama kama watajitosa na kuripoti uhalifu. Kama mipango ya kuwafikia jamii inashauriwa, fahamu kiwango gani kinatakiwa kabla ya kupokea taarifa kuhusu kesi za unyanyasaji wa kijinsia katika jamii yoyote. Zaidi ya hapo, watendaji wakumbuke kwamba taarifa muhimu kuhusu unyanyasaji wa kijinsia zinaweza kukusanywa kutoka katika vyanzo vingi, sio walionusurika/mashahidi tu. **(Angalia Kipengele cha 6, "Ushahidi".)**

## 5.1 Kutambua moja kwa moja

Walionusurika na mashahidi wengine watajitokeza wakati mwingine na kupendekeza kutoa ushahidi kwa hiari yao wenyewe. Watendaji wawe tayari kujibu haraka, kwa ufanisi na kwa usalama kama jambo hili litatokea. Utafiti mwingi, tathmini za athari na mipango iwe tayari kabla ya watendaji kujishirikisha na walionusurika/mashahidi.

Wakati mwingine walionusurika hutambulika moja kwa moja kutokana na tathmini, vifaa vya uchunguzi na tafiti zingine. Kama itakuwa hivi, ni muhimu kwamba maombi yoyote yatakayofanywa kwa walionusurika/mashahidi yawe na uhusiano wa moja kwa moja na matakwa yaliyo wazi na yenye upendeleo watakayokuwa walionyesha pale walipokubali kujumuika katika kufanya tathmini. Hii ni pamoja na maombi yoyote kuhusu majina kufichwa au hatua za usalama ambazo lazima zichukuliwe kabla maombi kufanywa.

**Kuwatambua watoto** Tahadhari kubwa inatakiwa pale watoto walionusurika na walio mashahidi wanapojongelewa – kama watendaji hawana uhakika wa kuweza kuwajongelea watoto inavyotakiwa, hawawezi kuhakikisha kwamba watoto wataweza kutumwa kwingine kama inavyotakiwa, au hawafahamu jinsi ya kupata rasilimali za kuwasaidia watoto wakati wa mgogoro, wasijaribu kuwajongelea watoto hawa. Watendaji wanatakiwa pia wafahamu kwamba kama watakutana na watoto ambao wao wanafikiri kuwa wamedhuriwa basi ni lazima kutoa taarifa kuhusu jambo hili kwa mamlaka yanayohusika.

Katika zile kesi ambapo unyanyasaji wa kijinsia umefanywa na watoto wanaohusika na makundi yenye silaha au majeshi, ni lazima watendaji wakumbuke kwamba watoto wanaofanya matendo ya ngono ambayo ni unyanyasaji wa jinsia hutumiwa kihila au hulazimishwa kufanya matendo hayo na huwa waathirika wao wenyewe. Watoto wachukuliwe kama walionusurika/mashahidi na sio kama watuhumiwa, hii ni kutokana na Miongozo ya Umoja wa Mataifa kuhusu Masuala ya Haki Yanayowashirikisha Waathirika Watoto na Watoto ambao ni Mashahidi wa Uhalifu[36] na Mkataba wa Haki za Watoto wa Umoja wa Mataifa.[37]

## 5.2 Wasuluhishi

Wasuluhishi ni watu ambao watendaji wanaweza kuwaita ili kuwasaidia kutambua na kuwasiliana na wanajumuiya wa hiyo jamii waweze kuondokana na vipingamizi vya kitamaduni na kijamii, na kutambua wale ambao wanaweza kuwa wamenusurika na mashahidi wengine. Wasuluhishi wanaweza kutumiwa pale mtendaji anapokuwa hana uzoefu wa jamii na wanajumuiya na mienendo ya jamii hiyo, ambapo walionusurika na mashahidi wengine wanaweza kuwa hatarini kama wakiwafuata watendaji moja kwa moja au pale ambapo walionusurika na mashahidi wengine wana hofu kuhusu kujumuika na watu wanaotoka nje ya jumuiya.

Wasuluhishi wanaweza kuwa wazungumzaji wafanisi mno wa jamii, ingawa ni lazima uangalifu uchukuliwe ili kuhakikisha kwamba hawana upendeleo. Mara nyingi huwa wanachama wa mashirika ya ngazi za chini, mashirika ya kitaifa na kimataifa ambayo si ya kiserikali (NGOs), watoa huduma, na mitandao mingine ya kijamii na vyombo vya msaada mathalan makanisa na makundi ya wanawake.

Kabla ya kujaribu kuwatambua walionusurika na mashahidi wengine kwa kupitia wasuluhishi, watendaji wanatakiwa kufanya yafuatayo:

- Kupata taarifa kuhusu wahusika waliokuwapo ndani ya jamii wakimzingira aliyenusurika/shahidi ili kumwezesha mtendaji kuchagua wasuluhishi sahihi. Hii ni pamoja na kupanga

36 UNICEF, UNODC, Guidelines on Justice Matters Involving Child Victims and Child Witnesses of Crime, 2005 (Miongozo ya juu ya Masuala ya Haki Yanayowashirikisha Watoto Waathirika na Watoto Mashahidi wa Uhalifu). Kwa makala rasmi ya mwongozo wa Umoja wa Mataifa angalia – Economic and Social Council resolution 2005/20 of 22 July 2005. (Azimio la Baraza la uchumi na Kijamii) Toleo la hapo juu, ambalo limekuwa linatolewa na UNICEF na UNODC kwa msaada wa Kituo cha Utafiti cha Innocenti na IBCR, limekusudiwa kama mwongozo kwa ajili ya watoto na wataalamu wa mtoto na sio hati rasmi ya Umoja wa Mataifa.

37 Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, Mkataba wa Haki za Mtoto, Novemba 20, 1989.

uongozi wa jamii, ikijumlisha uongozi wa wanawake ndani ya jamii (mfano wazee, wakunga, walimu, machifu wa kijiji ambao ni wanawake au viongozi wa dini wanawake). Kila jamii ina muundo wa uongozi na kila jamii ya wanawake itakuwa na kiongozi au viongozi ambao watamsaidia au kumzuia mtendaji kwenye kuwapata walionusurika/mashahidi. Mara nyingi uongozi wa wanawake utatumika kutoa msaada kwenye kazi inayofanywa na timu, lakini hii ni kama timu inafanya kazi kimaadili, kwa heshima na kwa uwazi.

- Unapojaribu kuwatambua hasa wanaume walionusurika, tafuta wasuluhishi wanaofaa – kwa mfano wanachama wa mashirika ya vyama vya kiraia ambao wanafanya kazi na wanaume tu- pia ufahamu mitazamo maalum ya kitamaduni hisia zinazozingira unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya wanaume.

- Tathmini kwa makini kama ni kweli au si kweli kwamba kuwatafuta walionusurika na mashahidi wengine kwa kupitia wasuluhishi kutawaweka hatarini walionusurika na mashahidi wengine, watu binafsi ambao ni wanajumuiya wa jamii au mashirika. Tathmini, hasa, kama ni kweli au si kweli kwamba wasuluhishi wanalazimisha kushiriki au wanawafichua walionusurika na hawana matendo yanayoendana na maadili ya kiwango cha msingi.

- Hakikisha kwamba wasuluhishi wanalipa kipau mbele zoezi la kuwatambua watoto zaidi, hasa wale ambao wamo katika makundi ya walio kwenye mazingira magumu kama vile watoto walio peke yao na wasio na makazi, na watoto wanaohusika na makundi yenye silaha au majeshi.

- Fahamu migawanyiko yoyote katika jamii, na kama wanachama wa 'makundi' pingamizi wanaishi pamoja katika jamii hiyo hiyo.

- Kama itaonekana kuwa salama, fanya kazi pamoja na wanajumuiya wa jamii, viongozi wa jamii, watoa huduma za matibabu na makundi ya msaada na taasisi za kusaidia kuwatambua walionusurika na mashahidi wengine.

- Jiunganishe na mashirika ya wenyeji na anzisha miradi ya kuwawezesha walionusurika na mashahidi wengine kujitokeza, ikiwa ni pamoja na kuendeleza majukwaa ya wanawake ili kuwawezesha, kuwa na nafasi zenye usalama, siri na hatua zingine.

- Kuhakiki wasuluhishi wowote wanaoweza kufaa (kwa kuona rekodi za uhalifu, uadilifu, uaminifu, uwezo wao kwa nafasi hiyo ya kazi, uhusiano wao na uwezo wao wa kufanya kazi).

- Kufanya uangalifu ili watendaji wenyewe na wasuluhishi wowote wasionekane kwamba wanatoa kitu chochote ambacho kina thamani ili kupata ushahidi, ikiwa ni pamoja na kutoa msaada wa kifedha au vitu au kurahisisha uwezo wa kupata msaada. Hata hivyo, jambo hili halizuii kutambulishwa kwa rufaa kwenye huduma zingine, jambo ambalo lifanywe kila itakapowezekana **(angaliae Nyongeza 5, "Kuwapeleka Rufaa Walionusurika kutokana na Unyanyasaji wa Kijinsia ili kupata Msaada")**.

- Kuweka wazi kwa wasuluhishi kuhusu matarajio ya majukumu yao, mipaka, na pia kiwango cha msaada na mwongozo ambao wataupata kutoka kwa watendaji.

- Kuhakikisha kwamba wasuluhishi wowote wana njia yenye kuaminika ya kuwasiliana na watendaji.

- Kutayarisha nyaraka za miingiliano yao na watendaji ili waweze kutetea maamuzi yoyote waliyoyafanya kuhusu wasuluhishi.

- Kumbuka kuhakikisha kwamba wasuluhishi hawajihusishi na uchunguzi kwa kupindukia mamlaka ya majukumu yao na uwezo wao.

- Komesha kiasi cha taarifa ambacho msuluhishi yeyote anapewa kuhusu aina za walionusurika/mashahidi ambao mtendaji anatafuta.

- Epuka kuwaruhusu wasuluhishi wowote kuwafundisha walionusurika/mashahidi wowote ambao hao wasuluhishi wamewatambua.

## 6. Ushahidi

Mara nyingi ushahidi kutoka kwa walionusurika/mashahidi huwa ni aina ya taarifa ambayo hupatikana kirahisi sana kwa watendaji, lakini pia huwa ni ile aina ambayo inatakiwa kushughulikiwa kwa uangalifu zaidi. Walionusurika/mashahidi wanaweza kutoa taarifa muhimu sana kwa watendaji kuhusu mashambulizi yenyewe – hii ni kwa uzoefu wao wenyewe, au kwa kuangalia – lakini wanaweza pia kutoa taarifa kuhusu vipengele vinavyohusika na mazingira ya mashambulizi na watuhumiwa na pia njia zao za kushiriki katika matendo ya jinai yaliyoonekana. Mashahidi wa "kiujumla" kama vile madaktari, wauguzi, watoa ushauri na viongozi wenyeji ambao wanaweza kuwa na taarifa kuhusu kuwepo kwa walionusurika/mashahidi wengi, muda na sehemu ya matendo ni mambo muhimu sana ili kufahamu vipengele vya uhalifu.

Ushahidi unaweza kutoka:

- Walionusurika/mashahidi wenyewe wa unyanyasaji wa jinsia.

- Wanafamilia, wanajumuiya, watoa huduma, wasaidizi wa mashirika, watu wa ndani ambao walishuhudia au wanafahamu kuhusu mashambulizi kwa kupitia, kwa mfano, kushuhudia shambulizi, kusikia kuhusu shambulizi kutoka kwa walionusurika/mashahidi, au kuwatibu walionusurika/mashahidi baada ya shambulizi.

- Wanafamilia, wanajumuiya, watoa huduma na wasaidizi wa mashirika, wanaoweza kutoa taarifa kuhusu hali ilivyokuwa wakati wa ushambulizi, kutumwa kwa kufanyika mashambulizi haya ambako kunaendelea, kumesambaa au kunafanywa kwa makusudi, sehemu na aina ya ushuhuda wa zaidi, wanaoshutumiwa kuwa watuhumiwa, muundo wa utawala, asili na aina ya mashambulizi, mazingira ya kisiasa na mahusiano ya ndani ya kimamlaka.

- Walio ndani na wanachama wa zamani wa majeshi au makundi yenye silaha, wanaoweza kutoa taarifa kuhusu mazingira ya mashambulizi, kutumwa kwa kufanyika mashambulizi haya ambako kunaendelea, kumesambaa au kunafanywa kwa makusudi, sehemu na aina ya ushuhuda wa zaidi, wanaoshutumiwa kuwa watuhumiwa, muundo wa utawala, asili na aina ya mashambulizi, mazingira ya kisiasa na mahusiano ya ndani ya kimamlaka. Wahusika walioshirikiana na watuhumiwa ambao wanajuta, mara nyingi hutoa ushahidi muhimu zaidi unaojiunganisha moja kwa moja kwa wahalifu - lakini kuwakaribia mashahidi walio ndani ni kitu ambacho lazima kifanyike kwa uangalifu mkubwa na kifanywe na wapelelezi ambao wamefanya mafunzo.

Zaidi ya hilo, watendaji na wasuluhishi wanatakiwa kuwatafuta walionusurika/mashahidi ambao wana taarifa inayohusika na tendo lenyewe lakini pia wale watu ambao wanaweza kusaidia kutoa ushahidi wa kimazingira wa hatia hiyo, au kutambua watuhumiwa na mifumo ya dhima. Watuhumiwa wafahamu kwamba taarifa muhimu inaweza kutoka kwa:

- wanajumuiya wote wa jamii, na si wale wanaosikika zaidi, maarufu zaidi, wenye elimu zaidi, wanaosema zaidi au wale ambao ni viongozi kwa kawaida: na

- ukivuka jamii yenyewe na kuendelea hadi kwa wanachama wa shirika wanofanya kazi katika eneo, ambao wanaweza kuwa walishuhudia matukio yenyewe au wana taarifa ambayo itasaidia katika kutayarisha nyaraka.

## 6.1 Ridhaa kamili

Kuchunguza kanuni ya 'ridhaa kamili' ni muhimu pale unapokusanya taarifa kuhusu unyanyasaji wa kijinsia, bila ya kujali asili ya taarifa zilizopatikana. Ni lazima walionusurika wote na mashahidi kukubali kufanyiwa mahojiano na kuchunguzwa, kupigwa picha, kutoa taarifa zao ili zirekodiwe, kutambulishwa kwa rufaa kwenye huduma yoyote ya msaada, na kwa taarifa zinazowahusu na njia za kuwasiliana nao, kuonyeshwa wahusika wengine.

Kupata ridhaa kamili kabla ya kutayarisha nyaraka za taarifa za ushahidi kunahakikisha kwamba aliyenusurika/shahidi anadhibiti mamlaka ya uzoefu wake mwenyewe, na kwamba anafahamu na anakubali kushiriki katika mchakato wa haki. Kutokupata ridhaa kamili kunavunja haki ya aliyenusurika/shahidi, inamvunjia heshima na kumletea  madhara. Matokeo ya mahojiano yaliyoendeshwa bila ya kupata ridhaa kamili yanaweza pia yasikubaliwe kwenye mahakama fulani ya kisheria, kwa misingi ya kwamba taarifa ilitolewa chini ni ya aina fulani ya kushinikizwa au kulazimishwa, au kutokana na ahadi za uongo.

Ridhaa kamilii si tu kanuni muhimu ya kujihusisha na mchakato wa haki; ni wajibu wa kimaadili kwa yeyote anayekusanya taarifa kuhusu hatia chini ya sheria ya kimataifa, ikiwa ni pamoja na uvunjwaji muovu wa haki za binadamu, kwa aliyenusurika/shahidi.

Maana ya ridhaa kamili

Ni lazima, watu wote wanaotoa taarifa kuhusu unyanyasaji wa jinsia au kukubali ukusanyaji wa data wapewe taarifa, na kuelewa:

- madhumuni na yaliyomo katika zoezi la kukusanya data;
- maana ya siri na jinsi inavyohusika, au isivyohusika, na taarifa inayotolewa;
- utaratibu utakaofuatwa – ikiwa ni pamoja na taarifa itakayotakiwa kutolewa siku zijazo, na jinsi inavyotegemewa kutumiwa; na
- athari na faida za kushiriki kwao wenyewe.

### Ili kuhakikisha ridhaa kamili inatumika, watendaji wanatakiwa kufanya hivi:

**1. Kutumia muda sahihi ili kuwafahamisha walionusurika/mashahidi mambo yote yanayohusika**

- Kutambua wanachama wa timu waliokuwapo, kazi zao, wanayemfanyia kazi na taarifa zinakusanywa kwa ajili ya nani.
- Kufahamisha kikamilifu kazi na asili ya zoezi la kukusanya taarifa, na jinsi timu ilivyo, inahusiana na nani na mamlaka yake.
- Eleza matumizi yote ya taarifa inayotolewa, ikiwa ni pamoja na uwezekano wa taarifa hii kuonyeshwa, hata kama huyo mtu ataombwa au hataombwa kutoa ushahidi kwenye mashtaka ya aina fulani.
- Fichua aina za maswali ambayo anaweza kuulizwa aliyenusurika/shahidi.

- Onyesha taarifa kwa njia ambayo ni wazi kwa aliyenusurika/shahidi na hakikisha taarifa imeeleweka. Ni vyema kwa watendaji kumwuliza aliyenusurika/shahidi arudie kuwafahamisha wao wenyewe jambo ambalo aliyenusurika/shahidi ameelewa kuhusu mchakato.

**2. Kuhakikisha kwamba ridhaa inayotolewa na aliyenusurika/shahidi imetolewa kwa misingi ya hiari yake mwenyewe.**

- Unda mazingira ya uaminifu wa kweli ambayo yatamwezesha aliyenusurika/shahidi kukubali mwenyewe na kwa kujitolea au kujihisi kuwa ana uhuru wa kukataa Mapendekezo machache kuhisi jinsi ya kujenga uaminifu yameorodheshwa kwenye **Nyongeza 3**, **"Mahojiano: Kanuni za Msingi na Vielelezo Muhimu kwa Vitendo vya Kazi"**.
- Mfahamishe kwa wazi kabisa aliyenusurika/shahidi kwamba wanalo chaguo na kuongea au kutokuongea na watendaji na kwamba chaguo hili linaweza kutumika wakati wowote katika mchakato.
- Chukulia vizuri mamlaka yako kama mtendaji na jishirikishe na ingiliana kwa heshima na aliyenusurika/shahidi.
- Hakikisha kwamba aliyenusurika/shahidi anao muda wa kutosha ili kufanya uamuzi. Hii iangalie pia madhara makubwa na yenye utata kwa walionusurika, familia zao na jamii kushiriki, hivi sasa na kwa muda ujao. Pia itambue changamoto ya kuhitaji kutathmini athari wakati wa mazingira magumu na ndani ya mazingira ya mfarakano yanayobadilika kwa haraka.
- Kila unapowasiliana na aliyenusurika/shahidi, hakikisha kwamba hajabadili mawazo kuhusu kutumia kauli zake au taarifa hizi kupewa mashirika mengine husika.
- Chagua lugha ambayo inaeleweka kirahisi na aliyenusurika/shahidi, na hasa toa fomu zozote katika lugha ya aliyenusurika/shahidi.
- Tumia wakalimani ambao wana uwezo kwa kutafsiri neno-kwa-neno na hakikisha kwamba wanaelewa kabisa maana na mahitaji ya ridhaa kamili.

**3. Pata ridhaa iliyo wazi kwa shughuli maalum**

- Ridhaa itolewe kwa matumizi ya vyombo kama vile mashine ya kurekodi au kamera ya video wakati wa mahojiano. Hakikisha kwamba aliyenusurika/shahidi anajua kwamba unamrekodi kwa kutumia chombo cha kupokonya sauti au video.
- Walionusurika/mashahidi wanatakiwa kukubali wenyewe kuhusu uhamisho wa utambulisho, mawasiliano na taarifa nyingi kupelekwa kwenye mashirika mengine yanayohusika, hasa kwa wachunguzi wa kitaifa au kimataifa au mashirika, mahakama na polisi.

**4. Wakati wa kuhoji watoto, hakikisha ridhaa imepatikana ipasavyo**

- Ni lazima watoto wote wakubali kwa kuidhinisha kushiriki katika uchunguzi.
- Fahamu kwamba ni lazima kupata ridhaa kamili kufanywe na umri maalum wa mtoto, mahitaji yake na kiwango cha uelewa wake kiakili. Kwa mfano, kwa wale wenye umri ulio chini ya miaka 18, kwa kawaida ridhaa kamili hupatikana kutoka kwa wazazi; hata hivyo, vijana waliobaleghe wanaweza kujitolea ridhaa kamili.

- Pata ridhaa kamili kutoka kwa wazazi au walezi ili watoto washiriki.

- Fahamu kwamba watoto wataweza au hawataweza kuwa na ujasiri wa kujileta mbele na kuongelea kinaganaga mbele ya wazazi au walezi; inawezekana kwamba watoto na walezi au wazazi hawakufahamu kwamba mtoto alinyanyaswa kwa kutumia ngono hadi pale mtendaji anapowafuata.

- Watoto watahadharishwe kuhusu athari zinazohusiana na kutoa taarifa kwa njia ya makini, namna inayojali umri ili kutokuwatisha bure. Inashauriwa kufanywa maongezi binafsi pamoja na walezi au wazazi bila ya kuwepo mtoto kabla ya kuanza mahojiano yoyote na mtoto.

- Ni lazima watoto wapewe chaguo zote na matokeo yanayoweza kutokea kutokana na chaguo, na waajiriwa waliofanya mafunzo ambao wanaweza kushughulikia uwezo tofauti wa mtoto. Watoto wana haki ya kuambiwa haki zilizokuwepo kwa ajili yao chini ya Mkataba wa Haki za Watoto wa Umoja wa Mataifa na Azimio la Kanuni za Msingi za Haki kwa Waathirika wa Uhalifu na Matumizi Mabaya ya Mamlaka.[38] Watendaji wafahamishe kwa makini kwa watoto kinachotokea katika kila hatua ya mchakato na jambo gani linategemewa kutoka kwao.

## 6.2 Siri

Siri ni kanuni ya kimaadili kwenye kutayarisha nyaraka zinazohitaji watendaji walinde taarifa wanazokusanya kuhusu unyanyasaji wa kijinsia, na kutumia kanuni hiyo wakati wa zoezi zima la kutayarisha nyaraka. Masharti ya siri ni muhimu ili kujenga uaminifu na aliyenusurika/shahidi; hata hivyo kuna mipaka ya siri na ni lazima mipaka hii ifahamishwe kwa aliyenusurika/shahidi.

Hasa, watendaji wanatakiwa kufanya yafuatayo:

**1.** Kuhakikisha kwamba wanachama wote wa timu wanaelewa na wanatumia vigezo vya siri vilivyowekwa wakati wa zoezi la kutayarisha nyaraka, na hawazungumzii habari zote kuhusu kesi na familia, marafiki au wafanyakazi wenzao ambao hawamo kwenye timu.

**2.** Kuhakikisha hatua za kulinda taarifa zipo kuhusiana na utambuaji wa taarifa kuhusu aliyenusurika/shahidi na ushahidi wao, pia chaguo la kupewa rufaa litakalotumika au hatua za kulinda zitakazowekwa **(angalia kipengele cha 9, "Kuhifadhi taarifa").**

**3.** Kuwafahamisha walionusurika/mashahidi kinagaubaga kuhusu masharti na mipaka ya siri; hii ina maana kwamba:

- Kuna hatua gani za siri ambazo zimewekwa, kama zipo, na ni vipi taarifa zinazowahusu zitalindwa?

- Mipaka ya siri ambayo inaweza kuhakikishwa na wale wanaokusanya taarifa – ikiwa ni pamoja na tofauti kati ya hatua za vitendo zinazowezesha taarifa kuwa za siri na kushindwa kuhakikisha kuwepo kwa siri kama haki ya kisheria.

- Jinsi gani siri inaweza kuvunjwa, ikiwa kutajitokeza hatari ya aliyenusurika/shahidi kujiua au kujiumiza binafsi au suala la ulinzi wa watoto.

38 Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, Azimio la Kanuni za Msingi za Haki kwa Waathirika wa Uhalifu na Matumizi Mabaya ya Mamlaka: azimio limepitishwa na Baraza Kuu tarehe 29 Novemba 1985. (UN General Assembly, Declaration of Basic Principles of Justice for Victims of Crime and Abuse of Power: resolution adopted by the General Assembly).

- Mipaka ya siri ikiwa ni pamoja na njia maalum ambazo taarifa yake inaweza kufichuliwa kama aliyenusurika/shahidi ataridhia kwa taarifa iliyopatikana kutumwa kwa mashirika mengine husika, ikiwa ni pamoja na polisi, wapelelezi na mahakama **(angalia kipengele cha 6.1, "Ridhaa kamili")**.

## 6.3 Rufaa

Kabla ya kuanza mchakato wa kutayarisha nyaraka, watendaji wanatakiwa kujitahidi kutambua chaguo kwa ajili ya kuwatambulisha kwa ajili ya rufaa walionusurika/mashahidi ili kupata msaada, na kutayarisha taratibu kwa mchakato wenyewe wa kufanyiwa rufaa. Walionusurika/mashahidi wanaokutana nao wanaweza kuwa wahahitaji msaada wa haraka wa kimatibabu, msaada wa kijamii unaohusika na saikolojia au usalama, au wanaweza kukuta kwamba mchakato wenyewe wa kufichua taarifa ni mzito kihisia, unaleta trauma/kiwewe au unawaweka kwenye hatari. Walionusurika wote na mashahidi wana haki ya kujua huduma gani za kiafya, kisaikolojia, kisheria na kijamii wanaweza kupata kabla ya kuhojiwa.

Kama huduma rasmi hazipatikani au hazifikiki, watendaji watathmini mifumo isiyo rasmi ambayo ipo na ambayo inaweza kuwa msaada kwa aliyenusurka/shahidi, ikiwa ni pamoja na mifumo ya msaada wa kifamilia na kijamii. Ni lazima aina hizi za msaada wa kifamilia na kijamii zifikiriwe pale watoto walonusurika na mashahidi wanapotambuliwa.

Watendaji watambue kwamba uwezo wa aliyenusurika/shahidi kupata huduma za kutambulishwa kwa rufaa na msaada zinaweza kutegemea jinsia yao – wakati mwingine walioathirika wanaume na wanaweke hufanyiwa matendo tofauti pale wanapotafuta msaada. Watendaji wanatakiwa pia wafahamu kwamba kama watakutana na watoto ambao wao wanafikiri kuwa wamedhuriwa basi ni lazima kutoa taarifa kuhusu jambo hili kwa mamlaka yanayohusika.

Aina ya msaada unaoweza kuwepo kwa walionusurika/mashahidi imeelezewa katika **Nyongeza 5, "Kuwapeleka Rufaa Walionusurika kutokana na Unyanyasaji wa Kijinsia ili kupata Msaada"**. Unapotaka kuwapeleka rufaa walionusurika na mashahidi ili kupata msaada zaidi, watendaji wanatakiwa:

1. **Kutambua kama kuna mifumo imara ya rufaa ambayo ipo. Hii inaweza kuwa ni pamoja na:**

- taratibu za rufaa za kitaifa, wilaya au kienyeji zinazohusu unyanyasaji unaohusina na jinsia kati ya mashirika ya misaada ya kimataifa na kitaifa;
- njia za kupelekea rufaa watoto wanaoweza kudhuriwa, ikiwa ni pamoja na viongozi wa jamii wasio rasmi na watu wenye majukumu maalum, makundi yanayoongozwa na watoto, na msaada maalum unaolengea trauma/kiwewe;
- taratibu za kitaifa kuhusiana na kesi za unyanyasaji wa kijinsia;
- namba za simu za vituo vya msaada au namba ya simu ya moja kwa moja kwa wakuu wahusika kwa aliyenusurika/shahidi; na
- huduma ya msaada wa mkusanyiko wa sekta mbalimbali uliopo kwa ajili ya rufaa zinazohusiana na shambulio linalotumia ngono vituo/"duka moja kwa mahitaji yote".

2. **Endeleza uhusiano na huduma za msaada:**

- Tayarisha mikataba, utaratibu wa kiwango cha uendeshaji na maandiko ya kukumbushia makubaliano na watoa huduma ili kurahisisha ufanisi wa rufaa.

- Kuwa makini kuhusu mipaka ya ugavi na usafirishaji, kifedha na kimaadili kwa mashirika yanayotoa huduma za msaada kwa walionusurika/mashahidi na upangilie ipasavyo.

**3. Tathmini usalama na uwezekano wa kupata huduma za msaada:**

- Amua mipaka ya uwezo wako wa kutambulisha kwa rufaa ipasavyo, na kama hili litaathiri uwezo wako wa kushirikina na walionusurika/mashahidi. Mapungufu yanaweza kujumlishae:

  *Mipaka ya Usalama:*

  - Je kuwapeleka walionusurika/mashahidi kwenye huduma ya msaada kutakuweka kwenye hatari zaidi? Kwa mfano, kunaweza kuwa na matatizo ambapo huduma za afya na usalama zinaletwa na serikali au ambapo taarifa hazizingatiwi kwa viwango vya siri.
  - Je makundi ya jamii au watu wenye majukumu maalum watawasaidia walionusurika na mashahidi au watawalazimisha kufanya matendo dhidi ya matwakwa yao?

  *Mipaka ya kiusafiri na kifedha:*

  - Je huduma za msaada zipo mbali mno au labla ni mbali kwa walionusurika/mashahidi kuzifikia?

  *Mipaka mingine, kama vile imani za kitamaduni zenye ubaguzi na mitazamo ya kibaguzi:*

  - Je kuna imani za kitamaduni zilizoshamiri, kama vile ubaguzi wenye taswira potovu au sera, ambazo zinazuia kumtambulisha kwa ajili ya rufaa aliyenusurika/shahidi ili kupata huduma zilizo kwenye eneo alipo?

**4. Kutekeleza taratibu za viwango vya kazi kwa kuwapeleka rufaa walionusurika/ mashahidi:**

- Fahamu vigezo vitakavyoonyesha:
  - Watendaji watamtambulisha nani ili kupata msaada zaidi – hii ni pamoja na walionusurika/mashahidi, wanafamilia au jamii kwa ujumla.
  - Kwa nini watendaji wafanye hiyo rufaa.
  - Aina gani za huduma watendaji watamtambulisha mtu kwa rufaa.
- Tambua kuna sera gani kuhusu kuwasafirisha walionusurika/mashahidi.
- Fahamu jinsi ambavyo rufaa itafanywa – katika hatua gani ya kutayarisha nyaraka na kufanya mchakato wa mahojiano.

**5. Wasiliana wazi wazi na walionusurika/mashahidi:**

- Fahamisha wazi kwa walionusurika/mashahidi mipaka ya msaada ambao unaweza kutolewa.
- Wasilisha kikamilifu chaguo lililokuwepo kwa aliyenusurika/shahidi.
- Fahamisha kwamba msaada hautegemei kuwepo kwa ushahidi, na pia si lazima kwa ushahidi kutolewa kwa njia fulani ili kupata msaada.

**6. Wakati wanaposhughulika na watoto walionusurika na mashahidi, ni lazima watendaji wahakikishe kwamba watoto wanatambulishwa kwa rufaa ya huduma zitakazohitajika.**

- Elewa kwamba ni lazima mahitaji ya muda mrefu ya watoto yashughulikiwe ili kuhakikisha usalama wa mtoto kimwili na kihisia, bila ya kujali uamuzi wa mtoto wa kutoa ushahidi. Mahitaji ya muda mrefu yanajumlisha:
  - Kimwili: Baada ya kupelekwa rufaa kwa matibabu ya dharura, watoto wanaweza kuwa na matatizo ya muda mrefu ya afya na watahitaji matibabu ya ufanisi.
  - Kisaikolojia: Watoto wanaweza kuhitaji msaada ili kukabiliana na dhiki ya baada ya trauma/kiwewe na katika kujenga mahusiano ya kuaminiana na kufahamu hisia zao.
  - Jamii: Watoto wanaweza kuhitaji msaada ili kuwafungamanisha tena kwenye shule na kuwasaidia kuwa na mahusiano mazuri.
  - Mipango ya utunzaji: Watoto wanahitaji sehemu salama ili kupata nafuu kupona kama unyanyasaji ulitokea nyumbani.
- Ikiwa ni pamoja na kuelezewa kwa kina kwa chaguo la rufaa ndani ya **Nyongeza 5**, **"Kuwapeleka Rufaa Walionusurika kutokana na Unyanyasaji wa Kijinsia ili kupata Msaada"**, pia huduma za rufaa kwa watoto zinahitaji kufanya hivi:
  - weka bayana umri na jinsia ya mtoto aliyeathiriwa;
  - toa fursa ya kupata nafasi kwenye sehemu ambazo zinakubaliana na watoto na vijana; na
  - toa fursa kwa mifumo ya kulinda watoto iliyo kwenye jamii, ikiwa ni pamoja na kamati za kulinda watoto na makundi yanayoongozwa na watoto.
- Pale watoto wanapokuwa hatarini kutokana na kupungua au kutokuwepo kwa msaada wa kijamii, fanya utambulisho wa rufaa unaofaa, hii ni pamoja na hatari ya watoto kutengwa na familia na kupitia kutengwa na jamii.
- Weka mazoea wazi kuhusu kupeana taarifa za siri ili kuhakikisha kwamba maslahi bora ya watoto yanapewa kipaumbele.
- Kuwasaidia wazazi na walezi, kuwaarifu kuhusu huduma zilizokuwepo za kumsaidia mtoto na familia.

## 7. Mahojiano

Walionusurika na mashahidi wengine wakishatambuliwa, kuwahoji ndiyo njia iliyozoelewa na mara nyingi huwa ndiyo njia yenye kufaa zaidi kukusanya taarifa, lakini pia ndiyo njia ambayo inaweza kuwaumiza zaidi, kuwaweka kwenye hatari zaidi, na kama haijafanywa vizuri, inaweza kuathiri ubora na utegemevu wa taarifa iliyotolewa.

Wakati mwingine, kuwafanyia mahojiano walionusurika/mashahidi si lazima na wala haipendekezwi, na inabidi watendaji waweze kuhalalisha kwa wazi kuhitajika kufanya hivyo.

Kama wanafanya mahojiano, ni lazima watendaji wawe na mafunzo yanayofaa ili kuyafanya mahojiano, wawe na uzoefu maalum wa kuwahoji walionusurika/mashahidi wa unyanyasaji wa kijinsia. Wakati wanapowahoji hasa watoto, ni lazima watendaji wawe wamefunzwa inavyotakiwa ili kushughulikia mahitaji binafsi na uwezo wa mtoto.



## 7.1 Mipangilio ya mahojiano

**1. Angalia mahali mahajiano yanapofanywa:**

- Fanya mahojiano kwenye mahali ambapo pana usalama, faragha, panafaa na kuna hali bora kwa aliyenusurika/shahidi.
- Tafuta kama kuna mahali ambapo hakuruhusiwi kwa sababu za dini, umuhimu wa kitamaduni, au dhana za usahihi.
- Fanya mahojiano kwenye sehemu ambapo aliyenusurika/shahidi anaweza kupafikia na pasiwe mbali sana, pia angalia hasa kama:
- Je aliyenusurika/shahidi ana uwezo wa kifedha ili kufika katika sehemu hiyo?
    - Je watendaji watatoa usafiri kuenda na kurudi kutoka katika sehemu hiyo? Kama ni hivyo, angalia jinsi gani jambo hili linaweza kuathiri usalama na faragha ya anayehojiwa.
    - Je haitakuwa hatari kwa aliyenusurika/shahidi kufika na kuondoka? Je itakuwa giza mahojiano yatakapokwisha?
- Ni lazima watendaji waepuke:
    - sehemu za umma zenye hatari ya kuwa na ufuatiliaji;
    - sehemu za umma zenye hatari ya kusikika;
    - kliniki, ofisi za wafanyakazi wa mashirika ya msaada, sehemu za jamii na vituo vya wanawake bila ya kufanya makubaliano na mipangilio tangu awali na wafanyakazi na wanajumuiya wanaoendesha sehemu hizi;
    - kuwahoji walionusurika na mashahidi wengine, mbele ya walionusurika/mashahidi, ili kuepuka maelezo kuathiriana;
    - kuwahoji walionusurika na mashahidi wengine mbele ya watu wengine ambao wanaweza kushawishi mahojiano au kuwatisha;
    - kuwahoji walionusurika na mashahidi wengine mbele ya watoto wanaoweza kuhisi shida, au wanaoweza kuongezea athari ya kukiuka sheria za siri.

**2. Fikiria kama aliyenusurika/shahidi anaweza kupata msaada:**

- Aliyenusurika/shahidi anaweza kuomba kusindikizwa na mtu anayeweza kumsaidia. Mtu huyo:
    - Asiwe shahidi mwingine. Kama akiwa ni shahidi, ahojiwe peke yake.
    - Awe ni mtu ambaye anayehojiwa anamwamini kuwa mwenye kuweka siri na asitangaze kwamba mawasiliano yamefanywa.
    - Awepo wakati wa mapumziko, na si wakati wa kuhojiwa kwenyewe.
    - Inaweza kuwa tofauti kwa watoto, ambao waruhusiwe kuwa na wanafamilia wa karibu, au walezi, kama hii itawasaidia.

**3. Fahamu tofauti ndogo ndogo maalum zinazoweza kumwathiri anayehoji:**

- Chunguza kuhusu majukumu ya jinsia, mipaka ya kuwasiliana na wanawake walioolewa na wale ambao hawajaolewa, na kushirikiana na watoto.

**4. Angalia siku, muda wa siku hiyo ambapo mahojiano yanaendeshwa:**

- Chunguza kuhusu desturi za kila siku za watu na za jamii, muda gani unafaa zaidi kwao, na pia masaa gani au siku gani haziruhusiwi, hazifai au ni takatifu, na kwamba ni lazima ziheshimiwe.

## 7.2 Orodha muhimu kwa mahojiano

Bila ya kujali dhana ya mahojiano, ni lazima, hata kwa uhaba, mahojiano yote yawe na hatua zifuatazo:

1 Kujitambulisha wewe mwenyewe na timu yako na elezea majukumu ya kila mtu aliyekuwepo na mashirika au mamlaka na malengo ya shirika lako.

2 Mtambulishe hasa mkalimani kwa aliyenusurika/shahidi, mwelezee majukumu yake na mfahamishe vizuri kabisa kwamba mkalimani pia anachukulia mahojiano na yote yatakayosemwa kwa kufuatilia miongozo ya kuweka siri ambayo wote kwenye timu wanafuatilia.

3 Pata ridhaa kamili ya aliyenusurika/shahidi kabla ya kuanza mahojiano rasmi **(angalia kipengele cha 6.1, "Ridhaa kamili")**. Watendaji wapate ridhaa kamili ya aliyenusurika/shahidi kabla na baada ya mahojiano.

4 Elezea aina za maswali ambayo mtu anaweza kuulizwa.

5 Kama aliyenusurika/shahidi akikubali taarifa iliyokusanywa kupelekwa kwenye mashirika mengine yanayohusika, ikiwa ni pamoja na polisi, wapelelezi na mahakama, basi umfahamishe kwa wazi kabisa mipaka ya siri ikiwa ni pamoja na njia maalum ambazo taarifa zake zinaweza kufichuliwa.

6 Mfahamishe anayehojiwa kwa wazi kabisa kwamba ana chaguo la kuongea au kutokuongea na wewe. Ni muhimu kwamba walionusurika/mashahidi wote, ikiwa ni pamoja na watoto, wanaelewa haki yao kuhusu siri.

7 Tathmini matarajio ya aliyenusurika/shahidi kuhusu mchakato, majukumu yako, taarifa atakazotoa na msaada ambao ataweza kuupata. Hakikisha kwamba matarajio haya yanawezekana na yasahihishe kama hayawezekani.

8 Rekodi taarifa kamili kuhusu aliyenusurika/shahidi, ikiwa ni pamoja na jina, tarehe ya kuzaliwa, jinsia na taarifa za mawasiliano, na uraia, kabila na dini pale inapohusika.

- Wakati ambapo mawasiliano ya simu hayapo au hayana hakika, na anwani za kawaida haziwezi kutegemewa, zinajulikana kwa majina mbali mbali, au hazipo, tumia njia mbadala kwa kurekodi taarifa za mawasiliano za aliyenusurika/shahidi, ikiwa ni pamoja na jina la ukoo, la kabila au jamii, au shirika au kundi ambalo aliyenusurika/shahidi yupo nalo karibu kimawasiliano.

9 Mwulize aliyenusurika/shahidi kuhusu njia anayopendelea kwa mawasiliano.

**10** Fikiria kuhusu kuwasiliana na aliyenusurika/shahidi miezi kadhaa, au mwaka, baada ya kuwahoji. Kwa mfano, kwa ridhaa ya aliyenusurika, rekodi majina ya wanafamilia, marafiki wa karibu ndani ya jamii, kanisa lake au kundi – yeyote ambaye ataweza kukusaidia kumpata aliyenusurika.

**11** Fikiria vipi aliyenusurika/shahidi atakavyoweza kuwasiliana na watendaji.

## 7.3 Aina za maswali

**"Kitabu cha kazi cha Ushahidi kwa ajili ya Nyaraka za Uhalifu wa Unyanyasaji wa Kijinsia", Nyongeza 1 ya Itifaki hii**, ina mifano ya maswali na majibu yaliyopangiliwa kutokana na vipengele vya hatia, kuwasaidia watayarisha nyaraka kukusanya taarifa ya kutosha wakati wa mchakato wa kutayarisha nyaraka. Kitabu cha ushahidi cha kazi kina mifano ya aina ya maswali ambayo yanaweza kuulizwa ili kupata taarifa ambazo zinaweza kutosheleza kila kipengele cha kila hatia inayoshukiwa kutendwa. Maneno hapa chini ni ufupisho wa sehemu za kitabu cha ushahidi cha kazi, ambacho kimejumlishwa kama nyongeza ili kurahisisha matumizi yake kama kifaa cha kutumika. Watendaji wanashauriwa kukitumia kwa kina na ufanisi kitabu chote cha kazi ili kukusanya ushahidi wa unyanyasaji wa jinsia kama hatia ya kimataifa.

Wakati wa mahojiano, aina ya maswali ambayo watendaji wanatakiwa kumwuliza aliyenusurika/shahidi yalenge katika kupata taarifa kuhusu jambo moja au zaidi kati ya yafuatayo:

**(i) Taarifa kuthibitisha kwamba kitendo chenyewe hasa (kwa mfano ubakaji, utumwa wa ngono, n.k) kilitendeka.**

**(ii) Taarifa kuthibitisha kwamba tendo hilo lilifanyika katika mazingira ambayo yanathibitisha tendo kuwa uhalifu dhidi ya utu, uhalifu wa kivita, au kitendo cha mauaji ya kimbari.**

**(iii) Taarifa kuthibitisha kwamba mtu fulani aliwajibika yeye binafsi katika uhalifu kwa tendo hilo (kwa njia gani ya mfumo wa dhima - yaani moja kwa moja au kupitia amri/mwenye jukumu kuu?).**

**(i) Aina ya maswali ya kukusanya taarifa kuhusu tendo**

Wakati wa kuwahoji walionusurika/mashahidi kuhusu tendo lenyewe, watendaji waulize maswali ambayo yatasaidia kuthibitisha vipengele vyote vya hatia maalum.

Kwa mfano, kwa hatia ya ubakaji, ni lazima watendaji waulize maswali ambayo yatalenga kutoa taarifa inayojenga shitaka kwamba:

1) Mtuhumiwa alivamia mwili wa mtu kwa njia ambayo matokeo yake yalikuwa kuingiliwa mwilini, hata kama ilikuwa ni kidogo tu, kwa kupitia katika sehemu za siri, sehemu ya nyuma/mkundu au njia yoyote ya kizazi kwa kutumia kitu chochote au kwa sehemu yoyote ya mwili.

Na kwamba:

2) Uvamizi ulifanywa kwa nguvu, au kwa maguvu ya kutishia, au kulazimisha, kama yale ambayo yanayosababishwa na woga wa vurugu, shinikizo, kuwekwa kizuizini, ukandamizaji wa kisaikolojia au matumizi mabaya ya madaraka, dhidi ya mtu huyo au mtu mwingine, au kwa kujinufaisha wakati wa mazingira ya kulazimisha, au uvamizi ulifanywa dhidi ya mtu ambaye hawezi kutoa ridhaa ya kweli.

Mifano ya maswali kwa (1) na (2):

(1) Kama inawezekana, kama si vigumu kwako, unaweza kunielezea walikufanya nini? Ninafahamu kwamba jambo hili si jepesi, tafadhali usiharakishe. (Kama akisema kwamba watu wale 'walimbaka' mmoja baada ya mwingine au akitumia maneno fulani ya mtaani au msamiati unaotumika katika jamii ambao unaufahamu kumaanisha kubaka, ni lazima ufuatilie tena ili kupata maelezo kamili ya kuingiliwa kimwili.) Unaposema wamekubaka, unaweza kuniambia kwa usahihi kamili ni kitu gani walifanya walipokuwa wanakubaka? Walitumia nini, sehemu gani ya mwili wako waliiumiza?

(2) Tafadhali unaweza kutuelezea matukio haya yalipotokea kulikuwa na hali ya mazingira gani? Utaweza kutuambia ulikuwa wapi, nani alikuwa hapo, nini kilikuwa kinatokea, na elezea mazingira?

**(ii) Aina ya maswali ili kukusanya taarifa kuhusu muktadha au mazingira**

Ili kuthibitisha kama uhalifu huu maalum ulitendwa kama uhalifu wa kivita, hatia dhidi ya utu au kitendo cha mauaji ya kimbari, ni lazima watendaji waulize maswali ambayo yatashawishi kutolewa kwa taarifa ambazo zitakidhi kila kipengele cha uhalifu.

Kwa mfano, kwa ubakaji *kama hatia dhidi ya utu* ni lazima watendaji waulize maswali ambayo yatashawishi kutolewa kwa taarifa ambazo zinaunga mkono madai kwamba:

1) Hatia zilifanywa zikiwa kama sehemu ya mashambulizi *yaliyotapakaa* au *yana mfumo wa mpangilio*.

2) Mashambulkizi yalikuwa dhidi ya raia wowote.

3) Mtuhumiwa wa moja kwa moja alijua kuhusu shambulio hilo dhidi ya raia.

4) (Kipengele cha mamlaka ya utawala ambacho kinaweza kikatakiwa au kisitakiwe katika mamlaka ya utawala ambamo watendaji wanashughulika kutayarisha nyaraka): Shambulio hilo lilifanywa kwa mujibu wa au katika kuboresha sera za taifa au shirika za kufanya mashambulizi kama hayo.

Mifano ya maswali

(1) na (2) Unaweza kuniambia kipi kingine kilikuwa kinaendelea, wakati na baada ya matendo uliyoyaelezea? Unaweza kuniambia kuhusu watu ambao unasema walishambuliwa – walikuwa wamevaa nini, walikuwa wamebeba nini? Walikuwa wanakaa wapi na je, kulikuwa na kituo chochote cha kijeshi au vifaa au watumishi wa aina yoyote katika maeneo ya jirani? Unaweza ukanielezea jinsi mashambulizi unayoyaongelea yalivyotokea? Nini kilitokea kwanza, na nini kilifuata, na nini baada ya hapo? Uliweza kugundua mfumo wowote kwenye mashambulizi ya aina yoyote? Nini kilikufanya ufikie uamuzi huo? Uliona matukio mengine yoyote yanayohusika na mashambulizi kama hayo uliyoyaelezea? (Atakupa maelezo ya kina ya matukio hayo ambayo alikuwa shahidi ili uweze kuona nani, nini, lini, wapi, kwa nini, vipi na alijuaje.)

### (iii) Aina za maswali ya kukusanyia taarifa kuhusu mtuhumiwa

Ili kukusanya taarifa juu ya namna ambayo mhusika binafsi ambaye ni mtuhumiwa au watuhumiwa (wanaotuhumiwa) kutenda uhalifu – ni lazima watendaji waulize maswali ili kufahamu ni nani ambaye anatuhumiwa kuwa alihusika na kwa kupitia njia gani ya dhima-moja kwa moja au kwa kupitia madaraka ya amri/ukuu.

Kwa mfano, kufahamu kuhusika kwa moja kwa moja, ni lazima watendaji waulize maswali ili kutambua nani anashutumiwa na kama yeye alifanya hivi:

*alitenda* (moja kwa moja, si kwa dhahiri, au kama mtuhumiwa-mwenza), *aliamuru*, *aliomba*, *alishawishi*, *alitenda jinai*, au vinginevyo alichangia kimatendo (au jaribio la tendo) la uhalifu na kundi lililokuwa likifanya kazi kwa lengo moja.[39]

Mifano ya maswali Je unaweza ukanielezea kuhusu hao watu ulioniambia walikufanyia vitendo hivyo? Je unaweza ukaniambia kuhusu nguo zao? Alama zozote za cheo? Walivaaje kwenye vichwa/miguuni, walikuwa wamebeba nini, kitu kingine chochote kilichojitokeza ambacho ni tofauti jinsi walivyoonekana? Silaha zao, vifaa vyao, magari yao n.k Je ulipata nafasi kumwona mtu mwenye wadhifa? Nani, nini, lini, wapi, kwa nini, vipi na unajuaje, au jambo gani lilikufanya ufanye uamuzi wako wa mwisho kwamba huyu mtu ana cheo cha madaraka? Ulipata nafasi ya kumsikia mtu huyu (watu hawa) wakisema kitu? Walisema nini, walimwambia nani, ilikuwa kwenye mazingira gani, na nini kilitokea au hisia ya jibu la alichokisema? Je ulipata nafasi ya kuangalia ushirikiano kati ya watu binafsi kwenye kundi hilo? Ni kitu gani uliweza kuona kuhusu ushirikiano wao? Ulipata nafasi ya kuwasikia wakiitana, kwa majina, kwa vyeo/daraja, kwa nafasi n.k?

## 7.4 Mbinu za mahojiano

Kutumia mbinu sahihi, tabia na mtazamo wakati wa kufanya mahojiano ni muhimu sana ili kumfanya aliyenusurika/shahidi ajihisi anaheshimika, amewezeshwa na amestarehe ili kuweza kutoa taarifa. Kwa hivyo, watendaji wanatakiwa kufanya yafuatayo:

**1. Kuwa makini na kuwa na mkakati kwenye namna ambayo wanauliza maswali:**

- Wamhamasishe aliyenusurika/shahidi asimulie hadithi yake na waruhusu watoe taarifa kwa njia wanayoipendelea kabla ya kuuliza maswali maalum kuhusiana na kitendo cha ukatili wa kijinsia.
- Usiulize maswali ambayo yatamfanya atoe majibu ambayo wewe unayataka.
- Rudia maneno yake kila inapowezekana ili kumhakikishia kwamba umeelewa – halafu omba ufafanuzi kama maneno yoyote aliyotumia yanahitaji maelezo. Kamwe usibadili maneno yake – jambo hili litamaanisha kwamba anatakiwa kusema unachokitaka wewe.
- Kila mara uliza "umejuaje" au "nini kilikufanya ufikie uamuzi huo?"
- Uliza maswali ya ziada kama inahitajika ili kuunga mkono, kuimarisha au kupanua kauli iliyofanywa.
- Kamwe usimsaidie aliyenusurika/shahidi kwenye kupata jawabu au kukumbuka jambo.

39 Tume (Sheria ya ICC Ibara ya 25 ya 3(a)) inaweza kuwa ama binafsi/ya moja kwa moja ya kufanya uhalifu wa pamoja na watu wengine. Utuhumiwa-wenza una msingi wa kudhibiti kwa pamoja uhalifu, au kufanya uhalifu kwa kupitia mtu mwingine. Kutoa amri kunaongoza mtu mwingine kufanya uhalifu. Kukusanya/kushawishi husababisha mtu mwingine kufanya hatia. Kutenda jinai kunasaidia katika kufanya hatia kwa njia ambayo ina athari kubwa kwenye kufanya uhalifu.

- Kamwe usidhani unafahamu ukweli wowote - hata kama walionusurika/mashahidi 50 ambao wamepita wametambua eneo la tukio fulani, kamwe usidhani kwamba aliyenusurika/shahidi wa 51 ataripoti eneo hilo hilo. Uliza swali kwa kila aliyenusurika/shahidi.

- Kamwe usiwalazimishe walionusurika/mashahidi kukumbuka maelezo ambayo mwanzoni hawawezi kuyakumbuka (jambo hili linaweza kuwa na madhara mabaya kwa walionusurika/mashahidi).

- Chukua tahadhari maalum kuhusu jinsi mahojiano yanavyohitimishwa, hasa pale ambapo aliyenusurika/shahidi ana majonzi au anajitenga. Jitahidi kumalizia masimulizi pale ambapo aliyenusurika/shahidi anajihisi salama.

**2. Mwenendo wako uwe ni ule wa kumheshimu na kumwezesha aliyenusurika/shahidi:**

- Mpe kipaumbele aliyenusurika/shahidi kuliko taarifa.

- Kaa sawa na aliyenusurika/shahidi, yaani muwe katika upeo wa macho yenu, au kaa chini yake.

- Mara kwa mara mpe aliyenusurika/shahidi uwezo wa kukubali au kukataa, kujibu au kutojibu, kuuliza maswali na majibu kurudiwa mara kwa mara, yaani mara nyingi iwezekanavyo, au wacha au endelea na mahojiano.

- Kumbuka kwamba ridhaa kamili ni mchakato: mara kwa mara toa taarifa ili kuhakikisha kuwa uchaguzi anaoufanya yeye wakati na baada ya mahojiano unatokana na taarifa kamili. Kama huna uhakika kwamba yeye ameelewa, mwulize akuelezee wewe taarifa hii kwa kutumia maneno yake yeye mwenyewe.

- Mpongeze na mheshimu usimwonyeshe huruma.

- Daima kuwa mpole, mwenye heshima na makini. Hasa ufahamu matarajio ya kitamaduni ya mwenendo wako katika uhusiano wa hali ya kijamii, jukumu na hasa sifa fulani ya mtu binafsi ambaye wewe unamhoji.

- Jiweke kitaalamu. Wakati wote, kuwa mwangalifu sana usionekane kama unahukumu, hukubali au huamini, ikiwa ni pamoja na matumizi yako ya lugha ya mwili au hisia za uso ambazo unaweza kuzitumia.

- Jipe muda (kumbuka kuwacha muda wa kutosha kwa kufanya mahojiano) na uwe na subira kufuatana na jinsi walionusurika/mashahidi wanavyojibu maswali yako.

**3. Usifanye ahadi za aina yoyote. Tambua kwamba ahadi zinaweza kufanywa kwa mtu kukubali, au zinaweza kupendekezwa kwa kutokuwepo ufafanuzi. Usiahidi (kwa kusema au kukaa kimya), kwa mfano:**

- Siri **(angalia** **kipengele cha 6.2****, "Siri")**.

- Kumsaidia kwa kumpatia huduma.

- Kuleta haki.

- Kumlinda yeye au familia yake.

- Kurudi tena kumwona - unaweza kukubali kufanya mkutano mwingine, lakini weka wazi kwamba jambo hili halina uhakika.

**4. Fikiria lugha ambayo unaweza kutumia unapohusika na aliyenusurika/shahidi:**

- Ongea vizuri na wazi na toa maelezo au ufafanuzi kama aliyenusurika/shahidi haelewi maswali.

- Wanaofanya mahojiano na wakalimani wafanye kazi pamoja ili kutengeneza orodha ya maneno na maneno ya staha/tafsida, ambayo walionusurika/mashahidi wanaweza kutumia ili kuelezea unyanyasaji wa kijinsia au viungo vya uzazi.

**5. Pale unapomhusisha mkalimani katika mahojiano:**

- Hakikisha kwamba mkalimani anamwangalia na anamsemesha aliyenusurika/shahidi moja kwa moja na anafahamu kuhusu uzito wa sauti, ukali wa sauti au toni, kusema haraka na kubadilisha sauti.

- Mwongeleshe aliyenusurika/shahidi moja kwa moja ("ulisema nini baada ya hapo?"), na sio kwa mkalimani ("mwulize alisema nini baada ya hapo").

- Epuka au punguza kuandika wakati mkalimani anatafsiri maswali yake (ni muhimu kuangalia lugha ya mwili wa aliyenusurika/shahidi na toni ya sauti).

- Hakikisha kwamba unafahamu maneno yanayohusu unyanyasaji wa kijinsia katika lugha ya mtu unayemfanyia mahojiano ili uweze kuonyesha hisia inavyofaa pale unyanyasaji wa kijinsia unapoongelewa. Shughuli ya kusikiliza (mfano kutingisha kichwa, hata wakati aliyenusurika/shahidi anaongea lugha tofauti na mtendaji) kutaongeza imani na kuleta ufunuzi wa taarifa.

**6. Fahamu kwamba walionusurika/mashahidi watakuwa na mienendo na wataonyesha hisia kwa njia maalum na tofauti pale wanapohadithia au wanaposimulia tena hadithi zao. Mienendo haina njia "moja". Usidhani tu kwamba aliyenusurika/shahidi atakuwa na mwenendo fulani maalum au ataonyesha hisia kwa njia maalum:**

- Walionusurika/mashahidi wanaweza kupata majonzi, kuwa na matatizo kuonyesha hisia zao, au kukasirika na kujitenga.

- Walionusurika/mashahidi wanaweza kukasirika, kutoa hisia, kujitetea, kuhamasika, kukataa kujibu maswali mengine, au kuongea kirefu kuhusu maelezo ambayo yanaweza kuonekana kwamba hayana maana.

- Walionusurika/mashahidi wanaweza kuwa shwari, wametulia, wanasema kwa wazi, na kuweza kukumbuka na kuhadithia kwa kina na kwa usahihi matukio yote na mazingira ya tendo hilo.

- Walionusurika/mashahidi wanaweza kuona vigumu kukumbuka maelezo madogo madogo na mpangilio wa matukio unaweza kubadilika. Hakuna kiunganisho cha moja kwa moja kati ya kiwewe (trauma) na kuaminika – wala kumbukumbu. Kila mtu anaathirika tofauti na kiwewe; usibuni tu.

- Waeleze walionusurika/mashahidi kwamba wanaweza kuchagua kuacha mahojiano wakati wowote wakijihisi hawana raha au wana majonzi.

**7. Usidhani unajua kisicho na uhakika kuhusu yafuatayo:**

- Aliyenusurika/shahidi ataona aibu.

- Hatotaka kuongea.

- Yeye ni dhaifu sana.
- Yeye ana trauma/kiwewe.
- Kiwewe chake kitaathiri kuaminika kwake.
- Walionusurika/mashahidi wanawake watataka kuongea na wachunguzi wanawake tu na walionusurika/mashahidi wanaume watataka kuonghea na wachunguzi wanaume tu. Hata hivyo, pale ambapo chaguo lipo, suala hili ni lazima liulizwe, je aliyenusurika/shahidi angependelea nini.
- Kwamba wao wanavyoona ni kuwa, unyanyasaji wa kijinsia ndiyo jambo 'baya kuliko yote' kati ya matukio yote waliyoyapitia.
- Atakuwa na majeraha ya mwili.

**8. Uangalifu maalum wakati wa kuwahoji watoto**

Ni lazima kwa watendaji wanaotayarisha nyaraka kuhusu unyanyasaji wa kijinsia unaowashirikisha watoto, waweke kipaumbele kwenye maslahi bora ya mtoto katika mchakato wote wa kutayarisha nyaraka. Ni lazima kwa watendaji kuhakikisha kwamba watoto wanatambua haki yao ya kuheshimiwa na huruma, kwa faragha, kupewa taarifa, kupewa msaada, kuwa salama, kwa fidia na kwa hatua zinazoweza kuzuilika. Ni lazima watoto kufahamishwa haki yao ya kusikilizwa na kipau mbele maalum kitolewe ili kuhakikisha kwamba mchakato unaelezwa kulingana na uwezo binafsi wa mtoto.

Wakati wa kuhoji watoto, ni lazima watendaji wawe na mafunzo maalum ya kufanya hivyo, na washirikiane na watoto kwa mujibu wa mwongozo wa kina uliowekwa katika IRC, UNICEF, Utunzaji wa Watoto Waathirika wa Unyanyasaji wa Kijinsia: Miongozo kwa ajili ya Watoa Huduma za Afya na Kisaikolojia katika Mazingira ya Kibinadamu[40] na UNICEF, UNODC, Miongozo juu ya Masuala ya Haki Yanayowashirikisha Watoto Waathirika na Watoto Mashahidi wa Uhalifu.[41]

Wakati wa kuwahoji watoto, watendaji wajitahidi kufanya yafuatayo angalau hata kidogo:

- Wazingatie kwamba watoto wanaweza wasifahamu kabisa asili ya ngono ya tabia fulani na kujitengenezea mbinu zinazoamini hivyo.
- Badala ya kulielewa tendo fulani maalum kama ubakaji au uvamizi, jitahidi utumie maneno yenye kuelezea viungo vya mwili na matendo ambayo yalitokea.
- Badala ya kuuliza "alikuumiza kwenye sehemu zako za siri?" na kuufanya mwili wako uonyeshe kama vile wewe unafahamu kwamba hilo ni swali la kutisha kuliuliza au kulijibu, wewe mwulize tu mtoto akuhadithie kwa kina nini kilitokea.
- Fikiria kuhusu kutumia michoro au madoli ili kumsaidia mtoto kuelezea kitu gani kilimtokezea.
- Hakikisha kwamba huonyeshi hisia ya chukizo, hofu au kuonyesha mshtuko katika kile ambacho mtoto anakisema – kile ambacho kinachoweza kuwashtusha wanaotayarisha nyaraka kinaweza kisilingane na mawazo na hisia za mtoto aliyenusurika/shahidi.
- Kaa urefu sawa na mtoto; katika upeo wa macho yako na yake, usimwinamie au usimwangalie kwa chini ili kukuza hisia za heshima na kupunguza vitisho.

40 IRC, UNICEF, Caring for Child Survivors of Sexual Abuse: Guidelines for Health and Psychosocial Service Providers in Humanitarian Settings, 2012.

41 UNICEF, UNODC, Guidelines on Justice Matters Involving Child Victims and Child Witnesses of Crime, 2005.

…kama walionusurika tumepitia mateso kwenye mikono ya wale waliotakiwa kutulinda – ama ndani au nje ya mfarakano Kushiriki kwenye mchakato wa kutayarisha nyaraka hakutakiwi kuleta madhara zaidi. Kuongea ili kusikika na kupata haki kunatakiwa kuwa ni mchakato wa kuwawezesha walionusurika.

**Survivors Speak OUT! Mtandao, 2014**

- Punguza idadi ya nyakati ambazo mtoto anahojiwa na kuulizwa maswali na fanya mahojiano katika mazingira mazuri kwa mtoto, kwa nyakati mwafaka, ukihakikisha kuwepo kwa mapumziko wakati wa kutoa ushahidi.

### 7.5 Kurekodi taarifa za mahojiano

Unapowahoji walionusurika/mashahidi na huku unaandika, hakikisha kwamba unafanya yafuatayo angalau kwa kiasi  kidogo:

1. Weka data binafsi kwa kiasi kikubwa iwezekanavyo **(angalia Nyongeza 4, "Kigezo kwa data binafsi za kukusanywa kutoka kwa walionusurika/mashahidi")**.
2. Weka maoni na mawazo na uchambuzi wa anayefanya mahojiano tofauti na maelezo ya mahojiano.
3. Andika kwa kutumia nafasi ya mtu wa kwanza kama vile aliyenusurika/shahidi anavyoongea.
4. Usifupishe au kupunguza au kukata sehemu za taarifa ya aliyenusurika/shahidi.
5. Msomee ulichoandika aliyenusurika/shahidi kabla ya kuhitimisha mahojiano. Ingawa hii inachukua muda mwingi, ni muhimu ili kuhakikisha taarifa ulizozikusanya kutoka kwa shahidi ni sahihi kama iwezekanavyo.
6. Andika ushahidi wowote mwingine uliopatikana kwa kupitia huyo aliyenusurika/shahidi - picha zilizopigwa za ushahidi dhahiri, ndani ya maelezo hayo, na tumia mfumo wa kuorodhesha kihesabu, ili kuwezesha kulinganisha kumbukumbu.
7. Weka majina na data zingine binafsi tofauti na maelezo kwa sababu za usalama.
8. Tumia mfumo wa kiwango cha kawaida ili kutoa majina kwa maelezo yaliyotolewa kwenye mahojiano.
9. Weka kila ushahidi wa aliyenusurika/shahidi tofauti.
10. Weka taarifa kuhusu aliyenusurika/shahidi tofauti – masuala ya usalama, mazigira ya maisha, masuala ya afya, au masuala yanayohusiana na aliyenusurika/shahidi.
11. Weka vidokezo vilivyotolewa na aliyenusurika/shahidi tofauti - orodha yako ya vidokezo ni amana ya kazi na ihifadhiwe katika mahali penye usalama na tofauti.

## 8. Vyanzo vingine vya Taarifa

### 8.1 Ushahidi dhahiri

Ushahidi dhahiri unahusu kitu chochote dhahiri au chenye kiwiliwili au jambo ambalo linaweza kutoa taarifa na kusaidia kuonyesha kwamba uhalifu ulifanyika, au kutoa kiungo kati ya uhalifu na waathirika wake au kati ya uhalifu na wahusika watuhumiwa wake.

Kwa sheria za kawaida, watendaji hawapaswi kuchukua bidhaa yoyote ya ushahidi wa dhahiri isipokuwa kama wao wamepata mafunzo kama wapelelezi au kama mhudumu wa afya katika ukusanyaji sahihi wa ushahidi wa kisayansi kuhusu uhalifu (forensiki). Kama watendaji wataamua kukusanya ushahidi wa dhahiri bila ya kufanya mafunzo sahihi, wanaweza kumpa madhara makali aliyenusurika, na wanaweza kuchafua ushahidi, na kuufanya usiweze kutumika tena. Hata hivyo, katika baadhi ya mazingira ambayo ni machache sana, ambapo kuna usalama na ambapo hilo ndilo chaguo pekee, ukusanyaji wa ushahidi wadhahiri unaweza

kuwa sahihi. Uamuzi wa kukusanya ushahidi dhahiri uchukuliwe kwa uzito na tahadhari, na ufikiriwe kwa makini sana.

Watendaji wanaweza kukutana na ushahidi dhahiri wa unyanyasaji wa kijinsia:

- kuhusu waathirika/mashahidi wenyewe, kulingana na muda uliokuwepo na asili ya majeraha; na/au
- katika sehemu ambapo unyanyasaji wa kijinsia ulifanyika.

Kutegemea muda unaohusika na asili ya majeraha, walionusurika kutokana na unyanyasaji wa kijinsia wanaweza kuwa na ishara juu ya miili yao kama vile alama au majeraha ambayo yanathibitisha masimulizi yao ya ushambulizi. Pia wanaweza kuwa na matokeo ya afya kutokana na shambulio hilo, ikiwa ni pamoja na majeraha mwilini, mimba, magonjwa ya zinaa na kiwewe cha akili. Kimsingi, mwathirika anatakiwa kuwa na uwezo wa kupata msaada wa matibabu ya haraka baada ya kuvamiwa kijinsia; na daktari mwenye mafunzo anapaswa kurekodi majeraha yoyote na madhara mengine ya afya kwenye rekodi ya matibabu ya siri ambayo aliyenusurika anaweza kuipata wakati wowote **(angalia Nyongeza 10, "Mfano wa Cheti cha Uvamiaji wa Kijinsia")**.

Kabla hata ya kuzingatia kukusanya kifaa cha ushahidi dhahiri, kwanza ni lazima watendaji wafanye yafuatayo:

- waandike kumbukumbu ya vifaa ambavyo wamepata;
- wachore eneo la uhalifu;
- wapige picha hicho kitu na eneo la uhalifu; na
- kama itawezekana wapige video ya hicho kitu na eneo la uhalifu **(angalia Nyongeza 8, "Mwongozo wa Kupiga Picha, Kupiga Video na Kuchora Maeneo ya uhalifu, Ushahidi Dhahiri na majeraha ya kimwili")**.

Pia watendaji wanapaswa, ikiwezekana na ikiwa salama, kufanya mahojiano na walionusurika/mashahidi wowote karibu na eneo la uhalifu na kufuata vidokezo kwa mashahidi wengine wa uhalifu huo **(angalia Nyongeza 3, "Mahojiano: Kanuni za Msingi na Vidokezo Muhimu kwa Vitendo vya Kazi")**. Taarifa hii nyingine - ikiwa ilikusanywa vizuri - inaweza kuwa na uzito mkubwa sana na huweza kuondoa haja ya ushahidi wa dhahiri. Wakati wa kukusanya taarifa hizi nyingine, ni lazima watendaji kuchukua hatua kutoigusa wala kuiathiri kwa namna yoyote ile, au kuharibu au kusogeza ushahidi wa dhahiri (ulio kwenye eneo hilo lenyewe au kwingine kabisa).

Ni muhimu sana kukumbuka kwamba ingawa ushahidi wa dhahiri unaweza kuonekana kuwa kama vile ni ushahidi "bora" wa uhalifu, hii si lazima kuwa kweli. Ushahidi wa dhahiri ambao haukutolewa na aliyenusurika/shahidi, na unaoelezea asili, umiliki na matumizi ya kitu au matukio yaliyoletea kupatikana kwa hicho kitu, hayatakuwa na manufaa sana kutokana na maoni ya ushuhuda. Wakati ushahidi wa aliyenusurika/shahidi unaweza kuchukua nafasi ya ushahidi wa dhahiri, kinyume cha hili sio kweli; kwa kawaida ushahidi wa dhahiri hauwezi kuchukua nafasi ya ushahidi wa aliyenusurika/shahidi. Katika mifumo ambayo inahitaji uthibitisho wa ushahidi wa unyanyasaji wa kijinsia (mfano katika baadhi ya mahakama ya kitaifa), ukusanyaji wa ushahidi wa dhahiri unaweza kupewa kipaumbele kuliko katika ile mifumo ambayo haihitaji (mfano mbele ya mahakama ya ICC) **(angalia Nyongeza 9, "Kanuni za Ushahidi na Utaratibu kama Zana ya Kuwalinda Walionusurika/Mashahidi")**. Mapolisi na madaktari wanazidi kushirikiana katika kukusanya ushahidi kutoka katika eneo la uhalifu na, kitu bora zaidi, hupata mafunzo pamoja katika njia bora za kutayarisha nyaraka za uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia kwa namna salama na fanisi ambazo zinaheshimu haki za waathirika.

Zaidi ya hayo, ikiwa watendaji si wapelelezi wa jinai, watataka kuepuka kujiweka kwenye nafasi ambapo wanaitwa kama mashahidi ili kueleza jinsi walivyokuta hicho kitu cha ushahidi wa dhahiri. Wakati mwingine, ukusanyaji wa ushahidi wa dhahiri ukifanywa na mtu yeyote zaidi ya polisi huwa ni kinyume cha sheria na jambo hili huweza kuwa na adhabu.

Katika mazingira yasiyo ya kawaida sana ambapo mtendaji anaamua kuchukua ushahidi wa dhahiri, kanuni za "Mlolongo wa Utunzaji" zilizowekwa katika **Nyongeza 6**, **"Ushahidi Dhahiri: Kanuni za mlolongo wa Utunzaji"** zifuatwe.

Hata hivyo, ni lazima mtendaji atambue kwamba ukusanyaji wa ushahidi dhahiri unaambatana na mkusanyiko wa uthibitisho na/au ushahidi wenye maelezo ili uwe na maana.

### (i) Maeneo ya mashambulizi

Pia watendaji wanaweza kupata, au kujua, maeneo ambapo uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia ulifanyika. Si eneo la shambulizi tu ambalo lina umuhimu kama chanzo chenye thamani kwa ushahidi wa dhahiri, lakini pia mahala na kuwepo kwa eneo hilo, kunaweza kuthibitisha kuwepo kwa wanaoshukiwa katika eneo; na kuchambuliwa kama sehemu ya mfumo wa harakati za wanaoshukiwa kuwa watuhumiwa, na vipengele vingine vya kimuktadha au vipengele vya mifumo ya dhima. Ni muhimu kutambua kwamba "maeneo ya mashambulizi" ni pamoja na miili ya waathirika au miili ya wahalifu, kama hai au marehemu. Kushirikiana na wataalam wa tiba au wanasayansi wanaochunguza ushahidi wa kisayansi kuhusu uhalifu (forensiki) kunaweza kuwa muhimu katika kupata uthibitisho huo.

Ushahidi wa dhahiri unaopatikana katika maeneo unaweza kusaidia kuonyesha:

- kwamba mashambulizi dhidi ya raia yalifanyika;
- kwamba kitendo cha unyanyasaji wa kijinsia kilifanyika;
- hali ya mazingira ya kitendo, ikiwa ni pamoja na aina na/au muda wa kuwekwa kizuizini na matumizi ya nguvu;
- utambulisho wa wanaoshutumiwa kuwa watuhumiwa;
- shirika na muundo wa kundi la anayetuhumiwa; na
- ushahidi wa aliyenusurika/shahidi kubainisha (katika mifumo ya kisheria ambayo inahitaji jambo hili).

Ushahidi unaokutwa katika maeneo unaweza kuwa:

- nguo, ikiwa ni pamoja na sare/unifomu au sehemu za sare na nguo ambazo zinaweza kuwa zilivaliwa na aliyenusurika/shahidi, mashuka na mablanketi;
- silaha, visu, risasi na vifuniko vya risasi;
- madoa, damu, matapishi, shahawa, maji maji ya uke na/au kinyesi;
- ushahidi wa nyaraka;
- kompyuta na vifaa vya mawasiliano;
- miili au sehemu za mwili;
- ushahidi wowote unaoonyesha kwamba watu wanaishi au waliishi kwenye eneo, na

- ushahidi wa maelezo ya upangiliaji na maelezo ya dhahiri ya sehemu hiyo ambayo yanafanana na ushahidi wa shahidi.

Wakati wa kushughulikia maeneo ya unyanyasaji wa kijinsia, na ushahidi ulio dhahiri unapopatikana katika maeneo hayo, watendaji wasiutoe ushahidi ulio dhahiri na badala yake ni lazima:

1 warekodi kwa sahihi eneo ulipotokea unyanyasaji wa kijinsia;

2 wachague mtu kuwa meneja wa eneo na wafungue jarida la kuandika majina ya watu wote wanaofanya ziara kwenye eneo;

3 Wachore eneo la tukio, ikiwa ni pamoja na eneo ambalo linawezekana kuwa na ushahidi dhahiri;

4 wapige picha eneo la tukio, ikiwa ni pamoja na eneo na maelezo yanayoweza kuwa na ushahidi ulio dhahiri; na

5 wawache eneo kama walivyolikuta.

### 1. Rekodi sehemu lilipo eneo

Ni lazima watendaji warekodi kwa usahihi sehemu lilipo eneo ambapo unyanyasaji wa kijinsia unatuhumiwa kufanyika. Hili litawezesha wachunguzi au wale walio na uwezo wa kutayarisha nyaraka na kukusanya ushahidi kwa ufanisi kutoka katika eneo waweze kulipata siku zijazo.

Watendaji wanatakiwa:

- warekodi maeneo kwa kutumia GPS au ramani;
- warekodi taswira zozote muhimu za eneo hilo, ikiwa ni pamoja na alama, taswira dhahiri na majina ya maeneo na jamii zilizo jirani, vijiji na miji, kama GPS au kumbukumbu za ramani hazitapatikana au si sahihi; na
- Weka taarifa hii salama na usifichue lilipo na kuwepo kwa eneo hili kwa jamii kwa ujumla.

### 2. Chagua mtu kuwa meneja wa eneo na fungua jarida la kuandika majina ya watu wote wanaofanya ziara kwenye eneo

Meneja wa eneo anatakiwa:

- aanzishe na kuweka jarida; na
- aamue mbinu za kulinda eneo kama ni lazima.

### 3. Chora tukio na eneo la ushahidi

Watendaji wanatakiwa kuchora mchoro wa eneo kwa kuingiza maelezo mengi iwezekanavyo huku wakiangalia vikwazo vya muda, rasilimali na usalama.

Watendaji wanatakiwa:

- kuweka mchoro unaoonekana kutokea juu katika fomu:
- weka vipimo katika mchoro;

- onyesha taswira muhimu;
- onyesha eneo na aina ya ushahidi unaowezekana kupatikana; na
- saini na weka tarehe kwenye mchoro.

### 4. Piga picha eneo la tukio na ushahidi

Kupiga picha eneo la tukio, eneo la jirani linalozunguka, na taswira muhimu au ushahidi ndani ya eneo kunaweza kuwa ni jambo muhimu lenye thamani sana kwa wachunguzi au wataalam watakaofanya uchambuzi hapo baadaye.

Watendaji wanatakiwa:

- wachukue picha ya eneo na yaliyomo bila ya kuathiri au kuyaondoa;
- kuchukua picha kwa ujumla, za mazingira na za karibu kwenye eneo:
- kwa ujumla picha ziwe na picha za eneo la jirani, hatima ya kijiografia na iliyo dhahiri, majengo na barabara;
- picha za mazingira zinapaswa kuonyesha uhusiano kati ya taswira ambayo mtendaji anaipiga na vitu vingine au taswira nyengine; na
- picha za karibu zinapaswa kuonyesha kwa undani ushahidi au taswira ambayo mtendaji anairekodi;
- inapowezekana, chukua picha inapokuwa na vipimo na pia bila vipimo; na
- weka jarida la picha jinsi unavyozipiga. Kwenye jarida weka jina na jukumu la mtu anayechukua picha; tarehe, muda na mahali; aina ya filamu; na maelezo ya kamera. Toa maelezo mafupi ya kila picha.

### 5. Liwache eneo kama ulivyolikuta

Ni muhimu kuzingatia kwamba eneo halivurugwi, hauondoi vitu au kuondoa ushahidi kutoka kwenye eneo. Kufanya hivyo kunaweza kuathiri vibaya manufaa na umuhimu wa eneo na yaliyomo na thamani yake ya ushuhuda. Wakati mwingi, kurekodi kwa usahihi ushahidi ulioukuta inatosha.

Kukusanya ushahidi wa dhahiri kutoka katika eneo kufanywe tu na wale wenye mamlaka, uwezo na ujuzi wa kufanya hivyo. Ushahidi wa dhahiri uondolewe tu kutoka kwenye maeneo kama:

- watendaji hawana njia yoyote ya kurekodi ushahidi na wanatambua hatari kuu iliyopo ya uharibifu au kusumbuliwa; na
- watendaji wana ujuzi na uwezo wa kukusanya ushahidi; na kuutoa kutoka kwenye tukio; na
- watendaji wana uwezo mkubwa wa kuhakikisha hifadhi ya nyaraka, usimamizi, usafirishaji na hifadhi za ushahidi ulioondolewa, hivyo kuhakikisha kwamba "mlolongo wa utunzaji" unaendelezwa **(angalia Nyongeza 6, "Ushahidi wa Dhahiri: Kanuni za Mlolongo wa Utunzaji")**.

## 8.2 Ushahidi wa nyaraka

Nyaraka, zote zilizo rasmi na zisizo rasmi, zinaweza kuwa chanzo cha taarifa muhimu sana wakati wa kuweka kumbukumbu za nyaraka na kuchunguza unyanyasaji wa kijinsia. Taarifa zinazopatikana katika nyaraka zinaweza kusaidia kuanzisha yafuatayo:

- Mfumo, marudio na mkazo wa kuripotiwa kwa unyanyasaji wa kijinsia: Hii inaweza kupatikana katika rekodi zinazowekwa na wafanyakazi wa matibabu na afya pamoja na miundombinu, takwimu za usimamizi wa kesi, ripoti zenye ushahidi, tafiti na masomo ya unyanyasaji wa kijinsia.[42]

- Utambulisho wa watuhumiwa na wakuu: Taarifa zinazopatikana katika rekodi za jeshi au serikali zinazoonyesha harakati na kuwepo kwa wanaoshukiwa kuwa watuhumiwa, mashirika, muundo wa amri, na mamlaka rasmi na yasiyo rasmi; kumbukumbu za ushahidi wa aliyenusurika/shahidi zinazoelezea muonekano, mavazi na alama maalum za watuhumiwa; na kumbukumbu za mashirika ya kitaifa na kimataifa zenye taarifa, wasifu na/au harakati za wanaoshukiwa kuwa watuhumiwa.

- Kuwepo kwa mpango au mkakati na mifumo ya dhima: Katika nakala za amri zilizotolewa, mipango iliyofanywa kushambulia baadhi ya maeneo, na kumbukumbu za mawasiliano yaliyofanywa kati ya vitengo/sehemu mara moja kabla ya, wakati au baada ya shambulio hilo.

- Njia za uchunguzi zaidi: Taarifa zilizopatikana katika nyaraka rasmi au zisizo rasmi zinaweza zenyewe zisionyeshe kikamilifu ukweli wowote lakini zinaweza kutoa kidokezo cha taarifa kwa juhudi za uongozi wa uchunguzi wa baadaye.

### (i) Aina za nyaraka

Aina ya nyaraka muhimu ambazo watendaji wanaweza kupata, au tayari kuwa katika milki yao, zinajumlisha zifuatazo.

### Rasmi

- Kumbukumbu na ripoti zinazohusiana na vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia na/au mshtakiwa, ikiwa ni pamoja na wakuu, kama vile kumbukumbu za ugavi na usafirishaji, kumbukumbu za matukio halisi, kumbukumbu za mipaka, mipango au mikakati ya kijeshi, kumbukumbu za mawasiliano, maelekezo yaliyoandikwa na maagizo.

- Nyaraka zingine rasmi kama vile vyeti vya matibabu, maelezo na ripoti. Hata hivyo, aina za kumbukumbu hizi za hati haziwezi kupatikana bila ya ridhaa ya walionusurika, na watoa huduma za afya wengi watachagua kutoshiriki katika aina hizi za nyaraka kutokana na wasiwasi wa faragha.

- Orodha ya wafungwa na kumbukumbu za polisi.

### Zisizo rasmi

- Ripoti na kumbukumbu za mashirika ya kimataifa na ya kitaifa, kama vile usajili na kuorodhesha kumbukumbu za watu waliosambaratika nchini kwenyewe na mbinu za ufuatiliaji; data ya tukio; na ripoti ya haki za binadamu, hasa zile zenye uchambuzi wa

42 Ingawa aina hii ya data juu ya unyanyasaji wa kijinsia inaweza kuwa na manufaa kama historia ya utafiti, au ikaunga mkono madai fulani ya shutuma au madai ya shutuma ya unyanyasaji wa kijinsia, data zilizokusanywa kupitia tafiti, ripoti za kesi na tathmini nyingine haziwakilishi ujumla wa matukio ambayo yalitokea. Kwa mwongozo zaidi juu ya vitu vinavyoruhusiwa na vitu visivyoruhusiwa kuhusu unyanyasaji wa kijinsia, angalia makala ya UN Action inayoitwa Reporting and Interpreting Data on Sexual Violence from Conflict-Affected Countries: "Dos And Don'ts", 2008.

ukiukwaji uliofanyika, matokeo ya ukiukwaji huo, mbinu za kutoa maonyo mapema, na maelezo ya kauli kutoka kwa walionusurika na mashahidi wengine.

- Maelezo ya ripoti za hatia zilizopokelewa na viongozi wa kienyeji wa jadi na kidini, na maelezo ya sasa yaliyotolewa na walionusurika au mashahidi wengine.
- Tafiti za ushahidi, ripoti, utafiti na tathmini zinazokamata taarifa juu ya aina ya marudio na ukubwa wa unyanyasaji wa kijinsia uliofanywa, utambulisho wa wanaoshukiwa kuwa watuhumiwa na wakuu, na kutambuliwa kwa athari kwenye mahitaji ya waathirika/mashahidi.
- Picha, video na picha za satelaiti.

Wakati wa kushughulikia ushahidi wa maandishi, ni lazima, kwa uhaba, watendaji wafanye yafuatayo:

1. heshimu siri;
2. sahihisha rekodi na fanya nakala kama inawezekana; na
3. kutonyang'anya nyaraka.

### 1. Heshimu siri

- Kushirikiana katika kugawana kokote kwa kumbukumbu, ripoti, utafiti na takwimu za kesi za unyanyasaji wa kijinsia kufanyike kwa usalama na kimaadili na kwa heshima kwa kuweka siri ya mhusika aliyenusurika/shahidi **(Angalia Kipengele 6.1 na 6.2).**
- Ni lazima takwimu ya taarifa isiwe na jina, lakini ni lazima watendaji kutathmini kama hata taarifa isiyo na jina inaweza kuhusishwa na kikundi fulani au jamii, ambayo ingeweza kuwaweka walionusurika/mashahidi hatarini.[43]
- Ni lazima taarifa za ngazi binafsi zigawiwe kwa wanaohusika wengine kama tu kuna ridhaa kamili ya aliyenusurika/shahidi.

### 2. Weka kumbukumbu kwa usahihi na nukuu kama itawezekana

- Angalau fanya kumbukumbu sahihi inayoelezea yaliyomo ndani ya nyaraka iliyopatikana au kupokelewa, mazingira ambayo kumbukumbu ilibainika au kupokelewa, eneo ambapo ilipatikana, kutoka kwa nani imepokelewa, na nani mwingine alikuwepo wakati nyaraka ilipopatikana au pokelewa.
- Kama ushahidi wa nyaraka umetolewa na mhusika mwingine, pata maelezo kutoka kwa mhusika huyo ikielezea mazingira ambayo mhusika huyo aliipata nyaraka; wapi na waliipokea kutoka kwa nani; kama nyaraka ni halisi au nakala; maelezo ya maana au umuhimu wa mihuri, saini na majina katika nyaraka; na jinsi mhusika huyo mwingine alivyopata kujua taarifa hii.
- Kama nyaraka imenukuliwa, hakikisha kwamba nakala inaeleweka na kwamba, kama ni lazima, basi kote mbele na nyuma kumenukuliwa, na rekodi jinsi na wakati iliponukuliwa na nani.

43 Angalia UN Action, Reporting and Interpreting Data on Sexual Violence from Conflict-Affected Countries: "Dos And Don'ts", 2008.

### 3. Usipokonye nyaraka

- Kwa kawaida, kisheria, wale ambao si wapelelezi waepuke kupokonya nyaraka kutoka katika shirika lolote, serikali au jeshi, au mtu binafsi. Watendaji wanapaswa kuweka taratibu ambazo zinaeleza hatua gani zichukuliwe kama wanajikuta katika hali ambapo wanapewa nyaraka muhimu kwa kazi zao. Ingawa, kamwe, watendaji wasipokonye nyaraka bila idhini ya kuwaruhusu kufanya hivyo, inawezekana kukubali nyaraka zinazokabidhiwa kwa hiari ilimradi taratibu zipo na mtendaji anakusanya taarifa za kutosha kuhusiana na nyaraka yenyewe **(angalia kipengele 2 "Rekodi nakala yoyote kwa usahihi kama inawezekana" hapo juu)**.
- Kuhifadhi nyaraka kufanyike tu kama nyaraka imepatikana au imepelekwa kwa watendaji.
- Hata hivyo, taarifa sahihi kuhusu yaliyomo na eneo la kumbukumbu fulani inaweza kuwa na matumizi ya uchunguzi wa baadaye na kupatiwa mamlaka au idhini ya kupokonya ushahidi.
- Angalia **Nyongeza 7, "Ushahidi wa Nyaraka: Kanuni za mlolongo wa utunzaji"** kwa taarifa zaidi

## 9. Kuhifadhi Taarifa

Kama watendaji watakusanya taarifa juu ya unyanyasaji wa kijinsia (mfano picha za eneo la uhalifu au nyaraka zilizorekodi mahojiano yao na aliyenusurika/shahidi) ni muhimu kuhifadhi na kuweka taarifa hii katika namna ambayo haivunji uadilifu wake au kuwaweka walionusurika na mashahidi katika hatari ya madhara zaidi.

Asili nyeti ya taarifa kuhusu unyanyasaji wa kijinsia na uwezekano wa madhara yanayoweza kutokea iwapo taarifa hizi zitatumiwa vibaya, inafanya kwamba ni muhimu sana kwa mtu yeyote anayekusanya taarifa hizi kuzihifadhi katika namna ambayo inahakikisha usalama wa aliyenusurika/shahidi, jamii na wale wanaokusanya taarifa

Kuhifadhi na kudumisha taarifa juu ya unyanyasaji wa kijinsia katika hali ya usalama, watendaji wanatakiwa:

1. Panga ambapo habari itahifadhiwa na nani atakuwa na udhibiti juu yake. Kimsingi, watendaji wanapaswa kutumia eneo maalum la kuhifadhi ambalo linasimamiwa na kampuni ya ulinzi, hata kama shirika lao linabaki kuwa ndiyo lenye "umiliki" wa taarifa.
2. Hifadhi taarifa ambazo zinabainisha aliyenusurika/shahidi tofauti na kwa usalama kutokana na kauli na ushahidi uliotolewa na aliyenusurika/shahidi (kwa mfano kielelezo cha kulinganisha namba za siri na taarifa/majina fulani yanayotambulika ambayo ni ya walionusurika/mashahidi).
3. Ambapo inawezekana, epuka kuhifadhi habari nyeti za umma kwa pamoja, ili kuhakikisha ulinzi bora wa hili.
4. Panga taarifa ili iweze kupatikana kirahisi na kwa mantiki pale itakapohitajika.
5. Funza wafanyakazi katika taratibu sahihi kwa: (i) kuhamisha taarifa zilizohifadhiwa pale mafaili yatakapofungwa; na (ii) weka salama taarifa hizi wakati wa dharura au uokoaji.
6. Beba taarifa ambazo ni muhimu kabisa tu pale unapofanya safari ambayo huenda ikawa na vituo vya ukaguzi, kwa vile watendaji wanaweza kuulizwa kufichua au kutoa taarifa wanayoihifadhi kwenye mwili wao au katika gari lao. Fikiria matumizi ya teknolojia ili kuhifadhi na/au kuficha taarifa kwa kuenkraipti.

## 9.1 Kuhifadhi nyaraka na taarifa nyingine zilizo dhahiri

- Kama watendaji wanahifadhi taarifa katika mfumo wa nyaraka au vitu vingine vilivyo dhahiri, wanapaswa kuweka habari katika kabati lililofungwa au sefu salama ambalo upatikanaji wake ni mdogo. Kuna haja ya kuwa na sera ya wazi juu ya nani anaweza kupata taarifa na nini.

- Katika mazingira ya dharura, inaweza kuwa muhimu kuhakikisha usalama binafsi wa hao wafanyakazi ambao wanashughulika na kuhifadhi taarifa.

- Kuweka rekodi ya ruhusa zilizotolewa ili kupata taarifa kutoka kwenye kabati (kwa mfano jina la mtu, tarehe, muda na lengo la kuingia viwekwe kama kumbukumbu).

- Kama taarifa inaweza kuharibika (kwa mfano negativu za picha za kawaida), ziweke mbali na joto na mwanga.

- Kama taarifa ni sehemu ya seti (kwa mfano mkusanyiko wa nyaraka au picha zilizochapishwa), zifunge na kikaratasi kinachoelezea seti kamili ina vitu gani.

- Ni lazima kuorodhesha ndani ya mfumo imara wa kihisabati rekodi za picha zote na video (na taarifa zingine zilizo dhahiri), na mfumo huo wa kuorodhesha unapaswa kuunganishwa na ushahidi mwingine thabit hasa kuhusiana na picha/video hizo (mfano ushahidi wa aliyenusurika/shahidi).

- Kama rekodi ya sauti au video imefanywa kwa madhumuni mengine na si kurekodi mahojiano tu, ni lazima mtu anayewajibika awe na uwezo wa kuhalalisha kuendelea kuhifadhi huko na atoe maelezo ya kuhifadhi siri ya wale watu walioshiriki katika rekodi, hasa kama rekodi hiyo itahifadhiwa kwa muda wowote mrefu.

## 9.2 Kuhifadhi taarifa za dijitali

- Faida za kutumia mfumo wa dijitali kuhifadhi (pale ambapo hii inapatikana) badala ya mfumo wa kuhifadhi wenye kiwiliwili (kama vile makaratasi), ni kwamba mfumo wa dijitali hauchukui nafasi dhahiri ya kiwiliwili, kwa kawaida huwezesha kutafuta kirahisi na uchambuzi, na kwa kawaida ni rahisi kuboresha na kutoa ripoti zake na huweza kulindwa kwa kiasi fulani. Hata hivyo, ubaya wa mfumo wa dijitali kuhifadhi ni kwamba unaweza kuchukua muda mwingi zaidi kuingiza data, upatikanaji unategemea ugavi wa umeme na wakati mwingine upatikanaji wa mtandao. Pia mfumo huweza kukabiliwa na kuporwa kitaalam au virusi. Zaidi ya hayo, kama taarifa inapitia kwenye simu za mkononi au kupitia mtandao wa intaneti, kuna hatari ya mamlaka kuwalazimisha watoa huduma ya simu au intaneti kuwakabidhi habari nyeti.

- Kabla ya kuanza kukusanya taarifa ambazo zitahifadhiwa kidijitali, tathmini ya athari ifanywe na itifaki ya usalama wa dijitali iwekwe. Wasimamizi wa taarifa na wataalamu wa usalama wa dijitali waulizwe ushauri kwa ajili hiyo.

- Taarifa zote za dijitali lazima zilindwe kwa neno la siri (na upatikanaji wa neno la siri uwe mdogo) na siri ifichwe kutumia mtindo wa kuenkraipti. Pale inapowezekana, watendaji wanapaswa kuchukua hatua za ziada ili kulinda taarifa nyeti kwa kutumia taratibu za ziada na mbinu kama vile kuenkraipti na kuhakikisha upatikanaji salama wa taarifa za dijitali.[44]

- Katika mazingira ya dharura, inaweza kuwa muhimu kuhakikisha usalama binafsi wa wale wafanyakazi wanaoyajua hayo maneno ya siri.

44 Kwa mwongozo wa ziada juu ya usalama wa data, angalia ICRC, Professional Standards for Protection Work, 2013 toleo lenye marekebisho, hasa Sura ya 6 katika kusimamia taarifa nyeti.

- Kama taarifa ni ya dijitali, hamisha yaliyomo kwenye kompyuta, chomea CD ya aina ya WORM (Andika Mara moja, Soma mara nyingi) au hifadhi taarifa kwenye ufunguo wa kumbukumbu. Nakala mbili zifanywe.

- Chukua tahadhari sahihi kama vile programu za kupambana na virusi na kuweka hifadhi ya mafaili ya data, yaani 'back-up'.

- Fikiria kuhusu kutumia vifaa kabambe vya ukusanyaji wa data, kama vile kamera za GPS, programu za App za kwenye simu ya mkono ambazo hukusanya taarifa mbalimbali za ziada (yaani taarifa kuhusu lini, wapi na jinsi data zilivyokusanywa), na App za nyaraka za simu za mkononi ambazo kimsingi hufanya siri kwa kutumia tendo la kuenkraipti data zote.

- Fikiria kutumia App za ukusanyaji wa data kwenye simu za mkononi ambazo hazihifadhi nakala za data kwenye simu, hivyo kupunguza hatari ya kuonekana kwa data nyeti kama kifaa kitapotea, kitaibiwa au kitanyang'anywa. Thamani ya ziada ya kutumia programu za App ili kusambaza data kwenye seva (server) iliyo mbali ni kutunzwa kwa "Mlolongo wa Utunzaji".

- Inaweza kuwa sahihi kutumia njia ya kuhifadhi data inayoitwa 'cloud' – yaani mbingu, pale unapohifadhi taarifa. Faida ya mifumo kama hii ni pamoja na kuzuia uharibifu ulio dhahiri unaoweza kutokea kwenye vifaa vya kuhifadhi, uwezekano wa kuvitumia kwa umbali wowote na kuwa na kazi ziada. Kama unatumia kwa kupitia huduma za biashara, lazima kuchukua tahadhari kubwa ili kuhakikisha uadilifu wa data, umiliki na upatikanaji wa data uwe wa kipekee.

- Kuwa na orodha ya mlolongo wa kuhariri kwenye msingi wa data ili mabadiliko yoyote kwenye maandishi au kumbukumbu yaingizwe kufuatana na mtumiaji fulani.

### 9.3 Kuhifadhi matibabu kisheria/ushahidi wa kisayansi kuhusu uhalifu (forensiki)

- Hii ifanywe tu na wale wenye mafunzo katika ukusanyaji wa ushahidi wa matibabu kisheria (kwa mfano damu, shahawa au nguo zilizochafuliwa). Kama watendaji hawajapata mafunzo katika ukusanyaji wa ushahidi wa matibabu kisheria/ushahidi wa kisayansi kuhusu uhalifu (forensiki) wanaweza kusababisha madhara zaidi kuliko mema yoyote kwa kukusanya vitu hivi **(angalia Nyongeza 6, "Ushahidi Dhahiri: Kanuni za mlolongo wa utunzaji" na Nyongeza 10, "Mfano wa Cheti cha Uvamiaji wa Kijinsia")**.

- Uchunguzi wa tiba inayohusu ushahidi wa kisayansi kuhusu uhalifu (forensiki)/mkusanyiko wa ushahidi wa matibabu na sheria ufanywe wakati mmoja na utoaji wa huduma za afya - na walau iwe na mtu huyo huyo **(angalia Nyongeza 10, "Mfano wa Cheti cha Uvamiaji wa Kijinsia").**

- Kama ushahidi ni wa kibaiolojia (kama vile damu, shahawa au mavazi) na watendaji wana mafunzo ya kukusanya vitu hivi, ni lazima taarifa hii ifungwe kwenye vyombo tofauti na ipelekwe maabara mara baada ya ukusanyaji, kwani kuna uwezekano kwamba itahitajika kuwekwa kwenye friji au kugandishwa kama barafu.

- Kwa mwongozo wa ziada kuhusu kukusanya ushahidi wa kimatimabu wa kisayansi kuhusu uhalifu (forensiki), watendaji wanapaswa washauriane na World Health Organization Guidelines on Clinical Management of Survivors of Rape: A Guide to the Development of Protocols for Use in Refugee and Internally Displaced Person Situations, 2004; na PHR, OHCHR, Istanbul Protocol: Manual on the Effective Investigation and Documentation of Torture and Other Cruel, Inhuman or Degrading Treatment or Punishment, 1999.



# BIBLIOGRAFIA

## Vyanzo

1. Amnesty International, International Criminal Court: Updated Checklist for Effective Implementation, London 2010

2. Amnesty International, Agnes Callamard, A Methodology for Gender-Sensitive Research, 1999

3. ICC, Draft Policy Paper on Sexual and Gender Based Crimes, February 2014, www.icc-cpi.int/iccdocs/otp/otp-draft-policy-paper-february2014-eng.pdf

4. ICRC, Professional Standards for Protection Work, 2013, revised edition

5. ICRC, Sexual violence in armed conflict: questions and answers, 7 March 2014

6. Institute for International Criminal Investigations (IICI), Investigator's Manual 7th Edition, 2013

7. Institute of Medicine, Social and Economic Costs of Violence Against Women: The Value of Prevention, 2011

8. IRC, UNICEF, Caring for Child Survivors of Sexual Abuse: Guidelines for Health and Psychosocial Service Providers in Humanitarian Settings, 2012

9. OHCHR, PHR, Istanbul Protocol: Manual on the Effective Investigation and Documentation of Torture and Other Cruel, Inhuman or Degrading Treatment or Punishment, 1999

10. OHCHR, Monitoring the Convention on the Rights of Persons with Disabilities – Guidance for Human Rights Monitors (Professional Training Series No. 17)

11. Save the Children, Children, Not Soldiers: Guidelines for Working with Child Soldiers and Children Associated with Fighting Forces, 2001

12. UN Action, Reporting and Interpreting Data on Sexual Violence from Conflict-Affected Countries: "Dos And Don'ts", 2008

13. UNHCR, Sexual and Gender-Based Violence against Refugees, Returnees, and Internally Displaced Persons: Guidelines for Prevention and Response, 2003

14. UNICEF, Innocenti Research Centre, Innocenti Insight: Birth Registration and Armed Conflict, 2007

15. UNICEF, The Paris Principles. Principles and Guidelines on Children Associated With Armed Forces or Armed Groups, February 2007

16. UNICEF, UNODC, Guidelines on Justice Matters Involving Child Victims and Child Witnesses of Crime, 2005

17. WHO, Ethical and Safety Recommendations for Researching, Documenting and Monitoring Sexual Violence in Emergencies, 2007

18. WHO, Clinical Management of Survivors of Rape. A Guide to the Development of Protocols for Use in Refugee and Internally Displaced Person Situations, 2004

19. Women's Initiatives for Gender Justice, Gender in Practice: Guidelines and Methods to Address Gender Based Crime in Armed Conflict, 2005

20. World Bank, The Costs and Impacts of Gender-Based Violence in Developing Countries: Methodological Considerations and New Evidence, 2004

## Vitabu vya Ziada

21. Amnesty International, CODESRIA, Ukweli: Handbook on Monitoring and Documenting Human Rights Violations in Africa, 2000

22. Amnesty International, International Centre for Human Rights and Democratic Development, Investigating Women's Rights Violations in Armed Conflict, 2001

23. Amnesty International, Rape and Sexual Violence: Human Rights Law and Standards in the International Criminal Court, 2001

24. Bassiouni, M. Cherif, International Crimes: Jus Cogens and Obligatio Erga Omnes, Law and Contemporary Problems, 1996

25. Bergsmo, Morten (editor), Thematic Prosecution of International Sex Crimes, 2012

26. de Brouwer Anne-Marie, et al. (editor), Sexual Violence as an International Crime: Interdisciplinary Approaches, Intersentia, 2013

27. Hitesh, Raval, Tribe, Rachel, Working with Interpreters in Mental Health, 2002

28. Human Rights Council, Report of UN Special Rapporteur On Violence Against Women, 2010

29. IASC, Guidelines for Gender-Based Violence Interventions in Humanitarian Settings, Geneva 2005

30. ICTR, Best Practices Manual for the Investigation and Prosecution of Sexual Violence Crimes in Situations of Armed Conflict: Lessons from the International Criminal Tribunal for Rwanda, 2008

31. ICTR, Best Practices Manual for the Investigation and Prosecution of Sexual Violence Crimes in Post-Conflict Regions: Lessons Learned from the O→ffice of the Prosecutor for the International Criminal Tribunal for Rwanda, 2014

32. ICTY-UNICRI, Manual on Developed Practices, 2009

33. Inter-Agency Standing Committee (IASC), IASC Guidelines on Mental Health and Psychosocial Support in Emergency Settings, 2007

34. Isikozlu, Elvan, Millard, Ananda S., Brief 43: Towards a Typology of War Time Rape, BICC, 2010

35. No Peace Without Justice, Closing the Gap: The Role of Non-judicial Mechanisms in Addressing Impunity, 2010

36. OHCHR, Training Manual on Human Rights Monitoring, PTS number 7, 2001 and 2011

37. Population Council, Ethical Approaches to Gathering Information from Children and Adolescents in International Settings: Guidelines and Resources, 2005

38. Redress/Vahida Nainar, Litigation Strategies for Sexual Violence in Africa, 2012

39. Redress, Nairobi Declaration on Women's and Girls' Right to Remedy and Reparation, March 2007

40. Sá Couto, Susana, Investigation and Prosecution of Sexual and Gender-Based Violence by the International Criminal Court: Mandate, Good Policy, or Both? 2012

41. Save the Children, Policy Brief – Unspeakable Crimes: Changing the Law, London 2013

42. Save the Children, So You Want to Involve Children in Research: A Toolkit Supporting Children's Meaningful and Ethical Participation in Research Relating to Violence Against Children, 2004

43. Schenk, Katie, Williamson, Jan, Ethical Approaches to Gathering Information from Children and Adolescents in International Settings: Guidelines and Resources, Population Council, 2005

44. Sivakumaran, Sandesh, Sexual Violence Against Men in Armed Conflict, The European Journal of International Law, Vol. 18, 2007

45. UN Action Against Sexual Violence in Conflict, Analytical and Conceptual Framing of Conflict-Related Sexual Violence, New York, May 2011

46. UNHCR, Working with Men and Boy Survivors of Sexual and Gender-Based Violence in Forced Displacement. Guidance Note (4), 2012

47. UNICEF, Children Participating in Research, Monitoring and Evaluation (M&E): Ethics and Your Responsibilities as a Manager, 2002

48. Women's Initiatives for Gender Justice, Modes of Liability: A Review of the International Criminal Court's current Jurisprudence and Practice, 2013

49. Women's Initiatives for Gender Justice, Sexual Violence and International Criminal Law: An Analysis of the Ad Hoc Tribunal's Jurisprudence and the International Criminal Court's Elements of Crimes, 2005

Nataka kuwaambia dunia kuwa tunahitaji amani – acheni vita

Tunahitaji kuhakikisha kuwa wanawake na watoto wanalindwa

Wabakaji wanahitaji kukamatwa.

**Felicite (siyo jina lake la ukweli, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo DRC)**

NYONGEZA 1

# Nyongeza 1

## Kitabu cha ushahidi cha nyaraka za uhalifu wa kijinsia: Kifaa cha kusaidia wapelelezi kuziba mapengo ya ushahidi

**Onyo: Kabla ya kutumia mfumo huu kuandaa zoezi lako la kutengeneza nyaraka, ni lazima ufanye vifuatavyo:**

**A. Fikiria kwa makini iwapo wewe ndiye mtu unayefaa kukusanya taarifa hizi kwa ufanisi na kwa usalama.**

**B. Fikiria kwa makini masuala yote ya hatari ya usalama kwa aliyeathirika, taarifa zake, familia na jumuiya yake, na timu ya kukusanya nyaraka.**

**C. Fikiria kanuni za msingi, kama zilivyowekwa kwenye muhtasari wa Nyongeza 3.**

## Utangulizi wa kitabu cha kazi za ushahidi

Kitabu cha kazi za ushahidi ni kifaa kilichopendekezwa kama nyenzo na wale wanaokusanya ushahidi wa uhalifu wa kimataifa Kitabu cha ushahidi kinasaidia watendaji kuhakikisha kuwa, wanapochunguza na kuhakiki nyaraka za uhalifu ulioshutumiwa, hayaachwi mapengo kwa upande wa mahojiano/nyaraka na mtu au kwa upande wa uchunguzi kijumla. Yaliyomo kwenye hiki kitabu yamekita kwenye maainisho ya uhalifu na vipengele vya uhalifu, kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Roma na vipengele vya Uhalifu ya Mahakama ya Kimataifa ya Jinai (ICC). Hata hivyo, muundo unahusu masuala yote ya ushahidi na unaweza ukabadilishwa kuambatana na mazingira husika. Jinsi kitabu cha kazi za ushahidi kilivyoundwa, kinaweza kurudiwa, kuakisi uainisho na vipengele vya ukiukaji wowote, kwenye mamlaka yoyote ambapo uhalifu unapelelezwa. Hiki chombo kinakusudiwa kusaidia kukuza ufanisi wa mchakato wa kukusanya ushahidi, na kulinda mashahidi kutokana na mahojiano yanayorudiwa rudiwa, kurahisisha tathmini ya vidokezo, na kupunguza haja ya kurudi kwenye maeneo ya kazi ili kukusanya ushahidi wa nyongeza ili kuziba mapengo Wataalamu wa kuhifadhi nyaraka za haki za binadamu wanaweza kutumia kitabu cha kazi za ushahidi kama chombo, cha kupanga taarifa wanazokusanya – kubadilisha kama itakavyobidi na kukusanya ushahidi wa jukumu la taifa, badala ya jukumu la kibinafsi. Unapofanya kazi kwa mujibu wa mfumo wa kitabu cha kazi na kukijaza kwa ushahidi wa kina kwa jinsi iwezekanavyo, ushahidi unaokusanywa na wataalamu wa kuweka nyaraka za haki za binaadamu, utakuwa na manufaa kwa kijumla, pindi kukiwepo na mfumo wa utoaji haki au mfumo wa utoaji haki wa mpito, iwe kitaifa au kimataifa.

Kitabu cha kazi cha ushahidi kimegawanywa katika sehemu tatu, kama ifuatavyo

## Sehemu A: Vipengele vya hatia maalumu

**Nini kilitokea (tendo gani lilifanyika)?**

| NINI KILITOKEA? (kwa uhakika na kwa kina, nani, nini, lini, wapi, kwa nini, vipi na unajuaje?) | Mifano ya MASWALI kuhusu NINI KILITOKEA | Mifano ya USHAHIDI/ TAARIFA inayoelezea nini kimetokea |
|---|---|---|
| Ushahidi/taarifa gani unahitaji kukidhi Kipengele cha 1 cha uhalifu? | Maswali gani unaweza kuuliza ili kupata ushahidi kutosheleza Kipengele 1? | Nini mfano wa taarifa unazoweza kupata zitakazotosheleza Kipengele 1? |
| Ushahidi/taarifa gani unahitaji ili kutosheleza Kipengele 2 cha uhalifu huu? | Maswali gani unaweza kuuliza ili kutosheleza Kipengele 2? | Nini mfano wa taarifa ambazo utaweza kupata zitakazotosheleza Kipengele 2? |

## Sehemu B: Vipengele vya aina ya uhalifu (hatia za kivita, uhalifu wa utu na mauaji ya kimbari)

**Tendo lilifanyika katika mazingira gani?**

| TENDO LILITENDWA KATIKA MAZINGIRA GANI? | Mifano ya MASWALI kuhusu MAZINGIRA AMBAYO TENDO LILITENDWA | Mifano ya USHAHIDI/ TAARIFA itakayoweza kusaidia kuthibitisha kuwa tendo hili ni uhalifu dhidi ya ubinaadamu, uhalifu wa kivita au mauaji ya kimbari |
|---|---|---|
| Ushahidi/taarifa gani utahitaji kutosheleza Kipengele 1 cha aina hii ya uhalifu (yani uhalifu, uhalifu dhidi ya ubinaadamu au mauaji ya kimbari)? | Maswali gani unaweza kuuliza ili kupata ushahidi wa kutosheleza Kipengele 1 cha aina ya uhalifu? | Nini mfano wa taarifa unayoweza kupata itakayotosheleza Kipengele 1 cha aina ya uhalifu? |

## Sehemu C: Mfumo wa dhima

### Mshutumiwa alifanyaje tendo hilo?

| NANI ANAWEZA KUHUSIKA, na VIPI? | Mifano ya maswali ambayo yatadhihirisha taarifa kuhusu nani anaweza kuhusika | Mifano ya USHAHIDI/ TAARIFA ambayo itasaidia kuthibitisha kuwa mtu huyu au watu hawa wanaweza kuhusika na matendo haya na kwa jinsi hii |
|---|---|---|
| Ushahidi/taarifa gani unahitaji kutosheleza Kipengele 1 cha hali ya dhima (kwa mfano, kuagiza au kuamuru kuwajibika)? | Nini mfano wa maswali ambayo unaweza kuuliza ili kupata ushahidi kutosheleza Kipengele 1 cha hali ya dhima? | Nini mfano wa ushahidi unaoweza kupata utakaotosheleza Kipengele 1 cha hali ya dhima? |

Zinafuata chati za Sehemu A, B na C ya zoezi la kutengea nyaraka. Hizi zina mifano ya kina inayoeleza jinsi ya kuhakikisha kuwa maeneo yote ya taarifa yameingizwa kwenye mchakato wa kukusanya ushahidi.

**Ukumbusho muhimu:** Maswali haya - kwa mujibu wa mpangilio wa sehemu zote tatu - hayakukusudiwa kutumika kama kigezo cha mahojiano. Iwapo yatatumika kihivyo, yanaweza kusababisha mhojaji kukusanya taarifa zisizo kamili au zisizo sahihi; au vibaya zaidi, yanaweza kusababisha uharibifu kwenye ushuhuda wa mwisho wa matokeo au madhara kwa shahidi. Hapana kigezo kitakacho tengenezwa ambacho kitatosholeza sehemu zote za kumhoji shahidi. Haya maswali ni mifano, inayoelezea kwa maneno machache uwezekano wa njia tofauti ambazo ushahidi unaweza kupatikana kutoka kwa shahidi. Wahojaji wanashauri sana kutumia hiki kitabu cha kazi kama mwongozo kuhakikisha kuwa maeneo yote ya maelezo yanayohitajika yametekelezwa, badili ya kutumika kama kigezo kwa mahojiano, na kuhakikisha kuwa wanatumia ujuzi wa mahojiano uliopatikana kwenye mafunzo na unaofuata kanuni zilizowekwa kwenye Itifaki hii. Inasaidia kukumbuka kanuni ya "TED" kila mara. "Niambie, Nifafanulie, Nielezee." Hii kanuni inatumika kwa mahojiano yoyote - pamoja na mahojiano yanayohusu ushahidi wa unyanyasaji wa kijinsia

Mazingira halisi yasiyoelezwa kwenye safu ya tatu ni maelezo ya michoro inayoonyesha aina za ushahidi zitazoweza kusaidia vipengele maalumu vya huo uhalifu.

## Sehemu A: Nini kilitokea (tendo gani lilifanyika)?

### Mateso [45]

### Vipengele:

1) Mhalifu alimwumiza vibaya kimwili au kumpa maumivu ya kisaikolojia au kumpa mateso mtu mmoja au zaidi.

45 Kwenye mamlaka mengine ya ndani ya nchi, mashtaka ya kosa la kutesa huendeshwa kama kosa la kipekee (yaani sio tu kwenye utaratibu wa hatia za kivita, uhalifu dhidi ya utu au mauaji ya kimbari.) Itabidi watendaji kwenye mamlaka hizi warekebishe vipengele wanavyojaribu kukidhi kwa mujibu wa sheria husika za ndani ya nchi.

2) Mtu au watu husika walikuwa kwenye kifungo au udhibiti wa mtuhumiwa.

3) Uchungu huu na mateso hayo, hayakutokana tu, na asili na wala haikuambatana na, vikwazo halali.

4) Mtuhumiwa alisababisha uchungu na mateso kwa nia ya: kupata taarifa au mtu kukiri, adhabu, matisho au shurutisho, au kwa sababu yoyote inayotokana na ubaguzi wa aina yoyote (inatumika kwenye hatia za kivita tu).

| NINI KILITOKEA? (Umepata taarifa zinazosaidia kuonyesha kwamba tuhuma hizi za utesaji zilitendeka?) | Mifano ya MASWALI kuhusu NINI KILITOKEA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA inayoelezea nini kimetokea |
|---|---|---|
| Ni vitu gani halisi vinasaidia kuthibitisha kuwa mtuhumiwa alimpa maumivu makali sana ya kimwili au kiakili mtu mmoja au zaidi (kipengele cha kwanza)? | Unaweza kunieleza, kwa uhakika, nini hasa kilitokea? Iwapo utaweza kuelezea kwa kina alichofanya baadaye tu, kama ulivyosema, kwamba alikutupa chini kwenye sakafu juu ya rundo la matambara, tafadhali fanya hivyo? Unaweza kuniambia ulijisikiaje wakati unafanyiwa hilo? | **Ushahidi:**[46] "Alinivuta kwenye pembe ya chumba na kunitupa kwa nguvu kwenye rundo la matambara sakafuni. Katika hatua hiyo mimi nilikuwa na uoga mtupu, nikijua vizuri nini kitatokea, na kuwa na hofu kuwa nitapoteza mtoto wangu kwani nilikuwa na ujauzito wa miezi minne tu. Nilikuwa natetemeka kwa hofu na nikaanza kutapika. Alitupa matambara juu ya uso wangu kufunika matapishi, akachana nguo zangu kutoka kiunoni kwenda chini, akanipiga kunigeuza kwa pembeni na mguu wake, akatoa uume wake, na kuuingiza uume wake kwenye mkundu wangu. Maumivu yalikuwa hayavumiliki na kunguruma kwangu hakukuacha ingawa tumbo langu lilikuwa tupu. Ni Mungu aliyemlinda mtoto wangu, na mtoto wangu akaishi."[47]<br><br>**Ushahidi mbadala:** "Walitufanya tukusanyike uani kila siku, na kamanda alikuwa akienda na kurudi huku akituangalia na kutushika kabla ya kuchagua msichana mmoja. Alituambia kuwa ilikuwa ni ya msichana huyo |

46 Aina tatu za ushahidi zimeoneshwa kama mifano kwenye vitabu vingine vya kazi vya ushahidi, lakini siyo kwenye vifungu vyote. Kwa kila kipengele cha uhalifu ambao inabidi kuthibitishwa, kunaweza kuwepo ushahidi wa maandishi, wa nyaraka na wa picha/video. Ni vizuri zaidi kuwa na ushahidi mwingi zaidi, ila kutokuwa na ushahidi wa nyaraka na ushahidi wa picha/video au kutokuwa na ushahidi wa maandishi uliobainishwa haimaanishi kuwa ushahidi wa maandishi wa aliyenusurika au aliyeshuhudia tukio kwa macho yake haitotosha kuwa msingi wa shutuma za ukiukaji au uhalifu huo. Kwahakika, mara nyingi ushahidi wa maandishi ndiyo ushahidi pekee unaopatikana kwenye uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia, na kesi za kimataifa za makosa ya jinai zimeletwa (na watuhumiwa kupatikana na hatia) kwa uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia kutokana na ushahidi wa maandishi wa aliyenusurika au aliyeshuhudia tukio kwa macho yake tu. Kwa kanuni za kawaida za utaratibu na ushahidi, kwenye desturi za kimataifa za kesi za uhalifu, ushahidi wa maandishi wa aliyenusurika, hauhitaji kubainishwa katika uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia. Hata hivyo, mara kwa mara, ushahidi uliobainishwa huhitajika kwenye sheria za kitaifa. Wapelelezi wanatakiwa kufahamu kuwa aina tofauti za ushahidi zipo. Na inapowezekana kutafuta ubainishaji, kwa jinsi kesi ilivyo, kuruhusu mashtaka yafunguliwe kitaifa; ambapo kesi nyingi zinatakiwa kufunguliwa na mashtaka kuendeshwa. Hata hivyo, inashauriwa kujaribu kuto kukata shauri kuhusu uzito wa ushahidi kutokana tu na kutokuwa na ushahidi wa nyaraka, picha/video, au shahidi wa kubainisha ushahidi wa ukiukaji.

47 Ukumbusho kuwa mifano ya ushahidi haikusudiwi kuwa yote itoke kwenye shahidi huyo huyo, hata kwenye vipengele hivyo hivyo vya uhalifu. Nia ni kumpa msomaji, kama iwezekanavyo, uwezekano tofauti wa mazingira halisi ambayo yatakidhi vipengele fulani.

| NINI KILITOKEA? (Umepata taarifa zinazosaidia kuonyesha kwamba tuhuma hizi za utesaji zilitendeka?) | Mifano ya MASWALI kuhusu NINI KILITOKEA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA inayoelezea nini kimetokea |
|---|---|---|
| | | zamu leo, lakini itakuwa ni mmoja wetu kesho. Alimfanya mtu aliyemchagua avue nguo zake zote na kisha kumdondosha chini na kuwaachia wanajeshi wakiwaingilia kwa nguvu, mbele ya kila mtu. Tukijaribu kutoangalia au kuficha sura zetu walinzi walituzabua vibao au kutupiga."[48]<br><br>**Ushahidi Mbadala:** "Walinipeleka kwenye chumba ghorofa ya pili kila siku na kunihoji. Wakinifungia kwenye kiti kilichokamatana na ukuta, kisha kamba kuzunguka uume wangu na korodani/pumbu zangu. Upande wa pili wa kamba ilifungiwa na kitasa cha mlango, na nilivyowapa jibu wasilolipenda, walibamiza mlango. Nilikuwa kwenye maumivu makali mno, lakini nikinung'unika au wakiniona nimeshtuka walivuta kamba kwa nguvu/ghafla na kunipiga kwenye viungo vya uzazi. Siku moja walifunga kamba kwenye tofali na kutishia kuwa watalitupa nje ya dirisha. Walikuwa wanashindana iwapo uzito utatosha kuukata uume wangu au kama nitakufa kutokana na kupoteza damu, Waliniunguza na visu vya moto na kutishia 'kunifanya mwanamke' iwapo sitowaambia wanachotaka."<br><br>Ushahidi wa Nyaraka: Shahidi anakupa nyaraka za matibabu zilizoandikwa na madaktari waliopata mafunzo ya kuhakikisha uratibu kati ya watendaji wa kiafya na kisheria wanaofanya kazi pamoja kusaidia walionusurika. Hizi nyaraka za matibabu zinaonyesha kwa kina hali ya afya ya shahidi siku ya baada ya matokeo aliyoyaelezea, na pia taarifa. |

48 Kulazimishwa kushuhudia mtu mwengine akibakwa au kuvamiwa kijinsia, imeonekana kusababisha maumivu ya kisaikolojia au mateso ya kutosha kufanya kitendo chenyewe kuwa cha mateso Zaida ya haya, kulazimishwa kufanya kitendo cha kujamiiana mbele ya hadhara (kama wafungwa wawili ambao wanalazimishwa kusisimuana uume "fellatio" mbele ya walinzi) au kubakwa au kuvamiwa kijinsia mbele ya hadhara au watu wa familia yake, pia inaweza kuwa kitendo cha mateso.

| NINI KILITOKEA? (Umepata taarifa zinazosaidia kuonyesha kwamba tuhuma hizi za utesaji zilitendeka?) | Mifano ya MASWALI kuhusu NINI KILITOKEA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA inayoelezea nini kimetokea |
|---|---|---|
| | | kuhusu nini ameripoti juu ya majeraha yake. Ripoti ya matibabu inaelezea, miongoni mwa majeraha mengine, mbavu zilizovunjika na kuchunika pembeni, na kuchanika katika batana ya mkundu.<br><br>**Picha/video:** Shahidi anakupa picha za majeraha. **Kimwili:** Umeweza kuingia kwenye eneo la uhalifu. Unapiga picha za eneo la uhalifu kwa makini. Iwapo unapata vibali kutoka kwenye mamlaka, na iwapo una ujuzi na uwezo wa kufanya hivyo, kusanya baadhi ya matambara yaliyobaki, Tayarisha nyaraka zinazohusu ushahidi unaoonekana, na hifadhi ushahidi huo kwa usalama na ipasavyo kwa ajili ya matumizi katika siku zijazo kwenye kesi jinai. [49] |
| Hali ipi halisi itasaidia kuthibitisha kuwa mtu (au watu) hao walikuwa kwenye kifungo au chini ya udhibiti wa mhalifu (kipengele cha pili cha utesaji)? | Yepi yalikuwa mazingira ambayo ulipelekwa sehemu hiyo? Nani walikuwa wahalifu? Unaweza kuniambia iwapo kulikuwa na mtu mwengine yeyote kwenye chumba hicho wakati lilivyokuwa linatokea? Unaweza kuelezea mtu aliyekua anakufanyia hivyo alikuwa ameshika nini, kama alikuwa ameshika kitu? Alikwambia nini? Nani mwingine alikuwepo, iwapo kulikuwa na mtu mwengine? Walikuwa wameshika nini? Walikuwa wamevaa nini? Walikwambia nini? Je ungeweza kuondoka? Kwa nini, au kwa nini usingeweza? | **Ushahidi:** "Alikuwa hapo na rafiki yake, mlinzi mwingine, aliyesimama mlangoni akisukuma watu nje waliokuja kuona kelele zilihusu nini? Wote wawili walikuwa na silaha, na yule aliyekuwa ananishambulia mimi aliweka silaha yake pembeni ya rundo la matambara wakati ananishambulia Aliyekuwa ananishambulia aliniambia kuwa nikijaribu kukimbia atanipiga hadi mtoto wangu afariki. Aliniambia kuwa anachonifanyia kitawaonyesha wanaume wa jamii yangu nini wategemee kutokea iwapo hawatoondoka kwenye sehemu ile." |

49 Tafadhali kumbuka kuwa kikawaida haishauriwi, kwa mtendaji asiye na mamlaka, kukusanya ushahidi unaoonekana. Zaidi ya hayo, hata na mamlaka, bila uzoefu wa kukusanya na kuhifadhi ushahidi unaoonekana, ukusanyaji wa ushahidi huo haushauriwi. Kwa nadra - mfano kukiwa hamna uwezekano wa ushahidi unaoonekana kukusanywa na iwapo kuna uoga wenye msingi kuwa ushahidi utachezewa au utaharibiwa - watendaji wamaweza kujikuta kwenye hali ambayo wakaaamua kukusanya ushahidi unaoonekana dhahiri. Kwenye hali kama hiyo, hao watendaji wanasisitizwa kufuata mwongozo wa ukusanyaji wa ushahidi unaoonekana, kama ulivyoainishwa kwenye Itifaki. Pia kusoma mengine zaidi yaliyo kwenye Itifaki, na kuhakikisha kuwa ushahidi unalindwa.

| NINI KILITOKEA? (Umepata taarifa zinazosaidia kuonyesha kwamba tuhuma hizi za utesaji zilitendeka?) | Mifano ya MASWALI kuhusu NINI KILITOKEA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA inayoelezea nini kimetokea |
|---|---|---|
| Mambo gani halisi yanathibitisha kuwa maumivu na mateso hayo, hayakutokana tu na, hayakuwa na asili ya au kuambatana na, vikwazo halali (kipengele cha tatu cha utesaji)? | Yepi yalikuwa mazingira ambayo ulipelekwa sehemu hiyo? Nani walikuwa wahalifu? Ni kundi/lenye muundo wa mamlaka gani walikuwemo ndani, na unajuaje?[50] Waliwahi kuelezea kwanini ulikua unashikiliwa na kuteswa? | **Ushahidi:** "Kulikuwa na mashambulizi kwenye kijiji chetu na wanaume wote walizingirwa na kuondolewa. Wakati huo tulikuwa hatujui walikuwa wanapelekwa wapi, lakini baadaye tulijua kuwa wengi wao walipigwa risasi na kutupwa kwenye mto. Wanawake na wasichana vijana waliwekwa shule ambapo tuliwekwa chini ya ulinzi wa askari wenye silaha kwa wiki kadhaa. Wazee na watoto wengine au waliachwa majumbani kwao au waliwekwa shule na wanawake na wasichana vijana; ilikuwa ni kwenye hii shule ndiyo matokea niliyoyaelezea yalitokea." |

## Ubakaji

### Vipengele:

3) Mtuhumiwa aliuvamia[51] mwili wa mwingine kwa mwenendo uliosababisha kumuingilia, hata ikiwa kidogo, sehemu yoyote ya mwili wa mwathiriwa au wa mtuhumiwa na sehemu ya siri, au kwenye mkundu au uwazi wa sehemu ya siri wa mwathirika kwa kutumia kitu chochote au sehemu nyengine ya mwili.

4) Uvamiaji ulifanyika kwa nguvu, au kwa tishio la kutumia nguvu au shurutisho, kama inayosababishwa na woga wa vurugu, shinikizo, kifungo, ukandamizaji wa kisaikolojia au matumizi mabaya ya madaraka, dhidi ya mtu huyo au mtu mwengine; Au kwa kutumia vibaya mazingira ya kushawishi, au uvamizi ulifanyika dhidi ya mtu asiyeweza kutoa indhini halisi.

50 Kumbuka kuwa mifano mingi ya maswali yaliyomo kwenye kitabu hiki cha kazi, yanachukulia kuwa maswali mengine yameshaulizwa wakati wa mahojiano yaliyopita.

51 Vipengele vya Uhalifu wa Sheria ya Roma inaashiria kuwa "dhana ya 'uingilizi' imekusudiwa kuwa pana kiasi cha kutofungamana na jinsia yeyote".

NYONGEZA 1

| NINI KILITOKEA? (Umepata taarifa zozote zinazosaidia tuhuma ya kuwa ubakaji ulitokea?) | Mifano ya MASWALI kuhusu NINI KILITOKEA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA inayoelezea nini kimetokea |
|---|---|---|
| Mambo gani halisi yamethibitisha kuwa mtuhumiwa aliuvamia mwili wa mtu mwingine kwa njia ambayo matokeo yake yalikuwa kuingiliwa mwilini, hata kama ilikuwa ni kidogo tu, kwa kupitia sehemu yoyote ya mwili wa aliyeathirika au ya mtuhumiwa na sehemu ya siri, au ya mkundu au upenyo wa sehemu ya siri ya mwathirika na kitu chochote au sehemu yoyote ya mwili (kipengele cha kwanza cha ubakaji)? [52] | Ikiwezekana, iwapo haitokuwa vigumu sana, unaweza kujaribu kuelezea walikufanya nini? Ninafahamu kwamba jambo hili si jepesi, tafadhali usiharakishe. (Iwapo atasema kuwa "walimbaka" mmoja baada ya mwengine au akitumia aina ya maneno ya mitaani au lugha inayojulikana kumaanisha ubakaji, lazima ufuatilie tena ili kupata maelezo halisi ya kuingiliwa.) Unaposema wamekubaka, unaweza kuniambia kwa usahihi kamili ni kitu gani walifanya walipokuwa wanakubaka? Walitumia nini, sehemu gani ya mwili wako waliiumiza? | **Ushahidi:** "Alinilazimisha kuanguka magotini kwangu na kuniamuru nimsisimue uume 'fellatio'. Aliusukuma uume wake ndani sana ya mdomo wangu mpaka nikapaliwa, na kila mara nilipopaliwa alinizabua kibao."<br><br>**Ushahidi mbadala:** "Walivyokuja kijijini kwetu, walituambia tukusanyike nyuma ya nyumba tunapopikia. Walimpiga mama yangu nyuma ya kichwa chake na mabega na ncha za mwisho wa bunduki zao mpaka akadondoka sakafuni. Walimfanyia hivyo hivyo dada yangu. Kisha wananishika mimi na baba yangu na kutuambia tuvue nguo zetu na tulale juu yao - mimi juu ya mama yangu na baba yangu juu ya dada yangu. Watoto waliobaki walikuwa wamesimama wakituangalia na kulia. Kisha wakasimama nyuma yetu na bunduki zao nyuma ya shingo zetu na kutuambia kuwa lazima tuwathibitishie kuwa sisi ni wanaume wa ukweli na sio maadui kwa kufanya ngono na wanawake. Wote tulikuwa tunalia na kubembeleza, lakini kila tulivyokataa walitugonga na kutupiga na kutuambia kuwa watatupiga risasi chini tulipolala tusipofanya kama walivyosema. Baba yangu akasema bora afe kulikoni kumfanyia hivyo mtoto wake wa kike na alijaribu kupigana nao, hivyo walimpiga risasi juu ya dada yangu. Sikujua na kama yeye aliuawa, lakini alikuwa hasogei wala kuongea. Wakamshika mdogo wangu wa kiume wa mwisho na kuweka bunduki kichwani mwake na kusema kuwa watampiga risasi iwapo sitofanya wanachoniambia nifanye, hivyo nikafanya hivyo kwa vile sikutaka wengine wowote wa familia yangu |

52 Mahakama ya Jinai ya Kimataifa (ICC) imeweka wazi kuwa kipengele kinachohusu kumuingilia mtu, hakihitaji kitendo hicho kufanywa na mtuhumiwa mwenyewe. Pia inahusu matukio ambayo mtuhumiwa ndiye anayeingiliwa, au matukio ambayo analazimishwa kumuingilia mwathiriwa.

| NINI KILITOKEA? (Umepata taarifa zozote zinazosaidia tuhuma ya kuwa ubakaji ulitokea?) | Mifano ya MASWALI kuhusu NINI KILITOKEA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA inayoelezea nini kimetokea |
|---|---|---|
| | | kuuawa. Baadaye nilitamani wangekuwa wameniua mimi, kwa sababu sikuweza kuishi na mama yangu wala familia yangu baada ya kile nilichofanya. Mungu nisamehe. Sijui mtu wa aina gani anaweza kumfanyia hivyo mama yake mwenyewe, lakini sikuwa na uamuzi." |
| Mambo yepi halisi yanathibitisha kuwa uvamizi ulitendeka kwa nguvu, au kwa kitisho cha kutumia nguvu au shurutisho, kama inayoletwa na uoga wa vurugu, shinikizo, kifungo, ukandamizaji wa kisaikolojia au matumizi mabaya ya madaraka, dhidi ya mtu au watu hao, au kwa kupata manufaa ya mazingira ya kushawishi, au kuwa uvamizi ulitendwa dhidi ya mtu asiyeweza kutoa ridhaa kamili (kipengele cha pili cha ubakaji)?[53] | Tafadhali tuelezee mazingira ambayo tukio hili lilitokea? Utaweza kutuambia ulikuwa wapi, nani alikuwa hapo, nini kilikuwa kinatokea, na elezea mazingira? | **Ushahidi:** "Watu waliokuwa na silaha waliingia kijijini kwetu siku mbili zilizopita. Wanaume na wavulana wetu walikuwa wamejificha katika misitu, hivyo wanawake tu, wazee na watoto walikuwa kijijini. Watu wenye silaha walikuwa wanapiga kelele na kurusha risasi hewani, na kuwasha moto nyumba na kupora mali. Wanavijiji wengi walikusanyika pamoja katika chumba kimoja cha nyumba yao kujificha pamoja, wakiogopa nini kitatokea. Usiku tulijaribu kuweka chakula chochote na mabaki tuliyopata, na tukitoroka kwenye makundi madogo kwa ajili ya maji. Siku hiyo, wanaume watano wenye silaha waliingia kwenye nyumba nilipokuwa nimejificha na dada zangu na mama yangu. Walituchukua sisi watatu, wasichana wakubwa, na mama yangu alipiga kelele. Mama alipopiga kelele walimpiga kwa nguvu na akadondoka sakafuni, wakapiga risasi kwenye dari, na wakamwambia kuwa akitamka neno lolote watatuua sisi wote watatu mbele yake. Walituondoa na kutuweka nyuma ya lori na walinzi wenye silaha. Walituchukua kwenye kibanda msituni, na tuliwekwa huko usiku mzima. Watatu wao walituchukua kila mmoja wetu kwenye chumba kingine, ambacho kilikuwa na godoro chafu sakafuni, wakati wale wengine wawili waliwalinda wasichana wawili waliobaki. Ilionesha kama vile kila tulivyopiga kelele walitaka zaidi kutuumiza." |

53 Mahakam ya Kimataifa ya Jinai imeamua kwenye kesi ya Katanga kuwa kuthibitisha kipengele chochote kati ya hizi inatosha kuthibitisha kitendo cha kuingiliwa ambacho kimo kwenye uhalifu wa ubakaji. Sio lazima kuthibitisha kutoridhia kwa mwathirika, isipokua kwenye matukio ambayo mtuhumiwa amefanya hilo kosa dhidi ya mtu ambaye "hawezi kutoa ridhaa au kukubali" kwasababu ya umri, ulemavu au sababu zingine.

NYONGEZA 1

## Utumwa wa ngono[54]

### Vipengele:

1) Mtuhumiwa ametumia baadhi ya au madaraka yote yaliyoambatanishwa na haki ya kummiliki mtu mmoja au zaidi, kama kununua, kuuza, kuazima au kubadilishana huyo mtu au watu, au kuamuru kuwanyima uhuru kama hivyo.

2) Mtuhumiwa alisababisha mtu au watu hao kitendo kimoja au zaidi chenye asili ya ngono.

| NINI KILITOKEA? (Umepata taarifa zinazosaidia shutuma kuwa utumwa ulitokea?) | Mifano ya MASWALI kuhusu NINI KILITOKEA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA inayoelezea nini kimetokea |
|---|---|---|
| Mambo gani halisi yanasaidia kuthibitisha kipengele cha kwanza cha utumwa wa ngono (mhalifu alitumia nguvu zilizo kwenye haki ya umiliki)?[55] | Unaweza kuniambia mtuhumiwa alisemaje, iwapo alisema kitu, kuhusu uhusiano wako kwake? Alikuonaje wewe kwa jinsi unavyohusiana na yeye? Alikujulisha vipi kwa watu wengine? Je alikupa fursa ya kukataa au kuamua - na kama ndiyo, kwenye mazingira gani? Iwapo mtuhumiwa hakusema kitu chochote maalum kuhusu wewe, unaweza kuelezea ni nini kilikufanya ujihisi huna uamuzi?<br><br>Kuna mtu yeyote alisema kitu chochote kuhusu uhusiano wako na mtuhumiwa? | **Ushahidi:** "Mtekaji wangu mara nyingi alisema kuwa siwezi kufanya chochote bila yeye kuamua kama ninaweza - alisema kuwa ananimiliki. Alikuwa kama ananimiliki kwa kuniambia nifanye nini kila wakati na kunitishia kuwa nisipotaka kufanya alichoniambia, atawadhuru familia yangu."<br><br>**Ushahidi mbadala:** "Wamaume wawili walikuja kwenye ghorofa tulilokuwa tumewekwa. Niliambiwa niende jikoni na msichana mwengine ili mtekaji wetu aongee na hawa watu. Tulitambaa kutoka jikoni kwenda kwenye ukumbi ili kusikia maongezi yao. Tulimsikia mtekaji wetu akikubali kutuuza kwa wale watu kwa dola 50 kila mmoja na lori la sabuni ya unga. Tulivyowasikia wale watu wanasimama kuondoka, tulikimbia kurudi jikoni na kujificha humo. Siku iliyofuata wale watu walirudi kwenye ghorofa na gari na kunichukua mimi na yule msichana mwengine. Walivyotuingiza kwenye gari, tuliwasikia wanacheka kuhusu kuwa tumeuzwa kwa pesa kidogo na sabuni ya unga." |

54 Uhalifu wa utumwa wa ngono hutumika kwenye biashara ya binaadamu.

55 Mahakama ya Kimataifa Jinai imetoa ufafanuzi wa kina zaidi kuhusu kipengele hiki cha uhalifu wa utumwa wa ngono kwenye uamuzi wa kesi ya Katanga. Korti imeashiria kuwa ni lazima kutumia utaratibu wa kesi kwa kesi kwenye kuchambua aina za vitendo vitakavyo tosheleza kipengele hiki. Kwa kunyimwa uhuru, korti imeridhia kuwa ukweli unaohusu kifungo au uhabusu (ikiwemo muda wake), itahusika, kama jinsi taarifa zinazohusu juhudi za kuzuia uhuru wa kutembea au uhuru wa kuchagua, na taarifa juu ya hatua za kuzuia au kuvunja moyo juhudi za kutoroka. Ukweli unaoonyesha matumizi ya vitisho, nguvu au aina zingine za kutumia nguvu za kimwili au za kisaikolojia zina thibitisha kipengele hiki; kama vile ukweli unavyoonyesha katika matumizi ya shinikizo ya kisaikolojia, mazingira magumu ya mwathirika au jukumu la kulazimika kushiriki kwenye kazi za kulazimishwa. Korti ilisisitiza pia kuwa haki ya umiliki juu ya wengine haimaanishi moja kwa moja kuwa ni shughuli ya kibiashara - hali ya kijamii na kiuchumi chini ya nguvu za umiliki inahusika, ila msingi asili wa kiutumwa inatokana na mwathirika kutokuweza kurekebisha au kubadilisha hali yake.

| NINI KILITOKEA? (Umepata taarifa zinazosaidia shutuma kuwa utumwa ulitokea?) | Mifano ya MASWALI kuhusu NINI KILITOKEA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA inayoelezea nini kimetokea |
|---|---|---|
| Mambo gani halisi yanasaidia kuthibitisha kipengele cha pili cha utumwa wa ngono (tendo la ngono)? | Ulisema kuwa "alikutoa nje" karibu kila usiku. Unaweza ukatueleza kwa undani unamaanisha nini na hili? Alikutoa kutoka wapi? Alikufanya nini? Je unaweza kuelezea ni nini hasa alifanya? Alikufanya ufanye nini? | **Ushahidi:** "Alinifanya nivue nguo hadi niwe uchi kabisa na akinitukana, kuniita [tusi la kikabila] na kunishika mwilini mwangu kote." |

## Ndoa ya kulazimishwa

### Vipengele:

1) Mtuhumiwa kumuamrisha mwathirika kuingia katika ndoa ya kulazimisha

2) vitisho au nguvu za kimwili zinazotokana na manneo ya mtuhumiwa au vitendo vingine.[56]

56 Sheria ya Roma haikuingiza uhalifu wa ndoa ya kulazimisha. Hata hivyo, ndoa ya kulazimishwa iliamuliwa kuwa kitendo cha kinyama ambacho ni uhalifu dhidi ya utu kwenye maziringa ya Mahakama Maalumu kwa Sierra Leone. Uhalifu huo ulifafanuliwa kwenye hukumu ya kesi ya baraza la majeshi ya mapinduzi (Armed Forces Revolutionary Coucil (AFRC)), kwenye maoni yaliyopingana na Hakimu Doherty, aya 53. Hakimu Doherty alisema kwenye aya ya 36 ya maoni yake yanayopingana: "utekaji nyara wa wasichana na kutumia nguvu kuwaingiza kwenye ndoa, kama ilivyofafanuliwa na mtaalamu wa upande wa mashtaka na mashahidi, siyo sawa na ndoa za kupangwiwa au ndoa za jadi". Kwenye aya za 46-51 anasema: "Ushahidi unaonesha kuwa "ndoa za kulazimishwa" kwenye mazingira ya vita ya Sierra Leone yameingiza utekaji nyara wa nguvu wa wasichana na wanawake kutoka majumbani kwao au sehemu zingine walizokimbilia na kufungwa na vikosi vya AFRC walipozunguka kwenye wilaya tofauti. Wasichana na wanawake, bila indhini yao, walichukuliwa kama wake na waasi binafsi. Wasichana na wanawake waliolazimishwa kuingia kwenye ndoa walipata faida kutokana na hizo ndoa kwa kadiri ya kwamba kumilikiwa kwao na muasi fulani inaweza ikawa imemsaidia kutokubakwa au kutonyanywaswa kwa aina nyingine na waasi wengine. Hata hivyo, kutokana na mazingira ya kutumia nguvu kuangamiza, naiangalia hii kuwa ina kiasi cha faida au ni njia ya kumuwezesha kuishi, ambayo haiwezi kuchukuliwa kama kutoa idhini au kuwa na uhuru wa mwathirika kujitawala mwenyewe ndani ya mahusiano na kwa vyovyote haipunguzi makali ya vitendo. Wanawake na wasichana waliyoingizwa kwenye 'ndoa za kulazimishwa' huwa mara nyingi bado wadogo sana, na hivyo huweza kudhuriwa kirahisi. Kuweza kudhuriwa kwao huongezeka kwa wao kuondolewa kutoka kwenye familia zao na kuwekwa kwenye mazingira ya unyanyasaji wa kimwili na kijinsia. Madhara makubwa ya kisaikolojia na kimaadili hutokea kutokana na 'ndoa za kulazimishwa'. Wanawake na wasichana wanalazimishwa kuwa na mahusiano na mara nyingine kuishi na wanaume wanaowaogopa au kwachukia. Zaidi ya hayo, lebo ya 'mke' inaweza kufanya watu wawaogope waathirika na kufanya familia na jamii zao ziwakatae, kuathiri vibaya uwezo wao kurudi kwenye jamii na kurefusha muda mwathirika atakaoukuwa na trauma/kiwewe cha kisaikolojia. Kutokana na ushahidi, nimeona kuwa madhumuni ya 'mume' yalikuwa ni kumlazimisha mwathirika kumfanyia kazi na kumtunza yeye na mali zake, kutekeleza mahitaji yake ya ngono, kubaki muaminifu na mtiifu kwake na kumzalia watoto iwapo 'mke' atashika mimba. Kwa malipo yake, atamlinda 'mke' asibakwe na wanaume wengine, atampa chakula iwapo chakula kitakuwepo na, kutegemeana na hadhi yake, mke atapata hadhi inayolingana. Kiukweli, hizi ni aina za haki na wajibu ambazo mtaalam wa utetezi ameeleza zinakuwepo kweny ndoa za kimila, ila humu hamna makubaliano ya familia au ndugu wa 'mke' na hadhi hulazimishwa kwa vurugu na shurutisho kwa mwanamke. Hivyo nitatofautisha jambo hili na utumwa wa ngono. Ushahidi wa mashahidi unaonesha kuwa waathirika hawakulindwa kutokana na ubakaji na walichukuliwa na waasi wowote ila hawakutengwa au kudharauliwa kama 'wake wa waasi' au 'wake wa porini'. Kwa zaidi, nimetosheka na ushahidi wa mtaalam wa mashtaka kuwa utumiaji wa neno 'mke' unaonesha hadhi ya kuolewa iliyolazimishwa, ambayo ilibakisha madhara mabaya ya kudumu kwa waathirika. Nimeona kuwa lebo ya 'mke' wa muasi imeleta trauma/kiwewe cha kisaikolojia, waathirika kutengwa na imeathiri vibaya uwezo wa waathrika kuunganishwa na kurudi kwenye jamii. Hivyo ningeona kuwa kwenye ndoa za kulazimishwa, actus reus na mens rea za vitendo vya kinyama, zimeridhishwa na ushahidi uliopo".

NYONGEZA 1

| NINI KILITOKEA? (Umepata taarifa zozote zinazosaidia tuhuma za kuwa ndoa ya kulazimishwa au kujamiiana kwa kulazimishwa kulitokea?) | Mifano ya MASWALI kuhusu NINI KILITOKEA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA inayoelezea nini kimetokea |
|---|---|---|
| Taarifa gani zitaonyesha kuwa uhusiano wa kujamiiana ulilazimishwa kwa aliyeathirika)? | Alikuita nini? Ulikuwa una majukumu gani kwake yeye? Ulitakiwa kufanya nini kila mchana na usiku? Watu wengine walikutendeaje – wapiganaji wengine, wafungwa/waliotekwa, wanajumuiya wengine? Unaweza ukaelezea mtekaji wako aliona kuwa nafasi yako ni ipi? Nini kilitegemewa kutoka kwako? | **Ushahidi:** "Nilitekwa nyara kutoka kwa familia yangu usiku wa manane. Nililetwa kwenye sehemu katikati ya msitu ambapo waasi wakikaa. Nilikabidhiwa kwa Kapteni John na nikaambiwa kuwa nitakuwa mke wake. Alikuwa ana wadhifa mkubwa hivyo nilikuwa kwenye hali ya usalama kuliko wanawake wengine ambao hawakuwa 'wake' wa waasi, waliokuwa wakibakwa na genge kila baada ya vita. Kapteni John alinifanyia chochote akichotaka kwenye ngono, lakini hamna mwengine aliyeruhusiwa kunigusa. Pia nilikuwa nina chakula cha kutosha, wakati wengine hawakuwa nacho. Nilishikiliwa na Kapteni John kwa zaidi ya mwaka 1.5 na nilizaa mtoto wake, mvulana, ambaye ana miaka 10 sasa. Baada ya vita kuisha, hamna mtu kwenye familia yangu aliyeongea na mimi. Nilifukuzwa na mwanangu. Nimekuwa mwenyewe tokea wakati huo." |
| Ni taarifa gani zitaonyesha kuwa tendo lilifanywa kwa tishio au nguvu za kimwili, kutokana na maneno au tabia nyingine ya mtuhumiwa (Kipengele cha pili cha ndoa ya kulazimishwa au kujamiiana kwa kulazimishwa)? | Unaweza kinieleza mazingira ambayo ulitekwa? Unaweza kuniambia aliyekuteka alisema nini? Ulikuwa huru kuondoka? Kwa nini au kwa nini haukuwa huru? | **Ushahidi:** "Alivyokuja kunichukua alikuwa na wanaume wengine watano wenye silaha na walikuwa wagomvi sana. Walipiga risasi dirishani na kuvunja vunja nyumba na mapanga. Waliwaangalia familia yangu na kuninyoshea, wakisema 'huyu mzuri.' Walinipeleka msituni na sikujua nilikuwa wapi. Watu waliokuwepo walikuwa na silaha na angalau wengine wao walikuwa sehemu moja na mimi mda wote. Kapteni John alivyoniamuru kufanya kitu – iwe kupika, kusafisha, kuhudumia, kung'arisha viatu au vitu vibaya alivyonifanyia usiku – sikuweza kukataa. Mara moja nilikuwa na malaria na nilikuwa na homa kali sana na nilikuwa nazimia nikisimama – aliniita niende kwakwe na nilivyokuwa sijaenda alikuja na kunipiga vibaya sana mpaka sikuweza kutembea kwa masiku." |

NYONGEZA 1

## Ukahaba wa kulazimishwa

**Vipengele:**

1) Mtuhumiwa amesababisha mtu mmoja au zaidi kufanya tendo moja au zaidi lenye asili ya ngono kwa kutumia nguvu, au kwa tishio la vurugu au shurutisho, kama inayosababishwa na woga wa vurugu, shinikizo, kifungo, ukandamizaji wa kisaikolojia au matumizi mabaya ya madaraka, dhidi ya huyo mtu au watu au mtu mwengine; au kwa kuchukua faida ya mazingira magumu au ya mtu kutokuweza kutoa idhini ya kweli.

2) Mtuhumiwa au mtu mwengine alipata au alitegemea kupata pesa au faida nyingine badala ya, au inanyohusiana na, vitendo vyenye asili ya ngono.

| NINI KILITOKEA? (Je umepata taarifa zinazosaidia tuhuma kuwa ukahaba wa kulazimishwa ulitokea?) | Mifano ya MASWALI kuhusu NINI KILITOKEA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA inayoelezea nini kimetokea |
|---|---|---|
| Ni mambo gani halisi yanasaidia kuthibitisha kuwa mtuhumiwa alisababisha mtu mmoja au zaidi kutenda tendo moja au zaidi lenye asili ya ngono kwa nguvu au shurutisho, kama litakalosababishwa na woga wa vurugu, shinikizo, kifungo, ukandamizaji wa kisaikolojia au matumizi mabaya ya madaraka, dhidi ya huyo mtu au hao watu au mtu mwengine, au kwa kutumia mazingira yenye ushawishi au huyo mtu au watu kutokuwa na uwezo wa kutoa idhini halisi (kipengele cha kwanza cha uhalifu wa kijinsia)? | Je unaweza, kama itawezekana, tafadhali niambie nini hasa kilitokea? Je unaweza kufafanua unamaanisha nini hasa unaposema "Aliwalazimisha kushambuliana"? Je unaweza ukatuambia alifanya nini hasa, kwa kutumia nini? Je aliagiza nini kifanywe, na nani akifanye na amfanyie nani? Je unaweza ukaniambia kuhusu mazingira, hili lilitokea wapi? Hiyo sehemu ilikuwaje? Ulikuwa wapi ilivyokuwa inatokea? Je uliona nini kingine? Nani mwingine alikuwepo? Unaweza ukaielezea sehemu? Je kulikuwa na madirisha na milango? Hiyo sehemu ni wapi kijijini/ mjini? Ni karibu na wapi? Nani alikuwa ndani na nini kilizunguka eneo? | **Ushahidi:** "Nilikuwa kijijini kwangu na wote tulikusanyika shuleni. Kama mwalimu, nilijua sehemu zote za kujificha kwenye shule na nilijaribu kuhakikisha kuwa kila mtu alikuwa salama. Lakini nilikuwa sina nguvu dhidi ya wanamgambo walioingia shule. Walivamia chumba hadi chumba na kupiga kelele za matusi kama 'Nyinyi wote ni minyoo, angalia minyoo yote eneo hili!' Kabla sijajua, wanamgambo waliingia kwenye chumba tulichokuwa tumejificha. Mmoja wao aliwachukua wasichana wote vijana na kuwaamuru kupanga msitari ukutani. Wanamgambo wengine walikuwa wanacheka. Walikuwa wanaongelea wepi wawili/ jozi watakua na thamani zaidi.<br><br>Baada ya muda mrefu kupita kiasi, na kila mtu akipiga kelele na kulia na wanamgambo kutunyooshea silaha zao wote kutunyamazisha, mgambo mkubwa ambaye ilionekana kabisa kuwa alikuwa mtu mwenye mamlaka – kila mtu alisimama na kumsalimia. Alivyokuja na kubweka maagizo kwa wengine wote – aliingia kwa mbwembwe ndani ya chumba na tabasamu kwenye uso wake. 'Muda wa sarakasi ya minyoo', alisema. Akaonyesha vidole na wanamgambo wengine wakawasindikiza ndani ya chumba wavulana waliokua wametolewa kwenye chumba mwanzo. Wote wakiwa vijana waliobaleghe kwani vizuri. Alisema, 'Wacha mapatano yaanze!' Kisha akaanza kuwauliza watu |

| NINI KILITOKEA? (Je umepata taarifa zinazosaidia tuhuma kuwa ukahaba wa kulazimishwa ulitokea?) | Mifano ya MASWALI kuhusu NINI KILITOKEA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA inayoelezea nini kimetokea |
|---|---|---|
| | Unaweza ukaelezea hawa watu walikuwa wamevaa nini? Walikuwa wamevaa kitu chochote kichwani? Walikuwa wamevaa viatu vya aina gani? Ulipata fursa ya kuona gari lolote? Unaweza kuyaelezea magari? Ulipata fursa kuziona silaha? Uliweza kusikia maongezi yao yoyote? Unaweza kutuambia ulichosikia? Nani haswa alisema hivyo? | wake wawili wawili wepi wataleta utajiri zaidi. Watu wake wakawaweka wasichana na wavulana wawili wawili mbele yake, na wasichana wengine kwa wasichana na wavulana kwa wavulana. Wanamgambo wote walikuwa wanacheka. Mkubwa wao akawanyooshea wavulana wawili na kusema 'Hawa wawili ndiyo 'jozi ya dhahabu.' Alimwambia kila mtu mwingine afanye mduara; Wanamgambo wake walikuwa katika mduara na silaha, na mzunguko wa ndani ulikuwa na wavulana na wasichana. Akaonyesha vidole vyake na mmoja wa wanamgambo wake akaenda kwa wale wavulana wawilli na kuvuta suruali zao chini pale pale mbele ya kila mtu. Mama wa wavulana wote wawili walikuwa ndani ya chumba, na dada wa mmoja wao pia alikuwa ndani. Kila mtu aliyepiga kelele au kulia alizabuliwa klibao hadi akadondoka chini na kutishiwa kuuliwa Alimuamrisha mvulana mmoja kuweka uume wa mvulana mwingine katika kinywa chake na kuufyonza." |
| Ni ukweli upi unaoweza kusaidia kuthibitisha kuwa mtuhumiwa au mtu mwingine alipata au alitarajika kupata fedha au faida nyingine kutokana na, au kuhusiana na, vitendo vya ngono (kipengele cha pili cha ukahaba wa kulazimishwa)? | Maswali hayo juu yanayohusiana na kipengele, yanaweza kutoa jibu kwa kipengele hiki pia, iwapo mpelelezi atafuatilia kwa makini.) | **Ushahidi:** "Walivyozidi kufanya hivyo muda mrefu, walizidi kupanda thamani - hivyo wanamgambo wote walizidi kuongeza sauti, wakipiga kelele 'endelea, endelea!' Wakati yule mvulana aliyepiga magoti alivyodondoka chini - wakati huo sikujua iwapo alizimia au la - mkubwa wao alisema, 'mnyoo kwa mnyoo, unajua nini cha kufanya!!' Yule mvulana mwingine akasukumwa na wanamgambo wawili hadi mgongoni kwa yule mvulana aliyedondoka na alifanywa aweke uume wake kwenye mkundu wa yule mvulana aliyekuwa sakafuni. Wote walikuwa wanalia na kupiga kelele lakini yule mvulana sakafuni alikuwa kakauka. Mkubwa wao akasema bei ya mwisho ilikua 500 na kuwa wavulana wa dhahabu walifanya kazi yao. Walipigwa mateke kwenda kwenye kona ya chumba na wengine wawili walichaguliwa kuwa na thamani ya fedha. Hii iliendelea hadi wasichana na wavulana wakashambuliwa, kwa masaa na masaa." |

NYONGEZA 1

## Mimba za kulazimishwa

**Vipengele:**

1) Mtuhumiwa alimfungia mwanamke mmoja au zaidi na kumshikisha mimba kwa lazima, kwa nia ya kuathiri mchanganyiko wa kikabila au kutekeleza ukiukaji mwengine mkubwa wa sheria za kimataifa.

| NINI KILITOKEA? (Umepata taarifa zinazosaidia kuonyesha kwamba tuhuma hizi za utesaji zilitendeka?) | Mifano ya MASWALI kuhusu NINI KILITOKEA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA inayoelezea nini kimetokea |
|---|---|---|
| Ni mambo gani halisi yanayoweza kusaidia kuthibitisha kuwa mtuhumiwa alimfungia mwanamke mmoja au zaidi aliyelazimishwa kushika mimba, na nia ya kuathiri mchanganyiko wa kabila la watu wowote au kufanya uhalifu mwengine mkubwa kwenye sheria ya kimataifa (kipengele cha kwanza cha ulazimishaji wa mimba)? | Unaweza kuniambia lini ulishika mimba? Je watuhumiwa walisema kitu chochote kuhusu mimba yako? Iwapo ndiyo, je walisemaje? | **Ushahidi:** "Ni vigumu sana kuongelea hii, lakini nitajaribu. Ule wakati niliyokuhadithia mapema, kuwa niliumizwa na yule mgambo, wakati ananibaka alikuwa anasema kila mara, 'Nitapata mtoto mweupe!' Nililia na kulia kwani nilijua kuwa kuna uwezekano nitashika mimba, haswa kwa vile alinifanyia hivi mara nyingi kwa muda wa siku tatu, nilikuwa nina maumivu makali lakini hakujali vilio vyangu. Aliendelea kusema, 'mtoto mweupe, mtoto mweupe'. Sikushangaa ilipokuwa damu ya siku zangu hazikuja. Aliniweka humo mpaka nilipojifungua kwani aliogopa kuwa ningejaribu kutoa mimba. Sijawahi kumwambia mtu hili, na ninampenda mtoto wangu na ningependa kumlinda. Hajui baba yake ni nani, na sina mpango wa kumwambia hadi atimie miaka 18. Iwapo hauwezi kunithibitishia kuwa mwanangu hatogundua, sitokuruhusu kuweka ukumbusho wa mkutano wetu."<br><br>**Ushahidi mbadala:** "Nilipokuwa na miaka 14 nilichukuliwa kama askari mtoto. Nilipelekwa porini kutumikia kitengo nilichopangiwa. Kamanda alikuwa ni mwanamke, na tulivyofika tu alikuja kutukagua. Aliniona hapo hapo na kusema, 'Huyu ni wangu.' |

| NINI KILITOKEA? (Umepata taarifa zinazosaidia kuonyesha kwamba tuhuma hizi za utesaji zilitendeka?) | Mifano ya MASWALI kuhusu NINI KILITOKEA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA inayoelezea nini kimetokea |
|---|---|---|
| | | Akawapeleka wengine kikundi mbali na mmoja wa maofisa. Aliniambia kuwa nitakuwa mlinzi wake na kuwa itabidi nifanye kila atakachosema – kupika, kusafisha, kupigana, chochote. Alikuja kwangu usiku na kupanda juu yangu na kunifanya nimfanyie vitu. Aliniambia kuwa nisipofanya alichoniambia, nisipompa raha, basi atanipeleka vitani bila silaha na kuniwacha niuawe. Hii ilitokea kila usiku kwa wiki na wiki. Siki moja aliniambia kuwa ameamua kuwa anataka mtoto, na kuwa ilikuwa ni kazi yangu kumpa mtoto. Alinifanya nifanye naye ngono mara nyingi kwa siku na kuniambia kuwa asipopata mimba atajua kuwa ni kosa langu na atafanya nipigwe au kuuwawa. Baada ya wiki kadhaa aligundua kuwa ana mimba na aliniambia kuwa lazima nikae naye kambini kumtunza na kuhakikisha kuwa mtoto ana afya. Nilikasirika sana kuwa huyu mwanamke atazaa mtoto wangu wakati mimi sikutaka hilo, ila alikuwa kamanda na kulikuwa hamna njia. Alinifanya nikae naye kwa miezi, lakini kabla mtoto hajazaliwa aliniondoa. Sijui kama mtoto ni mvulana au msichana na kama aliishi, lakini ninabeba maumivu ya huzuni moyoni mwangu kujua kuwa mtoto wangu yuko chini ya amri ya yule mwanamke na wala hanijui." |

## Uhasishaji wa kulazimishwa

**Vipengele:**

1) Mtuhumiwa alimnyima mtu mmoja au mwingine uwezo wa uzazi wa kibiolojia.

2) Mwenendo haukithibitishwa na matibabu ya kidaktari au hospitali kwa mtu au watu husika, wala haukufanyika na idhini yao ya kweli.

| NINI KILITOKEA? (Umepata taarifa zinazosaidia kuonyesha kwamba tuhuma hizi za utesaji zilitendeka?) | Mifano ya MASWALI kuhusu NINI KILITOKEA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA inayoelezea nini kimetokea |
|---|---|---|
| Ni mambo gani halisi yanasaidia kuthibitisha kuwa mtuhumiwa alimnyima mtu mmoja au zaidi uwezo wao wa uzazi wa kibiolojia (kipengele cha kwanza cha utowaji kizazi/uhasishaji wa kulazimishwa)? | Katika mfululizo wa matukio unayoniambia, unaweza kuniambia iwapo uliwahi kuambiwa kuvua nguo zako? Umeniambia kuwa kutokana na matukio yaliyotokea kwenye jumuiya yenu miaka mitano iliyopita, wewe na mke wako mmeshindwa kupata watoto. Unaweza kunielezea nini ilisababisha hii? | **Ushahidi:** "Kilichotokea ni kuwa wanamgambo walikuja kwenye vijiji vyote na kututeka nyara mimi na wanaume na wavulana wote kutoka kijijini ambao tulishindwa kutoroka. Tulifungwa na kupelekwa kwenye sehemu iliyojitenga kwenye msitu. Kulikuwa na wanamgambo wengi huko, na mmoja mmoja tulitolewa kutoka kwenye lori. Ilivyofika zamu yangu, walinipigia kelele na kuniburuza nje ya lori. Wakanipeleka kwenye sehemu yenye miti ambayo ilikuwa imejaa damu kote, na moto ukiwaka na mapanga kote yaliyojaa damu. Niliona majirani zangu wanaume umbali mfupi kutoka kwangu na niliwasikia wakipiga kelele, wakati wamezungukwa na wanamgambo na wanaume wengine waliovaa makoti meupe utafikiri wanafanya kazi kwenye maabara. Walinifunga chini na mikono yangu na kuvua suruali yangu, walipanua na waliifunga miguu yangu wazi. Walivyotoa panga moja kutoka kwenye moto, nilijua nini watafanya. Walisema 'Mbegu yako haitosambaa tena!' Nilihisi maumivu makali kupita kiasi walivyokuwa wanakata pumbu zangu. Baadaye niligundua kuwa wale wanaume na makoti meupe walikuwa pale kutushona ili tusivuje damu hadi kufa. Walituacha wote kwenye rundo huku tumepoteza fahamu, tumelala kwenye damu zetu. Baada ya masaa mengi wake zetu na wanawake |

NYONGEZA
1

| NINI KILITOKEA? (Umepata taarifa zinazosaidia kuonyesha kwamba tuhuma hizi za utesaji zilitendeka?) | Mifano ya MASWALI kuhusu NINI KILITOKEA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA inayoelezea nini kimetokea |
|---|---|---|
| | | wengine kutoka kijijini waliweza kuja kutupata. Binamu zangu wawili hawakuishi." |
| Hali gani halisi inasaidia kuthibitisha kuwa kitendo hakikukubaliwa na matibabu ya kiafya au hospitali ya mhusika au wahusika, na wala hayakufanywa na ridhaa yao kamili (kipengele cha pili cha utoaji wa kizazi wa kulazimishwa)? | Hii ilitokea wapi [yaani kuelewa iwapo ilikuwa hospitali au kwenye usimamizi wa mhudumu]? Je ulikubaliana na hili? | (Ushahidi uliotolewa juu utatosheleza kipengele hiki pia.)<br>**Ushahidi Mbadala:** "Tulivyofika kambi walituambia kuwa wanatupa dawa kutukinga na magonjwa yanayotakana na maji, ili tusiumwe. Tulivyofika kwanza, walituchoma sindano na kutuambia kuwa sasa tutaweza kunywa maji. Baada ya muda huo, walituuliza kama tuliumwa kutokana na maji na tukasema ndiyo, hivyo wakatuambia kuwa tutahitaji kupasuliwa kuondoa vimelea. Ilikuwa ni operesheni ndogo, lakini tulipata maumivu kiasi fulani baadaye. Baadaye mwezi huo, niliona kuwa sijapata damu ya siku zangu nilipotakiwa nipate kawaida. Wanawake wengine walisema kuwa damu ilitoka kidogo zaidi au ilisita kabisa. Tuliogopa kuwa labda tulikuwa na mimba, lakini muda ulivyopita na matumbo yetu hayakukua tulitambua hii imetokana na huo ugonjwa au mambo tuliyopitia. Hadi tulipotokoroka kutoka sehemu ile na kwenda mjini ndiyo nikaweza kumwona daktari wa wanawake ambaye alikuwa anafanya kazi kwenye shirika lisilo la serikali, na akaniambia kuwa sitoweza tena kupata watoto wengine kwa sababu ya walichonifanyia. Dawa na operesheni walizotuambia zitatukinga zilitufanya tuwe tasa na kulikuwa hamna kitu ambacho daktari angeweza kufanya kurekebisha hilo. Hamna mwanamke ambaye nilikuwa naye kambi ambaye ameweza kupata watoto wengine, hivyo najua kuwa walitufanyia hivi." |

NYONGEZA 1

## Unyanyasaji wa kijinsia

### Vipengele:

1) Mtuhumiwa alitenda tendo lenye asili ya ngono dhidi ya mtu mmoja au zaidi au alisababisha mtu huyo au watu hao kufanya tendo lenye asili ya ngono kwa kulazimisha. Au kwa tishio la vurugu au shurutisho, kama inayosababishwa na woga wa vurugu, shinikizo, kifungo, ukandamizaji wa kisaikolojia au matumizi mabaya ya madaraka, dhidi ya huyo mtu au watu au mtu mwengine, au kwa kuchukua faida ya mazingira magumu au ya mtu kutokuweza kutoa idhini ya kweli.

2) Tendo hilo lilikuwa na uzito lenye usawa ukilinganishwa na uhalifu mwingine dhidi ya ubinadamu.

3) Mhusika alikuwa anafahamu kuhusu hali ya kweli inayoweka uzito wa tendo.

| NINI KILITOKEA? (Umepata taarifa zozote zinazosaidia tuhuma za kuwa unyanyasaji wa kijinsia ulitokea?) | Mifano ya MASWALI kuhusu NINI KILITOKEA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA inayoelezea nini kimetokea |
|---|---|---|
| Mambo gani halisi yanasaidia kuthibitisha kuwa mtuhumiwa alitenda tendo la aina ya ngono dhidi ya mtu mmoja au zaidi. Au alisababisha mtu au watu hao kuingia kwenye matendo yenye asili ya ngono kwa nguvu au shurutisho, kama litakalosababishwa na woga wa vurugu, shinikizo, kifungo, ukandamizaji wa kisaikolojia au matumizi mabaya ya madaraka, dhidi ya huyo mtu au hao watu au mtu mwengine; au kwa kutumia mazingira yenye ushawishi au huyo mtu au watu kutokua na uwezo wa kutoa idhini halisi (kipengele cha kwanza cha uhalifu wa kijinsia)? | Tafadhali, unaweza ukanielezea, nini kilitokea? (Angalia mapendekezo ya maswali zaidi hapo juu.) Mtuhumiwa alisemaje? | **Ushahidi:** "Mmoja mmoja tulipangwa kwenye ukumbi na mmoja mmoja kila mmoja wetu alipelekwa kwenye chumba. Sisi tuliokuwa tunasubiri tulisikia wavulana wengine walioingia ndani wakipiga kelele ndani ya chumba, na walivyotoka, nguo hazikuwepo na viunoni mwao kulikuwa na kitambaa chenye damu. Walitoka wakichechemea na kulia sana, wengine walizimia kutokana na maumivu na mshtuko. Baadaye tulielewa kuwa waasi walikuwa wanafanya aina ya utaratibu/matambiko ya kutuchuna uume wetu."<br>**Ushahidi mbadala:** "Walitenganisha wanaume mashoga na wanawake wa eneo letu lote na kutuleta kwenye shule ya kijijini iliyotelekezwa, ambapo tuliwekwa chini ya ulinzi. Kila siku wanaume walipelekwa kwenye chumba na chanja, ambako walining'inizwa kwa mikono na miguu na kufirwa. Walinzi waliotufanyia hivyo walikuwa wanasema, 'Hivi si ndivyo mnavyopenda?!' Mara nyingine waliwaingiza wafungwa wengine na kuwalazimisha kutufanyia vitu, na wanaume wakisisimka walicheka na kusema, 'Sasa wote ni mashoga'." |

NYONGEZA 1

| NINI KILITOKEA? (Umepata taarifa zozote zinazosaidia tuhuma za kuwa unyanyasaji wa kijinsia ulitokea?) | Mifano ya MASWALI kuhusu NINI KILITOKEA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA inayoelezea nini kimetokea |
|---|---|---|
| | | **Ushahidi Mbadala:** "Walitukusanya sisi kwenye uwanja wa kijiji na walitufanya tuvue nguo zetu zote, pamoja na nguo zetu za ndani. Tulikuwa pale katika uwanja mkuu mbele ya kila mtu. Kisha wakachagua kati yetu na kutuweka kwenye lori, wale waliotuchagua. Sisi wote tulikuwa wanawake na umri wetu ulikuwa kati ya miaka 14 na 22, takriban. Waliendesha kwa muda mrefu niliohisi kama masaa mengi kwenda kwenye sehemu iliyojitenga. Hapo walituchukua kwenye kibanda kilichotelekezwa. Hapo walituamuru tulale kila mmoja pembeni ya mwengine kwenye magodoro machafu sakafuni. Na tabasamu usoni mwake, aliyeonekana kuwa mkuu wa hiki kikundi alileta kitambaa kilichokunjwa kutoka chumba kingine. Wale wanaume wengine wenye silaha walipiga miluzi na makofi alivyokuwa anafungua kitambaa, na kuonyesha visu sita vya ukubwa tofauti, kutoka vidogo hadi vikubwa. Kila mmoja wetu alikatwa sehemu zetu za siri na kisu kimoja wapo, huku wengine wakiangalia na kutoa maoni kuhusu matokeo tofauti ya vile visu tofauti. Mimi nilikuwa wa nne." |
| Mambo gani halisi yalithibitisha kuwa hivi vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia vilifika kiwango cha uzito sawa na uhalifu mwingine dhidi ya ubinaadamu (kipengele cha pili cha unyanyasaji wa kijinsia)? | Tafadhali niambie ilikuwaje? Ulihisi vipi kimwili? Ulihisije kiakili wakati huu? Nini uliweza na nini hukuweza kufanya? Nini yalikuwa matokeo yake? | **Ushahidi:** "Makovu yalichukua wiki/majuma kadha kupona; wavulana watatu walipewa kazi ya kuchimba ambapo tuliambiwa tuchimbe kila siku. Tusipochimba sana tulipewa chakula pungufu, na kwa vile wengi wetu tulikuwa tunaumwa sana na tuna maumivu makali sana kufanya chochote, tuliishia kutochimba hata kidogo, na kwa matokeo yake tuliishia kupewa chakula kidogo sana kuweza kuishi. Tunashukuru tulikuwa na maji, ambayo, ingawa yalikuwa machafu/yanaambukiza na mara nyingi kutufanya tuharishe, ninaamini yalitusaidia kuishi." |

| NINI KILITOKEA? (Umepata taarifa zozote zinazosaidia tuhuma za kuwa unyanyasaji wa kijinsia ulitokea?) | Mifano ya MASWALI kuhusu NINI KILITOKEA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA inayoelezea nini kimetokea |
|---|---|---|
| Mambo gani yanasaidia kuthibitisha kuwa mtuhumiwa alikuwa anajua hali halisi iliyofanya haya matendo kuwa mabaya ya kutosha, kuwa ni uhalifu dhidi ya ubinaadamu? (kipengele cha tatu cha unyanyasaji wa kijinsia)? | Je uliwasikia waasi wakisema kitu chochote walivyokuwa wanawachuna? Wao walikuwa wapi hii ilivyokua inatokea? Je ilikuwa ni waasi wale wale waliofanya hilo kila mara? | **Ushahidi:** "Waasi walikuwa wachache katika eneo hilo - labda saba - lakini walikuwa wamejihami na silaha hadi kidoleni. Sababu yote ya kutupeleka huko, kama walivyosema, ilikua ni 'kutufanyia unyago sisi kama wanaume na kutuwekea alama kama watumwa wao. Walidai kuwa hii ni 'mila ya kiutamaduni wao' na walisema wanawafanyia hivyo watumwa wao wote'." |

**Mateso**[57]

**Vipengele:**

1) Kinyume na sheria za kimataifa, mtuhumiwa alimnyima kwa kiasi kikubwa mtu mmoja au zaidi ya haki zao za msingi.

2) Mtuhumiwa alimlenga huyu mtu au watu kwasababu ya utambulisho wa kundi au mkusanyiko, au alililenga kundi au mkusanyiko namna hivyo.

3) Kulenga huko kulitokana na misingi ya kisiasa, ubaguzi wa rangi, taifa, kabila, utamaduni, dini, jinsia **(kama inavyoelezwa katika Ibara ya 7, aya ya 3 ya Sheria)** au sababu nyingine ambazo hutambulika kuwa haikubaliki kwenye sheria za kimataifa.

4) Tendo lilitendwa nia kuhusiana na kitendo chochote kilichotajwa katika ibara ya 7, aya ya 1 ya Sheria au uhalifu wowote ulio katika mamlaka ya Mahakama.

57 Ukumbusho: uhalifu wowote uliotajwa hapo juu, ukifanywa kwa njia za mateso, kwa misingi ya siasa, ubaguzi wa rangi, taifa, kabila, utamaduni, dini au jinsia, unaweza pia kuhesabika kama uhalifu dhidi ya binadamu. Ni muhimu kumwuliza shahidi maswali kuhusu maneno ambayo yalitamkwa, ili kujua kama kulikuwa na dhamira yoyote ya kutesa. Vitendo vya mateso siyo lazima viwe na asili ya ngono, lakini kama watu binafsi wanalengwa kutokana na maoni yao ya kisiasa, au kwa sababu ya rangi, taifa, kabila, utamaduni, kushiriki kwenye dini au jinsia, na kama vitendo ni vya hatia ya unyanyasaji wa kijinsia, uhalifu wa mateso pia unaweza kuhusika.

NYONGEZA 1

| NINI KILITOKEA? (Umepata taarifa zinazosaidia tuhuma kuwa mateso yalitendeka?) | Mifano ya MASWALI kuhusu NINI KILITOKEA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA inayoelezea nini kimetokea |
|---|---|---|
| Ukweli upi ulisaidia kuthibitisha kuwa, kinyume na sheria za kimataifa, mtuhumiwa aliwanyima sana haki za msingi mtu mmoja au zaidi, (kipengele cha kwanza cha mateso)? | Maswali yoyote hapo juu ambayo yanashawishi kuhusu ushahidi wa uhalifu huu au makosa mengine makubwa pia itatosha kukidhi kipengele cha mateso.) | (Maelezo yoyote ya shahidi kuhusu kitendo kilichoelezwa kwenye viingilio hapo juu kwenye safu hii pia itaridhia kipengele hiki cha mateso.) |
| Ukweli upi utasaidia kuthibitisha kuwa mtuhumiwa alimlenga mtu au watu kutokana na kitambulisho cha kundi au jumuiya, au alilenga kundi au jumuiya kwa hivyo (kipengele cha pili cha mateso) | Je ulikuja kujua kwa nini ulishambuliwa? Je washambulizi walisema chochote kuhusu nani anashambuliwa? Walisema nini?<br><br>Iwapo shahidi ameelezea kuwa kuna watu fulani walilengwa: Je ulikuja kujua kwa nini ulilengwa? Unajuaje? | **Ushahidi:** "Tulikuwa tunachukuliwa kama watumwa, rasilimali, sio watu. Tulidhalilishwa na kila mara tuliteswa, iwe kijinsia au vinginevyo, tuliambiwa kuwa wanawake na wasichana waliumbwa kutumikia wanaume."<br><br>**Ushahidi mbadala:** "Walituambia kuwa walijua kuwa sisi ni mashoga kwa sababu walitupeleleza kwenye mkutano. Walitufuata nyumbani na kutuambua kuwa 'tuache kuvaa na kujiweka kama wafiraji' na kuwa 'inatubidi tuanze kufanya jinsi wanaume wa ukweli wanachotakiwa kufanya na sio kujifanya kuwa wanawake'. Walituambia kuwa hatukua watu wa kawaida na tulikuwa dhaifu na kuwa tulichofanya ni dhambi na chenye karaha;, kuwa tulikuwa tishio kwa usalama wa nchi kwa vile tulikuwa waongo na hatuaminiki. Walitupiga na kutuambia kuwa inabidi wakague mikundu yetu 'kuona ni kiasi gani cha athari tumefanya. Baadaye waliwaleta malaya wa kike wawili na wakatuambia kwamba 'watatuelimisha jinsi ya kuwa mwanamme' Walifanya wanawake watufanyie vitendo vya ngono, na kama hatujapata ashiki, walitupiga na kututukana. Kisha walitufanya tutende ngono na wanawake mbele yao huku wakitupigia kelele wakati tunafanya hivyo. Walituambia kuwa, nchi mpya itakapoundwa, kutakuwa 'hamna nafasi kwa wasichana kama nyinyi, ni kwa wanaume wa ukweli tu'." |

| NINI KILITOKEA? (Umepata taarifa zinazosaidia tuhuma kuwa mateso yalitendeka?) | Mifano ya MASWALI kuhusu NINI KILITOKEA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA inayoelezea nini kimetokea |
|---|---|---|
| | | **Video:** Mmoja kati ya wanajumuiya aliyetengwa alitoroka na aliweza kuja na simu ya mlinzi mmoja. Video inamwonyesha kamanda wa kituo akiwapiga wanawake wa jumuiya kwenye sehemu zao za siri na maziwa akitumia rungu, huku akiwaita wezi, wateka nyara na wapotofu. Kamanda aliwapigia kelele wanawake: "Tunawapiga ili uovu wenu utoke ile muwe wazuri wa kutosha kubeba mbegu zetu." Video imewekewa tarehe na wakati iliporekodiwa. |
| Ni mambo gani halisi yatasaidia kuthibitisha kuwa kulengwa kwa kundi au watu wa kikundi kulitokana na msingi unaolindwa (kipengele cha tatu cha mateso)? | Ni msingi gani unakufanya useme kuwa mlitendewa hivi kwa sababu nyie ni wanawake/wasichana? | **Ushahidi wa nyaraka:** Shahidi polisi wa ndani anakupa nyaraka ambayo ni barua rasmi ya tawi la wizara ya mambo ya ndani inayoongelea sehemu ambayo wanawake na wasichana waliripoti kuwa walipelekwa kwenye nyumba tofauti, wakafungwa na kushambuliwa kijinsia na vinginevyo, na kulazimishwa kuwafanyia kazi polisi, kufua nguo zao, kuwapikia chakua, kuwahudumia vinywaji, nk. Hiyo nyaraka inatoka kwa mkuu wa tawi hilo la polisi, na inaonyesha maagizo yao ya wiki hiyo, ikiwa ni pamoja na fungu la maneno: "Ruhusa ya kuwatumikisha kikazi wanawake kwa njia yoyote ili kusaidia jitihada za vita imeruhusiwa kwa matawi yote. "Mwanamke yoyote atakaye pinga atakuwa ni msaliti kwa lengo na kuadhibiwa ipasavyo." Nyaraka imesainiwa na afisa mkuu kabisa wa polisi katika tawi hilo, na kupigwa mhuri na mhuri rasmi wa tawi. |

NYONGEZA 1

| NINI KILITOKEA? (Umepata taarifa zinazosaidia tuhuma kuwa mateso yalitendeka?) | Mifano ya MASWALI kuhusu NINI KILITOKEA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA inayoelezea nini kimetokea |
|---|---|---|
| Mambo gani halisi yanasaidia kuthibitisha kuwa tendo lilitendeka kuhusiana na uhalifu dhidi ya ubinaadamu (Kipengele cha nne cha mateso)? | Kwa nini unadhani ulifanyiwa hivyo? Umeelezea jinsi ulivyoteswa, na ulituambia kabla kuwa ulikuja kuamini kuwa ilikuwa ni kwa sababu mlikuwa wanawake.[58] Nini kilikufanya ufikie uamuzi huo? Nini kingine kilikuwa kinakutokea na kinatokea kwenye mazingira yako? Nini kilikuwa kinawatokea wengine - wanaume, wanawake, wavulana, watoto, wazee...? | **Ushahidi:** "Kwa muda wote tuliokuwa tumeshikiliwa, iwe wakati walipokuwa wanatushambulia, au wanatupiga, au wanatuamuru kusafisha sakafu, au kufanya kazi zinginge, walikuwa wanarudia kwa mfululizo matamshi ya matusi, dharau kuhusu sisi, wakituita 'makahaba wachafu' au 'mbwa wa kike unayenuka'. Waliwaweka wanawake na wasichana tu kwenye mazingira haya, na kila mara walieleza karaha yao kwa wanawake na wasichana. Tuliendelea kuwa na matumaini kuwa hatimaye watatuona wa karaha mno na kutuachia tuondoke; lakini badala yake, walituweka, walitutania kwa kuwa wanawake na wasichana dhaifu, na kutupa maumivu mabaya ya kimwili and kila siku uoga wa jioni, ambapo ndiyo mashambulizi mengi ya kijinsia yalitokea." |

58 Mbinu hii hujulikana kama "kuonyesha/kuakisi". Mara nyingi, kwa kurudia alichosema shahidi, kunakuwa hakuna haja ya nyongeza kwenye swali: itamkumbusha shahidi kusema zaidi. Hata kama maswali ya ziada yatahitajika, kurudia maneno ambayo shahidi ametoka kuyasema ni njia nzuri ya kujenga mahusiano ya kuaminiana na kuheshimiana; inaonyesha umakini wa kusikiliza na kumfanya shahidi kuhisu kuwa amesikika vizuri. Ni muhimu, hata hivyo, kwamba maneno yake yasibadilishwe kutoka jinsi alivyoyasema. Iwapo mhojaji atabadili hayo, hii inaweza kuathiri ushahidi wa shahidi. Hii inaweza kuchukuliwa kama kumrubuni.

## Sehemu B: Nini ilikuwa asili/mpangilio/mazingira ya uhalifu (je uhalifu ulitendwa kama hatia ya kivita, uhalifu dhidi ya utu, mauaji ya kimbari, au zaidi ya moja ya hizo?)?

### Uhalifu dhidi ya utu

**Vipengele:**

5) Uhalifu ulifanyika kama sehemu ya mashambulizi yaliyoenea au ya mpangilio.

6 Shambulizi lilielekezwa dhidi ya raia.

7) Mtuhumiwa alijua kuhusu mashambulizi dhidi ya raia.

8) Shambulio lilifanywa kwa mujibu wa, au katika kuboresha, sera za serikali, au shirika za kufanya mashambulizi hayo (kipengele cha mamlaka ambacho kinaweza kuhitajika au pengine kutohitajika kwenye mamlaka ambayo unaweka kumbukumbu).

| TENDO LILITENDWA KATIKA MAZINGIRA GANI? | Mifano ya MASWALI kuhusu MAZINGIRA AMBAYO TENDO LILITENDWA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA ambazo zitaweza kuthibitisha kuwa tendo hili (mfano la utumwa wa ngono) ni uhalifu dhidi ya ubinaadamu |
|---|---|---|
| Taarifa gani zinasaidia thibitisho kuwa tendo hili (mfano la utumwa wa ngono) lilikua ni sehemu ya mashambulizi yaliyoenea? | Unaweza kuniambia nini tena kilikuwa kinaendelea, wakati na baada ya matendo uliyonielezea? Unaweza ukanielezea jinsi mashambulizi unayoyaongelea yalivyotokea? Nini kilitokea kwanza, na nini kilifuata, na nini baada ya hapo? Uliweza kugundua mfumo wowote kwenye mashambulizi ya aina yoyote? Nini kilikufanya ufikie uamuzi huo? Uliona matukio mengine yoyote yanayohusika na mashambulizi kama hayo uliyoyaelezea? (Huyo mwanamke anakupa taarifa za matokeo aliyoyaona, ili uweze kujua ni nani, nini, lini, wapi, kwanini na vipi, na pia amejuaje.) | **Ushahidi:** Shahidi anaelezea ilikuwaje, kwa muda wa miezi minane aliyokuwa anatoroka sehemu hadi sehemu, aliona vijiji vingi vikishambuliwa na alikuwa shahidi aliyeona matokeo mengi ya mauaji na kupigwa, ya kufungwa na kuondolewa mbele ya mtutu wa bunduki. Huyo shahidi amesema kuwa kwenye vijiji vingi alivyoviona kwanza aliona kuwa kulikuwa na mashambulizi ya anga; majeshi ya ardhini yaliingia kijijini na kumuamuru kila mtu kuondoka; na mwisho watu wenye silaha waliingia kwa miguu na farasi na kuwapiga risasi wanakijiji walivyojaribu kukimbia. Malori yalikuja na wanakijiji waliokamatwa walichukuliwa. Shahidi hakuwaona tena. (Mwanamke anakupa taarifa za matukio aliyoyaona, ili uweze kuonyesha ni nani, nini, lini, wapi, kwa nini na vipi, na pia amejuaje.)<br><br>**Ushahidi wa nyaraka:** Ofisi ya waangalizi wa kijeshi wa Umoja wa Mataifa imetoa ripoti inayoelezea mashambulizi ya silaha yanayotokea kwenye maeneo mbali mbali ya makazi ambayo yako mbali na maeneo ya mapambano, yanayotokea kwa wakati mmoja na inaonekana yameratibiwa. |

| TENDO LILITENDWA KATIKA MAZINGIRA GANI? | Mifano ya MASWALI kuhusu MAZINGIRA AMBAYO TENDO LILITENDWA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA ambazo zitaweza kuthibitisha kuwa tendo hili (mfano la utumwa wa ngono) ni uhalifu dhidi ya ubinaadamu |
|---|---|---|
| | | **Video/picha:** Shahidi anakupa video aliyorekodi ya wanawake waliovaa nguo za kiraia wakikamatwa na wanaume wenye silaha. Video inaonyesha eneo kwa mapana na marefu, kisha eneo kwa karibu, kwa kiasi iwezekanavyo, na video ina tarehe na wakati wa kurekodi. Pamoja na video, shahidi anakupa tamko linaloeleza ni nani, nini, lini, wapi, kwa nini na jinsi, na yeye amejuaje. Inatoa maelezo yote kuhusu mazingira ambayo video ilirekodiwa.<br>**Setilaiti:** Picha za setilaiti zilizorekodiwa kwa kipindi cha muda zinaonyesha vijiji kabla ya mashambulizi (na watu wanashughulikia mifugo yao na kutunza mashamba yao) na kisha vijiji baada ya shambulio hilo. Kila picha ya baada ya mashambulizi inaonyesha maelezo kama hayo, ikiwa ni pamoja na safu za wanawake na wasichana wakitembezwa kwenda nje ya kijiji. |
| Ni taarifa gani zinakubaliana na hitimisho kwamba mashambulizi yalifanywa dhidi ya raia? | Tafadhali eleza kitu gani kingine kilikuwa kinaendelea wakati unashuhudia/yanatokea mambo haya mabaya. Nini kinatokea kwenye eneo ambalo unaishi? Watu wa aina gani waliishi hapo? Walifanya nini? Unaweza kuniambia zaidi kuhusu unaosema walishambuliwa – walikuwa wamevaa nini? Walikuwa wamebeba nini? Walikuwa wanakaa wapi na je, kulikuwa na kituo chochote cha kijeshi au vifaa au watumishi wa aina yoyote katika maeneo ya jirani? Kwa ufahamu wako, walikuwepo wapiganaji wowote katika eneo lako wakati wa matukio unayoyaelezea? | **Ushahidi** Shahidi anaeleza kuwa waathirika katika kijiji chake walikuwa wamevaa nguo za kiraia. Hawakuwa wanamiliki silaha zozote zile, na kulikuwa hakuna jeshi wala kundi lenye silaha wakati wa mashambulizi:<br>"Katika siku na wiki kabla ya sisi kukamatwa na kushikiliwa, watu wenye silaha walienea kwenye kijiji chetu na vijiji vyote katika mkoa wetu. Wapiganaji wa eneo letu walikuwa wameondoka kutoka kwenye eneo letu muda mrefu kabla, lakini watu wenye silaha walifanya kama vile sisi wote tulikuwa ni walinzi wa kijiji. Walipitisha mizinga yao kijijini kwetu, na kuua mifugo yote na kuharibu mashamba yetu. Kisha walianza kubomoa nyumba na buldoza, na hii ilisababisha wengi wetu kukimbia nje ya nyumba zetu na kwenye eneo la wazi ambapo shambulizi hilo likifanyika. Walichukua wanawake na wasichana, na wavulana wadogo pia, wakatutupa kwa ukali nyuma ya magari makubwa/malori." |

| TENDO LILITENDWA KATIKA MAZINGIRA GANI? | Mifano ya MASWALI kuhusu MAZINGIRA AMBAYO TENDO LILITENDWA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA ambazo zitaweza kuthibitisha kuwa tendo hili (mfano la utumwa wa ngono) ni uhalifu dhidi ya ubinaadamu |
|---|---|---|
| Taarifa gani zinasaidia hitimisho kuwa mtuhumiwa halisi alijua kuhusu mashambulizi dhidi ya raia? | Unaweza kutuambia, iwapo kwa jinsi unavyojua, kulikuwa na uhusiano wowote kati ya watu waliokuja kijijini kwako na kutenda vitendo ulivyovitaja, na watu ulioleza kuwa walikushikilia kwenye vyumba vilivyofungwa na kukutesa usiku? | **Ushahidi:** "Wale watu walikuwa wamevaa sare sawa sawa, na wakitumia lugha moja, na walikuwa kati ya wale waliokuwa wanachukua kijiji chetu - kwa maneno mengine, baadhi ya waliovamia kijiji chetu walikusanyika kwenye kikundi na kuanza kutuingiza kwenye lori. Kisha walikuwa ni wao waliotuweka kwenye kituo, ambapo, kumbe, walikuwa na kambi yao." |
| Taarifa gani zinasaidia hitimisho kuwa mashambulizi yalifanyika kufuatana na, au kuendeleza, sera za nchi au serikali kushambuliwa (kipengele cha utawala)? | Uliweza kufikia hitimisho lolote kuhusu mwelelekeo wa shambulizi? Je uliweza kusikia au kuona sheria zozote zikifuatwa? Kuna matendo yoyote ya kujirudia ambayo yalijitokeza ? Je ulikuja kujua kwanini mashambulizi haya yalifanywa? Je hii ndiyo ilikuwa sababu ya mashambulizi muda wote? Je kulikuwa na, unavyojua wewe, lengo au azma ya mashambulizi? Nani aliweka lengo au azma hiyo na umejuaje? | **Ushahidi:** "Sisi [mashahidi ni 'watu wa ndani' kutoka kwenye mamlaka ya muundo wa kundi la wanaoshutumiwa kuwa watuhumiwa] tukijadiliana mpango wa kuhakikisha malengo ya eneo letu. Kwenye mkutano huu, tumeamua kuweka sera za kumtenga mtu yeyote wa kundi [X]. Nia yetu ni kuundwa kwa taifa safi, [X]-bure. Mkakati wetu wa kijeshi uliwekwa kwenye mstari sawa na lengo hili."<br><br>**Ushahidi wa nyaraka:** Amri ya kijeshi yenye marejeo ya mkakati wa ujumla wa kijeshi ya kuteketeza kila kitu, kwa mfano. |

## Hatia za kivita

### Vipengele:

1) Uhalifu ulifanyika wakati wa mapambano ya silaha (kimataifa au kitaifa).
2) Mfarakano uliunganika na mapambano ya silaha.
3) Mwathirika ni mkimbizi/mtu anayehifadhiwa (sio msingi kwenye uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia (SGBV).[59]
4) Mhalifu alijua kuwa mwathirika ni mkimbizi/mtu anayehifadhiwa.
   NA
5) Mtuhumiwa alikuwa anafahamu hali halisi iliyoanzisha hali ya mapambano ya silaha.

| TENDO LILITENDWA KATIKA MAZINGIRA GANI? | Mifano ya MASWALI kuhusu MAZINGIRA AMBAYO TENDO LILITENDWA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA ambayo inaweza kusaidia kuthibitisha kuwa tendo hilo (mfano la utumwa wa ngono) ni la uhalifu wa kivita |
|---|---|---|
| Taarifa gani inasaidia hitimisho kuwa tendo hili (mfano la utumwa wa ngono) lilitendeka wakati wa vita (kimataifa au kitaifa)? | Tafadhali elezea nini kilikuwa kinatokea eneo la mji wako wakati matukio unayoyaelezea yalivyokuwa yanatokea. Unaelezea risasi na milipuko: Unaweza kuniambia ni mara ngapi ulisikia hiyo, na mapigano ya risasi na milipuko yalikuwa makubwa kiasi gani? | **Ushahidi:** "Mwanzo kulikuwa na sauti za risasi na milipuko kila mara kwenye siku kabla ya kuvamiwa. Tulisikiliza redio kila mara na kusikia namba za majeruhi vitani, na tulijua kuwa mapambano yalikuwa yanakuja kwetu. Tulijaribu kuhama sehemu hadi sehemu lakini mwisho kulikuwa hamna sehemu yenye usalama." |
| Taarifa gani zinasaidia thibitisho la kuwa uhalifu ulikuwa na mahusiano na vita? | Unaweza kuniambia zaidi kuhusu mazingira ambayo haya matendo unayoyahadithia yalitokea? Umeshaelezea kusikia risasi na milipuko na kusikia ripoti za vita. Ilitokea nini mji wenu ulivyoshambuliwa? Unahisi nini yalikuwa ni mahusiano kati ya mapambano uliyoyasikia na kilichotokea kwenye mji wenu? | **Ushahidi:** "Jeshi lilipoingia kwenye mji, vitu vibaya vilianza kutokea. Jeshi lilizunguka mji, na liliingia kwa miguu na kwa vifaru vya jeshi na farasi. Walikuwa wanaziba barabara na kuingia kutoka pande zote mbili; watu walijaribu kutoroka kati kati ya nyumba, lakini kulikuwa na wanajeshi wengi hapo kiasi cha kwamba wengi wao walipigwa risasi walivyojaribu kutoroka. Walikuwa wanapiga risasi kote, wakiwasha moto majumba na mapori, na kupiga risasi kote. Walikamata wavulana na wanaume fulani, wakawafunga mikono yao nyuma, wakawapiga mateke hadi chini na kuwapiga mateke usoni. Tuligundua baadaye kuwa vikosi vya upinzani havikuweza kulinda mji na kuwa wengi wao waliuawa au walikamatwa nje tu ya mji, na kuuwacha mji bila ulinzi. Ni katika hali hii ndiyo wanajeshi walitukuta chini ya jengo lililojaa fleti |

59 Wakimbizi wanaohifadhiwa ni wale ambao ni raia au ambao hawashiriki ipasavyo kwenye vita.

| TENDO LILITENDWA KATIKA MAZINGIRA GANI? | Mifano ya MASWALI kuhusu MAZINGIRA AMBAYO TENDO LILITENDWA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA ambayo inaweza kusaidia kuthibitisha kuwa tendo hilo (mfano la utumwa wa ngono) ni la uhalifu wa kivita |
|---|---|---|
| | | zilizotelekelezwa, tumejificha chini ya meza kwenye pembe ya chumba. Wakatutoa nje, wakatukagua na tochi, na kuanza kucheka. Mmoja wao akasema 'Wacha furaha ianze! Tutawafundisha kuwatetea wapinzani; tutawaonyesha nini serikali inawafanyia wasaliti!'" |
| Ni taarifa gani inakufanya ufikie hitimisho kuwa aliyeathirika alikuwa mkimbizi anayehifadhiwa **(sio kipengele cha uhalifu wa SGBV)** | Unaweza ukawaelezea wanaume ambao, unasema, walikamatwa, walifungwa mikono, walipigwa mateke hadi wakaanguka chini na wakapigwa mateke usoni? Je unajua walikuwa ni kina nani? Je unajua iwapo waliwahi kuwa wajumbe au walihusika kwa njia yoyote na kikundi kinachotumia silaha za aina yoyote? | **Ushahidi:** "Hawa wanaume na wavulana ndiyo walikuwa wajumbe wa kikundi cha kiraia kinachoitwa Wakazi Wanaotaka Amani. Walikataa kujiunga na wapinzani - ninafahamu kwa sababu kaka na mjomba wangu walikuwa kati yao. Hawakutaka kuchukua silaha. Walitaka amani na walikataa kupigana. Walikuwa kwenye mkusanyiko wa kikao cha sala wakati mji ulipotekwa; Kwa jinsi ninavyojua, hakukuwa na silaha za aina yoyote sehemu waliyokuwa wanakaa, na wote walikuwa wamevaa nguo za kiraia, kwani walikataa, kufuatatana na maadili ya msimamo wao kuvaa kitu chochote kinachofanana na nguo za jeshi." |
| Taarifa gani zinasaidia hitimisho kuwa mtuhumiwa alikuwa akifahamu kwamba hali hii halisi iliyotendeka ni ya mapambano ya kisilaha? | Je uliweza kugundua ni nini kilitokea pale wanajeshi walipoingia kwenye sehemu ambayo Wakazi wa Wanaotaka Amani walikuwa wamejumuika katika sala? | **Ushahidi:** "Kaka yangu aliachiliwa baadaye, ila sijamwona tena mjomba wangu. Kaka yangu aliniambia kuwa wanajeshi waliingia na kuwakuta sakafuni wanasali kwenye mduara. Chumba kilikuwa na mwanga na umeme ulikuwa haujazimika bado, na kaka yangu na wengine waliwasikia wanajeshi wakija, lakini wakazidisha nguvu ya sala yao na hawakusogea kutoka kwenye sehemu zao za sala. Wanajeshi walivyokuwa wanaingia, kaka yangu alisema, alisimama kwenda kwa mjomba wake kwa sababu alikuwa ameogopa sana. Inasemekana mjomba wangu alimwambia kaka yangu kwa sauti kubwa, 'Usiogope, mwanangu, hawa wanajeshi hawawezi kamwe kudhuru amani |

| TENDO LILITENDWA KATIKA MAZINGIRA GANI? | Mifano ya MASWALI kuhusu MAZINGIRA AMBAYO TENDO LILITENDWA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA ambayo inaweza kusaidia kuthibitisha kuwa tendo hilo (mfano la utumwa wa ngono) ni la uhalifu wa kivita |
|---|---|---|
| | | watu kwenye sala.' Hapo basi wote waliburuzwa nje, mikono imefungwa, mateke, na walichukuliwa nyuma ya lori. Hivi ndivyo kaka yangu alivyoniambia aliporudi." |
| Taarifa gani zinasaidia hitimisho kuwa mtuhumiwa alikuwa akifahamu kwamba hali hii halisi iliyotendeka ni ya mapambano ya kisilaha? | Je ulikuja kujua chochote kuhusu watu walioshambulia kijiji? Je washambulizi walisema kitu chochote kuhusu mapambano nje ya kijiji chenu? Je walielezea matendo yao (yao wenyewe au ya wenzao) nje ya matukio ya kijijini kwenu siku hiyo? | **Ushahidi:** "Ninachojua mimi ni kuwa hawa ni watu kutoka vikosi vya watawala: sare zao zilikuwa na kitambulisho cha watawala na walivaa viatu vya jeshi. Magari yao yalijaa silaha za kijeshi - Sizijui ni nini, lakini ni kubwa na hizo silaha zilikuwa hazitumiki wakati mji ulivyoshambuliwa kwenye eneo nililokuwepo - angalau, sikuona hizo silaha nzito zikitumika. Zaidi bunduki za aina ya mashinegan, bastola na kombora tu ndiyo zilionyesha kuwa vifaa vyao kwa kushambulia wakaazi, lakini pia marungu na miguu yao, walipopiga mateke watu. Wanawake na wasichana waliokamatwa hawakunyanyaswa kijinsia tu lakini pia walichomwa. Najua hilo kwa sababu mimi nilikuwa mmoja wao: baada ya kuona nilichoona wakati wa mashambulio kijijini kwetu, nilikamatwa na kuteswa pamoja na wengine. Zaidi wanajeshi walikuwa wanacheka. Kila tulivyozidi kulia, walizidi kucheka." |

NYONGEZA 1

## Mauaji ya kimbari[60]

### Vipengele:[61]

Yeyote kati ya vitendo vifuatavyo, vilivyotendwa na nia ya kuharibu, kwa ujumla au kwa kiasi fulani, kikundi cha kitaifa, kikabila, rangi au dini na hivyo:

1) Kuua wajumbe wa kundi.

2) Kusababisha madhara makubwa katika mwili au kisaikolojia kwa watu wa kikundi hicho.

3) Kwa makusudi kushurutisha hali za maisha ili kuangamiza maumbile ya kikundi kwa ujumla au kiasi fulani.

4) Kuchukua hatua zinazokusudiwa kuzuia uzazi ndani ya kundi.

5 Kuhamisha watoto kilazima kutoka kikundi hicho kwenda kingine.

| TENDO LILITENDWA KATIKA MAZINGIRA GANI? | Mifano ya MASWALI kuhusu MAZINGIRA AMBAYO TENDO LILITENDWA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA ambayo inaweza kusaidia kuthibitisha kuwa tendo hilo (mfano la utumwa wa ngono) ni la uhalifu wa kivita |
|---|---|---|
| Taarifa gani zinasaidia hitimisho kuwa tendo hili (mfano la utumwa wa ngono au vitendo vyengine vya mabavu) lilifanywa na nia maalum ya kuangamiza jamii ya kikundi hichi (na taarifa gani zilizopo zinaonyesha kuwa kundi hili lina tabia la kipamoja kitaifa, kikabila, kidini au kikundi cha kikabila)?[62] | Je ulipata nafasi kumwona mtu yeyote aliyeonekana kuwa mwenye wadhifa wa mamlaka akija kambini wakati ulipokua umefungwa? Kama ni hivyo, je ulijuaje kuwa wana wadhifa wa mamlaka? Nini kilikufanya ufikie uamuzi huo? Je ulipata nafasi kumsikia hata mmoja wao akisema kitu chochote? Ulisema kuwa wewe na wengine mlioshikiliwa pamoja mkiitwa "mende". Je unajua hiyo ina maana gani | **Ushahidi:** "Kwa kweli, nilimwona afisa wa ngazi ya juu[63] akija kambini mara mbili katika miezi 10 nilokuwa nimeshikiliwa pale. Mara moja ilikuwa kwenye sikuu ya kidini ya Han, ambayo ni likizo inayosherehekewa na vikundi vya dini na kikabila ambayo wanamgambo wanashirikishwa nayo, waHan Nyingine ilikua ni siku ya kukagua vikundi vya wanamgambo. Siku zote mbili niliombwa kuvaa vizuri na nilipewa nguo nzuri za kuvaa; hizo ndiyo zilikuwa mara pekee nilizopewa nguo nzuri za kuvaa. Mtekaji wangu (ambaye akiniita mke wake) akinitoa nje kuwaonyesha watu 'mke wake wa shamba' mzuri, na ilibidi nivae ipasavyo. Nilizipenda siku hizo kwawsababu, kwa siku chache kabla, mtekaji wangu aliniwacha mwenyewe ili niweze kuwa mzima mbele ya wageni wa maana; alichomaanisha ni kuwa kuwa alikuwa mkatili na mimi alivyokuwa akinishambulia kiasi cha kwamba mara nyingi nilishindwa kutembea vizuri kwa siku chache |

60 Hiki Kitabu cha kazi za Ushahidi kimelenga kwenye uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia; hivyo matendo mengine hayakuingizwa hapa, kama kuua au kuhamishwa kwa nguvu.

61 Mauaji ya kimbari yanaweza kuhitaji hatua mbili: 1) ushahidi unaoonyesha kuwa kitendo cha unyanyasaji wa kijinsia ni moja ya matendo matano ya mauaji ya kimbari yaliyoratibiwa, na 2) ushahidi ambao unaonyesha kwamba mtuhumiwa alitenda matendo hayo kwa nia ya kuharibu, kwa ujumla au kiasi, kikundi kwenye misingi iliyopigwa marufuku kiratiba. Jedwali la chini linachagua kitendo kimoja cha unyanyasaji wa kijinsia kama mfano na kuelezea kupitia vipengele.

62 Kipengele hiki ni kipengele cha dhamira maalumu ya mauaji ya kimbari, ambayo yanahitajika kuridhishwa kabla ya mtu yeyote kuweza kutiwa hatiani kwa vitendo vinavyohusiana na mauaji ya kimbari. Dhamira maalum ya kuharibu kundi lazima ionyeshe ushahidi maalumu. Hii ni pamoja na kutosheleza hali ya dhima, kama inavyoelezwa katika Sehemu ya C.

63) Hamna sharti linalosema kuwa mtu anayeshutumiwa kuhusika na vitendo vinavyojenga mauaji ya kimbari awe afisa mwenye wadhifa wa juu. Huu ni mfano mmoja tu kwa ajili ya hiki kitabu cha kazi.

| TENDO LILITENDWA KATIKA MAZINGIRA GANI? | Mifano ya MASWALI kuhusu MAZINGIRA AMBAYO TENDO LILITENDWA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA ambayo inaweza kusaidia kuthibitisha kuwa tendo hilo (mfano la utumwa wa ngono) ni la uhalifu wa kivita |
|---|---|---|
| | nini? Ni watu gani waliitwa "mende"? Je waliweza kuwa wamemaanisha mtu mwingine yeyote? Je unajua chochote kuhusu nini kiliwatokezea wajumbe wengine wa kundi? | baadaye, na mara nyingi niliumwa na nilishindwa kunyanyuka kabisa. Lakini kwa kutarajia hizi ziara za ngazi ya juu, mtekaji wangu alinilisha vizuri, aliniwachia nilale mwenyewe, na kutokunigusa. Aliniruhusu nioge na kuvaa vizuri na nilipata likizo kutoka kwenye mateso yake. Ziara za ngazi ya juu zilivyokuja, walimwita 'Mfalme'. Sijui alishika wadhifa gani, ila alikuwa ni mtu muhimu, kwani alifika na msururu mzima wa magari, na zaidi ya wanamgambo 20 wenye silaha walimzunguka. Alikuwa na mikufu ya dhahabu shingoni mwake. Alivyofika, alisema vitu kama hivi, kwa nguvu na wazi ili kila mtu asikie: 'Ah, kwa hiyo huyu ndiyo mke wako mende! Nimesikia mengi kuhusu yeye Walete wanawake wote mende niwakague. Nataka kuhakikisha kuwa watu wangu wana wadudu walio bora kuliko wote kuwafanya wawe na nguvu iwezekanavyo kusafisha sehemu. Waache wake zenu mende wawaonyeshe wapi mende wote wanajificha; kisha kazi yenu ikimalizika, angalau mtakuwa mmeijaza dunia na watoto walio na nusu Han, na kuua walio mende kamili wote waliowazunguka.' Walivyotuita mende walimaanisha kabila letu; watu wetu wanajenga nyumba ndani ya ardhi; hiyo ndiyo mila yetu. Hamna ambaye aliyekuwa wa kabila lingine aliyeitwa 'mende'." |
| Ni taarifa ipi inasaidia hitimisho kwamba kitendo hiki (kwa mfano cha utumwa wa ngono) kilifanyika kwa nia ya kusababisha athari kubwa za kimwili au kiakili kwa watu wa kikundi? | Je, ulikuja kuelewa au kujifunza yepi yalikuwa mawazo ya mtekaji wako, na kipi alichotaka kupata, haswa, kutokana na jinsi alivyokuwa anakutendea vibaya? Je aliwahi kusema chochote kuhusu kwa nini alikuwa anakutesa? | **Ushahidi:** "Sikuweza kusoma fikra zake. Lakini naweza kukuambia kuwa yeye aliendelea kuwa mbaya sana kwangu na kujaribu aina nyingine kubwa za ukatili. Kwa mfano mara moja, alijaribu kuona kama ataweza kuweka mshumaa uliowashwa ndani ya uke wangu bila kuzimika wenyewe. Alijaribu hili mara sita kabla hajakata tamaa, na alivyonibaka baada ya hapo, maumivu yalikuwa hayavumiliki. Vilio vyangu vilimfanya atafute njia nyingine za kuniumiza. Aliniambia kuhusu watu wote wa kabila langu aliowaua siku hiyo, kwa kutumia nguvu 'niliyompa' usiku. Mara nyingine alitaja majina ya familia ambayo yeye na wapiganaji |

| TENDO LILITENDWA KATIKA MAZINGIRA GANI? | Mifano ya MASWALI kuhusu MAZINGIRA AMBAYO TENDO LILITENDWA | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA ambayo inaweza kusaidia kuthibitisha kuwa tendo hilo (mfano la utumwa wa ngono) ni la uhalifu wa kivita |
|---|---|---|
| | | wenzake waliwaua, na aliniambia kuwa atawasaka kila mjumbe wa familia yangu iwapo nitamuacha'." |
| Ni taarifa ipi inasaidia hitimisho kwamba kitendo hiki (kwa mfano cha utumwa wa ngono) kilifanyika kwa nia ya kusababisha athari kubwa za kimwili au kiakili kwa watu wa kikundi? | Je, ulikuja kuelewa au kujifunza nini yalikuwa mawazo ya mtekaji wako, na kipi alichotaka kupata, haswa, kutokana na jinsi alivyokuwa anakutendea vibaya? Je aliwahi kusema chochote kuhusu kwa nini alikuwa anakutesa? | **Ushahidi:** "Kusema ukweli cha kushangaza nilikuwa ni mmoja kati ya walioonekana wana 'bahati'. Wasichana wengi na wanawake walichukuliwa pamoja na waume na baba zao kwenda sehemu nyingine, ambapo walitenganishwa kimakusudi. Kutenganishwa huku kulikuwa kwa muda mrefu, na baada ya muda ilieleweka kuwa kutenganishwa huku nia yake ilikuwa ni kuhakikisha kuwa hatuzai watoto wa kabila letu tena. Walikataza wanaume na wanawake kukutana, zaidi ya kukutana kwa kutenganishwa na fensi kwa dakika 30 mara moja kwa wiki. Kisha wakawaingiza ndani wanawake wa kiHan kubaka wanaume na wanaume wa kiHan kubaka wanawake, na wanawake wengi wa kiHan na wanawake wa kabila letu wakapata mimba kutokana na kubakwa huku. Wanawake wenye mimba waliwekwa sehemu nyingine, na iwapo watoto walitoka weusi sana basi waliuawa hapo hapo. Baada ya muda, ilieleweka kwa kila mtu kuwa waliweka mfumo wa kupata watoto wenye rangi nyeupe na kutoturuhusu tuzae watoto wa kabila letu wenyewe. Najua hili kwa sababu wanawake wote wa familia yangu, kasoro dada yangu mkubwa, waliwekwa katika eneo hilo. Wakati vita vilivyokuwa vinakaribia kuisha, watekaji wakaanza kukata tamaa, na mpango wao wa kuzaliwa watoto weupe na kuondoa kabila letu ulifanikiwa tu kwa hilo jambo la mwisho: wakaanza kukata sehemu za uzazi za wafungwa wa kabila langu. Wengi wao walifariki katika mchakato huo, na wengine walipata majeraha ya maisha." |
| Taarifa ipi inasaidia hitimisho kuwa kitendo hiki kilifanywa na nia ya hatua ya kulazimisha kuzuia uzazi wa kundi jingine? | Angalia maswali ya juu. | (Ukweli kama ulivyoonyeshwa juu unaonesha kukidhi kipengele hiki pia.) |

NYONGEZA 1

## Sehemu C: Nani (ameshutumiwa) Katenda uhalifu huo? (Nani ameshutumiwa kuhusika na mfumo upi wa dhima[64] – ndiyo kusema, moja kwa moja kwa amri/mwenye jukumu kuu?[65])

### Jukumu la moja kwa moja

**Vipengele:**

Mtuhumiwa ametenda (moja kwa moja, sio kwa dhahiri, au kama mhusika mwenza), alitoa amri, alisihi, alishawisi, alisaidia kutenda jinai, au kwa njia nyingine alichangia kutenda uhalifu (kwa kitendo au kutotimiza wajibu) - au kwa kujaribu kutenda kosa (kwa kitendo au kutotimiza wajibu) - na kundi lenye lengo moja.[66]

| NANI ANAWEZA KUHUSIKA, na VIPI? | Mifano ya maswali ambayo yanaweza kushawishi kupata taarifa kuhusu nani ni mhusika na kivipi | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA ambayo itasaidia kuthibitisha kuwa mtu huyu au watu hawa wanaweza kuhusika na matendo haya na kwa jinsi hii |
|---|---|---|
| Mambo gani halisi yatatumika kutambua mtu/watu au kundi/makundi ya watu wanaotuhumiwa kutenda uhalifu? Mambo gani halisi yaliyopo huonyesha kuwa mtu fulani alipanga uhalifu (mfano utumwa wa ngono) kama uhalifu dhidi ya ubinaadamu? Mambo gani halisi yaliyopo huonyesha kuwa mtu fulani anaweza akawa amefanya, ameamuru, amesihi, amesababisha, au amesaidia kutenda jinai? | Je unaweza ukanielezea kuhusu hao watu ulioniambia walikufanyia vitendo hivyo? Je unaweza ukaniambia kuhusu nguo zao? Alama yoyote? Vichwa vyao/viatu, walichokua wamebeba, mambo mengine yoyote tofauti yaliyojitokeza katika kuonekana kwao – silaha zao, vifaa vyao, magari yao, lugha yao, n,k? Je ulipata nafasi kumwona mtu mweye wadhifa? Umejuaje, nini kimekufanya uamini, kuwa huyu mtu alikuwa na wadhifa wa mamlaka? Ulipata nafasi kumsikiliza huyo mtu (hizi watu binafsi) wanasema chochote? Walisema nini, | **Ushahidi:** Aliyenusurika kutoka kwenye utumwa wa ngono kama uhalifu dhidi ya ubinaadamu anawaelezea wanaoshutumiwa kuwa walikuwa wamevaa sare ya unifomu ya buluu, walibeba mapanga na kombora, walivaa glavu na kofia, na walibeba redio. Aliripoti kwamba waliyotuhumiwa kuwa wahalifu walimsalimu mtu fulani ambaye wakimuita Bwana X, na alimwona akiwapa amri na wengine waliomsalimia wakifuata maagizo ya amri yake. Alikuwa karibu na kuweza kusikia na kuona usiku, wakati Mr X na wengine wakikaa na kupanga mipango ya siku inayofuata. Alikuwepo mara nyingi wakati Bwana X akipokea amri kutoka kwa mtu kwa kupitia redio/walkie-talkie.<br><br>**Ushahidi wa nyaraka:** Unapata ruhusa kuona nyaraka kukuu za kikundi hicho cha mapambano yenye mamia ya ripoti za mapigano za kila siku za kila wiki kutoka kwa mkuu mamlaka kutokana |

64 Aina hii ya ushahidi imekuwa kipengele dhaifu kuliko vyengine vyote kwenye mashitaka ya unyanyasaji wa kijinsia na ndiyo sababu ya watuhumiwa wengi wa kesi za unyanyasaji wa jikijinsia kukutwa hawana hatia au mashtaka kufutwa. Ni vizuri kutumia muda kuangalia mfumo wa dhima kwa makini na kuuliza maswali, kwa sababu bila hivyo, ushahidi uliobaki hautaweza kuwa na uzito. Imetokea mara nyingi ambapo majaji wamesema, "Sisi tumeridhika na hatuna chembe ya shaka kuwa unyanyasaji wa kijinsia ulitokea kabisa, lakini hakuna ushahidi wa kutosha kuthibitisha kuwa mshitakiwa ndiye mwenye hatia ya vitendo hivyo." Sehemu hii ya mchakato wa kukusanya nyaraka ni muhimu sana.

65 Mara nyingi hudhaniwa kuwa ni "aina" au "daraja" fulani tu la shahidi (kama shahidi wa ngazi ya juu anayejua mambo ya ndani) watakaemiliki taarifa kuhusu watuhumiwa, hasa kama watuhumiwa wanaochunguzwa hawahusiki kikaribu na tendo la uhalifu na uhusiano kati ya tendo na mtuhumiwa sio wa moja kwa moja. Wakusanyaji nyaraka na wachunguzi wanashauriwa kujitahidi kuepuka yale wasiyokuwa na uhakika nayo kuhusu shahidi yeyote. Mashahidi waathirika ambao hawajawahi kuwaona watuhumiwa (wanaoshutumiwa) ambao wako eneo tofauti na wana wadhifa wa juu, mara nyingi hutoa ushahidi wa nguvu zaidi kuhusiana na mashtaka ya viongozi wenye wadhifa wa juu wanaotuhumiwa kufanya uhalifu. Kila shahidi lazima ahojiwe juu ya mambo haya; Kutokuuliza kunaleta hatari ya kupoteza uhusiano muhimu wa ushahidi.

66 Kutenda kosa (Mahakama ya Kimataifa ya Jinai Ibara ya 25(3)(a)) inaweza kuwa kitendo cha binafsi/cha dhahiri moja kwa moja au cha kutenda kosa pamoja na wengine; ushirikiano unatokana na umuliki wa pamoja wa uhalifu, au kufanya uhalifu kupitia mtu mwingine; kuagiza ni kumwongoza mtu mwingine kufanya uhalifu; kusihi/kushawishi ni kumchochea mtu mwingine kufanya uhalifu; kusaidia kutenda jinai ni kutoa msaada wa vitendo (kwa mfano kwa kutoa njia ya kutenda uhalifu) au moja kwa moja kuwapa moyo au msaada wa maadili watuhumiwa.

| NANI ANAWEZA KUHUSIKA, na VIPI? | Mifano ya maswali ambayo yanaweza kushawishi kupata taarifa kuhusu nani ni mhusika na kivipi | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA ambayo itasaidia kuthibitisha kuwa mtu huyu au watu hawa wanaweza kuhusika na matendo haya na kwa jinsi hii |
|---|---|---|
| | kwa nani, kwenye mazingira gani, nini yalikuwa matokeo yake au hisia kutokana na walichokisema? Je ulipata nafasi ya kuangalia ushirikiano kati ya watu binafsi kwenye kundi hilo? Ni kitu gani uliweza kuona kuhusu ushirikiano wao? Je ulipata nafasi kuwasikia wakiitana kwa jina, cheo/hadhi, nafasi, n.k? | na askari ardhini, na pia ripoti za mapambano kutoka kwa askari ardhini hadi kwa kamanda au ma afisa wa juu.<br>**Video/rekodi ya sauti:** Unapata rekodi ya sauti ya Bwana X akipewa maelekezo kwenye redio ya mkononi, iliyorekodiwa na shahidi wa ndani. Pamoja na rekodi ya sauti, huyu shahidi anakupa tamko lenye taarifa zote za nani, nini, lini, wapi, kwa nini, vipi, na pia alijuaje kuwa ni Bwana X aliyepata maelekezo, pia taarifa zote alizonazo kuhusu nani alitoa maelekezo hayo - na nini kilimfanya aamini hivyo. |

### Wajibu wa amri/jukumu kuu

**Vipengele:**

Makamanda wa jeshi

- Kamanda wa jeshi, awe anaongoza kwa idhini ya watu au bila idhini ya watu (yaani de jure au de facto), alikuwa na madaraka kamili kwa udhibiti wa walio chini yake.
- Alifahamu au alitegemewa kufahamu kuwa walio chini yake walikuwa wanatenda uhalifu
- Alishindwa kuchukua hatua za busara ili kuzuia uhalifu, kuwaadhibu watuhumiwa, au kuwasilisha kwa mamlaka husika kwa ajili ya uchunguzi.
- Kwa matokeo yake, kosa likatendeka.

Makamanda wa kiraia

- Uhusiano kati ya mkuu na walio chini yake kimadaraka ulikuwa na sifa ya ufanisi na udhibiti kamili wa walio chini yake kimadaraka.
- Alijua au alipuuza kwa makusudi taarifa ambazo zilionyesha wazi kuwa walio chini yake kimadaraka walikuwa wanafanya uhalifu.
- Uhalifu ulikuwa ni kati ya shughuli chini ya madaraka na udhibiti wa mkuu.
- Alishindwa kuchukua hatua za busara ili kuzuia uhalifu, kuwaadhibu watuhumiwa, au kuiwasilisha kwa mamlaka husika kwa ajili ya uchunguzi.
- Kutokana na kushindwa kwake kuwadhibiti kikamilifu walio chini yake kimadaraka, uhalifu ulitendeka.

NYONGEZA 1


| TENDO LILITENDWA KATIKA MAZINGIRA GANI? | Mifano ya maswali ambayo yanaweza kushawishi kupata taarifa kuhusu nani ni mhusika na kivipi | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA ambayo itasaidia kuthibitisha kuwa mtu huyu au watu hawa wanaweza kuhusika na matendo haya na kwa jinsi hii |
|---|---|---|
| Nini ukweli unaonyesha kuwa mtu fulani alikuwa na mamlaka madhubuti (kwa kamanda wa kijeshi) au uhusiano wa mkuu na wa chini yake (kwa kamanda wa kiraia) kwa walio chini yake? | Uliweza kufikia hitimisho lolote kuhusu waliokuwa na silaha ambao walikuwa kwenye nafasi ya mamlaka juu ya wengine? Unaweza kuniambia nini haswa kilikufanya ufikie hitimisho hilo? Unaweza kuelezea? Je, uliona maingiliano yoyote kati ya watu waliokufanyia hivyo na wengine kutoka kundi lao ambao wanaweza kuwa walikuja na kuondoka? Nini ulisikia na kuona? Kulikuwa na mtu yeyote, au watu wachache, ambao walionyesha kuwa na mamlaka kuliko wengine? Tafadhali elezea. | **Ushahidi:** "Nilimwona Kamanda Alex akija kituo cha kizuizini nilipokuwa nimewekwa. Niliona hii angalau mara mbili kwa mwezi. Alikuwa na walinzi wawili karibu naye wakati wowote, kila mmoja upande mmoja; Yeye alikuwa nyuma ya gari aina ya jeep na walinzi wake walitoka nje na kumfungulia mlango kila alipowasili. Niliweza kuona na kusikia kila kitu, kwani kila mara walinifanya nitayarishe vitamtam na vinywaji vikali na kuvileta nje na kuwatumikia Kamanda alipofika. Wote walisimama kumsalimu, walisimama kwa makini na walifanya chochote alichotaka. Sijui jina lake la familia, lakini wengine walimwita Kamanda Alex. Hata mkuu wa walinzi kwenye kituo cha kizuizini - jina lake lilikuwa Milo Omin - ni wazi alikuwa mwenye wadhifa wa chini ya Alex - Omin alisimama kwa makini. Kamanda Alex aliposema 'Nizungushe', Omin aliruka kumwongoza Kamanda Alex kwenye kituo." |
| Nini ukweli unaonyesha kuwa mtu huyu hasa alijua au ilikuwa ajue (kwa makamanda wa kijeshi) kuwa walio chini yake walikuwa wanatenda uhalifu (katika kesi hii ya unyanyasaji wa kijinsia), au aliamua kupuuza (kwa makamanda wa kiraia) taarifa ambayo ilionyesha wazi kuwa walio chini yake walikuwa wanatenda uhalifu? | Kwenye uzoefu wako, una sababu zozote za kuamini kuwa Kamanda Alex alijua kuwa wewe na wanawake wengine vijana mlikuwa mnateswa, kijinsia au vinginevyo vyovyote? Vidokezo gani vinakufanya useme kuwa alikuwa anajua? Nini ulichoona au kusikia ambacho kilionyesha kuwa Kamanda Alex alikuwa anajua? Vinginevyo, vidokezo gani vinakufanya useme kuwa ilipaswa ajue, au kwamba alipuuza kwa makusudi taarifa ambazo zingemwonyesha wazi kuwa walio chini | **Ushahidi:** "Omin alimzungusha Kamanda Alex kituoni na kumweleza nani alikuwa anashikiliwa hapo. Kamanda Alex aliniona kila mara alipofika na kuzunguka chumba ambacho nilikuwa nimewekwa na wanawake wengine. Tuliwekwa pale kwa kipindi cha zaidi ya mwaka na alitembelea mara nyingi, na kuzungushwa kila mara. Kulikuwa na kufuli kwenye mlango wetu. Chumba kilikuwa kinaonyesha maisha magumu, na wengi tulikuwa tumewekwa humo, kama ilivyoweza kuonekana kutokana na idadi ya magodoro sakafuni na vitu kadhaa vilivyokuwa sakafuni; ikiwa ni pamoja na kutokana na ukweli kuwa wanawake hawa vijana wengi walikuwa ndani humo wakati Kamanda Alex akizuru. Kwa muda, aliona wanawake hao hao humo. Angeona uzito wetu ukipungua na afya zetu zikidhoofika. Angeona kuwa tulikuwa kwenye chumba hicho pamoja, na angekuwa |

| TENDO LILITENDWA KATIKA MAZINGIRA GANI? | Mifano ya maswali ambayo yanaweza kushawishi kupata taarifa kuhusu nani ni mhusika na kivipi | Mifano ya USHAHIDI/TAARIFA ambayo itasaidia kuthibitisha kuwa mtu huyu au watu hawa wanaweza kuhusika na matendo haya na kwa jinsi hii |
|---|---|---|
| | wanafanya hivyo kutenda uhalifu (kwenye kesi hii ya unanyasaji wa kijinsia)? | anafahamu kuwa walio chini yake walikuwa mbali na nyumbani kwao. Angeona pia kwenye vyumba vya mahojiano kwenye ziara yake, na kwenye vyumba vya mahojiano kuna magodoro, nguo za kila aina na ndoo za maji." |
| Hali gani halisi inaonyesha kuwa mhusika alishindwa kuzuia hilo tendo (kwenye kesi hii ya unyanyasaji wa kijinsia), kumuadhibu mtuhumiwa halisi (walio chini yake), au kuwakilisha kwenye mamlaka kwa ajili ya upelelezi? | Unaweza kuniambia iwapo umeona walinzi wowote wakikemewa au kukabiliwa na matokeo ya walichokufanyia wewe au wanawake wengine? Uliwahi kumwona mhusika akiwasahihisha au kuwadhibiti walinzi kwa aina yoyote? Tafadhali elezea nini kilitokea. Je, aliwahi kusema chochote kuhusu jinsi alivyokutendea wewe au wanawake wengine? Kama aliwahi, nini kilitokea? | **Ushahidi:** "Wakati wa kifungo chetu pale, ambacho kilikuwa zaidi ya mwaka mmoja, hamna mlinzi hata mmoja aliyetutesa, aliyetupiga na kutukata, aliyetunyanyasa kijinsia - hamna hata mmoja wao, kwa jinsi ninavyojua, aliyewahi kuadhibiwa. Kwa kweli, baada ya ziara za Kamanda Alex, na baada ya muda, walinzi wale wale walionekana kuzidi kuwa huru na sisi, na walizidi kututoa nje usiku, wengi wetu zaidi kwa wakati mmoja na kwa wingi zaidi. Hamna hata mmoja wao aliyehamishwa; na mmoja wao alipandishwa cheo kuwa mkuu msaidizi wa kituo wakati wa kifungo chetu pale. Mara moja Kamanda Alex alivyotembelea na kuona chumba chetu na sisi humo ndani, alicheka na kumwambia Omin, 'Ninakuonea wivu na raha unayopata, kijana!'" |
| Ni vitu gani halisi vinavyoonyesha kuwa, kutokana na kushindwa kuchukua hatua kuzuia uhalifu, kuwaadhibu wahalifu, au kuwasilisha kwenye mamlaka kwa uchunguzi, uhalifu ulitendwa ? | Je unaamini kuwa nini kingetokea iwapo angefanya kitu kuwaadhibu watuhumiwa? Je angewaamuru wasifanye hivyo kabla hawajafanya? | **Ushahidi:** "Alikuwa ana udhibiti kamili juu yao, wangelifanya lolote ili kumfurahisha. Niliwaona wanaogopa hata kwenda hatua moja mbele bila maelekezo yake. Hakuna shaka kuwa wangefuata maelekezo yake laiti angekuwa amewaambia wasifanye hivyo; wasingepumua angewaambia wasipumue, alikuwa na mamlaka kiasi hicho. Nilimwona akiwapiga watu wake kwa kutokufuata amri mara nyingi; lakini kamwe haikuwa kwa kuwaumiza wanawake." |

NYONGEZA 2

# Nyongeza 2

## Vipengele vya Msingi vya Majibu ya Sekta Mbalimbali juu ya Unyanyasaji wa Kijinsia



NYONGEZA 3

# Nyongeza 3

## Mahojiano: Kanuni za msingi na vidokezo vyenye manufaa

Mwongozo wa kina juu ya kanuni za msingi zinazotumika kwa watendaji kwenye kuendesha mahojiano ya waathirika/mashahidi wa uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia, kama ilivyopangiliwa katika kifungu cha 7 cha Itifaki. Hii inatoa muhtasari wa mwongozo huo kwenye vidokezo vingi vyenye manufaa.

### Masuala ya awali

1. Angalia rufaa na mifumo gani ya msaada/ulinzi unaopatikana kwa mwathirika/shahidi (na mweleze mwathirika/shahidi waziwazi mipaka ya huo msaada/ulinzi). Hasa, tafuta rufaa kwa msaada wa kisaikolojia na ulinzi wa shahidi, kama upo.
2. Tathmini vipengele vya hatari vinavyohusika kwa mwathirika/shahidi kukutanana na wewe, na fanya tathmini ya hatari ya kina.
3. Kupata uelewaji sahihi wa mazingira ambayo unyanyasaji wa kijinsia unatokea na wa vipengele mbalimbali vya uhalifu kwenye sheria za kitaifa na kimataifa.
4. Kuwa na ufahamu wa mienendo ya jinsia katika nchi au kanda ambapo uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia ulifanyika.

### Mafunzo na kuhalalishwa kwa wafanyakazi

5. Kupata kwa ajili ya wanachama wa timu yako (mfano wahojaji na wakalimani) mafunzo ya imara na kina kwa jinsi iwezekanavyo (kwa mfano katika kuhoji waathirika wa unyanyasaji wa kijinsia na/au kuhoji watoto, inapohusika).
6. Halalisha wafanyakazi wako wasaidizi (kwa mfano wakalimani, vyeo vyovyote vya kati na madereva) na jadili nao masuala kama vile siri na madhumuni/mbinu za mahojiano. Hakikisha kuwa wanaahidi kufuata miongozo ya siri na ulinzi wa taarifa uliyoistawisha. Kwenye kuhalalisha inapaswa kuangalia, hasa, rekodi ya makosa ya jinai ya mtu, lakini pia (iwapo inapatikana) rekodi yoyote inayoonyesha uwezo wa mtu binafsi kufanya kazi na watoto; mahusiano ya zamani au ya sasa na vikundi vinavyotumia silaha; mahusiano na wengine ambao wanauhusiano na makundi yanayotumia silala; usawa na unyeti; busara na heshima kwa mamlaka; na uwezo wa kuweka kando miundo ya kijamii na ya kiasili na kufanya kazi ndani ya muundo na mamlaka iliyowekwa na timu ya mtendaji.

### Kujitayarisha kwa mahojiano

7. Andaa mpango wa mahojiano (kwa mfano kigezo cha awali cha mahojiano au muhtasari, pamoja na orodha ya maswali/mada maalum ya vipengele vya uhalifu vinavyohusika na mazingira ambayo wewe unahifadhi nyaraka). Hakikisha unaangalia maswala ya "nani", "nini", "wapi", "lini" na "vipi" ya uhalifu (ukibaki muangalifu kuhusu kumwuliza aliyenusurika/shahidi maswali yoyote ya "kwa nini", ili kutokumlaumu aliyenusurika/shahidi). Kumbuka using'ang'anie sana orodha hii, na hakikisha kuwa unaonyesha hisia na unachokisikia kutoka kwa aliyenusurika/shahidi.) Usisahau kuuliza "Je unajuaje?" au "Nini kilikufanya ufikie uamuzi huo??" Mara nyingi jibu la maswali haya litakupa ushahidi muhimu.
8. Tafakari lugha utakayotumia wakati wa mahojiano, na jadili suala hilo na mkalimani. Hasa, tambua msamiati sahihi kwa vitendo vya ngono na viungo vya mwili. Jikumbushe na mkumbushe mkalimani kujitayarisha kuongelea masuala ya msamiati na aliyenusurika/shahidi, iwapo yatajitokeza wakati wa mahojiano.

9. Tayarisha nyaraka zozote, michoro, picha, ramani, video, nk ambazo unaweza kumwonyesha aliyenusurika/shahidi. Uwe na daftari la madokezo na kalamu kabisa. Leta Kamera na Rula iwapo utahitaji kupiga picha za majeraha. (Hata hivyo, kuwa makini, usimwonyeshe aliyenusurika/shahidi mchoro au picha au video zozote ambazo zinaweza kuwafanya wabadilishe ushahidi wao. Iwapo huna uhakika kama kumuonyesha aliyenusurika/shahidi nyenzo yoyote inayoweza kusababisha abadilishe ushahidi wake, basi usimwonyeshe.)

10. Ruhusu muda wa kutosha kuendesha mahojiano kamili (yaani kwa uchache masaa 3-6, pamoja na mapumziko). Haya si mahojiano ya kujaribu kuyaingiza katikati ya mahojiano mengine; yanaweza kuwa marefu. Usisite kurudi siku ya pili kuendelea, ili kuepuka uchovu au usumbufu mkubwa na kuvuruga utaratibu wa kila siku wa aliyenusurika/shahidi.

11. Mwulize aliyenusurika/shahidi iwapo angependelea muhojaji na/au mkalimani wa kiume au wa kike. (Kumbuka kutokuchukulia kuwa siyo walionusurika/mashahidi wote wa kike watakaopendelea wahojaji/wakalimani wa kike au kuwa walionusurika/mashahidi wote wa kiume watapendelea wahojaji/wakalimani wa kiume;. Kila aliyenusurika/shahidi anaweza kufanya uamuzi wake mwenyewe. Kila iwezekanapo, daima uliza nini upendeleo wa aliyenusurika/shahidi.)

12. Kuhusu mazingira halisi ya mahojiano yako, chagua eneo lenye usalama, faragha, linalokubalika kimila na maridadi (mfano epuka eneo la umma). Andaa eneo la mahojiano (kwa mfano kama inawezekana kutegemea na mazingira, weka maji ya kunywa kwenye chumba, choo cha kuweza kutumiwa; zima simu yako na hakikisha kuwa hakutokuwa na usumbufu). Iwezekanapo, tayarisha sehemu ya kukaa (kwa mfano viti, madawati, ambapo kila mtu atakaa) ili pawe panafarajisha na salama kwa aliyenusurika/shahidi na muhojaji. Tafakari jinsi gani aliyenusurika/shahidi husika atasafiri kuja kwenye mahojiano na kurudi kutoka kwenye mahojiano (kwa mfano angalia usalama, umbali na gharama ya usafiri kwa aliyenusurika/shahidi, na angalia wakati wa siku). Tafakari mipango ya huduma za watoto.

13. Amua mfumo wenye usalama na wa siri kwa ajili ya kurekodi taarifa zilizopatikana wakati wa mahojiano. Kama mhojiwa ana taarifa nyeti, jenga mfumo utakaosaidia asijulikane **(angalia Nyongeza 4)**.

### Kuanza mahojiano

14. Pata ridhaa ya aliyenusurika/shahidi kwa mahojiano (kwa mfano jadili lengo/asili ya mahojiano na jinsi gani taarifa hizo zilizopatikana kutoka kwa aliyenusurika/shahidi zitaweza kutumiwa, ikiwa ni pamoja na mipaka ya siri) na ongea na aliyenusurika/shahidi kuhusu wasiwasi wowote atakaokuwa nao. Mweleze aliyenusurika/shahidi wazi kuwa anaweza kuamua iwapo anataka au hataki kuongea na wewe, na kuwa anaweza kuamua hivyo kabla, wakati na baada ya mahojiano. Jadili suala la ridhaa na mkalimani Kabla ya kuendelea, mwulize aliyenusurika/shahidi kama ana maswali yoyote.

15. Mwulize aliyenusurika/shahidi iwapo amewahi kutoa kauli yoyote kabla ya hii au kama amewahi kuhojiwa, na/au uliza ni nani mwingine amewahi kujadili naye masuala haya.

16. Mjulishe aliyenusurika/shahidi kwa kila mtu aliye ndani ya chumba cha mahojiano na mweleze wazi majukumu yao, na ongea naye kuhusu majukumu yoyote atakayokuwa nayo.

17. Mweleze aliyenusurika/shahidi ni muda gani mahojiano yanaweza kuchukua na sisitiza ridhaa yako kuweza kufanya mabadiliko wakati wa mahojiano (kwa mfano maongezo kufanyika kwenye kipindi cha zaidi ya kikao kimoja, iwapo wataona ni bora zaidi). Pia mjulishe aliyenusurika/shahidi wazi kuwa anaweza kupumzika au kusitisha mahojiano wakati wowote.

## Wakati wa mahojiano

18. Kumbuka kuwa makini na mwenendo wako kwa aliyenusurika/shahidi kabla, wakati na baada ya mahojiano (yaani kubaki na adabu, heshima, subira na umakini; kumwangalia na kuongea na aliyenusurika/shahidi ana kwa ana, na kuwa makini na uzito wa sauti/ sauti yako na ya mkalimani wako). Kaa kwenye upeo mmoja wa jicho na aliyenusurika/ shahidi (au chini).

19. Kila mara, mpe aliyenusurika/shahidi uwezo wa kukubaliana/kutokubaliana, kujibu/ kutokujibu, kuuliza maswali na taarifa kuweza kurudiwa. Mpe aliyenusurika/shahidi taarifa za kutosha kuweza kufanya uamuzi kuhusu ridhaa yao.

20. Onyesha imani na heshima, na siyo huruma. Epuka kutoa ahadi za aina yoyote (kwa mfano kuhusiana na siri). Uwe tayari kukubali mabadiliko wakati wowote wa mchakato.

21. Mhimize aliyenusurika/shahidi kutoa taarifa kwa njia anayoiona bora kabla ya kuuliza maswali maalum yanayohusu vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia (yaani jenga uhusiano, epuka maswali yenye muelekezo, jadili masuala kwa ujumla na yenye wepesi kabla kujadili masuala nyeti; omba ufafanuzi na maelezo ya ziada, uwe tayari kukubali mabadiliko).

22. Kumbuka kamwe usichukulie tu kuwa unafuhamu kitu chochote kuhusu hisia au mawazo ya aliyenusurika/shahidi, kuhusu ukweli, kuhusu mapendeleo yake, au kuhusu ni jinsi gani trauma/kiwewe kimemuathiri.

23. Kumbuka kwamba walionusurika/mashahidi watajiweka na wataonyesha hisia kwa namna tofauti na mbalimbali wakati wanahadithia au wanarudia kuhadithia hadithi yao - yaani

    anaweza kuwa mwenye:

    - mashaka/wasiwasi/mpweke; au
    - hasira/anayependa kujitetea/anayekataa kila kitu; au
    - shwari/mtulivu/muwazi.

    Hamna njia "moja tu" ya mwenendo.

24. Kumbuka kutokufikiria tu kuwa aliyenusurika/shahidi atakuwa:

    - mwenye aibu/hofu ya majadiliano; au
    - dhaifu/mwenye trauma/kiwewe/asiyeaminika/mwenye hofu na watu; au
    - zaidi anakasirishwa kuhusu unyanyasaji wa kijinsia (kuliko vitu vingine vya jambo lililomkumba); au
    - kuumizwa kimwili.

## Kumaliza mahojiano

25. Rekodi taarifa za kutosha kuhusu aliyenusurika/shahidi ili kukuwezesha wewe kuwasiliana nao kama taarifa zaidi zitahitajika, na kuwapa taarifa za kutosha ili kuwawezesha kuwasiliana na wewe. Hakikisha njia ya kuwasiliana watakayopendelea **(angalia Nyongeza 4)**.

26. Rudia kwa aliyenusurika/shahidi mambo waliyo na wasiwasi nayo na taarifa walizozitoa, na shughulikia masuala yoyote ambayo wameeleza kuwa na wasiwasi nayo (kwa mfano masuala ya usalama, mipango ya kuwasiliana baadaye na rufaa). Tambua ushirikiano wa aliyenusurika/shahidi kushiriki katika mahojiano.

27. Mwulize tena aliyenusurika/shahidi iwapo wanatoa idhini yao kwa mahojiano (kuwapa fursa kubadili mawazo au kuondoa idhini yao wakitaka).

28. Mshukuru aliyenusurika/shahidi kwa kuongea na wewe.

29. Iwapo aliyenusurika/shahidi ataonekana kuwa na mashaka kutokana na mahojiano, jaribu kuwarudisha kwenye matokeo ya sasa na kumrejesha kwenye mawazo mazuri.

30. Kumbuka kutumia ishara sahihi kiutamaduni (mfano kushikana mikono, n.k) wakati wa kuagana.

# Nyongeza 4

## Kigezo cha Takwimu binafsi za kukusanywa kutoka kwa aliyenusurika/shahidi

Hii ni orodha ya taarifa za msingi ambazo watendaji wakusanye kutoka kwa aliyenusurika/shahidi wakati wa kufanya mahojiano:

1. Kanuni (huu utakuwa ni mfumo wa kanuni za kutumiwa na mtendaji na timu yake kwa ajili ya usalama na kuambatanisha hii takwimu binafsi na kauli halisi ya aliyenusurika/shahidi).
2. Jina la aliyenusurika/shahidi (jina la kwanza na la ukoo, na majina yoyote ya awali au ya mbadala ambayo aliyenusurika/shahidi anajulikana nayo).
3. Jinsia ya aliyenusurika/shahidi.
4. Tarehe ya kuzaliwa ya aliyenusurika/shahidi.
5. Sehemu ya kuzaliwa ya aliyenusurika/shahidi.
6. Jina la baba wa aliyenusurika/shahidi.
7. Jina la mama wa aliyenusurika/shahidi.
8. Lugha zinazoongelewa na aliyenusurika/shahidi (pamoja na lugha atakayopendelea kutumia aliyenusurika/shahidi).
9. Lugha ya mahojiano.
10. Mahali anapoishi/anuani ya aliyenusurika/shahidi.
11. Mahali pa kuishi/anuani ya kudumu ya aliyenusurika/shahidi.
12. Namba ya/za simu/barua pepe ya aliyenusurika/shahidi.
13. Kazi ya aliyenusurika/shahidi - ya sasa au ya zamani.
14. Hali halisi ya familia (majina, umri na sehemu, iwapo inajulikana, ya wanafamilia waliotajwa).
15. Uraia wa aliyenusurika/shahidi.
16. Dini ya aliyenusurika/shahidi (iwapo ina umaana na sahihi kwenye mazingira).
17. Kabila/asili ya kabila ya aliyenusurika/shahidi (iwapo ina umaana na sahihi kwenye mazingira).
18. Tarehe, sehemu na saa ya mahojiano.
19. Watu waliokuwepo kwenye mahojiano na vyeo/majukumu yao.
20. Ushahidi wa ziada uliotolewa na aliyenusurika/shahidi katika mazingira ya mahojiano (kwa mfano picha, michoro, ramani, video, taarifa za matibabu, nyaraka nyingine, n.k) na mfumo wa kanuni wa hiyo.

21. Taarifa zinazoeleza iwapo aliyenusurika/shahidi anakubali kuwasiliana tena.
22. Taarifa zinaoeleza iwapo aliyenusurika/shahidi anahitaji msaada wa kisaikolojia.
23. Taarifa zinazoeleza iwapo aliyenusurika/shahidi anakubali ushahidi wake kupelekwa kwenye mamlaka ya mahakama ya kitaifa (taja ipi).
24. Taarifa zinazoeleza iwapo aliyenusurika/shahidi anakubali ushahidi wake kupelekwa kwenye mamlaka ya mahakama ya kimataifa (taja ipi).
25. Saini ya aliyenusurika/shahidi baada ya kuisoma tena (iwapo mtendaji ameamua kuwa kauli itiwe saini).

# Nyongeza 5

## Kuwapeleka Rufaa walionusurika kutokana na unyanyasaji wa kijinsia ili kupata misaada

Kabla ya kuanzisha mchakato wowote wa kuweka nyaraka, watendaji wajitahidi kubaini njia mbalimbali za kuwatafutia walionusurika/mashahidi msaada, na wanapaswa kuweka taratibu za mchakato wa rufaa. Walionusurika na mashahidi wote wana haki ya kujua kabla ya mahojiano, ni misaada gani ya afya, kisaikolojia, sheria na huduma za jamii iliyoko kwa ajili yao.

Watendaji waweke jitihada zinazohitajika kutathmini iwapo huduma wanazowapelekea walionusurika ni sahihi na zinapatikana. Hii ni kweli hasa kwa watoto wanaohitaji rufaa, ambao mahitaji yao ya muda mrefu inabidi yatekelezwe ili kuhakikisha usalama wao wa kimwili na kihisia.

Watendaji wanapaswa kutambua kwamba uwezo wa aliyenusurika/shahidi kupata huduma za rufaa na msaada unategemea jinsia- wanaume na wanawake walionusurika wanatendewa tofauti wakati wa kutafuta msaada.

Aina ya misaada inayoweza kupatikana kwa walionusurika/mashahidi imewekwa hapo chini.

| Msaada wa matibabu | Msaada wa kisaikolojia |
|---|---|
| Hospitali, vituo vya afya na kliniki zenye vifaa vinavyofaa kutibu na kusaidia walionusurika baada ya kubakwa pamoja na mashahidi. Kwa kima cha chini, vutuo vitoe:<br>• matibabu na rufaa kwa matatizo yanayohatarisha maisha;<br>• matibabu au kinga kwa magonjwa ya zinaa;<br>• kuzuia mimba kwa dharura;<br>• huduma ya majeraha;<br>• ushauri wa kusaidia; na<br>• huduma za rufaa kwa msaada wa kijamii na ushauri wa kisaikolojia. | Huduma za ushauri, msaada wa kikundi kwa aliyeathirika, mashirika yenye uweza wa kuongoza kesi, na vituo vya jamii vinavyoweza kutoa:<br>• msaada wa kihisia na ushauri wa moja kwa moja wa siri;<br>• upatanishi na ushauri wa siri wa familia;<br>• kuunganishwa na jamii na misaada ya kimaisha; na/au<br>• mafunzo ya ujuzi na miradi ya kuzalisha mali. |
| **Msaada wa kisheria** | **Msaada wa ulinzi** |
| Kliniki za Kisheria, vikundi vya kusaidia waathirika, programu ambazo zinatoa:<br>• Elimu ya kisheria kuhusu haki za waathirika/mashahidi kwenye sheria;<br>• ushauri wa siri kuhusu haki za kisheria na chaguo; na/au<br>• uwakilishi wa kisheria kwa waathirika/mashahidi. | Mashirika, vikundi vya kusaidia waathirika, vituo vinavyotoa:<br>• hifadhi/malazi yaliyo salama;<br>• kuhamishwa na msaada wa usafiri; na/au<br>• mipango ya ulinzi wa shahidi. |

# Nyongeza 6

## Ushahidi unaoonekana: Kanuni za Mlolongo wa Utunzaji

1. Watendaji wanapokuwa kwenye maeneo ya kazi, wanaweza kukuta kitu kitakacho waonyesha kuwa kitendo cha unyanyasaji wa kijinsia kimetokea; au kitakachoweza kuonyesha unganisho kati ya uhalifu na mwathirika au na mtuhumiwa. Kwa mfano, katika eneo la uhalifu wanaweza kukuta kipande cha nguo iliyojaa au kuchafuliwa na damu; au wanaweza kupewa silaha ambayo aliyenusurika/shahidi anawaambia ilitumika kufanya ubakaji; au wanaweza kumrekodi afisa wa jeshi akisema kuwa aliamuru ubakaji utendeke kama sehemu ya kampeni za kijeshi.

2. Chochote kati ya vitu hivi vinaweza kuwa "ushahidi wa kuonekana" utakaoonesha kuwa unyanyasaji wa kijinsia umetokea. Kwa kanuni za kawaida, mtendaji asikusanye kitu chochote chenye ushahidi wa kujionyesha, isipokuwa tu iwapo amepata mafunzo ya upelelezi au mhudumu wa afya kwenye kukusanya kisahihi ushahidi wa kisayansi kuhusu uhalifu (forensiki). Iwapo watendaji watakusanya ushahidi unaoonekana bila ya kupata mafunzo ya kutosha, wataweza kumwumiza vibaya aliyenusurika na kuharibu ushahidi, kuufanya usiweze kutumika. Hata hivyo, katika baadhi ya mazingira machache, ambapo kuna usalama na ambapo hilo ndilo chaguo pekee, ukusanyaji wa ushahidi wadhahiri unaweza kufaa. Uamuzi wa kuchukua ushahidi unaoonekana uchukuliwe kimakini sana, na ufikiriwe vizuri sana.

3. Kabla hata ya kufikiria kukusanya vitu vya ushahidi unaoonekana, lazima kwanza watendaji: waandike vitu vyote walivyovikuta; chora eneo la uhalifu; piga picha vitu na eneo la uhalifu; na, kama ikiwezekana, wapige video vitu na eneo la uhalifu **[linganisha na Nyongeza zingine]**.

4. Moja ya sababu kuu kwa nini watendaji ni lazima kurekodi hivyo ni kwa sababu mbinu za utafiti walizotumia zinaweza baadaye kufanyiwa tathmini huru - hasa kwa kutathmini kama matendo yao yamebadilisha ushahidi. Pia, waendeshe mahojiano na mashahidi wowote waliokuwa karibu na eneo la uhalifu na kufuata vidokezo kwa mashahidi wengine ili kufikia kwenye hatia **[linganisha na Nyongeza zingine]** Ushahidi huu mwingine – ukikusanywa vizuri – unaweza kuwa na uzito wa nguvu sana na unaweza kuondoa haja ya ushahidi wa dhahiri.

5. Ni muhimu sana kukumbuka kuwa ingawa ushahidi dhahiri unaweza kuonekana kama ndiyo ushahidi "bora zaidi" kwenye kuonyesha uhalifu, hilo siyo kweli kila mara. Ushahidi dhahiri unaoonekana bila ushahidi wa aliyenusurika/shahidi unaoelezea asili, umiliki na utumiaji wa kitu, au matokeo yaliyotangulia kukusanya vitu, hautosaidia sana kutokana na upeo wa ushahidi. Wakati ushahidi wa aliyenusurika/shahidi unaweza kuchukua nafasi ya ushahidi dhahiri unaoonekana, kinyume cha haya si sahihi: ushahidi unaoonekana, mara nyingi, hauwezi kuchukua nafasi ya ushahidi wa aliyenusurika/shahidi.

6. Pia, kama watendaji si wachunguzi waliopata mafunzo au wahudumu wa afya, ingefaa kuepuka kujiweka kwenye nafasi ambayo wanaitwa kama shahidi ili kueleza jinsi walivyokuja kuona kitu cha ushahidi wa dhahiri.

7. Katika hali isiyo ya kawaida sana ambapo watendaji wanaamua kukusanya ushahidi unaoonekana, kanuni za "mlolongo wa Utunzaji" zilizowekwa katika Nyongeza hii zifuatwe.

8. Hata hivyo, watendaji lazima wakumbuke kwamba ukusanyaji wa ushahidi ni lazima wakati wote uambatane na ukusanyaji wa taarifa unaothibitisha ukweli wake na/au ushahidi na maelezo, ili kuwa na matumizi ya manufaa. "Mlolongo wa Utunzaji" ni njia ya kuonyesha ni wapi kitu kimetoka. Pia ni njia ya kuonyesha kwamba kitu hakijawahi kuharibiwa katika kipindi cha katikati baina ya kukusanywa na mtendaji na matumizi

yake kama ushahidi wa uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia. "Mlolongo wa Utunzaji" ni muhimu sana, kwa sababu bila ya hivyo mahakama inaweza kukataa kuchukulia vitu kama ushahidi katika mashtaka ya uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia, au inaweza kuamua kwamba hicho kitu siyo ushahidi mzuri sana wa uhalifu. Ni suala la iwapo unaweza kutegemea kitu - aliyegunduwa ukweli, hana budi ajihakikishie kwamba ukweli wa ushahidi unaweza kutegemewa, na kwamba haujapachikwa tu au kuchezewa au kuharibiwa kimakusudi. Utaratibu wa "Mlolongo wa Utunzaji" ni lazima uruhusu mtendaji kufanya hivyo - kwa jinsi hiyo, ushahidi utapewa uzito unaostahili.

**Kanuni**

9. Kumudu "Mlolongo wa Utunzaji" wa kitu, watendaji inabidi warekodi:

   A. jinsi kitu kilivyokusanywa; na

   B. iwapo (na jinsi) umiliki wa kitu ulihamishiwa kati ya watu binafsi na/au mashirika mbalimbali.

   Watendaji wanapaswa pia kuwa na ufahamu wa mahitaji ya kisheria katika mamlaka husika kuhusu "Mlolongo wa Utunzaji."

### A. Kitu kilikusanywa vipi?

Ingawa mbinu za kukusanya zitakuwa tofauti kutegemea na kitu husika (mfano maji ya mwili hukusanywa na kufungwa tofauti na kipande cha nguo au nyaraka), kanuni ya kawaida ni kwamba kila kitu lazima kiwe na alama yenye maelezo yafuatayo:

1. kitambulisho cha kesi - Namba iliyopewa kesi fulani ambayo inaweza kuhusisha maelezo yote yanayohusu kesi hiyo;
2. tarehe ya kukusanywa;
3. jina la mtendaji aliyekusanya hicho kitu na majina ya watu wengine wowote waliyokuwepo wakati wa kukusanywa;
4. eneo halisi kilipotokea hicho kitu wakati wa kukusanywa; na
5. aina ya ushahidi uliokusanywa.

Pia watendaji waweke maelezo kuhusu hatua zilizochukuliwa kuhakikisha kuwa hicho kitu kiliwekwa kwenye usalama wakati kilivyokuwa kwenye milki yao (kwa mfano kiliwekwa kwenye kabati lililofungwa ambalo ni timu ya mtendaji tu ndiyo walikuwa wanaweza kufungua).

Pia watendaji waweke kumbukumbu ya kuonesha ni muda gani baada ya tukio la unyanyasaji wa kijinsia ushahidi dhahiri unaoonekana uligundulika; ukaribu baina ya eneo la tukio na ushahidi unaoonekana ulipogundulika; na wamejuaje ukweli huu.

Kama mtendaji hakukusanya ushahidi mwenyewe, anapaswa pia kutoa maelezo ya makubaliano, masharti ya mazungumzo kuhusu utumiaji wa ushahidi kati ya mtu anayekabidhi ushahidi unaoonekana na mtendaji.

Kitu chochote anachokusanya mtendaji kiwekwe kwenye mfuko wa ushahidi (mfuko wa plastiki unaofungika kirahisi utatosha iwapo hamna maji/umaji umaji kwenye kitu; iwapo maji/umaji umaji upo, bahasha ya karatasi isiyo na asid inapendelewa). Mfuko/bahasha ifungwe na kupigwa mhuri; na mhuri utiwe saini na mtu aliyekusanya hicho kitu. Huu mfuko/bahasha isifunguliwe wakati wowote.

Ingependekezwa kuwa taarifa zote hizi ziwe kwenye karatasi moja ambayo iambatanishwe na mfuko/bahasha ya ushahidi ambayo hicho kitu kimewekwa.

Hizi habari hazihitaji kujazwa kwa kila kitu iwapo asili, tarehe na mahali ni hiyo hiyo na kama mtu anayekusanya ni huyo huyo. Hata hivyo, mchakato urudiwe iwapo kigezo chochote kati ya hivi kitakuwa tofauti, hasa chanzo cha  vitu.

### B. Je umiliki wa hicho kitu ulibadilika kati ya watu binafsi au mashirika?

Iwapo kitu kimewahi kubadili umiliki kati ya watu binafsi au mashirika, ni muhimu kuweka rekodi ya maelezo ya uhamisho huo. Hii inaweza kuoneshwa kirahisi katika "kitabu chenye habari za uhamisho".

Hiki kitabu chenye habari za uhamisho kionyeshe, kwa kila uhamisho wa kila kitu:

1. kitambulisho cha kesi – Namba iliyopewa kesi fulani ambayo inaweza kuhusisha maelezo yote yanayohusu kesi hiyo;
2. aina ya ushahidi uliyokusanywa;
3. tarehe ya uhamisho;
4. sababu ya uhamisho; na
5. saini ya anayehamisha na anayepokea.

Kimsingi, kitabu hicho kieleze hali ya usalama ulioshadidiwa wakati wa utunzaji na uhifadhi wa hicho kitu.

Kwa kawaida ni bora zaidi kujaribu kuweka namba za uhamisho ziwe pungufu kiasi iwezekanavyo.

NYONGEZA 7

# Nyongeza 7

## Ushahidi wa Nyaraka: Kanuni za Mlolongo wa Utunzaji

1. Wakati watendaji wako kwenye maeneo ya kazi, wanaweza kukuta nyaraka za maana. Kwa mfano, wanaweza kukuta nyaraka kwenye jengo la jeshi lililotelekezwa inayoonyesha muundo wa kutoa amri katika timu ya jeshi doria kwa wakati huo, au wanaweza kumkuta daktari kwenye kambi ya wakimbizi mwenye fomu ya ripoti ya matibabu kwenye milki yake ya aliyenusurika kutoka kwenye ubakaji, au wanaweza kukutana na afisa wa serikali ambaye anaweza kuwapa nyaraka itakayosaidia kumtambua mtuhumiwa. Chochote kati ya hivi vitu vinaweza kuwa "ushahidi wa nyaraka" unaothibitisha kuwa unyanyasaji wa kijinsia umetokea.

2. Kwa ujumla, watendaji wanaweza kukusanya hivi vitu hata kama hawakupata mafunzo ya uchunguzi kwenye makosa ya jinai, Kwa hiyo, miongozo inayotumika kwenye "ushahidi wa nyaraka" inatofautiana na inayotumika kwenye "ushahidi unaoonekana"**(angalia Nyongeza 6, "Ushahidi Unaoonekana: Kanuni za Mlolongo wa Utunzaji")**. Hata hivyo, kuna vikwazo:

   - Iwapo watendaji siyo wachunguzi waliopata mafunzo kwenye makosa ya jinai, wanaweza wakataka kuepuka kujiweka kwenye nafasi ambayo wanaitwa kama mashahidi kueleza jinsi gani walikutana na hiyo nyaraka.

   - Nyaraka asili za maana zikusanywe katika mazingira fulani tu. Kwa kawaida, ni njia bora kupata nakala za nyaraka zinazoongozana na uthibitishaji wa ushahidi. Kutumia mfaniuiliyowekwa hapo juu:

     a. Kama watendaji wakikuta nyaraka kwenye jengo la jeshi lililotelekezwa linaloonyesha muundo wa kutoa amri katika timu ya jeshi doria kwa wakati huo, wawe na sababu ya kuamini kuwa iwapo hii nyaraka ikiwachwa kwenye jengo hilo, inaweza kuharibiwa. Katika kesi hii, watendaji walenge kuchukua nakala ya nyaraka na kupata ushahidi utakaothibitisha (yaani ushahidi wenye maelezo ya kina juu ya hiyo nyaraka na mazingira ya ugunduzi, kama vile tamko la shahidi). Lakini, iwapo hilo haliwezekani, basi nyaraka ya asili inaweza kukusanywa.

     b. Iwapo watendaji wamemkuta daktari kwenye kambi ya wakimbizi mwenye fomu asili ya ripoti ya matibabu ya aliyenusurika kutoka kwenye ubakaji, wasiichukuwe hiyo nyaraka ya asili. Mgonjwa anaweza kuhitaji nyaraka ya asili kwa mahitaji yake, na kwa vyovyote fomu za ripoti za matibabu si ushahidi unaoaminika kwenye uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia kama ushahidi wa aliyenusurika. Lengo la watendaji liwe ni kuchukua nakala ya nyaraka iliyothibitishwa (iwapo ridhaa kufanya hivyo imepatikana) na kufanya mahojiano na daktari, aliyenusurika na mashahidi wengine husika **(angalia Nyongeza 3, "Kuhoji: Kanuni za Msingi na Vidokezo Muhimu kwa Vitendo vya Kazi")**.

     c. Iwapo watendaji wamekutana na afisa wa serikali ambaye anaweza kuwapa nyaraka itakayosaidia kumtambua mtuhumiwa, na wana sababu za kuamini kuwa wanaweza kukusanya kiusalama, kuhifadhi na kudumisha nyaraka mpaka hapo itakapohitajika baadaye, na iwapo wana sababu ya kuamini kuwa toleo jingine la nyaraka hii linaweza kutolewa na ofisa iwapo itahitajika, wanaweza kukusanya nyaraka hiyo halisi.

3. Katika hali ambayo watendaji wameamua kukusanya nyaraka (iwe nyaraka asili au nakala ya nyaraka), kanuni za "Mlolongo wa Utunzaji" zilizowekwa kwenye Nyongeza hii lazima zifuatwe. "Mlolongo wa Utunzaji" ni njia ya kuonyesha sehemu nyaraka ilipotoka. Pia ni njia ya kuonyesha kwamba nyaraka haijawahi kuharibiwa katika kipindi cha katikati baina ya kukusanywa na mtendaji na matumizi yake kama ushahidi wa uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia. "Mlolongo wa Utunzaji" ni muhimu sana, kwa sababu bila hivyo mahakama inaweza kukataa kuchukulia nyaraka kama ushahidi katika mashtaka ya uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia, au inaweza kuamua kwamba hiyo nyaraka siyo ushahidi mzuri sana wa uhalifu. Kudumisha "Mlolongo wa Utunzaji" wa nyaraka, watendaji wanatakiwa kurekodi vifuatavyo.

### Kanuni

A. Jinsi nyaraka ilivyokusanywa.

B. Iwapo (na jinsi) umiliki wa nyaraka ulihamishwa kati ya watu binafsi na/au mashirika.

### A. Je nyaraka ilikusanywa vipi?

Kanuni ya kawaida ni kwamba kila nyaraka lazima iwe na alama yenye maelezo yafuatayo:

1. kitambulisho cha kesi – Namba iliyopewa kesi fulani ambayo inaweza kuhusisha maelezo yote yanayohusu kesi hiyo;
2. tarehe ya kukusanywa;
3. jina la mtendaji aliyekusanya nyaraka na majina ya watu wengine wowote waliokuwepo wakati wa kukusanywa;
4. eneo halisi ilipokuwa hiyo nyaraka wakati wa kukusanywa; na
5. aina ya ushahidi uliokusanywa.
6. Pia watendaji waweke maelezo kuhusu hatua zilizochukuliwa kuhakikisha kuwa nyaraka iliwekwa kwenye usalama wakati ilivyokuwa kwenye milki yao (kwa mfano iliwekwa kwenye kabati lililofungwa ambalo ni timu tu mtendaji tu ndiyo walikuwa wanaweza kufungua).
7. Kama mtendaji hakukusanya nyaraka mwenyewe, anapaswa pia kutoa maelezo ya makubaliano, masharti ya mazungumzo kuhusu utumiaji wa nyaraka kati ya mtu anayekabidhi ushahidi unaoonekana na mtendaji.
8. Nyaraka yoyote anayokusanya mtendaji iwekwe kwa vizuri kwenye mfuko wa ushahidi (mfuko wa plastiki unaofungika kirahisi utatosha iwapo hamna maji/umaji umaji kwenye nyaraka; iwapo maji/umaji umaji upo, bahasha ya karatasi isiyo na asid inapendelewa). Mfuko/bahasha iwe na mhuri na mhuri utiwe saini na mtu anayekusanya hiyo nyaraka. Huu mfuko/bahasha isifunguliwe wakati wowote.
9. Ingependekezwa kuwa taarifa zote hizi ziwe kwenye karatasi moja ambayo iambatanishwe na mfuko/bahasha ya ushahidi ambayo hiyo nyaraka imewekwa.

Hizi habari hazihitaji kujazwa kwa kila nyaraka iwapo asili, tarehe na mahali ni hapo hapo na kama mtu anayekusanya ni huyo huyo. Hata hivyo, mchakato urudiwe iwapo kigezo chochote kati ya hivi kitakuwa tofauti, hasa chanzo cha nyaraka.

**B. Je umiliki wa hiyo nyaraka ulibadilika kati ya watu binafsi au mashirika?**

Iwapo nyaraka imewahi kubadili umiliki kati ya watu binafsi au mashirika, ni muhimu kuweka rekodi ya maelezo ya uhamisho huo. Hii inaweza kuoneshwa kirahisi katika "kitabu chenye habari za uhamisho".

Hiki kitabu chenye habari za uhamisho kionyeshe, kwa kina kila uhamisho wa kila nyaraka:

1. kitambulisho cha kesi – Namba iliyopewa kesi fulani ambayo inaweza kuhusisha maelezo yote yanayohusu kesi hiyo;
2. aina ya ushahidi uliyokusanywa;
3. tarehe ya uhamisho;
4. sababu ya uhamisho; na
5. saini ya anayehamisha na anayepokea.
6. Kimsingi, kitabu hicho kieleze hali ya usalama wakati wa utunzaji na uhifadhi wa nyaraka hiyo.

Kwa kawaida, ni bora zadi kujaribu kuweka namba za uhamisho ziwe pungufu kiasi iwezekanavyo.

NYONGEZA 8

# Nyongeza 8

## Mwongozo juu ya Kupiga Picha, Kurekodi-Video na Kuchora Maeneo ya Uhalifu, Ushahidi unaoonekana na Majeraha Mwilini

Unapokuwa kwenye maeneo ya kazi, unaweza kuona sehemu ambazo zinaonekana kuwa zinaweza kuwa sehemu ambazo unayanyasaji wa kijinsia umetokea (kwa mfano chumba chenye uchafu wa damu kwenye sakafu na godoro lililoroa), kitu kinachoashiria kuwa unyanyasaji wa damu umetokea (kwa mfano silaha ambayo unaambiwa na shahidi kuwa imetumika kutendea ubakaji) au aliyenusurika ambaye majeraha yake yanayotokana na vurugu yanaonekana (kwa mfano mwanamke mwenye majeraha ya mikwaruzo mgongoni ambaye anakueleza kuwa majeraha hayo yalisababishwa na matendo ya unyanyasaji wa kijinsia).

Pamoja na taarifa unazokusanya kutoka kwa walionusurika/mashahidi kwa njia ya mahojiano, ni muhimu kupiga picha, kuchora (na iwezekanapo) kurekodi taarifa hizi na video. Taarifa hizo – kama zikikusanywa sawa sawa – zinaweza kuwa na nguvu sana kwenye kesi za kisheria za baadaye.

Haswa kwenye ushahidi unaoonekana, ni *bora* zaidi kupiga picha, kurekodi video au kuchora ushahidi badala ya kuukusanya. Kwa ujumla, usikusanye ushahidi wowote wa dhahiri unaoonekana isipokuwa kama kuna mazingira yasiyo ya kawaida na kuwa umepata mafunzo sahihi **(angalia Nyongeza 6, "Ushahidi Unaoonekana: Kanuni za Mlolongo wa Utunzaji")** na una uwezo wa kusafirisha na kuweka kiusalama huo ushahidi.

Kwenye majeraha ya mwili, kwa ujumla inashauriwa kuwa wachunguzi wa kitibabu waliopata mafunzo ndiyo wayapige picha hayo majeraha. Hata hivyo, watendaji wengine pia wanaweza (iwapo miongozo iliyoelekezwa hapa chini itafuatwa) kupiga picha majeraha ya kawaida yasiyokuwa kwenye sehemu za siri za mwili, wakipata idhini ya mtu mwenye majeraha.

Miongozo hii kiujumla inahusu mtu yeyote anayeamua kupiga picha, kurekodi video au kuchora eneo la uhalifu, kipande cha ushahidi unaoonekana au majeraha kwenye mwili wa aliyenusurika. Hata hivyo, watendaji wengine wanaweza wasiwe na mamlaka ya kupiga picha, kurekodi video or kutengeneza michiro, hivyo kuna umaana wa kulinganisha muelekeo na watendaji wengine kwenye maeneo ya kazi na kuhakikisha kuwa mnabadilishana taarifa kawaida na kutokurudia kazi. Cha muhimu ni kile kilichowekwa katika mamlaka yako na sera za shirika lako kuhusiana na hali ambayo inaweza kulazimisha kufanya kazi nje ya mmalaka kwa muda.

Kumbuka kuwa kwenye hali ya hatari, cha muhimu ni usalama wa walionusurika/mashahidi na jumuiya yao; kama huwezi kupata picha/video ambayo inafuata mapendekezo haya yote, hiyo haimaanishi kuwa picha/video haiwezi kukubalika kama ushahidi.

## Kupiga picha na kurekodi-video maeneo ya uhalifu, ushahidi unaoonekana na mejeraha ya mwili.

Picha zinaweza kusaidia sana kama ushahidi kwenye kesi yoyote ya baadaye ya kisheria iwapo "uhalisi" wa hizo picha unaweza kuthibitishwa. "Uhalisi" unamaanisha kuwa hizo picha au ushahidi mwengine unaweza kuonekana kuwa ni wa kweli. Kuhakikisha kuwa una taarifa za kutosha za kuthibitisha uhalisi sio kitu cha urahisi kuweza kukifanya kila mara, na kuna hatua zinazoweza kuchukuliwa ili kupunguza uwezekano wa wengine kupinga uhalisi wa ushahidi.

Kabla ya uchunguzi:

1. Jifunze jinsi ya kutumia kamera yako na vifaa vingine vya kupigia picha. Haswa, jifunze jinsi ya kuweka tarehe na saa ya shughuli kwenye kamera yako na jinsi ya kusawazisha rangi na mwanga. Kama unafanya kazi katika maeneo yenye kupishana masaa, unapaswa kuweka muda wa Greenwich kwenye kamera yako.

2. Kwa njia ya mafunzo, uangalie mwongozo uliopo.

Ukiamua kupiga picha:

3. Iwapo watu binafsi wowote wanashiriki katika uchukuaji picha, pata ridhaa yao kupiga picha.
   - Hii inaweza kuhusisha kuomba idhini ya kupiga picha kutoka kwa: jamii ambayo ina mamlaka juu ya eneo la uhalifu; aliyenusurika/shahidi ambaye ana milki ya kipande cha ushahidi unaoonekana; au mwathirika ambaye alipata majeraha ya mwili.
   - Ufikirie faragha na siri ya mhusika. Kupiga picha kunaweza kuonekana kama tabia isiyokubalika kwenye mila nyingine. Hii haswa ina umuhimu unapopiga picha za majeraha mwilini.
   - Uwaeleze wahusika kuhusu matumizi ya picha yaliyokusudiwa. Hasa, kujadili suala la kutotajwa: kwa ushahidi kuweza kutumika katika kesi za kisheria zozote za baadaye, watu binafsi wowote waliopigwa picha (mfano aliyenusurika na unyanyasaji wa kijinsia) kwa kawaida hawewezi kubaki bila kujulikana.
   - Iwapo wahusika hawatatoa idhini yao, usipige picha. Waelezee wahusika matokeo ya kutokupiga picha.
   - Iwapo picha zinahusisha mabaki ya binadamu ya aina yoyote ile, ni muhimu kuyachukulia, na kuchukulia mazoea yoyote ya kiutamaduni, kwa heshima.
   - Picha zinapokuwa zimepigwa, unganisha maelezo ya mtu binafsi na hizo picha (kwa mfano kuhakikisha kwamba kila picha ina kitambulisho cha kesi au, njia nyingine, ni kuchapa au kuandika hicho kitambulisho cha kesi kwenye karatasi na kuipiga picha hiyo karatasi mwanzo na mwisho wa roli ya filamu na kadi ya kumbukumbu ya kamera - kumbuka kuwa hiki kitambulisho cha kesi kisiwe na maelezo yatakayotoa jina na anuani ya mtu binafsi).

4. Piga picha hapo hapo.
   - Iwapo unapiga picha eneo la uhalifu or kipande cha ushahidi unaoonekana, angalia usisogeze au kusumbua kitu kabla ya kupiga picha.
   - Iwapo unapiga picha majeraha ya mwili na unyanyasaji wa jinsia uliotokea karibuni, picha zipigwe mapema iwezekanavyo. Hata hivyo, ufikirie iwapo inafaa kupiga picha zingine baadaye kuonyesha majeraha, kwani majeraha mengine huchukua masaa kuonekana baada ya kiwewe/trauma.

5. Piga picha kutoka pembe tofauti na tumia alama za vipimo.
   - Kwa maeneo ya matukio ya uhalifu na ushahidi dhahiri unaoonekana:
     i. Kwanza, piga picha la eneo lote la tukio la uhalifu, kwa kutumia kitu cha kawaida kama alama ya kipimo (mfano gazeti).

ii. Piga picha za safu ya kati au zinazoonyesha mazingira kwa kila kitu tofautiili kuonyesha upangaji wa kitu kwenye eneo la tukio la uhaifu.

iii. Piga picha za karibu za kitu chochote chenye umuhimu ili kupata mazingira ya uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia (mfano nguo, madoa ya damu, au vifaa vilivyotumika kutenda unyanyasaji wa kijinsia).

- Kwa majeraha ya mwili:

i. Tumia njia yenye uthabiti katika kupiga picha: mfano kuchukua picha zote kutoka kushoto kwenda kulia na kutoka juu hadi chini ya aliyenusurika ili kuwa thabit.

ii. Hifadhi faragha na staha ya aliyenusurika wakati wa kupiga picha.

iii. Piga picha ya kwanza ya uso wa aliyenusurika ili aweze kutambulika. Hii siyo lazima iwapo mhusika aliyepigwa picha anaweza kutambulika kwenye kila picha

iv. Piga angalau picha mbili za kila jeraha kutoka kwenye pembe tofauti. Picha ya kidonda kutoka kwenye nyuzi 90 lazima ipigwe.

v. Piga picha za karibu za kila jeraha au kidonda na tumia alama ya kipimo/skeli kukuwezesha kupata vipimo sahihi vya majeraha aliyoyapata.

vi. Piga picha za safu ya kati za kila jeraha peke yake kuonesha ni sehemu gani ya mwili imeumia.

vii. Unapopiga picha za mwili mzima za aliyenusurika ili kuonyesha upeo wa majeraha mwilini, ufikirie kumvalisha au kumfunika aliyenusurika inavyostahiki.

6. Kumbuka kuwa picha zilizo wazi na sahihi ndiyo zitakazokubaliwa kwenye kesi za kisheria za baadaye.

- Iwezekanapo, picha zipigwe kwenye mwanga wa jua au mwangaza wa kiasi ili kukinga dhidi ya ufunukaji wa mwangaza.
- Eneo la kupigia picha lisiwe na rangi zilizofungamana na zingine kwa kiasi iwezekanavyo: eneo lenye rangi nyingi au msongamano wa rangi uepukwe kwani linaweza kubadilisha usahihi wa picha.
- Kamera ya dijitali inapaswa kuwa na kiwango cha uwezo wa anagalu mega-pikseli 4 au zaidi ya saizi ya picha. Kupiga picha na simu za mkononi hakushauriwi isipokuwa kama hamna njia nyingine ya kupiga picha.
- Iwezekanapo, weka ufito wa rangi kwenye picha ili kuhakikisha rangi sahihi itatokeza.
- Ni mara chache sana picha na video zinaweza kujidhihirisha kwa wazi - kwa maneno mengine, bila ya ushahidi wa aliyenusurika/shahidi na ushahidi mwingine wa kuelezea kilichopo kwenye picha/video na kueleza mazingira yake, picha/video ina hatari ya kutokuwa na thamani kama ushahidi.

7. Weka Tarehe ya picha.

- Tumia chaguo la tarehe na saa kwenye kamera, au, kama kamera haina hiyo, piga picha ya gazeti la siku hiyo mwanzo wa roli ya picha au kadi ya kumbukumbu. Kama unafanya kazi katika maeneo yenye kupishana masaa, unapaswa kuweka muda wa Greenwich (GMT) kwenye kamera yako.
- Kwa kufanya hivyo utaongeza thamani ya ushahidi wa picha na kusaidia kudhihirisha ushahidi.

8. Dumisha “Mlolongo wa Utunzaji”.

- Angalia **Nyongeza 6, "Ushahidi Unaoonekana: Kanuni za Mlolongo wa Utunzaji."**
- Lazima uweze kuthibitisha kuwa picha ni ya asili na haikubadilishwa. Iwapo zimebadilishwa - mfano kugeuzwa kutoka kwa urefu kwenda kwa upana - uelezee kwenye nyaraka, na uweze kufafanua kwa nini.
- Picha zote ziwe na vielezo vya wazi na “Mlolongo wa Utunzaji” lazima udumishwe.
- Ushahidi wote wa picha na video uorodheshwe kutumia mfumo imara. Na huo mfumo wa kuorodhesha, uunganishwe na ushahidi mwingine uliobainishwa na utaohusiana na picha/video husika (mfano ushahidi wa aliyenusurika/shahidi).
- Hakikisha kuwa unaandika taarifa zote zinazohusiana na picha/video - nani alipiga picha, lini, wapi, kwa nini na jinsi gani; nani alitoa taarifa zilizosababisha mpiga picha/ mtengeneza picha za senema kurekodi hii, na nani mwingine alikuwepo.
- Kwa picha zilizopigwa na filamu, kumbuka namba ya utoleshaji wa roli ya filamu na namba ya asili ya kila picha kwenye filamu iliyopigwa.
- Kwa kamera ya dijitali, tumia ufumbuzi kiteknolojia ambao unaweka alama (itakayoweza kufanya picha itambulike) kwenye picha wakati wa kupigwa na hatimaye inaweza kutumika kuthibitisha. Kila faili la picha ya dijitali itakuwa na metadata ambayo inaweka taarifa nyingi (kwa mfano tarehe na wakati uliochukuliwa, tarehe na muda picha kubadilishwa, aina ya kamera, uingizaji wa mwangaza na upimo wa urefu).
- Kwa picha kutumika kama ushahid, i ni lazima iwe Picha halisi. Kisifutwe kitu chochote kutoka kwenye picha halisi na kisiongezwe kitu kwenye picha halisi. Iwapo una nakala ya picha, lazima uwe na uwezo wa kuonyesha kuwa ni picha halisi; ni nakala ambayo haikubadilishwa kutoka kwenye picha halisi.
- Kama ikiwezekana, unaporekodi video, jaribu kutokusimamisha na kuanzisha mara kwa mara, ili kulinda dhidi ya fikra/dhana kuwa labda kitu kimeondolewa kutoka kwenye rekodi.

9. Hifadhi na boresha picha kwa njia ya usalama.

- Negativu za filamu zihifadhiwe mbali na joto au mwanga kwa sababu filamu zinaweza kuoza.
- Picha zilizochapishwa, ziwe za filamu au dijitali, zinapaswa kufungiwa pamoja na kuwekwa kumbukumbu itakayosema seti kamili ina jumla ya picha ngapi.
- Kwa upigaji wa picha za dijitali, hamisha yaliyomo kwenye kadi ya flashi kwenda kwenye kompyuta, tengeneza rekodi ya “CD” kwa njia ya “WORM” (Adika mara moja, Soma mara nyingi) au hifadhi picha kwenye kadi ya kumbukumbu yenye ulinzi wa neno la siri. Tengeneza nakala mbili.
- Weka roli za filamu, picha zilizochapishwa, CD na kadi ya flashi katika kabati lililofungwa na ambalo halifunguliwi funguliwi, na uweke rekodi ya kufunguliwa (jina la mtu, tarehe, muda, na lengo la kufungua viandikwe).
- Panga wapi ushahidi utahifadhiwa na nani ataudhibiti. Kimsingi, tumia sehemu ya kuhifadhi ambayo iko kwenye eneo ambalo rahisi kufikia na ambayo inasimamiwa na mlinzi wa ushahidi, hata kama shirika lako litabaki na “umiliki” wa picha.

- Kuwa mwangalifu wakati wa kupita vituo vya ukaguzi, kwani unaweza kuulizwa kuonyesha picha zote (zilizochapishwa na dijitali) au negativu ulizobeba.
- Kumbuka, picha zote na rekodi za video lazima ziorodheshwe kwa namba kwenye mfumo uliyowekwa, na huo mfumo uambatanishwe na ushahidi mwingine unaohusiana na hiyo picha/video uliobainishwa (mfano ushahidi wa aliyenusurika/shahidi).

10. Unaporekodi video:

- Jaribu kuepuka usimulizi ikiwezekana; badala yake, ongezea ushahidi wa video na ushahidi kutoka kwa walionusurika/mashahidi. Kwa maneno mengine, unaporekodi filamu moja kwa moja, matukio yanayoendelea, fanya hivyo kimya na iwe kama yanapotokea bila kufanya simulizi. Kisha fanya mahojiano na mashahidi walioshuhudia ambao wanafahamu nini kilitokea kama inavyoonekana kwenye rekodi ya video; na hakikisha kuwa kuna njia ya kuunganisha tamko la aliyenusurika/shahidi na rekodi ya video. Kwa pamoja, rekodi ya video na tamko la aliyenusurika/shahidi ndiyo ushahidi.
- Hakikisha kwamba unaandika taarifa zote kuhusu nani anarekodi sinema, nani mwingine alikuwepo, tarehe, muda na mahali pa kurekodi, na andika majina ya wote ambao ni waangalizi wa filamu kutoka wakati wa kuanzia kuhifadhi jalada na kuendelea **(angalia Nyongeza 6, "Ushahidi Unaoonekana: Kanuni za Mlolongo wa Utunzaji")**. Pia andika kuhusu nakala za video zilizotengenezwa na ni nina alitengeneza au kuweka nakala.
- Kumbuka kwamba ushahidi usioambatanishwa na jina la aliyeutoa unafaa tu kutumika kama kidokezo.
- Kwa jinsi iwezekanavyo, jaribu kutokusitishasitisha na kuanzisha filamu mara nyingi wakati unarekodi filamu kwenye tukio moja au mahali pamoja. Hii itasaidia kuepuka shutuma za kuwa sehemu yoyote ya video imekatwa.
- Video ikionyesha zaidi eneo, muda wa siku, tarehe, sehemu kubwa ya mazingira na sehemu ndogo ndogo kwa undani zaidi, kutakuwa na uwezekano mkubwa zaidi kuwa itakubalika kama ushahidi wa maana. Ushahidi wa aliyenusurika/shahidi uliobainishwa unaweza kusaidia kuimarisha ushahidi wa video.
- Epuka kutia chumvi - rekodi kama vile wewe haupo, kama vile wewe ni kamera iliyokuweko kwenye tukio lakini sio mtu anayejaribu kutuma ujumbe fulani. Onyesha kiasi kikubwa cha habari kamili iwezekanavyo; Ushahidi unaaminika zaidi iwapo hauko dhahiri sana, kwani matokeo kama haya hayawi dhahiri sana kikawaida.
- Wakati wa kurekodi filamu ya tokeo la vurugu inayoendelea, upe usalama wako kipaumbele kuliko ushahidi. Iwapo umeainisha kuwa kuna usalama wa kutosha kurekodi filamu, jaribu kwa jinsi iwezekanavyo kurekodi sehemu yote kubwa, na baada ya hapo rekodi eneo maalumu bila ya kusitishasitisha na kurudia kurekodi.
- Wakati wa kumrekodi muathiriwa (marehemu) au eneo jingine la uhalifu, rekodi huku ukizunguka nyuzi 360 kurekodi kote, kutoka mbali na kutoka karibu. Pia zunguka mwili wakati unaendelea kurekodi ikiwezekana, ukienda mbele na ukizidi kuukaribia mwili wakati unazunguka, na hatimaye rekodi kikaribu kuonesha majeraha yoyote yatakayotambuliwa.
- Ni wazo zuri kila mara kurekodi kukiwa na tarehe na wakati ukionekana kwenye skrini; lakini uzingatie kwamba hii inaweza kuchezewa, hivyo hakikisha kuwa unaweka tarehe na wakati sahihi.

NYONGEZA 8

## Kuchora eneo la uhalifu, ushahidi unaoonekana na majeraha ya mwili

Mchoro unaweza kutoa mbadala muhimu au akiba ya kuhifadhi picha kwa vile pia ni rekodi ya kudumu inayoonyesha uhusiano wa ukubwa na umbali wa ukubwa wa uhusiano wa eneo la uhalifu na ushahidi unaooekana uliomo humo. Ingawa mchoro huu unaweza usije kutumika kama ushahidi wa msingi, utakusaidia kujikumbushia.

Unaweza kuchagua kuchora mchoro ili kufafanua maelezo yaliopo katika picha zozote ulizopiga (ikiwa ni pamoja na sehemu ilipokuwa kamera na mpiga picha, nk).

11. Chora mchoro wako baada ya kupiga picha na kabla ya kitu chochote kusogezwa.

12. Chora eneo lote, vitu, na taarifa zilizomo (mfano tambulisha watu waliohusika).

13. Unaweza ama kuchora "mchoro usiokamilika" (kwa mfano kuonyesha mpangilio ghafi wa eneo la uhalifu na kurekodi vipimo vya vitu na miundo, na umbali kati ya vitu), au "mchoro uliokamilika" (kwa mfano kumalizia mchoro ulioanzwa, ambao kawaida hutolewa kama kielelezo wakati wa kesi za kisheria za baadaye).

14. Iwapo unachora mchoro wa eneo la uhalifu, unaweza kuchora mchoro kutokea kwa mbali (ambayo ndiyo aina ya kawaida ya mchoro, lakini ambayo haiwezi kuwakilisha urefu wa vitu) au kuingiza mitazamo mingine (kwa mfano mtazamo wa upande).

15. Hakikisha unaweka:

- kichwa cha habari kueleza mchoro unawakilisha nini;
- maelezo yanayofafanua alama zozote zilizotumika kwenye mchoro;
- tarehe, muda na sehemu ya mchoro (na taarifa zingine zozote za maana zitakazosaidia kutambua);
- jina la mtu aliyechora mchoro;
- mwelekeo (kwa mfano kaskazini);
- vipimo vya mchoro (kwa mfano 1:1); na
- maelekezo ya vipimo (kueleza umbali na vipimo vinavyohusu mchoro - ingawa kuwe na maelezo kuwa vipimo vyote vimekadiriwa).

16. Kama una uwezo, fikiria kuchora "ramani" ya eneo la uhalifu, ambayo unaweza kutumia:

- ramani ya msingi (kwa kutumia msingi, kwa mfano kutumia fensi kupima eneo la tukio kwa usahihi);
- kuratibu ramani yenye umbo la mstatili (kwa kutumia misingi miwili);
- ramani ya pembe tatu (kwa kutumia sehemu mbili imara); na/au
- kuratibu ramani ya ncha ya dunia/gridi (kwa kutumia sehemu imara au inayojulikana kuonyesha pembe na umbali) kurekodi eneo la tukio.

Pia fikiria kutumia "GPS" na "Total Stations" ambayo ni mifumo ya kuratibu ramani inayoweza kuchukua vipimo kutokana na ncha ya dunia na kisha kubadili vipimo kwenda kwenye gridi. Hii ni bora kufanywa na wataalamu. Iwapo unatumia GPS, iangalie kwa kiwango cha usahihi (kutakuwa na kipimo kwa hii - chache zitakuwa na usahihi wa pungufu ya mita).

Ni bora kuratibu GPS ya kitu kilicho kwenye sehemu ya kudumu ya kitu kisichohamishika na halafu kupima kitu mwenyewe kutoka hapo.

**Mifano ya picha, michoro na ramani**

Eneo la uhalifu lililo nje




Upigaji picha mbaya dhidi ya upigaji picha mzuri




NYONGEZA 8

Utumiaji wa vipimo na alama



Utumiaji wa vipimo na alama



NYONGEZA 9

# Nyongeza 9

## Kanuni za Ushahidi na Utaratibu kama Zana ya Kuwalinda Walionusurika/Mashahidi

Kuna utaratibu maalum ambao unaweza kutumika na watendaji mahakamani kwa lengo la kulinda walionusurika/mashahidi wakati wanatoa ushahidi wao. Kila mamlaka ni tofauti na kila mahakama itakuwa na sheria mbalimbali za utaratibu na ushahidi. Sehemu hii inaelezea kwa ufupi baadhi ya mifano ya utaratibu wa ulinzi mahakamani ambayo watendaji wanaweza kujitahidi kutumia kutokana na mazingira ya kesi zao (iwapo sheria za utaratibu na ushahidi zinazotumika zinakubali). Inatarajiwa kuwa mapendekezo haya pia yatawatia moyo waendesha mashtaka na majaji kuleta ufumbuzi wa ubunifu kwa ajili ya walionusurika/mashahidi wanapotoa ushahidi mahakamani.

Uzoefu wa jinai wa kimataifa umeweka kanuni za utaratibu na ushahidi: [67]

### 1. Kubainishwa hakuhitajiki kwenye uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia

Kwenye kanuni za utaratibu wa kimataifa za jinai, kubainishwa hakuhitajiki kwenye kesi za unyanyasaji wa kijinsia. Hii ina maana kuwa kwa kupitia uzoefu ushahidi wa aliyenusurika unakuwa ni ushahidi wa kutosha kwa uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia, iwapo utakosekana ubainifu wa aina yoyote nyingine kutoka kwa mashahidi, nyaraka, ripoti za matibabu, picha, au ushahidi wa kubainishwa mwingine wowote. [68]

Hata hivyo, mara nyingi jambo hili linaweza kumaanisha kuwa uaminifu wa aliyenusurika unaweza kuwekwa kwenye changamoto ili kujaribu kudhoofisha ushahidi wake. Watendaji wajue sheria ya kimataifa na kitaifa iliyotokana na kesi zilizoamuliwa ambazo zinaonyesha kuwa ushahidi wa aliyenusurika hauna dosari ya undani utakaoufanya usisadikike. Hivyo ubainishaji hauhitajiki ili kusadikika; na kwa nini hii huwa hivyo, hutokana na asili hiyo ya uhalifu.

### 2. Hairuhusiwi kumwuliza shahidi maswali kuhusu ridhaa bila ruhusa ya mahakama

Katika mazingira ya kitaifa, walionusurika baada ya uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia mara nyingi wanawajibika kuonyesha mahakama kuwa hawakutoa ridhaa kwa tendo la ngono kufanyika. Ukosefu wa ridhaa si kipengele cha uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia kwenye sheria ya kimataifa. Katika mazoea ya kimataifa ya uhalifu, falsafa ya sheria imeendelea kiasi cha kumlinda aliyenusurika kutokana na maswali yanayohusiana na ridhaa. Hii ni kutokana na ukweli wa kuwa unyanyasaji wa kijinsia uliofanywa katika mazingira ya mapambano ya silaha, mauaji ya halaiki na mauaji ya kimbari hufanywa katika mazingira ambayo yanatengua suala la ridhaa. Wamekiri kuwa itakuwa ni jambo la kushangaza kuweka maswali kuhusu ridhaa ya aliyenusurika baada ya uhalifu uliofanywa kwenye mazingira ya uhalifu wa kimataifa, na kwamba kuhakikisha kuwa aliyenusurika asipate madhara kutokana na maswala ya ridhaa. Hakuna umuhimu wala faida yoyote itakayopatikana kwa aliyenusurika kwa kuuliza hilo swali. Ridhaa halisi kwenye mazingira ya vurugu za wengi, shinikizo, kifungo, vitisho, shurutisho na hali zote ambazo uhalifu wa kimataifa unatendeka, huonekana kimsingi kuwa ni kitu kisichowezekana.

67 Dhana hizi zinajitokeza kwa njia mbalimbali katika Kanuni za Utaratibu na Ushahidi kwenye Mahakama ya Kimataifa ya Jinai (ICC), mahakama za hapa na pale na mahakama za mseto. Sehemu hii ya Itifaki inaonyesha dhana kiujumla bila kuangalia mamlaka maalum. Watendaji wanaweza kutumia sehemu hii kama rasilimali kutetea matumizi ya hizi na sheria nyingine ambazo zinaweza kutumika ili kuboresha ushiriki wa aliyenusurika/shahidi katika mchakato wa sheria na uwajibikaji kwenye uhalifu ambao watatoa ushahidi juu yake.

68 Kumbuka kwamba Sheria na Utaratibu wa Ushahidi za ICC zinaeleza wazi kuwa ubainishaji hauhitajiki kwa uhalifu wowote unaoshtakiwa kwenye sheria ya Roma. Kiukweli, ubainishaji unaweza kuimarisha kesi, bila shaka, lakini kukosekana kwa ubainisho haina maana ya kuwa ushahidi hautotosha kwa ajili ya mashtaka au hata kukutwa na hatia.

Sheria za utaratibu na ushahidi zinaweza kuilazimisha timu ya utetezi kumjulisha hakimu kwamba wanapanga kumwuliza aliyenusurika kuhusu ridhaa kabla aliyenusurika hajaingia mahakamani; katika kesi hiyo Jaji atatathmini kabla ya aliyenusurika kuingia mahakamani kuhusu ushahidi walionao unaodai kuwa aliyenusurika alitoa ridhaa, na kuamua kama upande wa utetezi unaweza kuruhusiwa kumwuliza shahidi maswali.

Kwa upande mwingine, upande wa mashtaka unaweza kubisha hilo lisikubaliwe na mahakama itaamua. Ili kuonyesha kwamba mazingira ambayo tendo lilifanyika yalikuwa ya kwamba ridhaa isingeweza kutolewa, mwendesha mashitaka lazima ahakikishe kuwa anatoa ushahidi wa kutosha kuhusu mazingira ambayo yalifanya kutoa ridhaa kusiwezekane.

Katika uzoefu wa kimataifa wa uhalifu, kama mahakama ikiruhusu kuhoji kuhusu madai ya ridhaa, basi kesi itasikilizwa faragha, yaani umma hauruhusiwi kuwepo na utangazaji wowote utasimamishwa. Ni uzoefu mzuri, kwa mahakama kuwa na kikao kisicho wazi kwa umma, ili kusikiliza hoja kuhusu shutuma za hiyo ridhaa.

### 3. Wasaidizi waliopo mahakamani

Katika baadhi ya mazingira inawezekana kutafuta kibali kutoka kwa jaji kuwe na msaidizi mahakamani kwa ajili ya shahidi ili kumpa msaada. Hili ni jambo ambalo linaweza kusaidia kumpa faraja shahidi aliye katika hali ya wasiwasi.

### 4. Kupiga marufuku maswali juu mwenendo wa kabla na baadaye wa ngono

Mahakama nyingi za kimataifa za uhalifu zinakataza maswali yanayohusiana na mwenendo wa aliyenusurika kabla ya tukio linalohusu ngono. Kanuni za ICC zinazuia pia kuhoji juu ya mwenendo wa ngono baada ya tukio. Maswali haya yanaweza kufedhehesha haswa, na katika mazingira ya uhalifu wa kivita, uhalifu dhidi ya ubinadamu na vitendo vya mauaji ya kimbari, yanaonekana kuwa hayahusiki na yasiofaa. Kwa mfano, maswali kama vile "Je, wewe ni/ulikuwa bikira?" yasiruhusiwe kwani yanaweza kuwapa dhiki walionusurika na hayahusiki na kuthibitisha au kukanusha madai ya uhalifu. Watendaji wanaweza kuangalia uzoefu wa kimataifa kama msingi wa kutetea taratibu zinazokataza maswali hayo.

### 5. Hatua nyingine za kinga

Waathirika, hasa (au familia zao na washirika wao wa karibu) kamwe wasihatarishwe kuwekwa kwenye hali ya kutaka kulipiza kisasi au kupata trauma/kiwewe upya kutokana na ushirikiano wao kuwa shahidi. Kila mfumo wa mahakama unapaswa kuwa na hatua za kinga za kutosha kwa ajili ya walionusurika/mashahidi. Hatua hizo ni pamoja na.

*Ulinzi wa kimwili/nje ya mahakama ya shahidi*

- Utaratibu wa kuhamisha shahidi.
- Hakikisha Usafiri na/au malazi salama wakati wa kutoa ushahidi.

*Ulinzi wa utaratibu/ndani ya mahakama*

- Kikao cha mahakama kisichoruhusu umma.
- Kutoa ushahidi ukiwa mbali, kwa mfano kwa kutumia video.
- Kutoa ushahidi kwa jina la bandia.
- Kutoa ushahidi kwa kutumia sauti na picha zilizovurugwa.

- Milango ya kuingilia na maeneo ya kusubiri tofauti kwa mashahidi.
- Utangazaji uliocheleweshwa (kwa kesi zinazotangazwa kwa televisheni).

*Msaada kwa shahidi*

- Ushahidi wa kisheria kuhusu haki na majukumu ya mashahidi.
- Maelezo kutoka kwa upande usiopendelea upande wowote kuhusu mchakato wa kutoa ushahidi.
- Ushauri.
- Msaada wa usimamizi na utaratibu wa ugavi na usafirishaji wa watu na vitu, kwa mfano tafsiri, usafiri, na kudai gharama.
- Kutoa "msindikizaji" kuongozana na shahidi kwenye mchakato wote wa kesi kama msaada wa ziada

Mtendaji ndiye anayetakiwa kutafiti uwezo wa hatua hizi na kutetea ziongezwe kwa ajili ya walionusurika/mashahidi wa uhalifu wa aina hii.

# Nyongeza 10

## Mfano wa Cheti cha Uvamiaji wa Kijinsia

Hiki cheti cha matibabu kuhusu ushahidi wa kisayansi kuhusu uhalifu (forensiki) kinachohitajika na mahakama ni sampuli inayoweza kutumika na madaktari na manesi wanaofanya tathmini ya matibabu inayohitajika na mahakama, na kuweka kumbukumbu za uchunguzi wa mwili na tabia katika vituo vyao vya afya, kwa kiasi iwezekanavyo.

### HATI YA UVAMIAJI WA KIJINSIA

**Nyaraka ya Siri**

Tarehe ya Leo / / Muda _____ : _____ | Eneo la uchunguzi wa matibabu

**A. TAARIFA ZA MGONJWA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Jina la mwisho | 2. Jina la uteuzi/cheo | 3. Jina la kwanza |
| 4. Anwani | | 5. Jinsia ☐ Mwanamke ☐ Mwanamme |
| 6. Umri ☐ Haijulikani | 7. Tarehe ya Kuzaliwa / / ☐ Haijulikani | 8. Sehemu ya Kuzaliwa ☐ Haijulikani |

9. Hali ya ndoa ☐ Huna Mwenza ☐ Mwanandoa ☐ Mjane ☐ Umeachana ☐ Umetengana

*Angalia: Kama mgonjwa ni mwanamme, vuka hadi swali la 14*

10. Tarehe ya mwisho ya kupata hedhi / / ☐ Kabla ya kuvunja ungo ☐ Baada ya kukatika hedhi ☐ Haijulikani

| | | |
|---|---|---|
| 11. Namba za mimba | 12. Namba za watoto waliozaliwa hai | 13. Sasa ana mimba ☐ Ndiyo ☐ Hapana ☐ Haijulikani |

14. Mgonjwa alijamiiana (ngono) kwa matakwa yake mwenyewe katika siku 7 kabla ya uvamiaji
☐ Ndiyo ☐ Hapana

15. Mgonjwa alikuwa na majeraha kwenye mkundu/uke, majeraha, alifanyiwa taratibu za uchunguzi au matibabu ndani ya siku 60 kabla ya kuvamiwa ambayo yanaweza kuuathiri tafsiri ya uchunguzi wa matibabu ya sasa
☐ Ndiyo ☐ Hapana *Kama "Ndiyo" elezea:* ____________________

| | |
|---|---|
| 16. Tarehe na muda wa uvamizi / / _____ : _____ ☐ Haijulikani | 17. Eneo la uvamizi ☐ Haijulikani |

18. Matumizi ya nguvu. vitisho au silaha *(Weka tiki kwa yote ambayo yanahusika)*
☐ Nguvu za mwili ☐ Matumizi ya silaha ☐ Vitisho kwa mgonjwa ☐ Vitisho kwa wengine ☐ Hakukuwepo vitisho vya nguvu ☐ Haijulikani

19. Aina za nguvu/silaha *(Weka tiki kwa yote ambayo yanahusika)*
☐ Fimbo ☐ Visu ☐ Kufunika macho ☐ Mikono ☐ Haijulikani ☐ Kwingine *(Kama vile kulazimisha uchi, kuning'inizwa, mateso ya umeme, shahidi au alihusika kwenye mateso ya wengine, n.k) :* ____________________
☐ Bunduki ☐ Kuzuia ☐ Kunyamazisha kwa nguvu ☐ Miguu

20. Kulazimishia ulevi wa kikemikali kwa mgonjwa *(Weka tiki kwa yote ambayo yanahusika)*
☐ Hapana ☐ Madawa ya kulevya ☐ Pombe ☐ Haijulikani ☐ Kwingine: ____________________

**B. TAARIFA ZA MTUHUMIWA**

1. Idadi ya watuhumiwa
☐ Moja (1) ☐ Mbili (2) ☐ Tatu (3) ☐ Zaidi ya watatu *Kama "zaidi ya watatu" andika namba:* _________ ☐ Haijulikani

| *Mtuhumiwa wa Kwanza: jibu maswali namba 2 hadi 6.* | *Mtuhumiwa wa pili: jibu maswali namba 7 hadi 11.* |
|---|---|
| 2. Uhusiano kati ya mtuhumiwa na mgonjwa ☐ Wanajuana ☐ Wanafamilia ☐ Hawajuani ☐ Mpenzi/Mpenzi wa zamani ☐ Haijulikani ☐ Kwingine: _______ | 7. Uhusiano kati ya mtuhumiwa na mgonjwa ☐ Wanajuana ☐ Wanafamilia ☐ Hawajuani ☐ Mpenzi/Mpenzi wa zamani ☐ Haijulikani ☐ Kwingine: _______ |
| 3. Jinsia ya mtuhumiwa ☐ Mwanamke ☐ Mwanamme ☐ Haijulikani | 8. Jinsia ya mtuhumiwa ☐ Mwanamke ☐ Mwanamme ☐ Haijulikani |
| 4. Takriban umri wa mtuhumiwa ☐ Haijulikani | 9. Takriban umri wa mtuhumiwa ☐ Haijulikani |
| 5. Mtuhumiwa ni ☐ Raia ☐ Polisi ☐ Jeshi ☐ Wanamgambo ☐ Haijulikani | 10. Mtuhumiwa ni polisi/jeshi/mwanamgambo ☐ Raia ☐ Polisi ☐ Jeshi ☐ Wanamgambo ☐ Haijulikani |
| 6. Lugha zinazozungumzwa na mtuhumiwa ☐ Haijulikani | 11. Lugha zinazozungumzwa na mtuhumiwa ☐ Haijulikani |

*Kama watuhumiwa watatu au zaidi, jibu swali la 12*

12. Mwelezee mtuhumiwa kwa undani *(Ikiwa ni pamoja na uhusiano kwa mgonjwa, jinsia, takriban umri gani, kama watuhumiwa ni polisi/jeshi/waasi, lugha wanazoongea n.k):* ____________________

____________________

____________________

| | | | |
|---|---|---|---|
| Jina la daktari | ____________ | NºC.N.O.M. | ____________ |
| Saini ya daktari | ____________ ukurasa wa 1 kati ya 4 | Tarehe | / / |

## HATI YA UVAMIAJI WA KIJINSIA *(inaendelea)*

### C. UFUPISHO WA MATUKIO KAMA INAVYORIPOTIWA NA MGONJWA

| 1. Kuingizwa kwenye sehemu za siri za mwanamke kwa: | Ndiyo | Hapana | Kujaribiwa kwa | Haijulikani | Maoni: |
|---|---|---|---|---|---|
| a. uume | ☐ | ☐ | ☐ | ☐ | ______ |
| b. kidole/vidole | ☐ | ☐ | ☐ | ☐ | ______ |
| c. kitu kigeni | ☐ | ☐ | ☐ | ☐ | ______ |

| 2. Kuingizwa kwenye mkundu kwa: | Ndiyo | Hapana | Kujaribiwa kwa | Haijulikani | Maoni: |
|---|---|---|---|---|---|
| a. uume | ☐ | ☐ | ☐ | ☐ | ______ |
| b. kidole/vidole | ☐ | ☐ | ☐ | ☐ | ______ |
| c. kitu kigeni | ☐ | ☐ | ☐ | ☐ | ______ |

| 3. Sehemu za siri kugusa mdomo kwa: | Ndiyo | Hapana | Kujaribiwa kwa | Haijulikani | Maoni: |
|---|---|---|---|---|---|
| a. mtuhumiwa kwa mgonjwa | ☐ | ☐ | ☐ | ☐ | ______ |
| b. mhusika mwengine kwa mgonjwa | ☐ | ☐ | ☐ | ☐ | ______ |
| c. mgonjwa kwa mtuhumiwa | ☐ | ☐ | ☐ | ☐ | ______ |
| d. mgonjwa kwa mhusika mwingine | ☐ | ☐ | ☐ | ☐ | ______ |

| 4. mdomo kugusa mkundu: | Ndiyo | Hapana | Kujaribiwa kwa | Haijulikani | Maoni: |
|---|---|---|---|---|---|
| a. mtuhumiwa kwa mgonjwa | ☐ | ☐ | ☐ | ☐ | ______ |
| b. mhusika mwengine kwa mgonjwa | ☐ | ☐ | ☐ | ☐ | ______ |
| c. mgonjwa kwa mtuhumiwa | ☐ | ☐ | ☐ | ☐ | ______ |
| d. mgonjwa kwa mhusika mwingine | ☐ | ☐ | ☐ | ☐ | ______ |

| 5. Kugusa uke/kuguswa: | Ndiyo | Hapana | Kujaribiwa kwa | Haijulikani | Maoni: |
|---|---|---|---|---|---|
| a. mtuhumiwa kwa mgonjwa | ☐ | ☐ | ☐ | ☐ | ______ |
| b. mhusika mwengine kwa mgonjwa | ☐ | ☐ | ☐ | ☐ | ______ |
| c. mgonjwa kwa mtuhumiwa | ☐ | ☐ | ☐ | ☐ | ______ |
| d. mgonjwa kwa mhusika mwingine | ☐ | ☐ | ☐ | ☐ | ______ |
| e. mgonjwa kwake mwenyewe | ☐ | ☐ | ☐ | ☐ | ______ |

| 6. Kumwaga manii wakati wa kujamiiana/kojoa: | Ndiyo | Hapana | Haijulikani | Maoni: |
|---|---|---|---|---|
| a. ndani ya kipenyo cha mgonjwa | ☐ | ☐ | ☐ | ______ |
| b. nje ya kipenyo cha mgonjwa | ☐ | ☐ | ☐ | ______ |
| c. elezea sehemu ya kumwagia manii/kojoa | ______ | | | |

### D. USAFI KWA MGONJWA BAADA YA KUVAMIWA

1. Baada ya kuvamiwa, mgonjwa *(Weka tiki kwa yote ambayo yanahusika)*

☐ Alikula ☐ Alikunywa ☐ Alipiga mswaki ☐ Alikojoa ☐ Alioga ☐ Alioga kwa kujiingiza ndani ya maji ☐ Haijulikani

### E. MASIMULIZI YA MGONJWA KUHUSU TUKIO

*Toa ufupisho wa vipengele vya muhimu kuhusu uvamizi kama vinavyoelezewa na mgonjwa. (Kama kuna matukio zaidi au uchunguzi ambao haupo kwenye fomu hii, tafadhali piga chapa maelezo hayo na uyapachike kwenye fomu.)*

______________________________________________

______________________________________________

### F. UCHUNGUZI WA JUMLA WA MWILI WA MGONJWA

| 1. Shinikizo la damu (mmHg) | 2. Mapigo ya moyo (mapigo/dakika) | 3. kupumua (mizunguko/dakika) | 4. Halijoto (Nyuzi) |
|---|---|---|---|
| / | | | |

5. Tabia na hali ya kisaikolojia *(Weka tiki kwa yote ambayo yanahusika)*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ☐ hofu | ☐ kujitenga | ☐ kusikitisha | ☐ aibu | ☐ hali kuharibika akili |
| ☐ hasira | ☐ kushtuka | ☐ kilio | ☐ bubu | ☐ wasiwasi |

**KUMBUKA KU:** KUSANYA USHAHIDI WA JUMLA *(Utoko/Mnyeso wa maji maji au mkavu, madoa, nguo, vitu vya kigeni kwenye mwili wa mgonjwa);* TUMIA VIFAA VYA KUPIMA UBAKAJI *(Kama vipo)* NA MLOLONGO WA FOMU ZA KIZUIZINI; na PIGA PICHA

Jina la daktari ______________ NºC.N.O.M. ______________

Saini ya daktari ______________ ukurasa wa 2 kati ya 4 Tarehe ____/____/____


## HATI YA UVAMIAJI WA KIJINSIA *(inaendelea)*


### F. UCHUNGUZI WA JUMLA WA MWILI WA MGONJWA *(inaendelea)*

**Simulizi: Matokeo ya utafiti**

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **A** Mchubuo | **BI** Ng'ata | **BU** Ungua | **DB** Mabaki ya Kuvunjika | **DF** Ulemavu | **DS** Utoko / Mnyeso mkavu | **EC** Chubua | **ER** Wekundu | **FB** Kitu kigeni (kieleze) |
| **FI** Ufumwele | **G** Jeraha la risasi | **I** Kukata chale | **L** Mkwaruzo | **M** Utoko/Mnyeso wa maji maji | **O** Majeraha mengine (eleza) | **P** Kuathirika (ikiwa na pamoja na maumivu) | **S** Kuvimba | **V** Uotaji (pamoja na udongo, uchafu) |

*Weka namba ya kila jeraha/utakachokiona cha kujificha kwenye picha hapa chini.*
*Kwenye jedwali hapa chini, andika namba na uwiano kwa alfabeti za ufupisho zinazohusika (angalia jedwali hapo juu)*





| Sehemu ya Mwili | Matokeo ya utafiti | Maoni: |
|---|---|---|
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |

### G. UCHUNGUZI WA SEHEMU ZA SIRI (MWANAMKE)


*Tumia simulizi iliyo hapa juu kutambua na kuonyesha vipengele vya uchunguzi wa sehemu za siri kwenye michoro iliyo kando. Chunguza ndani ya mapaja, nje mwa sehemu za siri, na msamba na mkundu (weka tiki kwenye visanduku kama kuna matokeo ya kuvamiwa kwa ngono)*


| | | |
|---|---|---|
| **1. Majeraha ndani ya mapaja** | ☐ Ndiyo | ☐ Hapana |
| **2. Uvimbe wa ngozi ya fumbatio** | ☐ Ndiyo | ☐ Hapana |
| **3. Majeraha ya sehemu kati ya mkundu na uke** | ☐ Ndiyo | ☐ Hapana |
| **4. Jeraha la mashavu ya sehemu ya siri ya mwanamke kwa nje** | ☐ Ndiyo | ☐ Hapana |
| **5. Jeraha la mashavu ya sehemu ya siri ya mwanamke kwa ndani** | ☐ Ndiyo | ☐ Hapana |
| **6. Jeraha la kizinda** | ☐ Ndiyo | ☐ Hapana |
| **7. Kisimi/jeraha la maeneo kukizunguka** | ☐ Ndiyo | ☐ Hapana |
| **8. Matako/ukingo wa mkundu/mikunjo/ majeraha ya mikunjo** | ☐ Ndiyo | ☐ Hapana |

**9. Maumivu ya kuma**
☐ Ndiyo ☐ Hapana

**10. Mlango wa kizazi**
☐ Ndiyo ☐ Hapana

**11. Hali iliyotumiwa kufanya uchunguzi**
☐ Kulala chali
☐ Goti - kifua
☐ Kwingine






### H. UCHUNGUZI WA VIUNGO VYA UZAZI (WANAUME)

*Tumia simulizi iliyo hapa juu kutambua na kuonyesha vipengele vya uchunguzi wa sehemu za siri kwenye michoro iliyo kando. Chunguza ndani ya mapaja, nje mwa sehemu za siri, na msamba na mkundu (weka tiki kwenye visanduku kama kuna matokeo ya kuvamiwa kwa ngono)*

| | | |
|---|---|---|
| **1. Majeraha ndani ya mapaja** | ☐ Ndiyo | ☐ Hapana |
| **2. Jeraha la kichwa cha uume au jeraha la uume wenyewe** | ☐ Ndiyo | ☐ Hapana |
| **3. Jeraha la pumbu** | ☐ Ndiyo | ☐ Hapana |
| **4. Jeraha la kende** | ☐ Ndiyo | ☐ Hapana |
| **5. Mgonjwa ametahiriwa** | ☐ Ndiyo | ☐ Hapana |
| **6. Matako/ukingo wa mkundu/mikunjo/majeraha ya mikunjo** | ☐ Ndiyo | ☐ Hapana |
| **7. Kutokwa damu sehemu ya nyuma** | ☐ Ndiyo | ☐ Hapana |



**Jina la daktari** ______________________ **NºC.N.O.M.** ______________________

**Saini ya daktari** ______________________ **Tarehe** ______ / ______ / ______

## HATI YA UVAMIAJI WA KIJINSIA *(inaendelea)*

### I. UCHUNGUZI WA MAABARA NA UTAFITI MWINGINE

| *UMEFANYWA:* | Ndiyo | Hapana | *MAJIBU:* |
|---|---|---|---|
| 1. UKIMWI | ☐ | ☐ | ________ |
| 2. Kaswende | ☐ | ☐ | ________ |
| 3. Homa ya manjano | ☐ | ☐ | ________ |
| 4. Vipimo vya njia ya uzazi (PAP smear) | ☐ | ☐ | ________ |
| 5. Uchunguzi wa mimba | ☐ | ☐ | ________ |
| 6. Uchunguzi wa mkojo | ☐ | ☐ | ________ |
| 7. Vipimo vya kuchunguza shahawa/kuambukizwa (wet mount for sperm) | ☐ | ☐ | ________ |
| 8. Vipimo vya mionzi (Ultrasound) | ☐ | ☐ | ________ |
| 9. Uchunguzi mwingine | ☐ | ☐ | ________ |

### J. MATIBABU/MPANGILIO

| | Ndiyo | Hapana | Maoni: |
|---|---|---|---|
| 1. Vipimo vya kinga baada ya mfichuo (PEP) | | | |
| a. PEP | ☐ | ☐ | ________ |
| 2. Dawa | | | |
| a. Kiuavijasumu | ☐ | ☐ | ________ |
| b. Dawa za maumivu | ☐ | ☐ | ________ |
| c. Kuzuia mimba kwa dharura | ☐ | ☐ | ________ |
| d. Nyingine | ☐ | ☐ | ________ |
| 3. Kupelekwa rufaa | | | |
| a. Mgonjwa atapelekwa rufaa kwa mtaalam leo | ☐ | ☐ | ________ |
| 4. Fomu ya polisi | | | |
| a. Fomu ya polisi imemalizika | ☐ | ☐ | ________ |
| b. *Kama jibu la 4a ni "Hapana,"* je mgonjwa anataka kuripoti polisi? | ☐ | ☐ | ________ |
| c. *Kama jibu la 4b ni "Hapana,"* je mgonjwa alishauriwa kuhusu umuhimu wa uchunguzi wa polisi? | ☐ | ☐ | ________ |

### K. TATHMINI YA MATOKEO

1. Historia ya matukio: ________
2. Uchunguzi wa mwenendo: ________
3. Matokeo ya dhahiri: ________
4. Uchunguzi wa Maabara: ________
5. Nyaraka zilizojazwa zimeunganishwa na cheti hiki:

☐ Matokeo ya uchunguzi wa maabara ☐ Masimulizi yaliyoandikwa (bora yaliyopigwa chapa) ☐ Picha ☐ Haihusu

### L. MWISHO WA TATHMINI

1. Matokeo ya tathmini ya matibabu ni: *(Chagua moja tu)*

☐ YANAKUBALIANA na
☐ YANAKUBALIANA SANA na
☐ UCHUNGUZI YAKINIFU wa
☐ HAYAKUBALIANI na

Uvamizi wa KIJINSIA

2. Matokeo ya tathmini ya matibabu ni: *(Chagua moja tu)*

☐ YANAKUBALIANA na
☐ YANAKUBALIANA SANA na
☐ UCHUNGUZI YAKINIFU wa
☐ HAYAKUBALIANI na

Uvamizi wa MWILI

### M. KIAPO CHA DAKTARI

*Mimi nimetoa ridhaa kwa mgonjwa kwa ajili ya tathmini, picha, na uhamisho wa hati ya kiapo kwa mfumo wa kisheria au kutekeleza sheria.*

☐ Ndiyo ☐ Hapana

*Mimi ninaapa kwamba taarifa zinazotolewa katika fomu hii ni za kweli na kamili kwa kadri ya ufahamu wangu na imani yangu.*

Jina la daktari ________
Saini ya daktari ________
Tarehe ____/____/____

Jina la daktari ________ NºC.N.O.M. ________
Saini ya daktari ________ ukurasa wa 4 kati ya 4 Tarehe ____/____/____

NYONGEZA
9

NYONGEZA
9

Viwango vya Msingi vya Njia Bora za Kutayarisha Nyaraka za Unyanyasaji wa Kijinsia kama Uhalifu chini ya Sheria ya Kimataifa

**TOLEO LA KWANZA: JUNI 2014**

Foreign & Commonwealth Office
King Charles Street, London
SW1A 2AH
United Kingdom (Uingereza)